# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 29 Mei, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendele na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, leo ni kikao cha Thelathini na Nane. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Nje na Ushirikiano, Dkt. Damas Daniel Ndumbalo, tunakushukuru.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Leo tunaanza na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali la kwanza linaulizwa na Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga, Mheshimiwa uliza swali lako.

Na. 316

### Maabara za Sayansi katika Sekondari za Kata

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE** aliuliza:-

Serikali inafanya juhudi katika kuendeleza elimu hapa nchini kwa kutoa elimu bure na hata kujenga Shule nyingi zikiwemo za kata.

Je, lini sasa Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Maabara za Sayansi katika Shule zote za kata nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la wananchi wa Mwanga, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Mwita Mwikwambe Waitara tafadhali!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMIESEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe, Mbunge wa Mwanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mpango wa ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi katika shule za sekondari kwa kushirikisha wananchi na wadau wa maendeleo wa ndani na nje. Katika mwaka wa fedha 2019/ 2020, Serikali imetenga kiasi cha jumla shilingi bilioni 107.1 zikiwemo shilingi bilioni 58.2 kupitia mpango wa lipa kulingana

na matokeo *(EP4R)* na shilingi bilioni 48.9 kupitia mgango wa kuboresha shule za sekondari *(SEQUIP)* ambapo sehemu ya fedha hizo zitatumika kukamilisha ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi kwa shule za sekondari za kata nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maghembe, swali la nyongeza!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nimejibiwa, kwa kuwa nchi yetu itahitaji wanasayansi huko mbele tuendako, na hivi sasa tunavyojenga uchumi wa viwanda. Je, Serikali haioni kwamba hali tuliyonayo katika shule zetu za sekondari ambapo shule za Serikali zina walimu wazuri sana lakini hazina maabara na shule zile za binafsi zina maabara, walimu siyo wazuri kama wale wa Serikali, lakini watoto wale ndiyo wanafaulu mitihani. Serikali ina mpango gani hasa kuhusu kuwaandaa wanasayansi watakaoiendeleza nchi yetu huko mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nimeona fedha hapa vimetengwa, kwa ajili ya maabara, si maabara peke yake kama ulivyoona swali lenyewe. Nilikuwa nataka nimuulize Waziri, kati ya fedha hizi ni shilingi ngapi zitapelekwa Mwanga kwa ajili ya kusaidia wananchi kujenga maabara ya Msalagambo yale yaliyojengwa sasa?

**SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa na takwimu kwa harakaharaka namna hii lakini, majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa, tafadhali!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Profesa ameuliza kwa uchungu na yeye pia ni mwanasayansi ni Profesa katika eneo hilo na tunatambua changamoto iliyopo ya masomo ya sayansi na hasa maabara, lakini niseme, fedha ambazo nimetaja hapa shilingi bilioni 58.2 ni mwaka wa fedha huu 2019/2020, lakini mwaka wa fedha uliopita tumepeleka fedha kwenye shule za sekondari 1964, lakini hapa tulipo tunafanya mchakato

wa kupeleka tena fedha za vifaa vya maabara katika shule zetu zaidi ya 2000.

Mheshimiwa Spika, lakini ujue kwamba sisi sekondari za Serikali ni 3632, kwa hiyo tunaamini baada ya mpango huu kukamilika ndani ya mwaka huu mpaka 2020 karibu kila maabara itakuwa na vifaa vya kutosha katika eneo hilo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa nimtoe wasiwasi kwa jambo hili na kwamba tumejipanga namna ya kufanya vuzuri, lakini tumeshatoa maelekezo, maeneo ambayo kuna upungufu wa maabara kuna namna njia mbadala zimefanyika ndiyo maana leo ukiangalia hata pale viwanja vya Jamuhuri kuna maonesho yanafanyika na walimu wetu wamefundishwa kufanya njia mbadala ili tuweze kufundisha watoto wetu kwa vitendo na ufaulu utakuwa unaongezeka kutoka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili la kuuliza, kama ulivyosema, kwamba sina *data* hapa lakini nadhani baada ya kipindi cha maswali na majibu ninaweza nikampa kumbukumbu, data kamili kwamba yeye katika eneo lake la Mwanga atapata shilingi ngapi katika shule aliyoitaja, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, bado tuko TAMISEMI, swali litaulizwa na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma. Mhehimiwa Kiteto tafadhali, kwa niaba yake.

Na. 317

## Halmashauri zisizotenga Asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake na Vijana

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA** aliuliza:-

Serikali imeziagiza halmashauri zote nchini kutenga asilimia tano ya vijana na asilimia tano ya wanawake kutoka mapato ya ndani ili kuchangia mfuko wa maendeleo wa wanawake na vijana:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa halmashauri ambazo hazizingatii takwa hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, asilimia 10 ya vijana wanawake na walemavu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMIESEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hapo awali utekelezaji na usimamizi wa mfuko wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, ulikuwa na changamoto kutokana na kutokuwepo kwa sheria na kanuni. Baadhi ya Halmashauri zimekuwa zikitenga asilimia 10 kutoka katika mapato yake ya ndani bila kujali vyanzo lindwa na fedha zenye maelekezo maalumu kama vile *CHF* na fedha zenye maelekezo maalumu.

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni, 2018, Serikali ilifanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura Na. 290 kwa kuongeza kifungu cha 37(a) ambacho kimeelekeza namna bora ya kusimamia fedha hizo. Kufuatia marekebisho ya sheria hiyo, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) imeandaa kanuni ambazo zimefafanua namna bora ya kutenga fedha hizo, kutoa mikopo na kusimamia utekelezaji wake. Kwa mujibu wa kanuni hizo, asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu itatengwa baada ya kutoa vyanzolindwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais (TAMISEMI) itaendelea kuzismamia halmashauri kuhakikisha zinatekeleza sheria hii na kanuni zake za mfuko wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa halmashauri zitakazoshindwa kutekeleza sheria hiyo na kanuni zake. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma, tafadhali.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini kwa umuhimu mkubwa sana wa suala hili, Serikali nimeuliza ni hatua zipi zinazochukuliwa, lakini Serikali imeniletea majibu kusema kwamba sheria imetungwa. Sheria tumeitunga sisi wenyewe Wabunge na tumeipitisha sisi wenyewe na imesainiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, lakini je, ni hatua gani zimechukuliwa? Ndiyo lilikuwa swali langu la msingi, lakini nasikitika kwamba halijajibiwa kwa sababu hakuna hatua amabazo zimeonyeshwa kuchukuliwa katika halmashauri ambazo hazitengi fedha hizi na ukizingatia kwamba fedha hizi zinasaidia maendeleo ya kiuchumi kule kwa yale makundi maalumu ambayo yametajwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali iweze kusema ni hatua zipi ambazo zimechukuliwa hasa baada ya Serikali ya kutungwa kwa sheria.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa kuwa zipo halmmashauri ambazo zina changamoto ya mapato, je, Serikali ina mkakati gani wa kuzisaidia halmashauri hizo ili ziweze kutenga asilimia 10 ya haya makundi ili waweze kuchochoe maendeleo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ni kweli alitaka kujua hatua, lakini nimesema kwenye jibu la msingi kwamba, sheria hizi na kanuni zimetungwa mwaka jana 2018 na mwaka huu wa bajeti tumepitisha fedha ambazo zinakwenda kwenye mwaka 2019/2020. Sasa hizi halamshauri ambazo zitashindwa kutekeleza sheria hii, baada ya sheria hii kuwa *in place,* tumetangaza kanuni wanazo, *then* hatua zitachukuliwa dhidi

ya hawa watu ambao wamekuwa wakichukua hizi fedha. Kwa sababu mwanzoni sheria haikuwepo na kanuni hazikuwepo ilikuwa halmashauri inatenga kwa kujisikia. Hayo ndiyo majibu ya Serikali na Mheshimiwa Mbunge avute subira.

Mheshimiwa Spika, na maelezo ya nyongeza ni kwamba, kwa bahati nzuri halmashauri zote, mikoa yote na wakurugenzi, kwenye mwaka huu wa fedha wakati wa mjadala wa bajeti ya TAMISEMI, kila Mkurugenzi alikuwa anaji-*commit* kwamba anarudi kwa hii awamu ya robo ya nne ya mwisho, ni lazima wakamilishe kutenga fedha kwa kiwango tulichokubaliana na mwaka wa fedha wa bajeti ujao, kama kuna mkoa utakuja bila kukamilisha zoezi hili na niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwenye ziara zetu katika majimbo na wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, nendeni kwenye halmashauri, Wakurugenzi wawaonyeshe fedha zilizotengwa, vikundi vilivyokopeshwa, miradi ambayo imeanzishwa ili mtupe taarifa tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, anauliza habari ya changamoto za mapato. Nimezungumza vilevile kwenye jibu la msingi, hata kama halmashauri inakusanya shilingi 100, imeelekezwa, ndani ya hicho ilichokusanya kidogo hicho, itenge asilimia 10 ya fedha hizo baada ya kuondoa mapato lindwa. Kwa hiyo, katika hoja hii na katika sheria hii na kanuni zetu, hakuna halmashauri ambayo itapata utetezi wa kwamba mapato ni ya chini. Hatukumlazimisha apeleke bilioni mbili, bilioni 10, bilioni 100, tumesema, 10% ya makusanyo ya mapato lindwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, nimekuona Mheshimiwa, uliza swali lako.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ukifuatilia *trend* ya utoaji wa hizi fedha za vikundi asilimia 10, mara nyingi Wakurugenzi wamekuwa wakijificha kwenye *revolving fund*, wakitoa ile *revolving fund* ambayo imerudishwa na vikundi, utadhani ya kwamba imetolewa

aislimia 10. Wizara mko tayari kuweka mchakato ambao utaweka wazi *revolving fund* na *10%* ya mapato ya kila mwaka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Yaani katika kuliweka vizuri Mheshimiwa Naibu Waziri kabla hujajibu swali la Mheshimiwa, hii asilimia 10 ni vizuri Wabunge wote wakapata nakala ya hili agizo lenu. Kwa sababu kuna 40% ya maendeleo, ambayo, katika mapato ya ndani lazima 40% iende kwenye hii miradi ya maendeleo, 20% iendende kwenye vijiji, 10% iende kwenye lishe. Sasa hii 10% hii, inatokana na 10% katika 40% ya maendeleo? Au hii 10% inajitegemea? Yaani wapate tu nakala fulani ambayo itaonyesha mchanganuo vizuri, enedelea na ufafanuzi wa swali la Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, naomba nikubali kwamba kwa maelekezo yako tutafanya hivyo ulivyosema kwa maana ya kupeleka nakala kwa kila Mbunge kueleza ufafanuzi tunamaanisha nini katika hii 10% ambayo inapaswa kuwa imetengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nijibu sasa swali la nyongeza la Mheshimiwa Ryoba, ni kweli, wakati wa mjadala wa bajeti Waheshimiwa wa Kamati ya Utawala na TAMISEMI waliliona hili, na kweli imeonekana kuna halmashauri zingine wakichukua fedha wamekopesha, wakizirudisha, wengine walituambia ilionekana wanatoa taarifa ya kwamba walishapata mpaka asilimia 180, 120, wakaulizwa, hii nyingine ya ziada mmeitoa wapi. Ikaonekana kwamba, kikundi kikitoa fedha, wakikirudisha wanajumuisha wanasema imekusanywa, kwa hiyo, tukaelekeza kwamba na sasa hivi tumefungua akauti, kwenye kanuni mpya iliyotengenezwa, kutakuwa na akaunti mahususi ambayo fedha hii inaingia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, umapokusanya fedha zitaonekana, zinaporejeshwa zitaonekana kwa hiyo, hakutakuwa na kuchanganya kati ya fedha ambayo imekopesha na fedha ambayo imekusanywa, lakini Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema, na hili nalo

tutaona na nakala na kanuni watazipata ili kuweza kusimamia vizuri utengaji wa hizi fedha lakini usimamizi wake na utekelezaji wake.

**SPIKA:** Ahsante naomba tuendelee na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, kwa niaba yake Mheshimiwa Rashid Shangazi nimekuona.

Na. 318

**Athari za Uzito Mkubwa wa Mwili**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI (K.n.y. MHE. KHADIJA NASSIR ALI)** aliuliza:-

Uzito mkubwa wa mwili ni dalili za mwanzo za magonjwa yasiyoambukiza:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupambana na magonjwa haya?

(b) Je, mbali na mazoezi ni mbinu gani nyingine za kitaalamu za kupambana na vitambi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Abdallah Ulenga, Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mnamo mwaka 2011 ilianzisha

rasmi kitengo cha kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa lengo maalum la kukinga na kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Aidha tumetengeneza mpango mkakati wa kupambana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza wa mwaka 2016-2020, ambao umewekwa malengo bayana, mikakati na utekelezaji wake ili kupambana na ongezeko la magonjwa haya. Mikakati inayotekelezwa katika mkakati huu ni pamoja na utoaji wa elimu kwa jamii kuhusu magonjwa haya na kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo vipeperushi, redio, runinga, mitandao ya kijamii, na nyinginezo ili kuongeza uelewa kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupunguza viashiria vya hatari ambavyo vinaweza kurekebishika kwa kuhamasisha juu ya ufanyaji wa mazoezi, ulaji unaofaa, kuhamasisha kuacha matumizi ya tumbaku na pia kupunguza unywaji wa pombe kupita kiasi. Kuhakikisha huduma za uchunguzi wa awali, yaani *screening for early detection*, kwa magonjwa haya zinapatikana katika vituo vya afya pamoja na fanya kambi za wazi za kupima na kutibu magonjwa haya. Kutoa chanjo kwa magonjwa yanayoweza kukingwa kwa njia hii mfano, chanjo ya *HPV* kwa ajili ya kujikinga na saratani ya shingo ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, ikitokea kwa bahati mbaya, ugonjwa umegundulika katika hatua za mwisho, pia eneo hili halijasahaulika. Wizara ina mkakati ambao unashughulikia uimarishaji wa huduma za tiba shufaa yaani *palliative care* na pia huduma ya tiba ya utengamao yaani *rehabilitation services.* Upo pia mkakati unaoangalia maeneo ya tafiti ili kuimarisha suala zima la upatikanaji wa takwimu sahihi za magonjwa haya.

Mheshimiwa Spika, kitambi ni dalili mojawapo ya uzito uliopita kiasi, hii si dalili njema na hupelekea magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Njia bora ya kupambana na kitambi ni kujikinga kwa kutokukipata kwa kuhakikisha unazingatia ulaji wa vyakula unaofaa na kufanya mazoezi. Iwapo mtu akiwa ameshakipata kitambi, basi njia mojawapo ya kuondokana nacho ni kuzingatia ulaji unaofaa kwa kupunguza kiwango

cha vyakula vya wanga, kupunguza kiwango cha sukari, chumvi na mafuta kwenye chakula. Kunywa maji yasiyopungua lita moja na nusu kwa siku kwa mtu mzima na kupunguza unjwaji wa pombe uliopitiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani sasa nyongeza ziwe za wenye vitambi! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Rashid Shangazi tafadhali, swali la nyongeza!

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa hapa amebainisha wazi kwamba kitambi kinasababishwa zaidi na vyakula vilivyopitiliza hasa vyenye wanga na kwa tamaduni zetu watanzania karibia vyakula vyote tunavyovitumia ni vya wanga. Je, Serikali inatushauri watanzania tule vyakula gani ili kuepukana na vitambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, utakuwa ni shahidi kwamba sasa hivi kuna ongezeko kubwa sana la uzito uliopitiliza kwa watoto, vijana lakini hata kwa akinamama na hapa tunapozungumza hivyo vitambi pia hata kina mama wanavyo. Sasa tunataka tuone kwamba Serikali ina mkakati gani mahususi, hapa wamezungumzia habari ya chanjo lakini pamoja na hizo elimu wanazotoa, ni nini kifanyike ili tatizo hili lisiendelee kuathiri haswa malika haya madogo ambayo nimeyataja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nini kifanyike kupambana na vitambi hasa vya watoto.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, wanga kwa nini ndiyo unaosababisha na Serikali ina ushauri gani? Kwa ruksa yako naomba niwakumbushe hatua za kibailojia kidogo Waheshimiwa Wabunge, wanga ni mzuri kwa mwili, lakini kazi ya wanga ni kuzalisha nguvu tu,

unapoliwa ukapitiliza kwa wale ambao mnakumbuka somo ya biolojia wanga uliozidi unageuzwa kwenda kuwa *complex compound* inayoitwa *glycogen* haya ni mafuta. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, sasa *glycogen* katika mwili wa binadamu hasa mtu mzima hauna kazi nyingine yoyote isipokuwa ni kuhifadhiwa, na huu hii *glycogen* ambayo kiasili ni protini inahifadhiwa katika maeneo mbalimbali ya mwili wa binadamu ikiwa ni pamoja na mishipa ya kupitisha damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunasema pamoja na *appetite* ambayo inaweza kukufanya ule ugali mwingi sana, lakini ni vizuri ukala kiasi kile ambacho kitakwenda kuzalisha *energy* kwa maana ya nguvu ya kuusukuma ule mwili wenyewe, unapokula ziada ndiyo huleta matatizo.

Sasa sisi ushauri wetu kama Serikali nini, kwanza ni kula ulaji ambao unazingatia mlo wenye tunaita mlo bora na hasa protini na katika upande wa protini pamoja na ubora wote wa protini za nyama, lakini protini iliyo bora zaidi ni ile protini inayotokana na mimea. Ushauri wetu Waheshimiwa Wabunge mle zaidi protini na hasa protini zinazotokana na mimea.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge Rashid Shangazi anauliza nini kifanyike ili hili rika ambalo linaonekana linaathirika zaidi kama vile vijana na hata wakinamama amewataja. Sisi Serikali tunashauri, kwa kawaida kisayansi inakubalika kwa watu wazima kuwa ndiyo waathirika zaidi wa upatikanaji wa vitambi, wanapopata vijana ni jambo lisilokuwa la kawaida. Sasa vijana wanachoshauriwa ni kubadilisha *lifestyle* namna ya uendaji katika maisha, ulaji wa chipsi uliopitiliza, na unywaji wa pombe uliopitiliza haya ndiyo yanayopelekea matatizo haya...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, lakini na ufanyaji wa mazoei pia, ninashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa niangalie wenye vitambi, wasiokuwa na vitambi hapa hawana ruhusa ya kuuliza swali, Mheshimiwa Mwalongo, alikuwa amesimama mwanzoni alisimama, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Hatib, Mheshimiwa Mwalongo swali fupi.*(Makofi)*

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kwa kifupi sina kitambi nina mwili mkubwa. Nashukuru sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa sisi Wabunge chanzo cha matatizo ambayo Wabunge wengi wanayo ni *canteen* yetu*. (Kicheko/ Makofi)*

Je, Serikali sasa ipo tayari kuwapa *menu* watu wa *canteen* waandae chakula ambacho kinaweza kikawafaa Wabunge ili wasiwe na miili hiyo waliyonayo sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hilo ni swali kwa Spika, tumelichukua ushauri huo moja kwa moja, na tunawaomba Waheshimiwa Wabunge kila mtu kwa wakati wake ajaribu kutuandikia kwenye karatasi yoyote ile aina ya *menu* ambazo mnapendekeza mzilete mezani hapa ili kutahikishe kwamba *canteen* yetu inakuwa na vyakula ambavyo ni vya kiafya zaidi, Mheshimiwa Nape. *(Makofi)*

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niiulize wali dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana mdogo wangu Ulega inaonekana shuleni alifanya vizuri kwenye somo la biolojia, na ni mfano mzuri nimefuata ule ushari wake ndiyo maana kitambi changu kimepungua. Serikali inajitahidi kupambana na magonjwa mbalimbali nchini hivi karibuni kuna ugonjwa wa homa ya Dengue ambao hali yake sasa ni mbaya na vimeanza kuripotiwa vifo kutokana na jambo hili*. (Makofi)*

Sasa Serikali inachukua hatua gani kwa kuhakikisha jambo hili linakwisha kwa sababu tukiendelea kulinyamazia vifo vitaendelea kuongezeka watu wanaendelea kumwa na hali ya Jiji la Dar es Salaam kwa sasa ni mbaya?

**SPIKA:** Ingawa ni pembeni kidogo lakini naruhusu mjibu, Serikali mnalipokeaje hili jambo la Dengue.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye Mbunge wa Mtama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hapa karibuni imeibuka ugonjwa wa Dengue na hasa katika Jiji la Dar es Salam, Serikali inafahamu juu ya tatizo hili na imeanza kuchukua hatua za makusudi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote na watanzania. Moja katika jambo kubwa ililoligundua Serikali ni kuwa gharama kubwa zinazolipwa na watanzania wanaopata matatizo hayo katika sehemu za kutolea huduma za afya. Sasa katika Serikali jitihada inayofanyika hivi sasa ni kuhakikisha matibabu ya Dengue yanakuwepo na yanapatikana kwa bei zilizokuwa nafuu ili kuweza kuwasaidia watanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib nishakutaja.

**MHE. KHATIB SAID HAJI**: Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Turudi kwenye kitambi sasa tuje kwenye maswali ya vitambi.

**MHE. KHATIB SAID HAJI**: Mheshimiwa Spika, ahsante, mara nyingi tunaambiwa kwamba wale wanaotaka kupunguza mwili ama vitambi wanakatazwa kula aina ya nyama na badala yake wanaelekezwa kula samaki na nyama za kuku, lakini katika hizi nyama za kuku kuna hawa makuku kutoka nje ambao kama yanauzwa kama *KFC* ambayo yanamapaja kama watu, Mheshimiwa hebu tunataka ushahidi juu ya kuku hawa wa kizungu *broilers* hasa katika kuongeza vitambi. *(Kicheko)*

Je, hawana mahusiano ya moja kwa moja kuku hawa? Ahsante.

**SPIKA:** Kuku anapaja kama mtu hiyo mbona hatujaona, Mheshimiwa Naibu Waziri ulishawaona kuku hawa, majibu tafadhali. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ulaji wa kuku *broilers* kwanza kuku ni katika protini na nimesema na nimesema katika jibu la msingi kuwa protini ni muhimu, protini ziko za aina inyotokana na wanyama na ile protini inayotokana na mimea. Lakini anataka uhakika ya kwamba *broilers* wanatatizo hilo la kuweza kumfanya mtu awe na kitambi au laa!

Mheshimiwa Spika, hakuna utafiti wa kisayansi unaokwenda kutupelekea kutuambia kuwa *broilers* wanashida katika afya ya wanadamu, jambo hili liko palepale, ulaji wa kupitiliza unaweza kukupelekea katika hayo matatizo. Lakini naomba niwahakikishie *broilers* hawana shida yoyote, kinachowafanya *broilers* wakue ni *hormones,* ambazo *hormones* kisayansi ni *vitamins*. Kwa hivyo sisi wanasayansi tunachokifanya vyakula vya *broilers* tunaweka *vitamins* za kutosheleza za kuhakikisha ukuaji wao unakuwa ni ukuaji wa haraka…

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kulinganisha na kuku wa kienyeji.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri na wasio na vitambi wamelalamika Mheshimiwa Musukuma kwa niaba ya swali la mwisho kabisa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali langu. Nilikuwa napenda kuiuliza Serikali kwamba sisi tusiokuwa na vitambi tunakula vyakula vyote hivyo ambavyo Mheshimiwa Dkt. Ulega amevizungumza na hatujawahi kuona mabadiliko

yoyote katika maumbile yetu. Je, Serikali inatushauri tule nini zaidi kwa sababu vya wanga, vinywaji vyote tumetumia bado tuko kwenye maumbile haya haya.

Je, Serikali inatushauri tule nini ili na sisi tubadilike tufanane na wao? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuna watu miili yao haina shukurani kama Mheshimiwa Musukuma wao nao wafanyaje Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nataka kujua watu wa aina yake ambao miili yao haina shukurani kama ulivyoiita wafanyeje? Na yeye anataka kupata kitambi, namshauri Mheshimiwa Musukuma na yeye ikiwezekana apate kuwaona watalaam wa lishe nina hakika watampangia *diet* ambayo itampelekea na yeye kupata mwili anaouhitaji.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete swali la mwisho eneo hilo tafadhali.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nitaenda kwenye swali la msingi kuhusu *non committable disease*, 2016/2020 ulitengenezwa mkakati maalum kuhusiana na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukizwa.

Je, mkakati huu wamagonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza ulikuwa ni kwa nchi nzima au ulikuwa ni *pilot project*? Na kama ni *pilot project* kwa maeneo gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri sijui kama utakumbuka kuhusiana na mkakati huu majibu tafadhali kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, mkakati ulikuwa ni *pilot* ama ulikuwa ni wan chi nzima. Utafiti kwa kawaida huwa ni *pilot* unachukuliwa eneo moja

halafu kwa njia labda kama ya *sampling* kisha matokeo yanatokana na eneo lile yanaweza kuwa ndio matokeo elekezi. Kwa hivyo naomba nimuhakikishie mama yangu kuwa kwa maelezo ziada ya matokeo ya utafiti huu uliofanywa niko tayari baada ya Bunge kuweza kuzungumza na wataalam wetu na kumtafutia zile takwimu na kuweza kumpatia.

**SPIKA:** Ahsante sana tunaendelea sasa na Wizara ya Maliasili na Utalii Waheshimiwa Wabunge swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel Mbunge wa Viti maalum uliza swali lako tafadhali Mheshimiwa.

Na. 319

**Kupanua Wigo wa Utalii Nchini**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutekeleza mojawapo ya malengo katika Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 kwa Taifa 2016/2017, 2020/2021 katika kupanua wigo wa Utalii nchi *(diversification)?*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii Mheshimiwa Costantine John Kanyasu, majibu kuhusu *diversification* ya utalii Tanzania.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kupanua wigo wa mazao ya utalii, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii inaendelea na jitihada za kuendeleza mazao mbalimbali ya utalii na kutangaza ikiwemo; kuanzisha mradi wa utalii wa utamaduni kwenye maeneo mbalimbali nchini; utalii wa fukwe kwa kuanzisha kurugenzi itakayosimamia uendelezaji

wa utalii huo nchini; utalii wamali kale kwa kuimarisha vitu mbalimbali vya mali kale, pamoja na kuimarisha utalii wa mikutano na maonesho *(Meetings Incentives Conference and Events-)* kwa kuboresha muundo wa Bodi ya Utali*(TTB)* utakaowezesha kuwa na kitengo kinachosimamia utalii huo, pamoja na kufanya tathmini ya ujenzi wa kumbi za mikutano katika eneo la Pwani la Bagamoyo na Dar es Salaam, na utalii wa meli kubwa za kitalii *(Cruiseship Tourism)* ambapo tunashirikiana na Mamlaka ya Bandari kuboresha miundombinu ya bandari ili kukidhi mahitaji ya utalii huo nchini pamoja na kuendeleza utalii wa Jiolojia katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Wizara imeanzisha shughuli mpya za utalii zikiwemo; safari za puto *(Hot air balloon)* katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha; utalii wa kutembea katika kamba*(canopy walkway)* katika Hifadhi ya Taifa Manyara; Utalii wa kuzoesha Sokwe *(habituated chimpamzees)* katika Hifadhi ya Taifa ya Rubondo pamoja na kuimarisha na kutangaza Hifadhi za Misitu ya Asili nchini ili kuvutia watalii kutembelea maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza kutekeleza Mradi wa *Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth (REGROW*) ambao kazi zake ni kuendeleza na kutangaza vivutio vya utalii, kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika Sekta ya Utalii pamoja na kuboresha miundombinu inayozunguka katika vivutio vya utalii vilivyopo Nyanda za Juu Kusini ikiwemo barabara na viwanja vya ndege. Ni imani yangu kuwa, utekelezaji wa mradi huu utasaidia ukuaji wa Sekta ya Utalii katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini sambamba na kupanua wigo wa mazao ya utalii katika utalii katika Ukanda wote wa Kusini kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel swali fupi kama lipo.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingi na pamoja na vivutio hivyo bado iko nyuma sana kwenye Utalii

kwa mfano Utalii wa fukwe kuliko nchi za wenzetu waliotangulia Kenya, Msumbiji na Zanzibar.

Sasa nataka kufahamu ni lini Serikali yetu itayazingatia na kuyapa umuhimu kipaumbele maeneo ya *Coco Beach* na kuona kwamba yanaendelezwa ili yaweze kufikia malengo hayo na kuleta watalii wengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ningependa kufahamu kwamba kwa mfano nchi zinazoongoza kwa kupokea watalii wengi kwa mfano Swaziland, USA Brazil na nchi nyingine za jirani zimewekeza katika aina mbalimbali za Utalii kwa mfano vitu vingine Mheshimiwa Waziri amevitaja kwa mfano, *Cable car* ikiwemo nchi jirani ya Rwanda *balloons*.

Je, ni lini sasa Tanzania itaona kipaumbele na kuwekeza katika maeneo hayo ili kuwepo basi kwa mfano kule Kilimanjaro *Cable car*s watalii waweze kuja wengi na kuliingizia pato nchi yetu ya Tanzania? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ushauri huo muhimu wa Mheshimiwa mdau wa Utalii Mheshimiwa Amina Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Amina Mollel kwa sababu katika maswali ambayo nimekuwa nikijibu hapa nimeshajibu maswali yake matatu yote yakihamasisha uhifadhi na Utalii nakupongeza sana Mheshimiwa Amina Mollel. Kama nilivyojibu ni kweli kwamba Tanzania tumekuwa na Utalii wetu wa asili ambao umezingatia sana safari kwa maana ya kutembelea mbuga za wanyama na maeneo mengi ambayo yamepatia nchi nyingine pesa nyingi za kigeni kama Utalii wa fukwe na aina nyingine za Utalii kwa kweli zimekuwa hazikuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ili kufikia katika malengo hayo Wizara imeliona hilo tuliunda kikosi kazi maalum cha kutafiti kwa nini Tanzania imekuwa nyuma katika Utalii wa fukwe na

tukagundua kwamba palikuwa na udhaifu katika usimamizi wa hizi fukwe, fukwe nyingi zimevamiwa, lakini fukwe nyingi zimepewa watu ambao wameshindwa kuziendeleza. Katika kulibaini hilo tumependekeza kuanzishwa Mamlaka maalum ambayo itakwenda kusimamia Utalii wa fukwe na kuhakikisha kwamba fukwe hizi zinaundiwa sheria maalum ili zisiweze kuvamiwa.

Mheshimiwa Spika, na katika eneo la *Coco beach* juhudu mbalimbali zimefanyika lakini kuna mgogoro unaoendelea kati ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika Manispaa ambayo iko katika eneo hilo na mwekezaji katika eneo hilo na Ofisi ya TAMISEMI imeingia na kuelekeza. Aidha, Manispaa wamlipe yule muwekezaji aondoke au amruhusu aendelee na kazi yake lakini kuna ucheleweshaji wa kufanya maamuzi ndio maana Wizara imeona tuanzishe Mamlaka maalum.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kweli kwamba watalii ambao tumekuwa tukiwapata katika Mlima Kilimanjaro karibu kufikia asilimia 100 ni miaka 18 na mpaka miaka 50, chini ya miaka 18 na juu ya miaka 50 hawawezi kuja kwa sababu hawawezi kupanda Mlima Kilimanjaro ili kuweza kuwapata hawa tumefikiria kushauri TANAPA kuangalia uwezekano wa kufikiria kufanya utafiti kuona kama tunaweza kuweka *cable car* na kama hili litafanikiwa litaweza kutuletea watalii wengi zaidi kama tulivyoona takwimu katika nchi alizozitaja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Kwasababu ya muda tuendelee swali linalofuata la maji linaulizwa na Mheshimiwa Antony Calist Komu.

Na.320

**Mradi wa Maji Kata ya Mbokomu**

**MHE. ANTONY C. KOMU** aliuliza:-

Serikali imetekelza mradi wa maji katika Kata ya Mbokomu lakini maji mengi yanavuja barabarani na kusababisha kukosekana kwa maji maeneo mengi ya mradi kama vile vijiji vya Korini Kusini, Kiwalaa na Korini Kaskazini.

Je, kwanini Serikali isihakiki ukamilifu wa mradi huo na kufanya marekebisho ikiwa ni pamoja na kubainisha waliohusika na kasoro zitakazobainika na kuwachukuliwa hatua stahiki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la maji, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Prof. maji Mbokomu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antony Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Korini ni moja ya miradi ya maji katika vijiji sita iliyotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kupitia Awamu ya I ya *program* ya maendeleo ya sekta ya maji na ulikamilika tarehe 31 Julai, 2014 ukiwa unahudumia wananchi wapatao 10467 wa Vijiji vya Korini Juu, Korini Kati na Korini Kusini.

Mheshimiwa Spika, wakati mradi huu unaanza kutekelezwa kulikuwa na mradi wa maji wa zamani ambao ulikuwa unahudumia Kata hii ambayo ni mradi wa maji wa Mbokomu Mashariki na mradi wa maji wa Mbokomu Magharibi. Katika kipindi cha Septemba mwaka 2018 kulikuwa na ukarabati wa barabara kwenye Kata ya Mbokomu ambao ulisababisha bomba la maji la mradi wa zamani kuharibiwa na mtambo wa kutengeneza barabara na kusababisha maji kuanza kuvuja barabarani. Hata hivyo, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa kushirikiana na Mkandarasi wa barabara waliweza kukarabati na kumaliza tatizo la uvujaji maji barabarani kwa gharama ya shilingi milioni 1,437,000,000.

**SPIKA:** Mheshimiwa Komu ameridhika, una swali la nyongeza haya twende.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kwa kweli ni majibu ambayo yamelenga kuuficha ukweli kwa sababu ukweli ni kwamba huo mradi baada ya kukabidhiwa ulianza matatizo hapo hapo na maji hayakutoka kabisa. Sasa baadaye Wizara ikaenda kule na ikabaini kwamba ule mradi ulijengwa chini ya kiwango na MUWASA wakakabidhiwa huo mradi wakaanza kuurekebisha na tunavyoongea sasa hivi, wameshapewa milioni 135 kwa ajili ya kuukarabati. Sasa nataka kujua hao waliofanya huo ujenzi *below standard* wamechukuliwa hatua gani? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, MUWASA wamepewa mzigo mkubwa sana kule Moshi Vijijini wamekabidhiwa Kata kama 12 kwa ajili ya kuzihudumia na zina matatizo ya miradi kama hiyo ambayo ni michakavu, ambayo imejengwa chini ya kiwango n.k lakini MUWASA wanadia kwenye Taasisi za Serikali kama Chuo cha Polisi-Moshi zaidi ya bilioni moja kwa hiyo wana tatizo kubwa sana la fedha. Nataka kufahamu kutoka Serikalini kuna *commitment* gani juu ya kulipwa hilo deni la MUWASA ili waweze kutuhudumia vilivyo?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Maji tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anthony Komu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni kuhusu chanzo hicho kama kilijengwa chini ya viwango; ni ukweli usiopingika kwamba kuna miradi mingi Nchi hii ya maji hasa iliyojengwa kutoka mwaka 2010 mpaka 2015 imejengwa chini ya viwango na ipo miradi kama 88 Tanzania nzima lakini nia ya Serikali ni

kuhakikisha Watanzania kwanza wapate maji. Kama mradi umejengwa chini ya kiwango au vipi nia yetu sisi ni kukarabati Watanzania wapate maji, hilo la kwanza na ndiyo muhimu. Kwa mtazamo huo ndiyo tukatoa milioni 135 kwa ajili ya kutarabati chanzo kile na hivi tunavyoongea kazi inaendelea vizuri isipokuwa kutokana na mvua zinazoendelea kidogo kazi imepungua lakini tunaamini wiki tatu zinazokuja chanzo kile kitakuwa kimekamilika na ndugu zetu wale Watanzania wanapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili inayofuata sasa ni kufanya uchunguzi wa kina kuelewa kwanini vyanzo hivi vilijengwa chini ya kiwango. Uchunguzi huo tunaweza kuoina kama ilikuwa kwa bahati mbaya ama kwa nini baada ya hapo taratibu za Kisheria zitachukua mkondo wake. Hatutaki kumuhukumu sasa hivi kitu muhimu mtu yoyote ni muhimu kwanza tufanye uvchunguzi tujiridhishe.

Mheshimiwa Spika, swali la pili nasema kwamba mamlaka ya maji ya Moshi imepewa majukumu mengi ni kweli na inafanyakazi nzuri na kuna madeni ambayo idara kama za Polisi wanadaiwa na naomba nimhakikishie tu kwamba jambo hilo tunalichukua na Taasisi nyingi za Serikali zinaendelea kulipa ili kuhakikisha kwamba mamlaka hizi za maji zote zinaweza kujiendeleza au kufanyakazi kwa kiwango kinachotakiwa.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum tafadhali.

Na. 321

**Bei ya Taulo za Kike**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018 Serikali iliondoa kodi kwenye taulo za kike *(pads)* jambo ambalo ni muhimu sana kwa maisha ya Wanawake na Wasichana mpaka sasa ni

mwaka mmoja tangu kodi hizo ziondolewe lakini bei ya taulo za kike haijashuka licha ya kuondolewa kwa kodi hizo Nchi nzima.

Je, ni lini Serikali itasimamia kwa ukamilifu suala hilo ili bei za taulo za kike zishuke na kusaidia afya za Wanawake hususani Wasichana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye taulo za kike ililenga kupunguza sehemu ya gharama za uzalishaji wa bidhaa hiyo na mojawapo ya athari chanya iliyotegemewa ni kushuka kwa bei ya bidhaa hiyo. Pamoja na Serikali kuchukua hatua ya kuondoa kodi imebainika kuwa hakuna mabadiliko ya bei ya bidhaa hiyo katika soko. Hii inatokana na ukweli kuwa, bei ya bidhaa katika soko inaamuliwa na nguvu ya soko pamoja na gharama nyingine za uzalishaji na uendeshaji kama vile gharama za malighafi, mishahara, uwekezaji, mifumo ya uzalishaji, teknolojia, ushindani katika soko, umeme, maji na majitaka, usambazaji, ubora wa bidhaa n.k. Hivyo basi kutokushuka kwa bei ya taulo za kike kunabainisha kwamba kodi inachangia sehemu ndogo sana katika kupanga bei ya bidhaa kama ambavyo Serikali imekuwa ikisisitiza na kutoa ufafanuzi mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mfumo wetu wa uchumi ni mfumo wa soko huria, bei ya bidhaa huamuliwa na nguvu ya soko yaani ugavi na mahitaji ya soko. Fursa pekee iliyopo ni kuhamasisha uwekezaji mkubwa kwa kutumia teknolojia yenye gharama nafuu katika kutengeneza taulo za kike,

kupunguza gharama nyingine sambamba na kuchochea ushindani wa bei katika soko na sio Serikali kuondoa kodi na kupanga bei ya bidhaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tulipoomba Serikali itoe kodi na ikakubali ilikuwa ni furaha kwa Wanawake wengi wa Nchi hii ya Tanzania. Jana ilikuwa ni siku ya hedhi salama kwa wanawake duniani. Tumeonana na wadau wanaoshughulikia *pads*, hakuna lalamiko walilolitoa juu ya uendeshaji zaidi ya kodi ambayo Serikali imetoa kwa wanao-*import* na kuwaacha watengenezaji waliko hapa nchini.

Swali langu; ni nini Serikali itafanya kuweza kusaidia wawekezaji wa ndani wanaotengeneza taulo hizi ikiwemo Jessy, HQ na wengineo ili kuweza kupunguza gharama ya taulo za kike?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Serikali itakubali kuweka ulazima wa wauzaji wanaouza taulo hizi kuweka gharama ya bei katika taulo hizo ili kufanya bei zote zifanane kama ilivyo kwa mazao kama ya *Coca cola* na *Pepsi* nchi nzima ina bei moja. Serikali itachukua wazo letu la kuona wkamba ni lazima iandikwe bei katika taulo hizo ili kukwepa kwa wale wanaoweza kuongeza hasa wasafirishaji na wauzaji na bei hii iweze kupungua.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango tafadhali, Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kusahihisha alichokisema kwamba wazalishaji wa ndani bado wanalipa kodi ya ongezeko la thamani kwenye bei ya bidhaa hizi, hapana. Tumeondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye bidhaa hii kwa bidhaa zinazotoka nje ya Nchi na zile zinazozalishwa ndani ya Nchi

ndiyo maana nikasisitiza kwenye jibu langu la msingi, majibu ambayo Serikali iliyatoa kwa swali namba 2938 ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Allex na kwa mwongozo wako naomba kulisoma swali lake liliuliza hivi:-

"Kutokana na umuhimu wa taulo za kike Nchini, Je, Serikali inaonaje ikiondoa kodi kwenye taulo hizi?"

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisema kwenye swali hili kwamba ukiondoa kodi haiwezi kuleta atahari moja kwa moja kwenye bei ya bidhaa husika kwa sababu bidhaa husika inategemea mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, tukienda Nchini Botswana, tukaenda Nchini Kenya ambako waliwahi kuondoa kodi kwenye bidhaa hizi hakuna athari yoyote iliyoonekana kwenye taulo hizi za kike. Kama tunataka kweli kumsaidia mtoto wa kike kama kweli tuna dhamira ya dhati ya kumsaidia mtoto wa kike, naomba tuisikilize Serikali inasema nini; Serikali siku zote imekuwa ikisisitiza kwamba, sisi kama Serikali tuna mpango na tayari tumeanza kufanya mchakato wa kuona ni jinsi gani ya kutoa bidhaa hii bure kwa watoto wa kike na siyo kuondoa kodi jambo ambalo halina athari yoyote zaidi ya kupunguza mapato ya Serikali. Jambo hili lilipelekwa kisiasa zaidi na mimi nawaomba kwenye mambo ya msingi yanayogusa Watanzania tusiingize siasa, hilo ndiyo suala ambalo nataka kuliweka hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili baada ya majibu yangu haya ya swali lake la kwanza, hakuna ulazima wowote wa kuandika bei kwenye bidhaa hizi kwa sababu tuko kwenye soko huria na Serikali yetu hatutaki kuingilia jambo hili, tunachohitaji ni kuja na mpango wa kibajeti wa ku-*deal* na jambo hili ili tuwasaidie watoto wetu wa kike.

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana. Nafikiri kwa majibu hayo turidhike tusonge mbele kidogo. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini uliza swali lako.

Na. 322

**Suala la Kupanga na Kupima Miji**

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO** aliuliza:-

Suala la kupima na kupanga Miji ni jukumu la Serikali:-

(a) Je, Kwanini Serikali isije na mkakati endelevu wa kupanga Miji yote ambayo imetangazwa kwenye gazeti la Serikali?

(b) Je, kwanini Serikali inatoa hoja nyepesi kwamba kazi ya kupima na kupanga Miji ni kazi ya halmashauri wakati inajua kwamba halmashauri nyingi nchini hazina nguvu ya kifedha kufanya kazi hiyo?

(c) Mji wa Kasulu ni mkongwe; je, ni lini Serikali itasaidiana na Halmashauri ya Mji wa Kasulu kupanga Mji huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, tafadhali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, heshima yako.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa mkakati wa kupanga Miji yote ambayo imetengazwa kwenye gazeti la Serikali kwa kuandaa mipango kabambe ya Majiji, Manispaa na Miji. Aidha, Serikali imeainisha upya maeneo yote ambayo yameiva kuendelezwa kimji kwa ajili ya kuyatangaza katika gazeti la Serikali kuwa maeneo ya

mipango yaani *planning areas* na hivi sasa maeneo ambayo tumeshayatangaza kwamba yameiva kimji mtayaona kila Mbunge ataona kwenye bajeti yangu vijiji na maeneo ambayo yametangazwa kuiva kimji yanayofika 455.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu namba 7(1) na (5) cha Sheria ya Mipango Miji namba nanne ya Mwaka 2007, jukumu la kupanga na kupima Miji ni la mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji na mamlaka ya Miji midogo. Hata hivyo Serikali imeendelea kuzisaidia halmashauri kupanga na kupima Miji yao kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Serikali kupitia Wizara imetoa jumla ya shilingi bilioni 6.4 kwa halmashauri 29 kwa ajili ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi. Aidha, inawezesha uandaaji wa mipango kabambe Miji 18 hivi sasa kupitia *program* ya kuzijengea uwezo mamlaka za Miji ambayo iko chini ya Ofis ya Rais, TAMISEMI.

(c) Mheshimiwa Spika, mwaka 2008 Serikali iliandaa mpango wa muda wa kati wa matumizi ya ardhi wa Mji wa Kasulu wa miaka 10 (2008 - 2018) ambao ulikuwa unatumika kuongoza na kusimamia uendelezaji wa mji huo wa Kasulu ambako ndiko Mheshimiwa Nsanzugwanko ni Mbunge wake. Mpango huo uliisha muda wake mwaka 2018 hivyo ni jukumu la Halmashauri ya Mji wa Kasulu kuanza mchakato wa kuandaa mpango mwingine kabambe wa kuongoza na kusimamia uendelezaji wa Mji wa Kasulu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel nilikuona swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza sijui kama wewe kwako kule Kongwa umesalimika. Miji mingi inageuka kuwa Miji holela, kuwa squarter kwa sababu haipimwi, haipangwi na halmashauri nyingi hazina fedha ya kufanyakazi hiyo, ndiyo

ulikuwa msingi wangu wa swali sasa nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hii *interim plan* ya Kasulu ya 2008 mpaka 2018 mwenyewe kwenye jibu lake Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba iliishia njiani haikukamilika na taarifa nilizonazo ni kwamba mpango huu haukukamilika, sasa swali la kwanza; Je, sasa Mheshimiwa Waziri madam wewe mwenyewe uko hapo Je, ni lini sasa mtakuja kukamilisha hiyo *Land use planning* ya Kasulu ili ikamilike? Maana iliisha tu 2018 haikukamilika 2018.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Miji 18 ambayo Waziri umeitaja Je, katika Miji hiyo ambayo itakuwa katika hiyo *program* ya kuendeleza na kupanga Miji Je, Mji wa Kasulu umo? Na kama Mji wa Kasulu haumo ni lini utakuwemo kwenye *program* hiyo? Suala la miji ni suala kubwa sana, kubwa sana vinginevyo Miji itakuwa *squarte*r yote katika nchi yetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa William Lukuvi majibu ya maswali hayo kutoka Kasulu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Nsanzugwanko aongee na Halmashauri ya Kasulu ili waonesha mahitaji ya master plan maana yake ukihitaji unaanza kwenye Kamati ya Mipango Miji na halmashauri yenyewe ya Wilaya inaonesha uhitaji wa kuwa na *master plan* ya Wilaya yake. Wakishaazimia hivyo, basi waweke bajeti kwenye halmashauri yao ya kufanya *master plan* ya Mji wao wa Kasulu na Miji yote.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara, wenye Miji yao maana mamlaka ya upangaji kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji ni wenye Wilaya (halmashauri) ambao ni Madiwani. Sisi kama Wizara hatuwezi ku-*dectate,* hata matumzi ya ardhi wanaosimamia zaidi ni halmashauri yenyewe kwahiyo wakishaazimia kwamba sasa wanafikiri ni

wakati muafaka watengeneze *master plan* basi waazimie vilevile na kuweka bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunajua liko tatizo la wataalam wa halmashauri, hatuna wataalam wa kutosha wa Mipango Miji lakini serikali imechukua jitihada ya kutambua weledi na utaalam uliko Nchi hii kwa hiyo tumeanzisha Makapuni chini ya Bodi ya Mipango Miji Makampuni ambayo ya Watanzania wenye weledi na utaalam mkubwa wa kufanya hizi *master plan* ambayo Halmashauri zinaweza zikawatumia.

Mheshimiwa Spika, lakini halmashauri ambayo haina uwezo huo, Wizara inaweza kusaidia wataalam wa Wizara tulionao wachache kuja kushirikiana na halmashauri ile katika kutoa usimamizi wa utayarishaji wa *master plan.* Kwa hiyo, nakushauri Mheshimiwa Nsanzugwanko utakapokuwa tayari Manispaa ya Kasulu basi tushirikishe na sisi lakini kama hujui mahali pakuanzia tuzungumze mimi na wewe naweza nikamtuma mtaalam mmoja kule Kasulu akawaeleze wale Madiwani namna *master plan* inavyoweza kuandaliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mipango hii ya hizi *master plan* 18 zinazoandaliwa naomba Mheshimiwa Nsanzugwanko nimuombe nitamtajia Wilaya zote ambazo ziko kwenye huu mpango wa *master plan* kwenye bajeti yangu ijumaa na Waheshimiwa Wabunge wote watasoma lakini ijumaa nitawapeni pia nafasi ya kujua pamoja na Miji hii ya Wilaya mnayoijua, lakini viko vijiji vyenu wengine hamvijui vimeshaiva sasa ili kuzuia hizo *squatter*, vijiji vingine Wilaya imeshaamua kuvitangaza vimeletwa kwangu na nimeshavitangaza na vyenyewe vipangwe kimji ili watu wanaoishi katika vijiji hivyo wapangwe, wapimiwe na wapewe hati kama za Mjini navyo nitawapa jedwali ili Waheshimiwa Wabunge wote mjue vijiji vyenu ambavyo vina hadhi ya kimji ambavyo tumeshavitangaza Tanzania nitawapeni ijumaa nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana nimekuona Kiongozi wa Upinzani Bungeni uliza swali lako tafadhali.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri na kwa sababu swali langu litafanana kidogo na swali la Kasulu linahusu Mji mdogo sio Mji mdogo, Mji wa Hai ambao zamani ukiitwa Bomang'ombe Makao Makuu ya Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa Spika, mji huu ni Mji ambao unakuwa na kwa kasi kuliko pengine Miji yote katika Mkoa wa Kilimanjaro ukiwa ni mkoa ni Mji ambao unaunganisha Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na Manyara kwa upande wa Simanjiro. Mji huu sasa hivi unakaribiwa kuwa na takribani na wakazi zaidi ya 100,000 na unahudumia eneo lenye viunga vya karibu watu 200,000 kuanzia Mkoa wa Manyara, Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Kilimanjaro na ni *get way to the* Kilimanjaro *international Airport* ambapo ni karibu sana na uwanja wa ndege wa Kimataifa na *of course* ndio njia na lango la kuingilia katika Mlima Kilimanjaro ambao ni chanzo kikubwa sana cha mapato kwa Taifa letu.

Mheshimiwa spika, sasa Mji huu ukiacha barabara Kuu ya Lami inayotoka Arusha kwenda Moshi na inayotoka kwenye ene la Hai kwenda Sanyajuu katika Jimbo la Siha Mji huu hauna barabara hata moja ya lami. Sasa katika kupanga Miji ni pamoja na ujenzi wa barabara za lami ili ujenzi na upangaji miti uwe kamili ni lazima uendane vilevile na mitaro ya maji pamoja na ujenzi wa barabara za lami.

Mheshimiwa Spika, halmashauri zetu sasa hivi hazina uwezo wowote wa kuweza kufanya miradi mikubwa ya kiwango hiki. Na natambua hapo nyuma kidogo kulikuwa kuna *program* kuna *project* ya *sustainable cities* ambalo nafikiri limekuwa *funded* na *World Bank* ambayo ilichagua baadhi ya Miji ambayo kwa umuhimu wake wa kiuchumi iliweza kuwekewa miundombinu ya barabara za lami. Na hata Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za 2015 Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli alitoa ahadi ya kujenga barabara kilomita 5 za lami ambazo kwa bahati mbaya bado tunazisubiri kwa hamu sana.

Mheshimiwa spika, sasa Mheshimiwa Waziri katika utaratibu huo wa kupanga Miji nini kifanyike ili Miji muhimu kama hii ambayo inahudumia watu wengi na ni sura ya Taifa inaweza kufanyika ili ipate lami? Nini kifanyike katika hiyo mipango Miji kuikamilisha kwa kujenga miundombinu ikiwemo barabara za lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Mheshimiwa William Lukuvi tafadhali, kuhusu Mji wa Hai.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa spika, *master plan* haijengi miundombinu *master plan* ni dira ya kuonesha mahitaji ya mpango au mahitaji ya huduma ndani ya Wilaya. *Master plan* wenye Wilaya yenu mtapanga kutaka kujua barabara zipite wapi, maeneo ya mazishi ni wapi, maeneo ya makazi ni wapi, maeneo ya biashara na huduma mbalimbali. Kwa sababu hata mkiwa na fedha ya barabara kama hamna maeneo mliyopanga kujenga barabara hazitafanya kazi na ndio maana mnakuwa na hela halafu mnaamua kufanya vyovyote au mnavunja nyumba za watu hovyo. Kwa hiyo, la kwanza nakushauri Mheshimiwa Mbowe pangeni *master plan* ili muone uhitaji wa leo mnahitaji kuwa na barabara kiasi gani, za saizi gani, za lami na kila kitu na mahitaji mengine.

Mheshimiwa Spika, *then* mkishapanga *master plan* kuainisha maeneo hayo mtakuja kuyapima lakini baadaye sasa ndio mtawaomba sasa huduma mbalimbali na kuziwekea bajeti ili ziwemo kulingana na *master plan* iliyopo.

Kwa hiyo, nimelichukua ombi lako hilo, lakini nashauri kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa Kasulu naomba halmashauri yako mkae kama *council* katika miradi kingi mnayobuni pale Hai basi mbuni utengenezaji wa *master plan* kama hamna mtu wa kuwaelekeza pale Moshi kuna Kanda na nimepeleka pale mtalaam mbobezi Afisa Mipango Miji Mkurugenzi Msaidizi wa Kanda mnaweza mkamualika yule bure akaja kuwapa maelekezo na utalaam wa awali wa namna ya kutayarisha *master plan* ya Hai ili

iweze kuwaoneshea huduma zenu zipangwe namna gani katika Wilaya ya Hai.

Mheshimiwa spika, lakini hilo jingine ulilosema nakushauri kwa sababu Wizara ya TAMISEMI iko hapa Dodoma pengine ukipata fursa ungepita pale kwenye Ofisi za TAMISEMI ili angalau hayo majibu mengine ya lini zitajengwa hizo barabara uweze kujibiwa pale ofisini.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa sababu ya muda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi mheshimiwa Haji Khatib Kai mkiangalia saa yetu mtaona bado tuna maswali.

Na. 323

**Sifa za Askari Kuwa OCD**

**MHE. HAJI KHATIB KAI** aliuliza:-

Je, ni sifa gani anastahili kuwa nazo Askari Polisi ili aweze kuteuliwa kuwa *OCD?*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi *Engineer* Hamad Masauni tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Haji Kai Mbunge wa Micheweni kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa muundo wa maendeleo ya Utumishi wa Maaifa wakaguzi na Askari wa Jeshi la Polisi ili Afisa aweze kuwa *OCD* ni lazima awe na sifa zifatazo;

- Awe na cheo cha Mrakibu Muandamizi wa Polisi.

- Awe na uwezo wa kuongoza ikiwa ni pamoja na kusimamia, kuratibu kazi za Maafisa, Wakaguzi na Askari walio chini yake kusimamia nidhamu katika himaya yake, kubuni na kuandaa mikakati ya ulinzi na usalama katika himaya yake.

- Awe na uwezo wa kufanya uamuzi, kutatua changamoto mbalimbali za kazi kuanzisha na kudumisha mahusiano mazuri na wananchi, pamoja na watendaji wengine wa Serikali na Taasisi zingine zilizo katika himaya yake na,

- Endapo kuna upungufu wa Maafisa wenye cheo cha Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Afisa mwenye cheo cha Mrakibu wa Polisi anaweza kupewa madaraka ya kuwa OCD ili mradi awe na uzoefu na uwezo wa kuongoza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Micheweni swali la nyongeza.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo masuala mawili ya nyongeza. Mkoa wa Kaskazini Pemba una Wilaya mbili za Kipolisi kwa maana ya Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni. Ma-OCD hawa walikaimu au wamekaimu zaidi ya miaka mitatu katika nafasi za OCD mwaka 2016 hadi mwaka 2019 na kwa OCD ya Wilaya ya Wete alikaimu nafasi hiyo hadi pale muda wake wa kustaafu ulipomfikia bila kupata maslahi yoyote ya cheo cha OCD. Mheshimiwa Naibu Waziri je, ni utaratibu gani wa Serikali kupitia Wizara yako inaweza ikafidia ma-OCD kama hawao kaimu bila kupata maslahi ya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa kukaimu nafasi ya *OCD* kuna changamoto za kiutendaji na si tu changamoto za kiutendaji hata changamotoza kimazingira. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa kiasi kidogo sana cha mafuta kwa mwezi shilingi 1,000,000 jambo ambalo linamfanya OCD anayekaimu kutumia fedha zake za mfukoni kama Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani na

unajua umuhimu wa mafuta kwa Polisi, umesimamiaje Serikali kuhakikisha kwamba inaongeza mafuta ili kuondoa tatizo la mafuta kwa Jeshi la Polisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana majibu ya maswali hayo kwa kifupi sana Mheshimiwa Eng. Hamad Masauni Naibu Waziri Mambo ya Ndani ya Nchi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimefarijika kuona Mheshimiwa Kai leo amekuwa mtetezi wa Askari wetu na hii inadhihirisha kwamba kumbe Askari wetu wanafanya kazi vizuri sana kule Pemba, wanashirikiana vizuri sana na Mheshimiwa Kai pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao kwa Pemba tunajua asilimia kubwa Wabunge wanatoka Chama gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nataka nimjibu kama ifuatavyo. Kwanza hakuna fidia katika kukaimu niseme tu labda nishee pamoja na yeye masikitiko yake kuhusu kukaimu kwa muda mrefu bila kupandishwa cheo. Maana kama amekaimu miaka mitatu maana anaiweza hiyo nafasi lakini nimthibitishie kwamba ili mtu aweze kupanda cheo kuna taratibu ambazo nimezieleza katika jibu la msingi. Na moja katika mambo ambayo yanapelekea vilevile kupandishwa cheo kwa Askari ni kutokana na kuwepo kwa hizo nafasi, sasa inawezekana kwa bahati mbaya katika kipindi hiki ambacho wanakaimu hakukuwepo na fursa za kuweza kupandishwa cheo kwa Askari wahusika. Na kama unavyojua kwamba mahitaji ya Askari ambao wanahitaji kupandishwa cheo ni wengi na wengi vilevile wana sifa, kwa hiyo nafasi ni chache lakini wenye sifa ni wengi na ndio maana tunapandisha kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na bajeti ya mafuta nimuhakikishie kwamba tutajitahidi kadri ya miaka inavyokwenda kulingana na hali ya ukuaji wa uchumi wetu kuongeza bajeti katika Jeshi la Polisi ikiwemo bajeti ya mafuta. Tunatambua kwamba bajeti ya mafuta katika maeneo mengi bado haikidhi lakini tutaendelea kuizidisha katika

maeneo yote ikiwemo katika Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Wete ili hatimaye tuweze kuhakikisha kwamba Askari wetu wanafanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali mawili yaliyobaki tutayapangia wakati mwingine swali la Mheshimiwa Bilakwate na Mheshimiwa Zainabu Katimba kwa sababu ya muda ili tuweze kwenda na ratiba yetu kama inavyopasa. Wageni waliopo katika Jukwaa la Spika ni pamoja na wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Atashasta Nditiye ambao ni ndugu Rosemary Nditiye Mke wa Mheshimiwa na ndugu Rehema Mwakyusa, ahsanteni sana Rosemary ni yupi? Ahsante sana jamani Mama Nditiye huyo karibu sana Shemeji yetu. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambao ni wageni 34 na miongoni mwao watatu ni Wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Madison kule Marekani wakiwemo na wanafunzi 31 kutoka jimbo la Virginia Nchini Marekani wakiongozwa na Profesa Emmy Auma, ahsante sana wageni wetu toka Marekani karibuni sana Tanzania, tunafurahi sana kwa kututembelea karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni Wachungaji kutoka Mkalama Mkoani Singida wakiongozwa na Mchungaji Abel Shija, karibuni sana Wachungaji tunashukuru sana kuja kwenu mtuombee. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni walimu wa shule za sekondari kutoka Nyamagana Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na mwalimu Antidius Mathias, wale kutoka Mwanza karibuni sana wako pale karibuni sana toka Nyamagana. Wageni watatu wa Mheshimiwa Flatei Massay ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbulu, wale wageni watatu toka Mbulu karibuni sana wapiga kura. Wageni wengine wa Mheshimiwa Fratei ni wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha St. John Jijini Dodoma St. John ahaa karibuni sana wageni wetu kutoka St. John chuo maarufu sana hapa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Makilagi ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam Jackson Juma na Bahati Ndimbo karibuni sana wale kule karibuni sana. Wageni wawili wa Mheshimiwa Hasna Mwilima ambao ni watoto wake kutoka Dar es Salaam ndugu Mireile Fenza na ndugu Saada Mwilima karibuni sana wale pale ahsante sana. *(Makofi)*

Kwa mafunzo wanafunzi 100 na walimu 10 kutoka shule ya sekondari ya Itega ya hapa Jijini Dodoma wakiongozwa na mwalimu Grace Mabula, wanafunzi kutoka Itega Dodoma ohoo! Karibuni sana watoto wetu mnapendeza sana. *(Makofi)*

Matangazo mengine Waheshimiwa Wabunge ni naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kufuatia kadi za mwaliko na hata kama hujaipata kadi ya mwaliko tunawataarifuni Waheshimiwa Wabunge kwamba leo jioni kutakuwa na Iftar kwa Wabunge wote ambayo imeandaliwa na uongozi wa Benki ya *CRDB*, kwenye Hoteli ya Morena mara tu baada ya kuhairisha shughuli za Bunge. Wabunge wote kabisa tunaalikwa kufika pale Morena tukiahirisha shughuli zetu tu jioni kuna Futari ambayo imeandaliwa kwa ajili yetu, tunaombwa sana sote tuweze kuhudhuria Futari hiyo na nilikuwa nimewaambia *CRDB* pamoja na mambo yote wakiweza kuandaa ile Futar ya kwenye bahasha ile na wamesema wanajitahidi kwa hiyo tunaombwa tufike ili tubebe wenyewe Futar hiyo Waheshimiwa Wabunge karibuni sana. *(Makofi/ Kicheko)*

Katibu wa Bunge anaomba niwatangazieni Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 6 Februali, 2016 Mheshimiwa Angeline Sylvester Lubala Mabula alitunikuwa shahada ya heshima ya Uzamivu katika masuala ya Utawala na Biashara toka Chuo cha *Africa Graduate University* cha Nchini Uingereza, kufuatiwa hatua hiyo Mheshimiwa Mabula sasa anatambuliwa rasmi kama Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula ahsante sana. Hii ni shahada ya heshima *Honoris Causa*. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Shally Josepha Raymond Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moo anawaomba Wakatoliki mkutane katika uwanja wenu ule wa kawaida kule ghorofa ya pili Pius Msekwa kwa ibada mchana wa leo. *(Makofi)*

Naomba Tume ya Huduma za Bunge tukiahirisha shughuli saa saba tukutane hapa katika Ukumbi wa Spika mara moja Tume tukutane mara tukimaliza shughuli hizi saa saba mchana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kuwasiliana na Wizara ya Mheshimiwa Waziri Mwakyembe kuhusiana na ushiriki wetu katika Mechi ambapo Tanzania *Stars* itacheza kule Misri katika mashindano ya AFCON. Ninaomba tuendelee kujiandaa maandalizi yanakwenda kwa kasi kubwa na itakuwa ni faraja sana kwangu na kwa Watanzania kama Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana wote tukaweza kushiriki na kuishangilia timu yetu. Kwa hiyo tunaendelea kuwasiliana na Wizara lakini mpaka sasa *indication* inaonesha kwamba ukiandaa kama dola 1500 unakuwa uko salama kabisa ku-*cover* usafiri, malazi na kila kitu. *(Makofi)*

Kwa hiyo tuendelee na maandalizi lakini taaifa za mwisho tutazipata kadri siku zinavyoenda kwa kweli ningependa kuwashawishi sana Waheshimiwa Wabunge tujitahidi sana tutumie nafasi hii pia ni sehemu ya kutembea na kujua maeneo na mkiwa wengi tunaweza tukapanga hata *program* nyingine tukiwa kule wakati wa mchana tukawapeleka kwenye *pyramids* na maeneo mengine muhimu.

Mnajua nchi ya Misri ni muhimu kihistoria katika dini zote nakadhalika, kwa hiyo ni fursa ambayo ningeomba kila mmoja wetu ajitafute ajiweke sawa yaani ningeshauri sana usikose fursa hiyo ya kuungana na Watanzania wenzetu katika kwenda Misri. Naamini kabisa na Mheshimiwa Waziri Mwakyembe mwenyewe naye atahudhuria huko, *Chief Whip* Jenista Mhagama lazima uhudhurie huko, *Chief Whip* wa Upinzani ukikosekana hatutakuelewa, Kiongozi wa Upinzani Bungeni usipokuwa nasi hatutaelewa, kwa hiyo, tunaomba

katika hili la *AFCON* tujiunge sote kabisa tukaishaingilie timu yetu kwa kadiri tunavyoweza kabisa.

Utawala wanaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kutokana na umuhimu wa zoezi la usajili kwa ajili ya kupatiwa hati mpya za kusafiria za kielektroniki *(E-Passport)* Maafisa kutoka Idara ya Uhamiaji wameongeza muda wa kujisajili kwa ajili ya upatikanaji wa hati hizo. Zoezi hilo linaendelea na linatarajia kuhitimishwa siku ya Ijumaa, tarehe 31 mwezi wa 5.

Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote ambao bado hamjajiandikisha kwa ajili ya kubadilisha hati hizo za zamani mnaombwa kutumia fursa hii, ili muweze kubadilisha hati zenu. Baada ya zoezi hili kuhitimishwa hapa Bungeni Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye atakuwa bado hajajiandikisha itamlazimu kufuata huduma hiyo katika Idara za Uhamiaji kule aliko; aidha, Waheshimiwa Wabunge waliokwishakujaza fomu za maombi mnaombwa kukamilisha taratibu za malipo ya kupatiwa hati hizo.

Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tufanye hivyo. Na pale unapoweza ni vizuri ukapata hati mbili, ukapata hati ya kibalozi na ukapata hati ya kawaida. Ya kawaida ikusaidie katika safari zako ambazo sio rasmi na hii nyingine itakusaidia katika safari ambazo ni rasmi.

Yuko Mbunge mmoja alienda Marekani alipata shida sana kule. Anafika pale anaulizwa enhee! Umekuja kufanya nini huku? Aah, nimekuja kwa shughuli zangu binafsi. Mbona unatumia hati ya kibalozi? Alikaa pale saa sita; mambo yako binafsi unatumia *Dilplomatic Passport?* Ikawa imeleta shida kidogo kwa hiyo, wakati mwingine ni vizuri kutofautisha kidogo.

Katibu!

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Nishati

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa kwa sababu ya muda na mambo yalivyo naomba tuendelee. Tutatafuta muda hapo mbele tutachukua miongozo yote tu, kwa leo naomba tuendelee na wachangiaji maana yake ninao wengi kweli kweli na ningependa kila mmoja katika hawa apate nafasi ya kuchangia.

Tuanze na Mheshimiwa Venance Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Almasi Maige na atafuata Mheshimiwa Nape Nnauye. Mheshimiwa Venance Mwamoto, dakika tano-tano, asiyekuwepo na lake halipo; hayupo anaondoka Mheshimiwa Almasi Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii ya Wizara ya Nishati iliyoko mezani kwetu sasa hivi. Kwanza natoa shukrani sana kwa Wizara hii na watendaji wa Wizara, Mheshimiwa Waziri Kalemani, Mheshimiwa Mgalu na Mheshimiwa Mwinyimvua kwa kazi nzuri ambayo mnaifanya katika kazi kubwa ya kueneza umeme na kuondoa blanketi la giza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imeondoa mgawo ambao ulikuwa tatizo kubwa sana miaka iliyopita na kwa kweli, wanastahili sifa kubwa, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuthubutu kujenga Kituo Kikubwa cha Umeme pale Mto Rufiji. Suala hili litatatua matatizo yote

na itakuwa mfano katika nchi za Afrika Mashariki, nchi yetu itakuwa na umeme wa kutosha kwa hiyo, kwa uwekezaji wa viwanda na kukidhi haja ya kuwa na siasa ya viwanda mwaka 2025 na kuwa siasa ya nchi ya kati kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameongelea Wabunge wengu kuhusu suala hili la kinu cha umeme huko Rufiji, leo nijikite katika kituo katika Mradi wa *REA.* mradi wa *REA* ambao Wizara hii inausimamia ni kichocheo kikubwa sana cha maendeleo vijijini, laki I mradi huu hauendi vizuri, mradi huu sasa umekuwa ni tatizo la Waziri, Waziri amekuja kwangu ameubeba mradi huu kama wa kwake mara tatu, lakini akiondoka Mheshimiwa Waziri huyu namshukuru sana, wakandarasi wanalala. Hatuoni maendeleo ya mradi huu vijijini kwetu, sehemu kubwa ya vijiji vyangu vyote havina umeme na sehemu ndogo iliyotiwa umeme haujawashwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nguvu za Mheshimiwa Waziri kuja kwetu, lakini wakandarasi wanamuangusha na ningependa atakapokuja Mheshimiwa Waziri kufanya majumuisho aje anieleze katika Jimbo la Tabora Kaskazini au Wilaya ya Uyui vijiji gani vina umeme au vina mpango wa kuviwekea umeme kwa sabbu, imekuwa kero tunausikia umeme wa *REA* kwa wenzetu sisi kwetu hatuuoni umeme huu, hata nguzo haziji. Nimeshaongea na mkandarasi ananiambia tatizo kubwa ni nguzo, lakini nguzo zimeshapatikana, tatizo ni nini katika kuendeleza mradi wa umeme katika eneo langu?

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalalamika sana, wanafurahi wanapomuona Mheshimiwa Dkt. Kalemani amekuja, tunamshangilia, karibu tumpe na mke na mbuzi tumpe, akiondoka umeme unapotea. Tunaomba Mheshimiwa Dkt. Kalemani utakapokuja kuongelea mwisho wa majumuisho yako utuambie Umeme wa *REA* katika Wilaya ya Uyui na hasa Jimbo la Tabora Kaskazini mpango ukoje? Mbona hatuoni unaendelea?

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali yetu ina mipango mizuri na kama ilivyoweka kipaumbele katika kitabu

hiki cha bajeti. Mipango yote ikikamilika nchi hii itakuwa mfano mkubwa wa kuwa na kiasi kikubwa cha umeme nchini, lakini pia tutapata faida kubwa kuuza umeme huu nchi za nje, jirani zetu, lakini vilevile sehemu kubwa ya umeme huu utachochea maendeleo ya viwanda ambapo Serikali itapata mapato, lakini utaleta maendeleo kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mambo mengi zaidi ya malalamiko hayo ya *REA,* lakini kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa mpango mzuri wa kuleta umeme katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Almasi Maige, nakushukuru sana. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu mnajitahidi sana hongereni sana. Ila mkiondoka hawa wakandarasi wenu nao wanaingia mitini, hao ndio mpambanenao hao wakandarasi wa mikoa hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nape Nnauye nilishakutaja, atafuata Mheshimiwa Augustino Masele, jiandae na Mheshimiwa David Silinde atafuatia baada ya mheshimkiwa Masele.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie kwenye mapendekezo ya bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya, wanafanya kazi nzuri sana na wasaidizi wao. Kwa kweli katika Mawaziri wasikivu na wanyenyekevu nadhani Mheshimiwa Kalemani na msaidizi wake wanafanya kazi nzuri sana. Na hii haimaanishi kwamba, hakuna changamoto, lakini usikivu wao na unyenyekevu wao unapunguza sana machungu ambayo yangekuwepo kwenye Wizara hii kwa hiyo, kwa kweli nawapongeza na nadhani waendelee hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nataka niipongeze sana Serikali kwa kuhuisha, kwa kufufua na kuendeleza mazungumzo juu ya mradi wa uwekezaji pale Lindi wa *LNG.* Tulipiga kelele hapa, nadhani bajeti mbili zilizopita, lakini

Serikali imesikiliza na imehuisha na Mheshimiwa Waziri juzi umekuja Lindi kwa mazungumzo yale tunayo matumaini sasa kwamba, mradi huu ambao kwa kweli kwanza ni mkubwa kuliko miradi yote mikubwa katika nchi yetu na hata ukijumlisha ukichukua reli, ukachukua *ATC,* ukachukua *Stiegler's,* ukijumlisha kwa pamoja Mradi wa *LNG* bado una thamani kubwa kuliko miradi yote kwa pamoja. Kwa hiyo, naamini uamuzi huu ni uamuzi wa busara, uamuzi mzuri, nimesimama kuipongeza kwa dhati Serikali yangu kwa kazi nzuri mnayofanya kwenye mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu pamoja na kwamba, ni mkubwa lakini mradi huu ni ushahidi wa ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza miradi mikubwa ya namna hii kwa sababu, hela za Serikali zitakazoingizwa ni kidogo sana. Sehemu kubwa ya fedha hizi karibu dola bilioni 30 ni fedha ambazo zinaletwa na sekta binafsi kwa hiyo, ni mfano mzuri wa ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miradi mikubwa. Ninaipongeza Serikali kwa uamuzi huu, sasa ninayo mapendekezo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza tukamilishe mazungumzo yamechukua muda mrefu na wenzetu wanaotuzunguka wata-*take advantage* ya kuchelewa kwetu na halitakuwa jambo zuri. La pili, ushiriki wa wazawa, *local contents* kwenye huu mradi, Serikali haiwezi kukwepa wajibu wake, tukiwaachia wazawa peke yake ushiriki wao utakuwa mdogo; wito wangu kwa Serikali vizuri Serikali ikajihusisha kwenye maeneo mawili, moja kuzionesha fursa na kuwapa elimu wazawa ili washiriki vizuri, lakini ya pili kuwawezesha hawa wazawa washiriki.

Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu huwaachi wananchi wako wakaenda wenyewe. Ukiwaacha wataenda kushiriki kuuza nyanya, lakini kama tunataka washiriki kwa ukweli kwenye Wizara yako, lakini Wizara ya Uwekezaji, vizuri tukaanzisha *room* ambayo itawachukua wazawa na kuwawezesha kiuchumi ili washiriki, ili *local content* yetu iwe nzuri. Kwa hiyo, pamoja na pongezi, lakini malizeni mazungumzo ya huu mradi, lakini pia Serikali ijipange

kuwawezesha wazawa kushiriki kwenye huu uchumi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nataka nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya kwenye *REA* yeye na Naibu wake. Wanafanya kazi nzuri sana, wanakimbizana sana, najua wakandarasi kwenye maeneo mengi wanawaangusha kwa sababu kasi yao ndogo, lakini kwa kweli mnyonge mnyongeni, Waziri Kalemani na Naibu wake wanafanya kazi nzuri, wanakimbizana, wanajituma. Ninaamini kama kuna Wizara Mheshimiwa Rais ameweka Mawaziri wazuri, hii Wizara amefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninayo mapendekezo mawili; la kwanza nadhani ni vizuri tukaligawa Shirika letu la *TANESCO,* mapendekezo haya yamekuwa yakizungumzwa. Hebu fikirieni kwa miaka mingi inazungumzwa tugawe uzalishaji, usambazaji na uuzaji yawe ni maeneo tofauti yanayojitegemea, itasaidia sana kuboresha utendaji wa Shirika letu la *TANESCO.* Na kwenye upande sasa wa uzalishaji kwa sababu tunakwenda kwenye kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo tofauti, vizuri tukavutia wawekezaji binafsi kutoka kwenye *private sector* watusaidie kwenye kazi ya kuzalisha umeme halafu kazi ya kusambaza iendelee. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja na mapendekezo ya Wizara hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana, asante. Mheshimiwa Mbunge wa Mbogwe, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, dakika tano.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili pia na niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Kama wenzangu walivyokwishakutangulia kusema Wizara hii inao

watendaji wazuri sana. Na kwa maana hiyo, nipende tu kwa kweli, kuwapongeza; nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Medard Kalemani na dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi nzuri sana ambayo wanaendelea kuitendea nchi yetu. Ninaamini kabisa kwamba, Tanzania ya viwanda inakuja na niseme tu kwamba, kwa kweli, ninaunga mkono shughuli mbalimbali ambazo zinafanywa na Wizara hii ukiwemo mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge* ambao unatekelezwa na Taifa letu ambao tunatarajia kupata megawati 2100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua kwamba, lengo letu kama Serikali ni kupata megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025. Nina imani kubwa kwamba, ndani ya kipindi hicho kama kweli watendaji hawa wataendelea na morali waliyonayo ninaamini kabisa kwamba, Tanzania itafikia uzalishaji wa megawati 10,000 kipindi hicho kitakapokuwa kimefikia na Tanzania ya viwanda itawezekana kwa sababu, hakuna viwanda bila kuwa na nguvu za umeme zinazoweza kuwa za uhakika tukaweza kufanikiwa kwenye sekta hiyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, kwa kweli Wizara hii imekuwa ni Wizara ya mfano.

Mheshimiwa Spika, na kwa wale ambao wanapinga kuendelea kuzalisha umeme katika *Stiegler's Gorge* na wanaosema kwamba, wao wanataka *return* kwenye *REA* ambayo imewekezwa katika Tanzania hii, basi mimi niwaombe kwamba, kwa kweli, wabadilike mawazo kwa sababu, Watanzania ambao wamepata huduma hii ya umeme kupitia Mradi wa *REA* na *TANESCO* leo hii ukisema kwamba, uuzime au uondoe hiyo huduma, kelele ambazo utazisikia hapo hutakaa usahau. Kwa hiyo, nimeona kwa mfano kabisa katika Wilaya yangu ya Mbogwe baada ya huduma hii ya umeme kuwekwa kwa Wananchi, Wananchi kwa kweli wamefurahia huduma hizi na kwamba, maisha yamekuwa marahisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe tu kwamba, utekelezaji wa Mradi huu wa *REA* Awamu ya III uendelezwe kwa kasi zaidi na kwamba, wakandarasi kama wewe

Mheshimiwa Kalemani umekuwa ukifika mara kwa mara katika Wilaya yangu ya Mbogwe na umehamasisha utekelezaji wa Mradi huu wa *REA* Awamu ya III, lakini naona kasi bado kidogo, lakini naomba tu kwa kweli, Mungu akujalie na msaidizi wako Mheshimiwa Mgalu muendelee kufanya kazi hii kwa ustahimilivu ambao mnauonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine nikushukuru Mheshimiwa Waziri baada ya kuwa umekuja umeweka umeme katika eneo la Nyakafuru, wachimbaji wangu wadogowadogo katika eneo hilo la dhahabu ninaamini kwamba, kwa kweli shughuli za uzalishaji wa dhahabu katika eneo la Nyakafuru litakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ninachotaka kuomba tu ni kwamba, *REA* imekuwa inatoa huduma katika maeneo machache. Naomba ule mradi wa *densification* na wenyewe ufanyiwe wepesi, ili kusudi uanze utekelezaji mara moja. Na vile vijiji ambavyo bado havijafikiwa katika utekelezaji wa *REA* naomba Serikali ifanye haraka ili ikiwezekana mwaka 2020/2021 vijiji vyote viweze kuwa vimepata hii huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu, tumeshuhudia kwamba maeneo mbalimbali yanachangamka sana yanapopata huduma hii ya umeme. Kwa hiyo, niombe tu kwamba, kwa kweli, kwa wale ambao watakuwa hawahitaji umeme kwao basi, huko Mbogwe sisi tunauhitaji kwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo mimi naomba tu niendelee kuwaombea kwa Mungu Wizara hii waendelee kufanya kazi zao kwa ukamilifu, ili kusudi Tanzania ya viwanda iweze kufikiwa. Baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri asilimia 100 kwa 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Silinde dakika 10, utafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Asia.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nichangie makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/2020. Jana wakati wajumbe wanachangia ilinifanya nikumbuke miaka mitano iliyopita tukiwa ndani ya Bunge lako Tukufu, wajumbe wengi waliokuwa wanachangia baadhi walikuwepo kwenye Bunge lililopita ambalo ilikuwa ikifika kwenye hotuba ya Wizara ya Nishati, wakati huo ilikuwa inaunganika na madini, jambo moja lilikuwa ndio wimbo wa Taifa, lilikuwa gesi; kila mtu alikuwa gesi, gesi.

Mheshimiwa Spika, wakati huo Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Muhongo, Profesa, alikuwa akisimama hapo mbele anakwambia sasa Tanzania inaenda kuwa kama Dubai. Sisi wajumbe wa Kamati ya Nishati wakati huo tulikuwa tunasafirishwa kwenda kujifunza gesi. Kila mwisho wa mwezi Waziri anasimama anasema leo gesi imegunduliwa trilioni kadhaa, sasa Tanzania ina gesi zaidi ya trilioni kadhaa, mbili imegunduliwa, tatu, mpaka ikafika hamsini na saba. Tangu ameondoka Mheshimiwa Prof. Muhongo hatujasikia tena taarifa ya ugunduzi wa gesi nchini ambazo zilikuwa zinatangazwa mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili, ile gesi ambayo tulikuwa tunaambiwa Tanzania inabadilika kuwa kama Dubai leo hakuna hata mmoja anayeizungumzia tena, tumesahau leo. Sasa leo, jana wajumbe wamechangia nitarudia tena, wakati ule wa gesi imepamba moto Serikali ikaleta mpango kwamba, sasa tunatengeneza bomba refu ambalo lili-*cost* karibu *US Dollar 1.2 billion* mpaka Ubungo. Gesi hii italeta umeme wa kutosha, leo bomba lilelile tuliloliimbia wimbo ndani ya Bunge, yaani kila mmoja alikuwa anaimba wimbo, bomba lile linatumika kwa asilimia 6. *Six percent* mtu ana-*justify* kwamba, hiyo ndio iko sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa haya ndio mambo ambayo leo mimi nataka tuyajadili na Serikali itupe majibu. Serikali hapa imeomba kwenye hotuba yake, inaomba trilioni 1.86 ile ya bajeti ya ndani ambayo itakwenda kwenye maendeleo, sawa na 95.1%. Kati ya hizo trilioni 1.44

zinaombwa kwa ajili ya *Stiegler's Gorge,* megawati 2,115 ukisoma chini wanakwambia wanaomba bilioni 60 kwa ajili ya *extension* ya megawati 185. Sasa nataka *to think beyond the box* na niko tayari kukosolewa; *Kinyerezi Extension* megawati 185 bilioni 60, hesabu ya kawaida *in a layman language* ukiwa na bilioni 600 ukafanya *extension* ya Kinyerezi maana yake una uwezo wa kuzalisha megawati 1,850. Hesabu ya kawaida, ukiwa na trilioni 1.2 una uwezo wa kufanya *extension* ukapata *megawatt* 18,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia hela iliyotengwa, kwa mfano ukinipa hela ile ya Rufiji trilioni 1.44 mwakani Tanzania kwa kufanya *extension* tu itakuwa na *megawatt* 18,500. Hii trilioni 1.44 ni kwa ajili ya *megawatt* 2100 ambazo ili zije zikamilike unahitaji trilioni 6. Kwa trilioni 6 unapata *megawatt* 2115, kwa kufanya *extension* ya Kinyerezi kwa trilioni 6 unapata *megawatt* 18,500. Hivi ukijiuliza Tanzania tumerogwa na nani kwenye kufikiri? *(Makofi)*

**MHE. MAULIS S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Nani amesimama taarifa?

**MHE. SAID M. MTULIA:** Mtulia

## T A A R I F A

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana mchangiaji na mchango wake ni mzuri lakini nataka nimpe taarifa kwamba kuna tofauti kubwa sana kati ya umeme wa maji na umeme wa gesi.

Mheshimiwa Spika, pesa tunazotumia pamoja na wingi wake kwenye kuzalisha umeme wa maji, yale maji hatutayalipia, hatutalipa bili ya maji, ni maji ya mto. Na umeme utakaotumika wa Kinyerezi I kuzalisha gesi, ile gesi ina gharama tunalipa gesi; kuna pesa kwanza unalipa gesi halafu kuna pesa ya kutengeneza mtambo ambao utatoa umeme. Gesi ni ya *TPDC* na umeme ni wa *TANESCO,* lazima ulipe na bei ya gesi, hilo nampa taarifa.

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa David Silinde, unaipokea?

**WABUNGE FULANI:** Ngoja kwanza, haiwezekani.

**SPIKA:** Utaratibu hauendi hivyo, tunaenda na mmoja mmoja, aipokee taarifa; hajaongea chochote sasa taarifa yako labda kama unampa taarifa yule aliyeongea kule mwanzo, sasa inakuwa tabu kidogo, Mheshimiwa Silinde.

Waheshimiwa Wabunge, tuokoe muda, leo muda dakika zenu chache sana hapa

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, taarifa ile aliyotoa ndugu yangu Mheshimiwa Mtulia ni suala la kutokusoma na hili ndilo tatizo kubwa sana la nchi yetu, watu hawasomi na *poverty mentality* imekaa Tanzania, watu hawafikiri. Gesi yenyewe ni mali yetu, siyo mali ya mtu mwingine, ukitumia gesi ukazalisha *megawatt* 18,500 tutauza Burundi, Rwanda, Kenya na nchi zote kwa kutumia fedha hizi hizi, hela hii inayopatikana tuna uwezo sasa wa kurudi tukaanzisha *Stiegler's Gorge. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa una-*ignore* jambo moja, unakwenda jambo lingine; unajiuliza tumerogwa wapi? Ndiyo hizi hoja mtu anakuja bwana mnapinga kila kitu kwa sababu ya uchaguzi, kushinda uchaguzi siyo hoja ambayo inatuleta hapa, ni kuishauri Serikali ili iweze kufikia yale malengo. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ambacho nilikuwa nataka kukizungumzia, hoja ya kusema…

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde naomba, Mheshimiwa nakuruhusu.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, namuheshimu sana Mheshimiwa anayezungumza ni mdogo wangu lakini asifanye *direct costing* kwamba ukiwa umetengeneza umeme kwa mwanzo wa shilingi 10 kwa eneo hilo hilo ukifanya kitu kilekile unazidisha mara mbili inakuwa 20. Kuna *exponential,* kuna *extra cost* zinazokuwa pembeni ambazo yeye hana *details. (Makofi)*

**SPIKA:** Unapokea taarifa ya Mheshimiwa Charles Kitwanga? Makatibu mlinde muda wa Mheshimiwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Wabunge wamenielewa na hata Mheshimiwa Kitwanga amenielewa. Pamoja na kwamba nakubaliana na hoja yake kwa maana ya kunakuwa na *other overhead cost it's true* lakini pamoja na hivyo, sikilizeni muwe mnakubali kusikiliza kwanza msiwe mna haraka, sikilizeni muelewe. Hapa tunachoshindana ni ku-*think beyond the box,* nimefikiria nje na mnavyofikiria ninyi. Kwa hela yenu tutapata umeme mdogo tofauti na hiki ambacho tayari tulishakuwa tumekianza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa mmekuja na mpango mzuri tu, kwa mfano *issue* ya *LNG. LNG* baada ya ugunduzi wa gesi mwaka 2010, mwaka 2014 Serikali ikasema sasa lazima tuunde *LNG* ili tuanze kusafirisha gesi. Makampuni yakajitokeza; *British Gas, State Oil, Exxonmobil Tanzania, Ofil Energy* wakasema sisi kwa umoja wetu tunaweza tukafanya.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 mwezi Agosti, Mheshimiwa Rais Magufuli akawaagiza *TPDC* kuharakisha mchakato kwa kuhakikisha *LNG* inaanza kujengwa, unakuja unasoma ripoti ya Mheshimiwa Waziri anakwambia ndiyo kwanza *government negotiation team* inakwenda kuanza mazungumzo. Miaka mitano tangu wazo la kuanzishwa kwa *LNG, we are still discussing with this mindset* Haki ya Mungu hatuwezi kwenda popote, *with this mindset* hatuwezi kwenda popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajiuliza, nini kinakwamisha? Mwaka 2017 tulitunga sheria nzuri za kulinda rasilimali zetu lakini kuna baadhi ya vifungu havitekelezeki, huo ndiyo ukweli. Juzi juzi nilikusikia ulitoa mfano mzuri tu na nakumbuka juzi wakati Mheshimiwa Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Mahiga wakati anajibu swali moja akasema mnapoangalia hii mikataba, msiangalie tu upande wa *negative,* wakati mwingine muangalie mazuri ya mikataba... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naambiwa ni kengele ya pili, makatibu wananiambia kwa hiyo, ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Ghasia nilikutaja atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Simbachawene jiandae, Mheshimiwa Ghasia dakika tano tano.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nadhani sifa ambazo wanapewa kwa kweli wanastahili sana; si wachapakazi tu lakini pia ni wasikivu, wanyenyekevu na wanashaurika, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu ni mchache, naomba niende moja kwa moja katika maeneo ya Jimbo langu. Nishukuru sana kwamba vijiji vingi katika Jimbo langu vimepata umeme lakini nina kata mbili; Kata ya Muungano na Kata ya Moma hazina hata kijiji kimoja ambacho kina umeme. Nikushukuru Mheshimiwa Waziri juzi ulivyokuja umeniahidi vijiji viwili katika Kata ya Muungano na Vijiji viwili katika Kata ya Moma, nakushukuru sana na pia umeniahidi umeme katika Sekondari ya Nanguruwe. Pia niombe umeme katika sekondari yangu ya Lilido na yenyewe

Mheshimiwa Waziri nayo niweze kupata umeme ili wanafunzi wangu waendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana kwa kuanzisha mpango wa kupeleka gesi ya majumbani. Mwaka jana tulifanya uzinduzi pale katika Sekondari ya Mtwara kwa sababu sasa hivi inachukua na wasichana, Sekondari ya Ufundi Mtwara lakini mradi ule naona kama unaenda taratibu na nilivyosoma katika kitabu chako cha hotuba naona kwamba bado mko katika usanifu. Nikuombe Mheshimiwa Waziri huo usanifu uharakishwe ili mradi ule uanze kutekelezwa kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, eneo ambalo ningependa kulisisitiza ni suala la utoaji wa leseni za utafutaji na uendelezaji wa gesi. Mheshimiwa Waziri nimeshakuja kwako zaidi ya mara mbili na Kampuni ya *Ndovu Resource* wakiomba leseni kwa ajili ya kuendelea kutafuta gesi na pia wakiomba leseni kwa ajili ya kuendeleza maeneo yale ambayo tayari gesi imepatikana, huu unaingia mwaka wa pili. Mheshimiwa Waziri nikuombe chondechonde tunasema kwa Kimakonde hivi vibali au hizi leseni kwa nini zinachukua muda mrefu hivi? Mji wa Mtwara sasa hivi unasinzia, kipindi kile wakati utafutaji unaendelea, mji ulichangamka na uchumi ulikuwa unakua.

Mheshimiwa Spika, tukuombe hayo majadiliano yakamilike, mnachojadiliana ili leseni zitolewe kwa watafutaji wa gesi na wale ambao tayari wameshapata gesi wanataka kuendeleza vitalu vyao haswa hao watu wa *Ndovu Resource* wamechimba katika Jimbo langu wamegundua zaidi ya maeneo matatu, sasa wanaomba leseni ya kutaka kuendeleza shughuli tangu mwaka 2017 mwezi wa kumi wameleta maombi mpaka leo bado majadiliano naambiwa sijui mkataba upo kwa *AG.*

Mheshimiwa Spika, nakusudia kutoa shilingi ili niambiwe ni lini leseni zitatolewa kwa watafutaji na waendelezaji wa gesi kwenye vile vitalu vyao. Mheshimiwa Kalemani tangu umeingia hujatoa leseni hata moja na watu

wapo wanaotaka kutafuta hiyo gesi, wapo wanaotaka kuendeleza hizo gesi lakini leseni imekuwa ni mtihani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa *AG* bahati nzuri upo, utasaidia katika kurudisha hiyo shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Waziri hastahili hata kidogo kunyang'anywa shilingi lakini naambiwa mambo yote yapo kwako lakini ili nifike kwako ni lazima nipitie kwa Waziri. Kwa hiyo, nitachukua shilingi ya Waziri ili Mheshimiwa *AG* ufanye kazi kwa haraka ya kumuwezesha Waziri kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nilitaka nalo nipate ufafanuzi ni kuhusu Kiwanda cha Mbolea cha Msanga Mkuu kupitia Kampuni ya *HELM*…

**SPIKA:** Bahati mbaya dakika tano zimeisha.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja lakini Msanga Mkuu na suala la leseni nipate majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mheshimiwa George Simbachawene dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Zungu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya na hasa ya kupeleka umeme vijijini, wanafanya kazi nzuri wanazunguka na kufanya kazi ambayo Taifa hili ipo siku litapiga hatua kubwa kwa sababu umeme ndiyo uchumi.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwenye eneo hili ni kwamba umeme huu utakuwa na maana kijamii na kiuchumi endapo utakwenda kwenye huduma za jamii; uende kwenye shule, zahanati, vituo vya afya, visima vya maji na sehemu za

uzalishaji vijijini ndipo tutakapoona namna umeme huu unavyokuwa na maana kwa kupelekwa vijijini. Vinginevyo, kama si hivyo basi umeme huu utakuja kutafsiriwa baadaye kwamba ni kitu ambacho tumewekeza sana lakini hakijaleta tija katika uchumi lakini ikifika katika maeneo hayo utatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hotuba yangu ambayo niliiandaa lakini hapa ninaihairisha kwa sababu nataka nijaribu kuchangia kwenye line ambayo mdogo wangu Mheshimiwa Silinde amechangia na natambua kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na hivyo ana ufahamu mkubwa na anayajua mambo mengi na tunashirikiana katika mambo mengi na sina mashaka hata kidogo juu ya uwezo wake, lakini nilitaka tu nimuongezee ujuzi juu ya masuala ya uchumi wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Dunia kwa sasa katika masuala ya umeme ni *energy mixing,* kwa nini? *Energy mixing* kwa sababu hakuna chanzo *sustainable* kwa sasa, iwe gesi inaisha; hiyo gesi unayosema inaisha, yawe maji yameathiriwa na uharibifu wa mazingira na yenyewe yanaisha, upepo mara utakuwepo mara hautakuwepo, chochote kile sasa hakina *sustainability* na ndiyo maana falsafa ya sasa ni mchanganyiko wa uzalishaji wa umeme wa aina mbalimbali. Sasa ume-*derive* hoja nzito sana hapa kwamba Serikali haijaliangalia hili jambo *economically* badala ya kuwekeza katika miradi ya kuzalisha umeme wa gesi, inawekeza kwenye umeme wa maji...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kelele zipo nyingi tutulie Mheshimiwa Silinde anapelekwa shule, endelea Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Silinde anajaribu kutushawishi tuione Serikali imekosea, sisi Wabunge wenzie, Watanzania na dunia kwa kuwekeza katika umeme wa maji *megawatt* 2100 kutoka kwenye maporomoko ya Mto Rufiji na badala yake tuendelee

na gesi ambayo hoja ya kwanza kabisa inaisha, hiyo gesi unayosema inaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unasema *size* ya bomba...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Hebu tuvumiliaje kidogo...

**WABUNGE FULANI:** Aaaah! Kaa chini.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Ally Saleh. *(Kicheko)*

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema, kwa heshima unatakiwa ukae kitako.

Mheshimiwa Spika, ni kweli anachosema kwamba gesi inakwisha lakini jua haliishi, utafiti duniani unaonesha *the cheapest* ya kufanya umeme ni jua ambalo haliishi, lipo siku zote. (*Makofi)*

**SPIKA:** Kuna mawingu siku nyingine, jua halifiki.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Una *store,* sayansi ipo ya kutosha ya kuonesha utafiti wa jua au umeme wa jua unakutosha na una *storage,* ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hayo mabetri ya ku-*store* umeme usafirishe nchi nzima labda jumba hili dogo. Hoja yake kwamba kuna *limitations* kwa hiyo *energy mixing* ni muhimu, nafikiri katika kujenga hoja yake yupo sahihi tu. Endelea Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Ally Saleh rafiki yangu kwa kusema anatukumbusha pia kwamba tuweke na umeme wa jua, nimezungumza *energy mixing means all sources of energy;* inaweza ikawa ya makaa ya mawe, vyovyote vile ambavyo vinatoa *energy* lakini lazima tuwe na mchanganyiko kwa sababu hakuna ambacho ni *sustainable,* hata hilo jua yako

maeneo hayana jua ambayo huwezi ukazalisha umeme. Na ili uhitaji umeme wa jua unahitaji kilometa za mraba nyingi mno kuzalisha *megawatt* moja, sasa tukienda huko na ardhi yetu na tunahitaji kulima na shughuli zingine za ufugaji, mzee tutapotea hata huko siyo kwa kwenda sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, amenitoa kwenye mstari lakini nirudi. Unazungumzia ukubwa wa bomba la gesi. *Essence* ya ukubwa wa bomba la gesi kwanza ilikuwa ni ndoto za baadaye, tungeweza kujenga la kipenyo cha sentimita 18, tukaamua kujenga cha 36 kwa sababu tulijua ugunduzi unaendelea na bomba hilohilo litatumika na eneo *potential* katika uzalishaji/ugunduzi wa gesi ni huko huko kusini. Kwa hiyo, tulipojenga bomba siyo kwamba tuli-*equate* gesi tuliyonayo leo na tunachokisafirisha, hapana hiyo sio *thinking.* Kwa hiyo, *equation* na yenyewe kidogo ina walakini.

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopongeza, na nipongeza Kambi ya Upinzani, *this time* kwenye hotuba yao wameeleza *conspicuously* kwenye Ibara yao ya 52, msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mradi wa Rufiji *(Rufiji Hydropower Project).* Wanasema pamoja na kukubaliana na dhana ya kuzalisha umeme wa megawati 2,100, wamekubali, kwa hiyo hawa ni wenzetu, hawa ni wazalendo ila wana mambo ambayo wanataka tuyatazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Serikali huu ni mchango mzuri wa Kambi ya Upinzani kwamba somo tulilolipiga kwa muda mrefu sasa wamelielewa na tuko pamoja katika jambo hili na ni hotuba hii wamesema hivi, haya maneno mengine tuendee tu kuwaelewesha.

Mheshimiwa Spika, *cost of production* katika uzalishaji wetu sisi Tanzania iko juu. Tunaposema uchumi wa viwanda hatuwezi kufika huko kama hatuja-*deal* na hili suala *basic* la umeme. Na ndiyo maana katika mpango mkakati wa uzalishaji wa umeme nchini tunasema *by* 2025 tuwe tuna megawati 10,000, megawati 10,000 unazitoa wapi kama una maporomoko kama yale ya Rufiji halafu unayaacha?

Mheshimiwa Spika, hizi kelele za *pressure groups* duniani zipo tu, huwa zipo tu, tusibadilishe mwelekeo kwa sababu ya kelele za *pressure groups,* hizi huwa zipo tu. Lakini kuna nchi gani imejitokeza na kusema inaupinga huu mradi, nchi kama nchi; hakuna nchi, ni *pressure groups.* Kwa hiyo, nasema mmeelewa, ni jambo zuri na sasa tuko pamoja tunakuunga Serikali Waziri kanyaga mafuta twende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu sasa, *TPDC* mmewawekea mzigo ule wa gharama za ujenzi wa bomba. Ukishaweka gharama za ujenzi wa bomba hatutayaona manufaa ya mnyororo wa thamani wa gesi kwa sababu lile bomba linachukua sehemu kubwa sana ya bei na ndiyo maana *negotiation* hata ya uzalishaji wa mbolea, *negotiation* ya kupeleka umeme viwandani bado zinasumbua.

Mheshimiwa Spika, na sisi kwenye Kamati taarifa hizi tunazo. Majadiliano yanasumbua, yako hapohapo kwa sababu wanabiashania visenti, visenti, mwenye kisima aliyegundua gesi – kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, gesi haiwezi kuchimbwa na Serikali kwa sababu ile biashara ni *risk.* Unaweza ukatumia hela za Watanzania wote ambao leo hii tunataka kujenga vituo vya afya, tuna tatizo la elimu, tuna tatizo la huduma za jamii kwa ujumla, ukaenda ukachimba uka-*hit dry well* na umetumia *billions of money.* Kwa hiyo kazi hii inafanywa na *Private Sector* lakini ikishagundua ndiyo mnakuwa na mkataba wa makubaliano ya uendeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hii ndiyo *trend* ya dunia nzima. Kwa hiyo, *negotiations* hizo tukishaweka na bomba la gesi – majadiliano hayaendi ndiyo maana viwanda vya mbolea vimesimama, hakuna kinachoendelea. Tuondoe bomba la gesi tulibebe kama Taifa kwa sababu tunafanya mambo mengi yenye gharama kubwa kuliko hata bomba la gesi, mbona haijawa-*pegged?* Ina maana *standard gauge* leo na yenyewe tuiwe *TRC,* ina maana barabara hizi tuweke *TANROADS;* itakuaje, tutaendeshaje?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, uchumi kwa sababu umeme ndiyo utakao-*tickle* uchumi mzima kuamka ninasihi Serikali ione umuhimu wa kuchukua hii gharama tuibebe kwa ujumla wake. Kwa sababu umeme huu ndiyo unaobeba uchumi pia, tukiongeza hizi megawati maana yake umeme ukisambaa kila mahali uzalishaji unakuwa na bei rahisi, uzalishaji wa bidhaa zetu zitashindana hata kwenye masoko mengine huko duniani. Kwa sasa wanachotushinda wenzetu walioendelea na wanaotuuzia bidhaa ni *costal production* ambayo *number one* ni *power,* sisi umeme wetu ni aghali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niliomba nitoe rai hii na nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, dakika tano.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini nichukue nafasi hii vilevile kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya, kwa kweli mnaitendea haki Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda wangu mi mdogo tu, nazungumzia suala la *LNG* ambalo mazungumzo yanaonekana yanachukua muda mwingi. Mazungumzo kuchukua muda mwingi yawe *productive,* yawe na uangalifu wa kutazama maslahi mapana ya nchi. Na e*cosystem* sasa hivi imekuwa *introduced* ambayo badala ya kufanya *LNG* wanafanya *FNG (Floating Natural Gas Products).*

Mheshimiwa Spika, na huu ni mtambo ambao unafungwa baharini kulekule kwenye meli na meli inabeba mzigo mkubwa sana wa mtambo huu na gharama za kuzalisha na kusafirisha gesi inakuwa ni ndogo. Na *results* zake ambazo Serikali itazipata na nafasi ya kutengeneza mtambo huu ni miaka miwili tu, tofauti na miaka tisa ambayo *LNG* inafanya kuleta kwenye *shore* ya nchi kavu, kwa hiyo watu wanaona labda ni muda mwingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba Serikali katika mazungumzo yao wa-*incorporate* na waone umuhimu wa ku-*introduce FNG* badala ya *LNG.* Najua *FNG* ni *component* moja, haitakuwa kwa mradi wote, lazima *LNG* iwepo, lakini tunaweza tukaanza na *FNG* ili Serikali ikaanza kuvuna mapato yake kwa haraka sana kwa gharama za *FDI* ambayo ni *Foreign Drect Investment,* bila Serikali kuweka hela zake. Na wana-*estimate FNG* kuweza kuiletea Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu labda *two billion US Dollars.*

Mheshmiwa Spika, kitu muhimu kwenye mikataba lazima wataalam wetu wawe na uhakika wa *outflow meter* waweke *digital wireless meters* ambazo zina *sensor* na kuona *gas* inayotoka. Hata wewe ukiwa ofisini hapa unaweza ukaona *sensors* za *outflow meter* ya *internet of things* ambazo zitakuwa zinafanya kazi huko Lindi, wewe utaona kiasi gani cha gesi kinatoka na hakuna nchi wala hakuna mahali popote wawekezaji hawa wataweza kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, naomba katika mazungumzo mjaribu ku-*introduce FNG* ili tunaze na *FNG* Serikali ipate mapato. Na katika kuanza mradi huu Serikali ihakikishe inaweka *digital wireless meters* za kuweza ku-*sense* gesi itakayokuwa inauzwa nje ili tusiibiwe katika mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Richard Mbogo nilishakutaja.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi.

**SPIKA:** Dakika saba.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kupongeza Serikali, nipongeze Wizara na watendaji kiujumla na taasisi zote zilizoko chini ya Wizara hii ya Nishati kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, na Waziri na Naibu wake wanazunguka sana katika Nchi yetu hii ya Tanzania kuhakikisha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unaenda vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye hoja zangu za jimboni, naomba kidogo kuna masuala niweke sawa. Nianze na alipoishia kaka yangu, Mheshimiwa Simbachawene, kuhusiana na rafiki yangu Mheshimiwa Silinde; katika mchango wake amezungumzia gharama za umeme hususan kwenye gesi pamoja na matumizi ya bomba, linatumika kwa asilimia 6 pamoja na gharama za kutanua Mradi wa Kinyerezi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Bunge litambue kwamba kuna wengine wanajua bomba lililopo ni moja tu ambalo linasafirisha gesi kutoka Mtwara, hapana, yapo mabomba mawili. Kwanza tuna bomba dogo na Serikali iliona kwamba hili bomba ni dogo ndiyo maana tulivyokuja kuongeza bomba lingine ikawa ni kwamba limetengenezwa bomba kubwa ili kuweza kuchukua ujazo mkubwa kutokana na ambavyo uwekezaji utakuwa unafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kutumika kwa asilimia sita tuna-*save future investment* kama tungekuwa labda tayari tuna bomba lingine ambalo ni dogo. Na pindi kwamba uzalishaji na visima vingine vya gesi vitaongezwa basi tayari tutakuwa na *means* ambayo ipo inayotosheleza kusafirisha hiyo gesi.

Mheshimiwa Spika, na uwekezaji ambao unafanyika wa kuongeza hapo Kinyerezi hizo bilioni 60 ambazo amezisema ikiwa ni moja wapo ni kuendana na Sera ya Nishati katika kuwa na *energy mix* kama ambavyo wengine wameweza kuchangia. Na kimsingi, masuala ya ku-*quantify investment cost,* kwamba unalinganisha mpaka zinafika trilioni sita, ni masuala ya kitaalam na wataalam wamekwishakaa wakaangalia kwamba uwekezaji wa

kwenye *Rufiji Hydropower* wa *more than six trillion* ni kwamba utakuwa na manufaa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, na manufaa hayo, kwanza umeme wa maji ndiyo umeme ambao ni wa gharama nafuu sana duniani kote. Uniti moja gharama yake ni shilingi 36 wakati umeme unaotokana na gesi ni shilingi 547. Angalia tofauti ya zaidi ya shilingi 500 kama na 11...

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** ...sasa kama tuna-*save...*

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mbogo; Mheshimiwa Silinde.

**T A A R I F A**

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa kutokana na kwamba anakwenda kwenye ule mchango ambao nilichangia. Na wakati nachangia nilisema tunachotaka sisi ni kufikiri kibiashara, na mantiki yangu ni nini; nilikuwa nachukua kwamba *think beyond the box,* kwamba ukichukua *1.4 trillion* ukaenda uka-*expand* Kinyerezi leo hii ndani ya miezi sita utapata megawati 4,440, ndani ya miezi sita. Hii *1.4 trillion* haileti ile megawati 2,000 leo wala kesho.

Mheshimiwa Spika, sasa nikasema leo ukipata *six trillion* ukaingiza ukafanya *expansion* utapata megawati 18,500 ambazo umeme wake tutazalisha nchi mbalimbali, tukiuza kule nikasema ndiyo tunakwenda kuweza kwenye *Stiegler's Gorge.* Sasa hii ni sawa na mtu ana nyumba pagala halafu ana kiwanja amepata milioni 10 anafukuzwa na mwenye nyumba, unaambiwa sasa nenda kamalizie pagala lako...

**SPIKA:** Ahsante, dakika yako imeisha.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** ...haya, ahsante, ameelewa lakini.

**SPIKA:** Utazipata hizo kwa gesi ipi wakati inayokuja ni *6% only?* Endelea Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba ulinde muda wangu. Nafikiri akafanye *cost benefit analysis* tena kuangalia uwekezaji kwenye *Hydropower* kwa miaka ijayo na *lifespan* ya gesi ni *by* 2047 inakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, suala la kutumia umeme wa maji pia ni suala la msingi kwa uchumi wa nchi yetu. Hii *Rufiji Hydropower* itakuwa na faida mojawapo, itapunguza gharama, kwa hiyo Watanzania zaidi ya milioni 50 watafaidika na unafuu wa gharama kwa sababu watatumia umeme ambao una bei nafuu. *Production cost* kwenye viwanda zitapungua upande wa *utility* kwa sababu umeme utakuwa una bei nafuu. Kwa hiyo, ile *economic benefit* itakuwa kwenye sekta karibu zote, mpaka kwenye kilimo, kwenye sekta zote *economic benefit* ya umeme wa bei nafuu itakuwepo.

Mheshimiwa Spika, jana wakati inawasilishwa hii taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani, walizungumzia kwamba ujenzi wa hii *Rufiji Hydropower,* kwamba utaongezeka kwa asilimia 30 na msemaji akasema itafikia bilioni 9 *US Dollars,* takribani trilioni 22. Lakini ukichukua kimahesabu ongezeko la asilimia 30 toka kwenye bilioni 3.7 unafika bilioni 4.8 – sijui hesabu zake alizifanyaje – na tunajua katika ujenzi siku zote *variation* huwa zinakuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo, nafikiri sentensi zingine za gharama zinakuwa zinapotosha Umma, kwamba huu mradi utakuwa ni wa gharama sana. Ingekuwa ni vyema sasa na Waziri uje uwaeleze vizuri gharama za mradi zitakuaje.

Mheshimiwa Spika, ilizungumziwa kuhusu matumizi ya fedha nje ya ukomo wa bajeti. Naomba niwakumbushe; Sheria ya Bajeti kuna kifungu kinaruhusu kutumia nje ya ukomo ambao tumeidhinisha na taarifa inaletwa Bungeni. Na tena

kuna asilimia, ikiwa inafika asilimia 9 ndiyo iko chini ya idhini ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, pia katika ile taarifa waliitisha mikataba kwamba iletwe Bungeni, lakini naomba nikumbushe; uliunda Kamati Maalum ya kwako ya kuchunguza Serikali itafaidika vipi na gesi asilia na ilitoa mapendekezo, mojawapo pia ni kupitia mikataba yote. Kwa hiyo, kazi uliifanya kabla hata wao wanaokuja sasa kuiagiza Serikali kwamba ifanye.

Mheshimiwa Spika, niseme tu Sheria ya Uchimbaji Gesi, gharama ya gesi ni kubwa sana na Serikali tumejitoa kwenye ile gharama. Kwa sababu ukichimba na usipopata inakuwa ni hasara kwa aliyechimba, na nakumbuka katika hili Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Zitto Kabwe aliwahi kuisifu sana Serikali kwa kuweka utaratibu huu katika Sheria ya Uchimbaji wa Gesi. Kwa hiyo, niombe tu kwamba Serikali inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, na kuhusiana na mazingira, kwamba *Stiegler's* inakwenda kuharibu mazingira yote; hapana. Angalia, tumejenga miundombinu mingi katika nchi yetu; barabara, reli, tulikata miti. Wangetoa ushauri kwamba hebu tutengeneze uoto maeneo mengine kama hii Dodoma pamoja na Singida.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niombe sasa Serikali kwenye suala la mafuta tuangalie namna gani Kampuni ile ya *TIPER* jinsi gani ambavyo sasa itakwenda kuhusishwa katika kutunza mafuta ili tu-*control* kodi inayotokana na mafuta na tuweze ku-*control* uhitaji wa mafuta katika nchi yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joram Hongoli atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi.

**SPIKA:** Dakika tano, tano.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya usiku na mchana, kwa kweli wanafanya kazi. Naomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda ili muendelee kufanya kazi zaidi kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Nishati ndiyo sekta wezeshi kwa maana ya viwanda nchini na nchi yoyote ambayo imeendelea kiviwanda ni lazima iwe na umeme wa kutosha. Kwa hiyo, naamini kwamba mipango iliyopo ya Wizara na miradi hiyo ambayo inakwenda kuanzishwa itasababisha nchi yetu iwe na viwanda vya kutosha na hatimaye kuongeza uchumi wa wananchi lakini pia nchi yetu kukua kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie juu ya usambazaji wa umeme, hasa kasi ya wakandarasi. Kasi ya wakandarasi wa umeme kwenye maeneo mengi siyo nzuri, hairidhishi. Kwa mfano kwenye jimbo langu mpaka sasa hivi kuna kata tatu hazina umeme kabisa lakini pia mkandarasi aliyepo kwenye eneo langu alianza kazi toka mwaka jana lakini mpaka leo hii ameweza kupeleka umeme kwenye vijiji viwili na katika vijiji hivyo viwili amepeleka kitongoji kimoja kimoja; amepeleka umeme Kijij cha Hang'ana kitongoji kimoja, lakini poa Kijiji cha Iyembela kitongoji kimoja, lakini bado kwenye maeneo mengi hajapeleka umeme. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri tusaidie ili kasi ya mkandarasi iweze kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya maeneo wananchi wameshajituma tayari kuanza, wameitikia agizo la Mheshimiwa Rais la Tanzania ya viwanda tu. Kwa mfano

Kijiji cha Ndinga wana kiwanda cha sembe wamenunua toka mwaka 2016 lakini mpaka leo hakifanyi kazi kwa sababu wanasubiri umeme uweze kufika katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna Kijiji cha Madeke, wana kiwanda cha kuchakata mananasi, bado hakifanyi kazi kwa sababu umeme haupo. Wamejaribu kutumia nishati ya dizeli, dizeli ni gharama; lakini pia wametumia *solar,* haina uwezo mkubwa wa kuweza kustahimili kwa sababu kule eneo la Lupembe ni eneo la mvua nyingi kwa hiyo muda mwingi ni mvua kwa hiyo haiwezi kustahimili kuweza kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukuombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo haya ya uzalishaji kwenye maeneo ya vijiji hivi, kasi iweze kuongezeka ili wananchi wa Jimbo hili la Lupembe waweze kupata umeme na hatimaye kuweza kuanzisha viwanda kwa sababu ni wakulima wa matunda, ni wakulima wa mananasi, ni wakulima wa miti, kwa maana ya mbao, wanataka viwanda ili kuweza kuongeza thamani ya mazao yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni juu ya umeme ambao unapelekwa kwenye viwanda. Eneo letu la Lupembe ni eneo la mvua nyingi na tuna viwanda vikubwa, hasa viwanda vile vya chai, tunavyo viwanda viwili katika eneo lile. Lakini pia viwanda vingine watu wanataka kuwekeza wanashindwa kwa sababu maeneo mengi hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna tatizo moja kwenye viwanda, kwamba umeme unapokuwa umekatika, kwa mfano transfoma inapokuwa imeungua, wamiliki wa viwanda wanatakiwa kununua hizo transfoma, kwa hiyo, imekuwa shida sana. Mara nyingi utakuta kwamba transfoma ikikatika zinaisha wiki moja mpaka mbili hawana transfoma na wananchi wanachuma chai hawawezi kuuza kwa sababu kiwanda hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuombe sana; utaratibu huu wa kwamba wawekezaji ndio wanunue transfoma naona kama siyo mzuri. Ni vizuri *TANESCO* wawe wananunua

hizi transfoma ili zinapokatika basi waweze kurudisha haraka ili wakulima waweze kuendelea kuuza chai yao, waweze kuendelea kuuza mazao yao na waweze kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ilivyo sasa hivi, kwa mfano zao la chai likichumwa tu lazima likauzwe na lazima lichakatwe siku hiyo hiyo, likilala siku ya pili chai inapoteza ubora na itakuwa ni ya kumwaga tu. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, hasa kwenye maeneo haya ya uzalishaji kwenye maeneo kama ya viwanda vya chai; *TANESCO* wawe na transfoma zao na ikiwezekana wawe na transfoma za akiba ili pale ambapo umeme unakuwa umekatika basi waweze kuzipeleka haraka ili wakulima ambao wamechuma zile chai zao waweze kuuza siku hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mwekezaji yeye anaangalia faida tu, ukikatika umeme anakwambia umeme haupo kwa hiyo leo hatuchukui chai. Kwa hiyo, mwisho wa siku wanaopata hasara kubwa ni wale wakulima ambao wamechuma hiyo chai na mazao mengine. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, tuwe na utaratibu kwenye viwanda hivi tuwe na transfoma za akiba.

Mheshimiwa Spika, niseme juu ya umeme, hasa umeme unaozalishwa na makaa ya mawe pale Mchuchuma. Nikuombe sana Mheshimiwa, huu mradi ni wa muhimu sana kwa sababu umeme ule utakuja kutusaidia muda ambapo maeneo mengine au vyanzo vingine vitakuwa haviwezi kuzalisha umeme.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joram Hongoli. Mheshimiwa Katani Ahmad Katan, atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Peneza.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nikushukuru wewe pia kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya. Lakini nina mambo kadhaa ambayo ningependa nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, sisi Mtwara pale tuna mitambo ya kuzalisha umeme, tunayo mitambo 11. Na Mheshimiwa Waziri unajua kila mtambo mmoja unazalisha megawati mbili kwa maana ya mitambo yetu 11 inazalisha megawati 22, japo miwili ni mibovu, na ninajua una taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye matumizi ya Mkoa wa Mtwara na Lindi kwa maelezo ya nyie wataalam wa umeme mnasema tunatumia megawatts 15 na tunakuwa na ziada ya megawats tatu, mara nyingi huwa napata shida mnaposema tunaziada ya megawatt hizo tatu kwasababu kama leo Tandahimba yenye vijiji 156 ina vijiji takriban 88 havina umeme lakini ukichukulia hesabu ya mkoa mzima wa Mtwara una vijiji vingi havina umeme kuliko vyenye umeme. Sasa sijui hii *extra* inaonekana kwamba inapelea, inapelea namna gani wakati watu kule hawapati umeme mtatusaidia kitaalamu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nirudi kwenye suala la mradi huu wa REA Mheshimiwa Waziri nashukuru sana tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara juu ya mkandarasi ambaye tunaye Mtwara, kwenye Jimbo langu nina vijiji 30 ambao vilitakiwa viwe na umeme na mkataba baina ya Serikali na yule Mkandarasi unaishia tarehe 30 Juni ya kesho kutwa lakini mpaka sasa ninapozungumza na wewe vijiji vitatu ndiyo wamewasha umeme sina hakika hizi siku zilizobaki anaweza kuwasha umeme kwa vijiji 27 ambavyo vimesalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini niliwahi kukwambia kwa Jiografia ya kwetu kwa Jimbo langu la Tandahimba maeneo

makubwa yenye watu wengi nikakwambia juzi nilikutumia na meseji Kata kama Mdimba ina wapiga kura tu elfu nane na kitu. Maana yake hiyo sehemu ina watu zaidi ya 12,000 au 13,000 na Kata nyingi za Tandahimba zina uwingi wa watu ukienda Tandahimba kwa uzalishaji wa korosho wa miaka mitatu, nyumba nyingi zimeshafanya *wiring* zinasubiri mapokeo ya umeme ukienda nyumba nyingi zimefanya *wiring*. Leo watu wanapata shida ya umeme ambao tuliamini kabisa kwa sisi watu wa Mtwara ambao gesi ambao tunasema asilimia 50 ya umeme tunaotumia ndiyo unatokana na gesi, lakini Mkoa wa Mtwara ndo unalalamika hauna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kwenda kwa Mheshimiwa Simbachawene nikapata maajabu makubwa vijiji vyake vyote vinawaka umeme. Lakini Mtwara ambako gesi inatoka leo tunakaa kulalamika umeme, umeme, umeme sasa hili Mheshimiwa Waziri niombe mnafanya kazi kubwa sana lakini kwa watu wale wa Mtwara ambao wameathirika kwa kiasi kikubwa na mradi ule tukazungumza habari ya mabomba hayo wale hawana umeme wapelekeeni umeme basi iwe kifuta jasho chetu tumepata umeme na wale wanauwezo wa kulipa hiyo 27,000 hata mngesema walipe 50,000 wanauwezo wa kulipa lakini umeme haujawafikia watu wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana kwenye jambo hili tunapoenda kwenye REA hii basi uingize vijiji vile vilivyobaki tuone suala la umeme kwa namna mlivyoandika hiyo 2021 watu wawe wamepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwanzo mlizungumza suala la viwanda ambavyo mama Ghasia amegusia suala la kiwanda cha Mbolea Msanga Mkuu, lakini mlizungumza suala la kiwanda cha Mbolea Kilwa Masoko kwenye kitabu chote cha Wizara sijaona hilo jambo sasa wakati una-*windup* utatuambia kwamba haya mambo ya viwanda hivi vya mbolea Kilwa Masoko, Mtwara kama vimepotea tujue vimepotea na kama vipo tujue vipo kwenye hatua gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la *LNG* ambayo wenzangu wamepongeza. Nipongeze lakini napata mashaka makubwa sana jambo hili limekuwepo tangu tunazungumzia suala lenyewe la gesi 2010 likazungumzwa suala la *LNG* Lindi, na tukaamini tutakuwa miongoni mwa maeneo ambayo uchumi wake ungepanda kwa kasi kusini ni pamoja na kama mngekweli mngejenga hii *LNG*. Leo mmehuisha mazungumzo kama mnavyosema tuone sasa haya mazungumzo mnayoyasema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Katani, sasa ni Upendo Peneza dakika 10, atafatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi na Mheshimiwa Fredy Mwakibete ajiandae.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, na nina mshukuru mungu kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Kama ambavyo umekwisha sikia wachangiaji wengine waliotangulia ni kwamba Bunge lako Tukufu ama Wabunge ambao wako ndani ya Bunge hili wana-*concerns* zao katika vitu viwili. Kuna *concern* ya kwanza kwa maana ya gharama, na kuna *concern* ya pili kwa maana ya mambo ya kimazingira yanayozunguka mradi huu wa *Stiegler's Gorge*.

Mheshimiwa Spika, lakini katika suala zima la gharama leo tumeambiwa na Serikali na tumekuwa tumeambiwa tangu bajeti iliyopita kwamba mradi huu utagharimu trilioni 6.5. Lakini ukiangalia katika namna ambavyo Serikali imekuwa ikitoa hela mpaka sasa, ni dhahiri kwamba mradi huu hauwezi kuisha kwa miaka mitatu kama ambavyo Serikali inatuambia na kama haitaweza kuisha kwa muda wa miaka mitatu, maana yake ni kwamba tutalipa hela zaidi, tutalipa hela zaidi na hatimaye inawezekana tukafika hata kwenye gharama tunazoambiwa za trilioni 22.9.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti iliyopita Serikali ilitenga bilioni 700 lakini mpaka tuna.. kwa maana mpaka

mwezi Desemba ulikuwa umetoa mia mbili sabini na kitu baadaye wamemalizia hizo bilioni 688 ambazo na bado hawajamalizia kwa maana ya kumlipa mkandarasi wa anayejenga huo mradi wa *Stiegler's Gorge*. Na sasa hivi tumetoa trilioni 1.4 maana yake ni kwamba kama Serikali inakusudia kwamba tumalize huu mradi kwa miaka mitatu, ni kwamba ingekuwa inatoa zaidi ya trilioni 2 kila mwaka, ili kuhakikisha kwamba mradi huu unaweza kuisha kwa hiyo miaka mitatu ambayo imetengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya yote ni kwamba leo tunazungumza gharama ya trilioni 6.5 kwa kujenga mradi mmoja. Mradi ambao ukiangalia kimazingira, watu wanaonesha *concern* kubwa na hata kama ukiuangalia mradi huu wenyewe je tukimaliza kujenga maji yatajaa kwa kutumia miaka mingapi ndani ya *dam* ili kuhakikisha kwamba huo umeme unaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kwamba itatumia takriban miaka 10 ili *dam* hiyo iweze kujaa maji na hatimaye kuzalisha umeme, kwahiyo mpaka kupata umeme huo wa megawatt 2100, itatumia takriban miaka 27. Sasa kwa namna hiyo maana yake ni kwamba tunatumia hela nyingi kujenga kitu ambacho hatutapata matokeo ya haraka kama ambavyo tunategemea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, leo tunawaaminisha watanzania kwa kiasi kikubwa sana kwamba huu mradi ukiisha tutapata megawatt 2100 kitu ambacho si kweli. Lakini hata ukiangalia miradi ambayo imekwishaendelea ambayo inatumia maji kuna miradi ya Kihansi na hapo Mtera mpaka leo hii hakuna hata asilimia 40 ya uzalishaji unaoendelea katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kama mifano tuliyonayo leo haitoi picha halisi mnatuambia vipi, kwa huo mradi ambao mnasema kwamba baada ya miaka mitatu utafika huko. Maana yake ni kwamba inawezekana tunataka tutengeneze historia kwamba awamu hii ilijenga huo mradi tukatelekeza vingine na ni uharibifu wa hela kama hatuwezi tukapata matokeo ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia vile vile tumeongelea suala zima la gesi na kuna pia vyanzo vingine ambavyo watu wamesema *mix energy* lakini katika hilo suala ukiangalia katika bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwakilisha hapa tuna miradi ya jua, tuna miradi ya upepo, tuna miradi ya maji hata katika maeneo mengine yote hii hiyo hela ya trilioni 6.5 kama ingegawiwa kwenye hiyo miradi midogo midogo tungepata zaidi ya hizo megawatt 2100 tena kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na zaidi ya hapo ni kwamba kama mradi wa umeme ungetengenezwa katika eneo moja usambazaji ungefanyika na hizo megawatt kuingizwa katika megawatt kuingizwa katika *grid* ya Taifa hata usafirishaji wa umeme kwenda kwa umbali mrefu kusingekuwa na upotevu wa umeme kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, tungeweza kuzalisha umeme wananchi wakapata umeme katika maeneo mbalimbali kwa kutumia hizo hizo trilioni 6.5 lakini kwa kuangalia au kuvipa vipaumbele miradi ambayo Serikali yenyewe imeweka kuna miradi ya maji, kuna miradi ya umeme, kuna miradi ya upepo ambayo Serikali sasa inaitupa pembeni na ukiangalia katika bajeti nzima ya maendeleo Serikali imetenga trilioni 2.1, trilioni 1.4 yote inatumika kwenye mradi wa Stiegler's tunabakiza bilioni 68 tu itumike katika miradi mingine na kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali kitu ambacho hakitupi picha halisi ya Serikali kutaka kuifanya Tanzania hii, Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninaomba nizungumzie kuhusu suala la gesi. Naomba nizungumzie suala la gesi Tanzania ni katika nchi ambayo imekubali kufanya uvunaji wake wa gesi katika njia ya *production sharing*. Kwamba Kampuni ya TPDC inaingia pamoja na hawa wawekezaji na kuna mgawanyo kwa maana ya pesa ya ku-*invest* lakini pia kuna kugawana baadaye baada ya kuivuna hiyo gesi yenyewe. Lakini pamoja na matatizo yote ambayo *TPDC* wanayo ukosefu wa hela ya kuwawezesha wao kufanya utafiti na vitu mbalimbali lakini bado wanaweza kupata mgao wa gesi kupitia hii *production sharing agreement.*

Mheshimiwa Spika, sasa tulipitisha hapa sheria ndani ya Bunge mwaka 2017 sheria ambazo zimefanya wawekezaji ambao wako katika upande wa gesi kukimbia na leo hii hatuna uzalishaji mkubwa katika upande wa gesi, gesi ni kama vile imelala sasa. Lakini katika Bunge lililopita, Bunge hili lilikaa na tukapitia upya vipengele ambavyo vilikuwa vinawakandamiza wale wachimbaji wadogo wadogo na tukasahihisha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natumia muda huu kukuomba kwamba kamati inayohusika na mambo ya madini na nishati, iweze kukaa pamoja na Serikali pamoja na hawa wawekezaji kujadili ni changamoto gani ambazo zipo katika hizo sheria na hatimaye tutoke na njia moja ya kuweza kusahihisha mapungufu yaliyopo ili tupate njia ya kwamba tupate gesi, huku na miradi mingine inaendelea ili kuhakikisha tunapata hiyo *mix energy production* katika nchi hii kama ambavyo imekuwa ikisemwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitaleta maana kama nchi imetumia takriban trilioni 3 kujenga bomba leo hii halina faida kwa nchi ni asilimia 6 tu haileti faida wala haileti *value for money*, kwa hiyo ni bora tukaboresha hizi sheria tukawekeza tukapata gesi na uzalishaji wa umeme pamoja na matumizi mbalimbali ya gesi yakaweza kuendelea ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwenye upande wa *REA*, kamati imetuonesha changamoto ambazo zipo katika mradi wa *REA* kwamba kuna ucheleweshwaji wa Serikali kutoa hela, kwa hiyo mnachelewesha katika huduma hizi za umeme wa *REA* kufanya kazi na huduma mbalimbali katika maeneo hayo, na hatimaye inazalisha ongezeko la pesa kwa maana ya hii mikataba wale *contractors* wanadai hela nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hapo pia hata wale *contractors* wenyewe wale waliofanya hizo kazi, na wenyewe pia wapo wanaochelewesha kazi hizo ni vizuri sasa Serikali ikaunda kitengo maalum cha *monitoring and evaluation* kwa ajili ya kazi hii tu ya umeme wa REA kuhakikisha ya kwamba

wanaweza kuwasukuma wale *contractors* waliowapa kazi lakini na wenyewe pia waweze kutoa hela kwa wakati na kuwapa mikataba kwa wakati kuhakikisha kwamba miradi hii inaweze ikafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, na kwenye hilo kwangu kwa upande wa Geita Serikali ilituahidi kutupa umeme kwa kupitia njia ya *REA* katika maeneo ambayo yanaitwa ni mitaa lakini kihalisia ni kama vile vijiji sasa tunaiomba Serikali iweze kutukumbuka katika Kata za Ihanamilo, Kata za Shiloleli, Kata za Bungw'ang'oko na maeneo mengine yote kuhakikisha kwamba umeme unaweza ukapatikana na ripoti ya kamati imeonesha kwamba Geita iko chini ya asilimia 40 na sisi tunahitaji umeme katika maeneo hayo kwa hiyo, tunaomba walau tuweze kupata umeme kupitia njia hii ya *REA*. Ahsante sana nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jerome Bwanausi atafatiwa na Mheshimiwa Fredy Mwakibete Mheshimiwa Jerome, dakika tano tano

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia, kwenye bajeti hii ya Wizara ya Nishati, nianze pia kwa kumpongeza Waziri wa Nishati na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii. Waziri na Naibu wake wamekuwa wakizunguka nchi nzima na ziara zao zimekuwa na tija kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Jimbo langu kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri hivi karibuni amefanya ziara katika Jimbo langu la Lulindi kule Wilayani Masasi ziara ambayo imeleta matumaini mapya kwa wakazi wa Jimbo la Lulindi. Lakini nimuombe tu Mheshimiwa Waziri kuweka msisitizo kwa yale aliyoyasema alipokuwa Jimboni Lulindi na hasa pale alipotoa maelekezo kwamba vijiji vile takriban tisa ambavyo viko katika Jimbo langu ambavyo vimepitiwa na umeme kwa miaka mingi lakini havijashushwa *TANESCO* uliwaagiza wafanye hiyo kazi katika vijiji hivyo vya Dagaga, Mkangaula, Mpita, Guluni, Maugura

na vijiji vile vingine vyote ambavyo uliviainisha vikiwemo na cha Chanika ili kuhakikisha kwamba vijiji hivyo vipatiwe umeme haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Lakini pia nikumekupongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa jinsi ulivyotoa maelekezo kwamba maeneo ambayo tayari yana umeme, yasisubiri tena mpango mwingine wa REA hakikisheni wananchi lipeni walipie ili nguzo Serikali iwapelekee kwa kweli huu ni mpango mzuri na tunaupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naushauri Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na usambazaji wa umeme vijijini tunalo tatizo kubwa sana kwamba tunatakuwa kuwa na vijiji vingi sana tunavigusa lakini matokeo yake wakandarasi wanakwenda kuweka umeme katika kijiji robo tu ya kijiji na eneo lingine linabaki. Hili jambo linatuletea mgogoro mkubwa sana tunategemea kwenye REA awamu ya tatu mzunguko wa pili hili jambo liangaliwe sana kama tunakwenda kwenye kijiji tuhakikishe kijiji chote kinapewa umeme badala ya kuwekewa katika eneo dogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia suala la kuruka vijiji, kijiji kimoja kinapata kingine kinarukwa kingine hakipati hili jambo Mheshimiwa Waziri umelisisitiza sana lakini wakandarasi wamekuwa hawatekelezi kama vile unavyowaagiza.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho nimemsikia dada angu Mheshimiwa Peneza kuhusiana na mradi wa Rufiji mimi nilikuwa nadhani ingekuwa busara kwa sasa kwa upande wa wenzangu kule ndugu zangu kutouzungumzia sana juu ya kana kwamba huu mradi usitekelezwe Serikali imekwishaamua na katika ukurasa wa 23 wa hotuba ya Rais...

**SPIKA:** Mheshimiwa Upendo unaelimishwa huku!

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Upendo nilikuwa nasema kwamba hivi sasa si vizuri sana kupoteza nguvu kubwa sana kujadili jinsi gani huu mradi utatekelezwa Serikali imekwisha dhamiria, imeshasema haiyumbishi na

utatekeleza kwa wakati na historia jinsi mnavyoona sasa Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt John Pombe Magufuli inatekeleza kwa wakati miradi yake yote. Kwa hiyo, huu mradi hauyumbishwi na mtu wa ndani wala wa nje kutokana na hotuba ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ahsante sana umechelewa alishamaliza Mheshimiwa Fred Mwakidete, utafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudensiana Kikwembe dakika tano.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana kunipa fursa nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Awali ya yote kwanza nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa kibali kuwepo katika Bunge lako hili Tukufu. Lakini kipekee sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara hii ya Nishati na kwa Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako mmekuja Jimboni kwangu Busokelo na mlifanya mikutano hata saa mbili usiku ilibidi kufanya ili tu wananchi wa Jimbo la Busokelo wapate umeme. Katika hili nawapongeza sana kwa niaba ya wananchi wangu Jimbo la Busokelo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina machache katika Wizara hii ya Nishati kwa sababu kwenye awamu ya kwanza REA III mzunguko wa kwanza Jimbo langu lilipata vijiji 50 kati ya vijiji 56 na katika hivi vijiji 50 ni vijiji 42 ambavyo vimepewa kipaumbele katika awamu hii ya REA III, kwa hiyo nipongeze sana Serikali katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tumepata vijiji 42 kuna changamoto ambazo zimeambatana na

mkandarasi kwanza kwa kuviacha vile vijiji 8 ambapo Mheshimiwa Waziri ulipokuja ulitoa amri na kauli kwamba lazima atekeleze vyote pasipo kujali aina ya nyumba ya nyasi ama si ya nyasi ama ya bati kwamba vyote vinastahili vipewe umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ningependa kushauri katika jambo hili la kupeleka umeme katika huduma za jamii, kuna baadhi ya maeneo hasa hasa mashule, zahanati, hospitali, makanisa vimerukwa. Kwa hiyo, ningeomba katika awamu hii ambayo tunaingia mzunguko wa Awamu ya III wa REA viweze kupatiwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine mwenzangu ameshauri hapa kwamba kuna baadhi ya vitongoji hasa hasa umeme unapofika kwenye kijiji kimoja ambacho kina vitongoji vitano na kinafika kwenye kitongoji kimoja vitongoji vingine vyote vinne vinakuwa havijapata umeme hii inakuwa ni shida sana kwa wakazi jirani. Nafikiri katika mpango huu wa Awamu ya III mzunguko wa pili, ingefaa sana kwanza umeme unapofika kwenye kijiji basi na vitongoji vyake vyote viweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa kushauri ni suala hili la miundombinu hasa hasa baadhi ya wakandarasi wanapopeleka hizi nguzo katika baadhi ya vitongoji ama vijiji, wanaweka karibu sana na miundombinu ya barabara na wakati mwingine watu wa TARURA wanapotaka kuanza kutengeneza zile barabara wanashindwa kwa sababu tayari nguzo zimeshasimama karibu kabisa na barabara nafikiri kungekuwa kuna umuhimu wa kushirikisha taasisi na Wizara zingine hasa hasa Wakala wa Barabara Vijijini ili wawe na umbali kiasi fulani ambapo itawezesha hizo nguzo ziweze kuwekwa badala ya kuweka karibu sana na barabara na baadaye inakuwa gharama tena ya kuanza kuzitoa maeneo yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningependa kushauri suala la kukatika katika umeme Mkoa wa Mbeya na Wilaya zake zote ni miongoni mwa Mikoa ambayo umeme

unakatika mara kwa mara na hasa katika Wilaya za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mbeya Vijijini, Chunya, hadi Mbarali na hii yote ni kwa sababu ya miundombinu imechakaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba kwamba Mheshimiwa Waziri kwa sasa tuna teknolojia nyingi ya kusimika nguzo na kwa kuwa kule mvua nyingi zinanyesha karibia mwaka mzima na upepo unakuwa ni mwingi sana nafikiri tungetumia teknolojia ya kuweka nguzo ama nyaya kwa maana ya *underground* badala ya kuweka angani ambapo kila mara baada kupigwa na upepo ama ikipigwa na mvua ama na radi mvua umeme unakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine napenda kuzungumza suala la *TPDC, TPDC* ni shirika ambalo hakika mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma linafanya kazi nzuri na tumejionea sisi wajumbe namna ambavyo wameanza mchakato na kuona hata nyumba ambazo zinapata umeme kwa kupitia njia ya gesi. Pia tumeshuhudia hata magari ambayo yanatumia gesi ya Kitanzania, ambayo inachakatwa kule Mtwara. Kwa hiyo niwapongeza sana *TPDC* pamoja hata na wataalam ambao akinamama wapo pale ma-*engineer* na ni wazalendo Watanzania. Kwa hiyo niwapongeze sana uongozi wa *TPDC* pamoja na Kaimu Mtendaji Mkuu wa shirika hili.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo wanayo *TPDC* hasa hasa katika suala zima la gesi asilia ambapo baadhi ya taasisi zingine zinapewa fedha kwa ajili ya kutengeneza miradi yao, lakini wao wanapewa fedha kwa maana ya kutengeneza mradi ambao fedha baadaye itakuwa *claimed* na *TPDC.*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakibete.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, dakika tano na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, dakika tano.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Nishati. Kwanza kabisa napenda niwapongeze viongozi wa Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Kalemeni pamoja na watendaji wengine Wizara.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika ukurasa wa 44 katika hotuba ya Waziri ambao unaongelea mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *KV* 400, mradi ambao unaanzia Iringa unakuja kufika mpaka Nyakananzi na unatekelezwa kwa awamu tatu. Niwashukuru kwamba mradi huu umeweza kuwekwa hata kwenye mpango na katika kazi zilizofanyika 2018/2019 ni pamoja na upembuzi yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga na uthamini wa mali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa mradi huu umeshafanyiwa uthamini na upembuzi yakinifu, basi ni vema sasa wakatafuta huyo mkandarasi wa kuweza kuratibu mradi huu ili uweze kufanya kazi. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu umeme wanaotumia hasa kutoka tunduma mpaka Sumbawanga umeme ule mwingi unatoka Zambia na umekuwa ukikatika mara kwa mara. Sasa tuondoshe hii adha ya wananchi wa maeneo haya ambao ni pamoja na Jimboni kwangu Kavuu katika Kata ya Kibaoni ambapo pia wanatumia umeme huu ambao umekuwa ukikatika mara kwa mara na hivyo kuwafanya wananchi ambao wamejiajiri kupitia sekta hii kutoweza kufanya maendeleo yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi katika Kata yangu ya Kibaoni katika Jimbo la Kavuu. Naomba niongelee *transformer* ya Kijiji cha Mirumba, *transformer* hii imekuwa ni tatizo, kila leo nimekuwa nikisema. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja anieleze tatizo lipo wapi katika *transformer* katika Kijiji cha Mirumba ambayo inapokea umeme kutoka Sumbawanga kupeleka pale Kibaoni ambapo umekuwa ukikatika karibu kila siku, kila siku kwa kisingio cha *transformer*. Kwa hiyo niombe kama *transformer* hiyo ni mbovu naomba mbadilishe *transformer* pale ili

wananchi waendelee na shughuli zao za utekelezaji wa shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nije katika Mradi wa *REA* awamu hii, naishukuru sana Serikali kwa sababu wameweza sasa na sasa hivi ninavyoongea wakandarasi wapo kule jimboni kwangu katika Kata ya Majimoto na Kasaka wakiendelea na kuweka nguzo. Kwa hiyo niombe sasa katika vijiji vilivyorukwa katika Kata ya Kasansa, ambavyo nasema ni Iziwasungu, Majimoto kuna Kijiji cha Luchima ukija Mbede kuna Kijiji cha Kansisi ukija Mbede hapo hapo kuna kijiji cha Nyambwe ukija Kata ya Majimoto kuna Kijiji cha Lunguya; naomba vijiji hivi viingizwe kwenye mradi kwa sababu vimerukwa na vipo kwenye mradi. Waziri alipokuja tulipoenda Majimoto aliongea kwamba ni lazima vijiji vyote viingizwe na vitongoji vyake kwenye njia hii ya umeme wa *REA,* awamu ya tatu ili wananchi na sisi kule tupate kuona umeme, kwa sababu nitoka uhuru hatujaona mwanga wa taa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa na kazi ya huyo mkandarasi iwe kubwa kiasi kwamba wananchi wana hamu ya kuwekeza. Mheshimiwa amefika Majimoto, yeye mwenyewe anapapenda na anataka awekeze pale, kwa hiyo namwomba sasa, kasi pale ya kusambaza huo umeme wa *REA* iwe kwa kasi kubwa ili tuweze kuendelea na shughuli zetu za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuongelea suala la nguzo zinazowekwa na *TANESCO.* Unaenda kuomba kuwekewa umeme, *TANESCO* wanakuletea nguzo unalipia laki tatu mpaka laki tano, lakini kuna mwingine jirani atataka naye kuunganishwa umeme atatumia ile nguzo, zimekuwa zikileta matatizo hasa kwa wananchi huku kwenye maeneo ambapo naye anataka kuunganishiwa kwenye ile nguzo, kwa nini? Kwa sababu yule aliyeweka mwanzo naye anataka arudishiwe gharama.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa sababu tunalipa umeme kila mwezi, kwa nini nguzo hizi ziwekwe bure ili wananchi waweze kupata na kuweka umeme kwa urahisi,

kwa sababu hata hapa Dodoma wapo wanaoshindwa kuweka umeme kwa sababu tu ya gharama za nguzo. Kwa hiyo, niombe kama kweli tuna nia ya dhati na wananchi wetu wapate umeme basi wananchi nguzo ziwekwe bure kwa sababu tunalipia umeme. Kwa hiyo kama tunalipia naomba hizo nguzo ziwekwe bure.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda ni mchache, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu dakika tano

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana...

**SPIKA:** Atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami niungane na wenzangu wote kwamba nami natambua kazi inayofanywa na Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze sasa kwenye Wilaya yangu halafu baadaye nitaongea habari ya *Stiegler's Gorge* pamoja na fidia kuhusu gridi ya Taifa. Wilaya Hanang ina vijiji 96 na ni moja ya Wilaya mbili, Mbulu na Hanang ndio tulipewa vijiji vichache sana mwanzoni, baadaye nikaongea na Waziri akaongezea vijiji, lakini kuna vijiji 30 ndio vipo kwenye mpango wa kuletewa umeme, lakini spidi ni ndogo na bado 40 hawajui ni lini kwa sababu kuna ahadi ya Serikali lini vijiji vyote vitapata, nafikiri atafanya kila linalowezekana na bado ahadi yake ya tarehe 2 kwenda kwenda Hanang pamoja name ipo pale ili tukaangalie matatizo ya Vijiji vya Hanang. Naomba sana spidi ya *contractor* iangaliwe.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu Gridi ya Taifa, kuna maeneo ambayo gridi ya Taifa imepita na wameahidiwa wapate fidia na wanalia kila siku hasa vijiji, hivyo naomba sana fidia ile iweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye *Stiegler's Gorge* mimi ni moja kati ya watu mbao tunafurahi sana mradi wa huu unatekelezwa katika nchi hii. Na sisi wote humu ndani tunajua chanzo cha maji kwa umeme ndio chanzo ambacho kina gharama ndogo na hatimaye bei ya umeme itakuwa ndogo na ndio itakayochochea viwanda nchi hii. Kwa hiyo namshukuru sana Rais na ninashukuru Serikali nzima kujielekeza kwenye *Stiegler's Gorge* jambo ambalo kwa kweli litawafanya wananchi wa Tanzania wapate umeme ambao sio ghali.

Mheshimiwa Spika, nataka niwambie wale ambao hawaelewi vyanzo vyote ni vyetu vya gesi vya jua vya maji na hata ile *nuclear* bado ni chanzo chetu tunacho, ni lazima tuchague vyanzo vile ambavyo tukianza navyo vitatuletea manufaa makubwa na *Stiegler's Gorge* ni mahali ambapo tutapata kweli gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati *NGO's* zikipiga kelele kwa ajili ya *Stiegler's Gorge* isitumiwe kama chanzo cha umeme walikuwa wanaongelea chura, jamani utalinganisha chura na wananchi? Haiwezekani! Namshukuru sana Rais huyu kwa kuwa imara na kuwa na ujasiri wa kukataa mambo ambayo hayana sababu na wengine wote humu ambao wanawaunga mkono wale watu kwa sababu zingine mbalimbali, naomba tuwe pamoja kwa hili kwa sababu ni manufaa ya Taifa hili la Tanzania, tumpe moyo Rais wetu na Waziri wetu ili waweze kukazania na hata kama hela itachukuliwa mahali pengine kwa manufaa ya sekta zote tusiwe na malalamiko ili tuwe tunapitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, watu wa Hanang wanaomba Mradi wa *REA,* wanufaike nao kama wilaya zingine zinavyonufaika na wale ambao hawapata fidia waweze kupata fidia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa moyo wangu wote bajeti hii ya Waziri Kalemani na Serikali hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Suleman Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ili nami niweze....

**SPIKA:** Dakika tano, tano.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa nichukue fursa hii niungane na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Kalemani na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu, kwa sababu hawa ni Mawaziri ambao wanasikiliza Wabunge na wanachukua hatua kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia bomba la mafuta ambalo linalotoka Uganda mpaka Tanga. Katika bomba lote hili la mafuta jimboni kwangu Kata ya Igusule, Kijiji cha Sojo ndipo itajengwa kambi na kituo kikubwa cha kuyafunika mabomba ili yasipate kutu na kuweza kuzuia joto mabomba yote ya njia nzima *coating* itafanyika pale Igusule ambapo ndio kijiji kwangu.

Mheshimiwa Spika, shughuli ya kujenga hiki kituo pale kijijini itaingiza bilioni 600. Ni shughuli kubwa sana bilioni 600 zitaingia pale. Sasa hoja yangu hapa ni *local content,* ni namna gani wananchi, Watanzania wa Kijiji cha Igusule, Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega na Watanzania wote watanufaika na huu uwekezaji wa hizi bilioni 600.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Wizara tuna Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 ambayo ina kipengele cha ushirikishwaji wa wananchi, ningeomba Wizara ijipange kutumia sheria hii ili kwa makusudi kuwa na mpango wa makusudi wa kusaidia Watanzania hasa wa Jimbo la Bukene pale Igusule kuhakikisha kwamba wananufaika na hizi bilioni 600. Hivyo, lazima kuwa na mpango wa makusudi, kwa hivyo watu wa maeneo yale lazima tujue kazi zitafanyika pale, kazi

za ujuzi, kazi za ujuzi wa kawaida, vibarua, huduma mbalimbali ambazo zitatolewa pale na Serikali imejipangaje ili kuwasaidia kwa makusudi watu wa maeneo yale waweze kufaidika na uwekezaji wa bilioni 600.

Mheshimiwa Spika, hili jambo tukiliacha hivi hivi, Watanzania wananchi wa Nzega, wananchi wa Jimbo la Bukene tukiacha hivi hivi bila hatua za makusudi, tunaweza tukajikuta bilioni 600 zimewekezwa pale mradi ukaisha, lakini ukipima manufaa ya wananchi wa pale utakuta kwamba hawajanufaika chochote. Tunachohitaji watu wa pale ni kwamba, hali za maisha za wananchi wa maeneo yale ambapo bilioni 600 zitawekezwa Igusule, Jimbo zima la Bukene na Wilaya nzima ya Nzega hali zao za maisha baada ya uwekezaji wa bilioni 600 ni lazima zibadilike zi-*reflect* kweli kuna bilioni 600 ziliingia, *otherwise* kutakuwa hakuna manufaa yoyote ya bilioni 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ushauri wangu kwa Wizara hapa ni kwamba, lazima kuwe na mpango wa makusudi, hapa na-*underline* neno makusudi; mpango wa makusudi, ukiacha kama ilivyo wananchi kwa kweli bila kusaidiwa, bila kuwa na mpango maalum, tutashangaa bilioni 600 zimewekezwa, lakini wanaweza wakaja watu ambao sio Watanzania, wajanja wengine ndio wakanufaika zao. Kwa hiyo lazima tulindwe, tuwe *protected* ili tuweze kunufaika na hizi.

Mheshimiwa Spika, hili la Miradi ya *REA* limeongelewa na Wabunge wengi, kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba natambua jitihada za Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani na Naibu wake katika kuwasukuma wakandarasi ili waweze kutimiza majukumu yao lakini pamoja na jitihada hizi bado wakandarasi wanasuasua katika maeneo mengi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwamba mwishoni wakati Mheshimiwa Waziri ana-*wind-up* atueleze ili tujue tatizo ni wakandarasi au tatizo ni Wizara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa atafuatiwa na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na baadaye Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Awali kabisa niungane na Waheshimiwa Wabunge walioongea kumpa pongezi sana Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wameendelea kuifanya katika sekta hii. Pia nampongeza Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Nishati kuendelea kufanya kazi nzuri ya kulijenga Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa Mradi wa *Stiegler's* kwa kweli mradi huu ni mradi wa maendeleo na mkombozi sana wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii yetu. *Megawatts* zile 2,115 zitatuchangia sana katika kuendeleza huduma ya maji, huduma ya afya, huduma za kielimu, viwanda, *standard gauge*, reli na kadhalika. Kwa kuzingatia lengo ni *megawatts* 10,000 ifikapo mwaka 2025 ni kwamba Mheshimiwa Waziri ajitahidi mapema hata kabla ya miaka mitatu kwa sababu tunahitaji bado *Megawatts* nyingi sana kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia kwa niaba ya Mkoa wa Pwani kama sisi wenyeji wa mradi huu kwa kweli tumeupekea kwa mikono miwili na tutajitahidi kwa kila hali kuhakikisha kwamba unafanikiwa na madhara yoyote yanaweza kujitokeza ya kimazingira bila shaka Tanzania tunao watalamu wetu wazuri ambao watajipanga kwa ajili ya kudhibiti madhara yoyote ya kimazingira.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia ahadi zile ambazo zinatolewa kwa ajili ya kupeleka umeme vijiji na maeneo yote yanaahidiwa kupelekewa umeme vijijini ni vizuri sana tukatekeleza ahadi hizo Waswahili wanasema ahadi ni deni. Katika Jimbo la Bagamoyo, Kijiji cha Kondo kilikuwa katika Mradi wa *REA* awamu ya pili mpaka Juni, 2016, mradi ulipomalizika kutekelezwa. Katika *REA,* awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza mpakaleo hicho kijiji hakimo kabisa na wala hatujui lini kitatekelezwa. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri aliahidi hapa Bungeni kwamba miradi yote ambayo itakuwa haijatekelekezwa katika awamu ya pili, basi itapewa kipaumbele katika awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, Sasa hili ni jambo ambalo kulitekeleza ni muhimu sana kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri na wananchi wakiwa wamesubiri tangu 2013, awamu ya pili ya *REA* mpaka leo 2019 wanasubiri, hata Mbunge akizungumza namna gani wanamwona tu kama anapiga maneno hana kitu cha kweli ambacho anaendelea kukisema. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri aendelee na ahadi yake ile ile ya *first in first out.* Waliokuwa kwenye awamu ya pili wapate na nisisitize katika awamu ya tatu waanze wao kutekelezewa kabla ya wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri kwamba kwa ufanisi wa miradi hii ya umeme vijiji basi *REA* izingatie mapendekezo ya Wabunge ambayo yanawasilishwa kwa utaratibu ambao umewekwa kwa maana kupitia katika ofisi za *TANESCO* Wilaya na *TANESCO* mikoa. Baada ya hapo inapelekwa *REA* lakini wasifanye vinginvyo. Katika Jimbo vya Bagamoyo vitongoji saba katika Kata ya Dunda vimeorodhesha katika awamu tatu ya *REA* ambavyo vyenyewe vina umeme, hakuna mahali pa kuweka umeme na havikupendekezwa na *TANESCO* Wilaya wala havikupendekezwa na *TANESCO* Mkoa, vimekuja namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nawaomba wataalam wa *REA* wawe wanaangalia mapendekezo ya Wabunge na hasa yale ambayo yamepita katika taratibu zilizowekwa na

hiyo ndio dira ya kutekeleza miradi hiyo isiwe wanachomekea chochote ambacho wamekipenda hata ambapo umeme upo hakuna shida yoyote wananchi wenyewe wanashangaa. Vile vitongoji ni vya Mjini Bagamoyo, hakuna nyumba ambayho haina umeme, vikawekwa mle. Kwa hiyo haina tija, badala yake tunahangaika kutoa *scope* mahali pamoja kupeleka sehemu nyingine katika hali nzito sana.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizi kwa kusema kwamba tunapotekeleza miradi hiii katika vijiji basi msisitizo uwe, Kijiji kile ikiwezekana basi kiwekewe kwa ujumla wake badala ya kuweka vijiji kwa mfano katika Jimbo langu, Kata ya Yombo, Kijiji cha Matimbwa kimewekewa umeme, lakini siyo kijiji chote, vitongoji kadhaa havina umeme, Kongo kadhalika. Kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo linafaa liangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vedasto Ngombale dakika tano pia, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Mtolea dakika tano.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, shukrani kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri na Naibu Waziri, mnafanya kazi nzuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitajikita zaidi katika maeneo ambayo yana tatizo kubwa sana, hasa kwenye suala zima la fidia. Wakati wa utekelezaji wa mradi wa gesi pale katika Kituo cha Somanga Fungu, walipokuwa wanapeleka umeme maeneo ya Rufiji na Ikwiriri wakati wa ujenzi wa njia ile ya umeme *TANESCO* ilifanya fidia kwa wananchi, lakini ilipofika katika Kijiji cha Somanga walifanya fidia na wakawasahau wananchi tisa.

Mheshimiwa Spika, Nimekuwa nikifuatilia fidia ya wananchi hawa mpaka leo haijapatikana, naomba

niwataje. Kuna mwananchi anaitwa Mohamed Mtombwane, Amir A. Mtauka, Athuman Kiwanga, Mpara, Mwinchande Mtauka, Yusuph Masendela, Ally Gumbi, Athuman Mchoro na Rashid Matana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hawa wananchi wananikera sana na suala hili mara nyingi nakuwa nawasiliana na watu wa *TANESCO* lakini mpaka sasa fidia zao hazijalipwa, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja basi awaone hawa wananchi, ni muhimu sana hawa wananchi walisahaulika.

Mheshimiwa Spika, lingine, wakati wa utekelezaji wa mradi huo huo, kuna eneo *TANESCO* walichukua pale Somanga Fungu, kulikuwa kuna eneo la wananchi lakini kuna eneo lilitambulika kama eneo la Kijiji, *TANESCO* ilifanya tathmini na ikaja kufidia. Wakati inakuja kufidia kwa bahati mbaya sana wananchi wakasema hapana lile eneo siyo la Kijiji ni la wananchi na wakajitokeza wananchi 63. Wakati hilo linafanyika tayari *cheque* ilishakuwa imeandaliwa, kukawa na mvutano matokeo yake zile pesa zikawa zimerudi tena *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Nimefuatilia sana tangu mwaka 2015 mpaka sasa wananchi 63 hawajapata fidia ya yale maeneo na maeneo yale yameshatumiwa na *TANESCO*. Kwa hiyo naomba sana, wananchi hawa fidia hizo wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie suala la mradi huu sasa kilovoti 400 ambao sasa unaendelea. Mradi huu una malalamiko makubwa sana hasa maeneo ya Somanga. Ifahamike eneo la Somanga ndilo eneo la kwanza ambalo limeanza kutoa umeme wa gesi kutokea Songosongo; lakini katika hali isiyoeleweka Mradi huu wa kilovoti 400 unafanyiwa tathmini na tayari asilimia 79 ya watu wameshaanza kulipwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni wa Somanga fungu Kinyerezi, lakini *TANESCO* wameanza kulipa Kinyerezi na bado hawaja walipa watu wa Somanga ambako gesi yenyewe imetoka, sasa kuna maneno ambayo hayapendezi maana

wale wananchi wananiuliza kwani sisi TANESCO wanatuona malofa au kwa kuwa tuko Kilwa, kwa nini, waanze kuwalipa watu wa Dar es Salaam na siyo sisi ambako gesi yenyewe ndiyo imeanza kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tumefatilia sana na sasa ni kama mwaka wa nne, mlichukua maeneo yao, wanashindwa kufanya shughuli za Kilimo, lakini bado hamtaki kufanya fidia, nikuombe Mheshimiwa Waziri utakapokuja basi uje na maneno yenye faraja kwa ajili ya malipo ya wale watu wa Somanga ambao wao ndiyo nafikiri ilipaswa wawe watu wa kwanza kufidiwa na si watu wa Kinyerezi kama ambavyo mlifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jingine, nijielekeze sasa kwenye suala zima la *REA*, naomba katika awamu hiyo sasa inayokuja basi TANESCO waangalie Kata ya Kandawale, Kata ya Kandawale, Kata nzima haijapata umeme ina vijiji vinne kuna Kijiji cha Kandawale, Mpopela, Ngarambi na Namatewa, lakini katika Kata ya Miguruwe kuna Kijiji cha Zinga, Kibaoni, Mtepela na Kingombe hawajapata umeme, lakini waangalie pia Kijiji cha Mwengei, Mkarango, Namakoro, na Nambondo havijapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jingine ambalo ningesema ni suala zima la ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea pale Kilwa Masoko. Inashangaza katika bajeti zilizokuwa zinapita taarifa za ujenzi wa Kiwanda tulikuwa tunaona katika hotuba ya Waziri, lakini katika hali ya kushangaza mwaka huu hatujaona chochote hakijasemwa chochote. Sasa Mheshimiwa Waziri awe wazi tu katika aina hii ya gesi tuliyoipata, maana sisi tumepata gesi kavu, gesi ambayo haija-*associate* na mafuta, je upo uwezekano wa kujenga Kiwanda cha mbolea ambacho kitakuwa kina manufaa, naomba Waziri aje atueleze hili kuliko kuwa tumebaki na matumaini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa *LAAC* nakushukuru, Mheshimiwa Abdallah Mtolea dakika tano.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, na nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini hata hivyo na mimi nisijifanye kuwa mpofu wa kutoona kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, pamoja na timu nzima ya Wizara hii ya kuhakikisha wanaitoa Tanzania gizani na kuiweka kwenye mwanga safi wa umeme, tena umeme ulio nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara na Serikali kwa ujumla, changamoto huwa haziishi, na kwa dakika hizi chache nilipenda niwasilishe changamoto ya kukatika katika kwa umeme katika Jiji la Dar Es Salaam.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kero kubwa hata baada ya ile ya migao ya kawaida kumalizika, migao ile ya umeme tuliyoizoea miaka ya nyuma, bado Dar Es Salaam kumekuwa na tatizo la kukatika katika kwa umeme. Ni ngumu sana ukae siku nne mfululizo bila kusikia umeme umekatika. Niliwahi kuuliza maswali hapa mara kadhaa, Mheshimiwa Waziri mwanzo alisema kwamba kwa kesi ya Temeke wanajenga *substation* nyingine Mbagala na Kurasini ambazo zitaondoa tatizo hili. Hata hivyo, Substation ya Mbagala ilimalizika na ndani ya mwezi mmoja tu ikawa tayari imeshazidiwa. Sasa hivi ukiuliza wanasema kwamba tunasubiri *Substation* ya Kurasini ambayo ilikuwa imelenga kusaidia watu wa Kurasini na watu wa Kigamboni; sasa maana yake ni kwamba bado hatujapata dawa ya kulitatua tatizo hili, na Dar Es Salaam ndilo soko kubwa la umeme ambao *TANESCO* wanaouza.

Mheshimiwa Spika, utagundua kwamba sasa hivi kuna *megawatt* 600 kati ya *megawatt* 1,600 zipo Dar Es Salaam. Sasa kama watumiaji wenyewe bado wanaendelea ku-*experience* kukatikakatika kwa umeme maana yake kuna tatizo la msingi ambalo ni lazima Wizara ije na mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba inakwenda kulitibu. Ukipiga simu kwenye vituo hivyo vya *TANESCO* wanakwambia kwamba eneo hilo umeme unakatikakatika kwa sababu *Transformer* imezidiwa, huko kwa sababu kuna nguzo imedondoka; tafsiri yake ni nini? Ama hatujui tuna idadi gani ya wateja

wanaohitaji umeme Dar es Salaam na je, ongezeko la wateja katika Jiji la Dar es Salaam ni wangapi kwa mwaka? Ili tunapoweka *Transformer* iweze angalau kuhimili ongezeko hilo la wateja angalau kwa miaka miwili mitatu; sasa badala yake kila kitu kimezidiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini uchakavu wa hizo nguzo na miundombinu yote ya umeme katika Jiji la Dar Es Salaam ni tatizo. Kwa hiyo ni vizuri Wizara wakati inafanya kazi nzuri ya kuongeza umeme na kusambaza katika mikoa mingine pia iwe na mpango wa kuhakikisha kwamba itanarabati miundombinu ya kusambazia umeme kwenda kwa wateja katika Jiji la Dar Es Salaam, ili wateja wa Dar Es Salaam waiingizie fedha nyingi *TANESCO;* kwa sababu kwa uwekezaji huu mkubwa ambao Wizara na Serikali unaifanya ni lazima *TANESCO* ifanye kazi kibiashara, kuuza umeme kibiashara, ili ipate faida kwa sababu hatimaye mtakuwa na jukumu la kuilea hiyo miundombinu yote ambayo leo inajengwa.

Mheshimiwa Spika, sasa msipofanya kazi kibiashara na mkatengeneza faida, mkaliachia soko lenu liwe linapoteza mapato maana yake na ninyi pia mnapoteza; kwa sababu umeme unapokatika Dar Es Salaam, kwenye eneo lolote hata kwa nusu saa tu maana yake na *TANESCO* mnapoteza kwa sababu umeme utakuwa hautembei. Kwa hiyo zile gharama zitakuwa haziongezeki, Kwa hiyo ni vizuri mkaliangalia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ningependa mpango madhubuti kabisa wa kuhakikisha tunakwenda kulitatua tatizo la kukatikakatika kwa umeme Dar Es Salaam. Tunapokuwa na umeme wa ziada kwamba tuna umeme mwingi tuliozalisha kuliko tunaoutumia, lakini kama bado umeme huku unakatika katika wananchi hawawezi kuona hicho tunachokizungumza; kwa sababu kama kweli tuna umeme wa kutosha kwa nini basi unakatika katika?

Kwa hiyo hizi sababu ndogo ndogo, za miundombinu za *Transformer*, tuhakikishe tunazimaliza ili watu waendelee kuutumia umeme, tena umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtolea. Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana...

**SPIKA:** Ajiandae Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze hotuba ya Kambi ya Upinzani ambayo imejaribu kurejea mambo mbalimbali ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Wizara hii ili waweze kuyafanyia kazi mambo ambayo yametolewa kama ushauri na mambo ambayo wameweza kuyaainisha kama sehemu zenye kasoro ndani ya Idara mbalimbali za Wizara hii. Pia nipongeze hotuba ya Kamati ambayo pia imeainisha mambo mbalimbali ambayo yanapaswa kuzingatiwa na Wizara hii ambayo bajeti yake tunaijadili.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia, kwa ufupi kabisa kutoa pole kwa wananchi wa Manispaa ya Bukoba ambao wamepatwa na dhahma ya mafuriko na ambapo mpaka sasa hawajaweza kukaa sawa. Ninaamini kwamba Wizara hii itajaribu kurudisha kwa kasi sana miundombinu ambayo ya umeme ambayo imeharibiwa na mafuriko haya ili watu waweze kurejea katika hali iliyo salama na kuendelea kutumia nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Katika tamko la Serikali ambalo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa aliainisha bayana kwamba Serikali inatoa ushauri na msukumo wananchi waanze kuhama katika maeneo mengi ya Mji wa Bukoba kwenda katika maeneo ya Vijiji Mji, ambavyo ni Nyanga, Kahololo, kuna Vijiji vya Ijuga Nyondo, Kibeta na Kagondo. Vijiji hivi, kama ambavyo nimekuwa nikieleza huko siku za nyuma, na Mheshimiwa Waziri anajua, sehemu nyingi hazina umeme. Sasa kama *alternatively* ya kukimbia mafuriko imekuwa kwenda kwenye vijiji hivi naomba huu mpango wa kuweka umeme kwenye

Vijiji Mji uweze kufanyika kwa haraka katika Mji wa Bukoba ili watu waweze kupata huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mambo mbalimbali ambayo yameshauriwa katika hotuba ya Kambi ya Upinzani na Kamati ya Nishati ningeomba kutoa ushauri kwa mambo mbalimbali yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa REA ni miongoni mwa Miradi ambayo inapata fedha, au ina vyanzo vya uhakika vya kupata fedha. Lakini pamoja na uhakika wa vyanzo hivi tumeona kupitia katika hotuba hususani ya Kambi Rasmi ya Upinzani figisu zinazojitokeza hasa za matumizi mabaya au usimamizi mbaya wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimejikita zaidi kuangalia tatizo linaweza likawa nini. Mimi binafsi sikubaliani na mfumo wa usimamizi wa fedha unaotumika ndani ya *REA*. Kuifanya *TANESCO* kuwa mshauri au kuwa *consultant* wa hii Miradi ya *REA* ni jambo kidogo ambalo mimi nafikiri linakosesha *transparency* inayopaswa kufanyika kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ni vyema *REA* ikawa na ma-*consultant,* ikatangazwa nafasi ya *consultant,* kazi za *consultant,* ili *TANESCO* ambayo kimsingi nayo unakuta kuna wakati inakuwa ni Kampuni shindani kwenye baadhi ya Miradi, lakini pia ni Kampuni ambayo inakuja kurithi Miradi ya *REA*; unapomfanya ni *consultant* mimi naamini unatoa nafasi ya baadhi ya mambo kufukiwa ndani kwa ndani na hata kufanya kazi ya *trace,* hata kama pesa imekuwa *misused* inakuwa ni kazi ngumu kwa sababu msimamizi ni yule yule, huyo huyo anachukua *contract* na anashindana na Kampuni nyingine. Hata wakati mwingine tumnapata taarifa kwamba nguzo ambazo *TANESCO* kama *consultant* anazikataa wakandarasi wasizitumie yeye anapokuja kufanya kazi yeye anatumia nguzo hizo hizo wakati ambapo anakuwa amezikataa kwa wakandarasi binafsi; hii ni *double standard.* Mimi ushauri wangu ni huo; kwamba kwa kweli ifike mahala hizi kazi wapewe ma-*consultant* ili *TANESCO* naye asimamiwe badala ya kuwasimamia watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala ambalo limezungumzwa katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ambapo mara nyingi Wizara au taarifa mbalimbali zinazotolewa na Kampuni za *TANESCO*, *REA* wamekuwa wanatumia kigezo cha kijiji usambazaji wa umeme kwa kigezo cha vijiji. Kama Kambi ilivyo shauri, ni vyema tukaanza kutumia kaya, Maana katika maeneo mengi tunaambiwa vijiji kadhaa vimepewa umeme au vimesambaziwa umeme lakini ukienda kwa uhakika unakuta kuna vitongoji vingi mno, vinakuwa havijapewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta kwenye kijiji ziko kaya kama 30, 40 lakini maeneo mengine ya vijiji, tukija hapa Bungeni tunaambiwa takwimu chungu nzima ya vijiji kwamba vimepata umeme; hii tunakuwa tunajitekenya na kucheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu imekuwa inaomba sana kukutana na wakandarasi ili waeleze maeneo wanayokwama, lakini imekuwa kizungumkuti, sasa nitaomba kujua kupitia kwa Waziri wakati ana-*windup;* tatizo liko wapi kwa Kamati kukutana na Wakandarasi? Kunafichwa nini la kutukutanisha na Wakandarasi hawa? Maana kukutana nao kutatupa picha wanakwama wapi au wanakwamishwa wapi na Serikali. Hata hivyo na wakandarasi wenyewe nasikia nao wanatishwa juu ya suala la kukutana na Kamati, wengine wanaogopa hata kukutana na Kamati kwasababu wanahisi wanaweza wakakosa hata tenda pindi wakija kuomba. Sasa ili tuwe wawazi mimi nafikiri mchakato wa kukutana na Wakandarasi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, Suala la tano, gharama za kuunganisha umeme. Tulipokuwa kwenye Kamati, Waziri alizungumza bayana kabisa, kwamba kuunganisha umeme wa REA pamoja na ile miradi inayorithiwa na *TANESCO* unapaswa kutozwa 27,000, ndicho kiwango kinachopaswa kutolewa. Ili kuweka mambo bayana mezani tulimuomba Waziri na akaahidi kwamba utatolewa waraka ambao utagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kipindi hiki cha bajeti waondoke nao kwenda kuwaelewesha na

kuwafahamisha wananchi kwamba wasitozwe pesa zaidi ya 27,000. Mheshimiwa Waziri tutaomba waraka huo utoke kwa sababu ni ahadi yako, ili watu tuondoke nao twende nao huko na kuufahamisha Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwisho ni Kuhusu Miradi Mikubwa. Ifike mahala Bunge linapokuwa linajadili mambo tuweke *binding* ya kutopindua maneno yetu. Nilikwenda *library* kusoma *Hansard* ya mwaka 2013/2014 baadhi ya Wabunge walioko humu ndio walishadadia gesi, kwamba gesi sasa tumepata biashara imekwisha mkombozi wetu ni gesi, na baadhi ya Wabunge wako humu, akiwemo na kaka yangu Mwijage. Leo hii wamehama wanakuja kwenye *Stiegler's Gorge*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mimi naomba Bunge lijiwekee utaratibu wa kuweka binding ya maneno ambayo tunakuwa tumepitisha na kushadadia badala ya kuwa tunaokota huku tunakuja huku, kesho kutwa tunaokota hili tunakuja hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana, bado nina dakika kama tatu nne, Mheshimiwa Deo Ngalawa kwa dakika tatu.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja iliyoko mezani. Kwanza niishukuru Serikali, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu, Katibu Mkuu na Idara zote zilizopo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipende kutoa pongezi kwa Taasisi ya *REA*, kwa kweli kazi inayofanywa ni kazi nzuri na tunaiona. Nakini nipende kusema kwamba kwa Ludewa bado mkandarasi hafanyi vizuri sana kwa sababu mpaka sasa ni kijiji kimoja tu ndicho kimewashwa. Kwa hiyo ninaamini kwamba kwa jitihada za Mheshimiwa Waziri na Mtendaji na Mkuu wa *REA* kadiri tunavyokuwa tunazidi kuwasiliana

ninaamini kwamba sasa hivi mkandarasi atajiweka sawa na kuweza kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuongelewa vyanzo vya nishati, hasa umeme. Tumeona kuna umeme wa maji, kuna umeme wa gesi, kuna umeme wa makaa ya mawe, upepo na jotoardhi; nianze na maji. Tunavyo vyanzo vingi sana vya maji na hasa hata kwetu kule Ludewa tuna mito mingi sana ambayo inamwaga maji ziwa nyasa na inaweza ikawa ni miongoni mwa vyanzo vizuri vya umeme.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo ningeomba sasa Wizara ijipange na iweke *master plan* ya maeneo yote ambayo yanaweza kuwa ndiyo chanzo kikubwa cha umeme wa maji ambao ndio unaonekana ni rahisi. Kwa hiyo kuna haja sasa Serikali ikaweka mpango mkubwa na tuweze kuona ni namna gani tunaweza tuka-*meet* zile *megawatt* 10,000 ambazo Serikali imezipania**.** *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, tunao umeme wa makaa ya mawe na hata nchi nyingi sasa hivi, *including* Marekani inaanza kutumia umeme wa makaa ya mawe. Tunayo makaa ya mawe pale Mchuchuma ambayo yanaweza yakatoa *megawatts* 600. Kwa hiyo, naamini kwamba Serikali ikijipanga vizuri, ikachukua na kuanzisha utaratibu mzuri wa kuweza ku- *tap* yale makaa ya mawe pale bado Serikali na nchi itaweza kufaidika kwa kiasi kikubwa na tukawa na umeme wa kutosheleza kwa sababu tayari tumejipanga kwamba Serikali na nchi imejipanga katika mfumo wa viwanda na viwanda vinahitaji umeme. Kwa hiyo kuna haja sasa makaa ya mawe kule Mchuchuma yakawa ni moja kati ya *resourceful* ya kuweza kufikia hizi megawati 10,000.

Mheshimiwa Spika, lengo letu kufika 2025 ni kuwa na megawati 10,000 sasa labda pengine nijaribu kuangalia mpango ukoje wa Serikali ili kuweza kufikia hizo megawati 10,000 tunazoziendea, kwa sababu naamini kwamba tuna ile mipango ya kufikia ule muda wenyewe na kuna ile mipango ya mwaka mmoja mmoja na kuna ile mipango ya

kati. Sasa Serikali ije na majibu tuone kwamba mpaka sasa kwa mwaka huu ni...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia Wizara ya Nishati, lakini zaidi sana nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukupongeza sana, unapokaa kwenye kiti chako Bunge linaendeshwa kisayansi na linaendeshwa kwa utulivu mkubwa sana. Wabunge tunaheshimiana na kuthamini kila mchango wa Mbunge anayesimama na hivi ndivyo inavyotakiwa iwe hata kwa wenzako wengine wote unaowaachia nafasi ya kiti wanatakiwa kwa kweli kulinda heshima ya Bunge na hasa pale Mbunge anaposimama na kutoa mawazo yake ambayo pengine wewe unaona kwako hayakufurahishi lakini ni lazima umpe nafasi ya kumsikiliza na zogo la Bunge la juzi halikuwa jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitoe pongezi sana kwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Mendrard Chanancha Matogolo Kalemani pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu pamoja na Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara. Watu hawa wanafanya kazi kubwa ya kuzunguka nchi nzima, lakini kubwa zaidi kwao hawa wawili ni mahusiano mazuri na Waheshimiwa Wabunge. Hili ni jambo zuri sana, lazima kujenga *PR* ya pamoja maana hii kazi ni ngumu, kazi inahitaji ushirikishwaji na ushirikiano wa karibu.

Mheshimiwa Spika, vilevile spidi ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake naiona ni kubwa kuliko spidi ya makandarasi, yaani Waziri anagawa umeme kwa spidi sana kuliko wajenzi, kama ni *forward* wakati mwingine unasema inaweza ikaingia

kwenye nyavu yenyewe ikaacha mpira nje, sasa kidogo hapo inatupa mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Jimbo la Mtera katika tarafa zangu tatu, Tarafa ya Mvumi Mission, Tarafa ya Makangwa na Tarafa ya Mpwayungu. Tunavyo vijiji ambavyo bado havijafikiwa umeme, lakini kama unavyojua ukijua kulaumu ujue na kushukuru. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufikisha umeme kwa mara ya kwanza katika Tarafa ya Mpwayungu katika Kijiji cha Nagulo na Kijiji cha Mpwayungu chenyewe.

Nimwombe sana vile vitongoji anavyovitaja, vijiji anavyovitaja kwamba umeme hautamruka mtu, wale watu wanaorukwa wote kimbilio lao ni kwa Mbunge. Kwa hiyo unajikuta Mbunge anafanya kazi kubwa sana baada ya Waziri kuondoka, wakisema mbona Waziri alisema tusirukwe, sasa kwa nini tunarukwa. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na timu nzima washughulike kwa namna ya pekee kuhakikisha kwamba yale maeneo waliyoagiza maagizo yao yanatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ukisoma ilani za hivi vyama ambavyo vina Wabunge humu unaweza ukacheka sana. Nimepitia ilani ya CHADEMA hapa sioni mahali wameahidi megawati 18,000 alizokuwa anazisema mzungumzaji wa CHADEMA, kwa hiyo unaweza ukaona wakati mwingine maneno haya yanayozungumzwa ni maneno ya kufurahisha tu Bunge. Unajua faida kwenye uongozi wa nchi wakati mwingine haionekani moja kwa moja...

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa Mheshimiwa Lusinde taarifa kwamba wakati Mheshimiwa Silinde anachangia alisema trilioni sita ambazo zinatarajiwa kujenga *Stiegler's Gorge* zikilinganishwa na *extension one* ya Kinyerezi ambayo inajengwa kwa bilioni 60

ambazo ni megawati 185 *equivalent* yake ni ya kujenga megawati 18,500, hakusema inatokana na Ilani ya CHADEMA.

**SPIKA:** Mzungumzaji pia hajasema hivyo kama inatokana ameuliza tu kwenye ilani yenu hakuona. Endelea Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, shemeji yangu Matiko nataka nimsaidie tu kwamba unajua wakati mwingine faida kwenye shughuli za Serikali haifananishwi na faida ya genge la nyanya au pengine mgahawa. Huwezi ukaiona moja kwa moja wakati mwingine unaona *MSD* wananunua dawa nyingi mpaka zile za ugonjwa wa *Ebola,* sio mpaka wasubiri ugonjwa uwepo ndio wanunue.

Kwa hiyo, wakati mwingine tunasema kwa nini dawa zina-*expire* zina-*expire* kwa sababu zilikuwepo na ugonjwa haukutokea, sasa huwezi ukangoja mpaka utokee ndio uanze kununua. Kwa hiyo kuongoza Serikali tunawafundisha tu, ni mambo makubwa sana, huwezi kufananisha na biashara ya genge au mama ntilie, kwa hiyo kuna faida unaweza ukazitafuta kwa macho usizione.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia sana kuhusu kuwabana wakandarasi ili waendelee kusambaza umeme katika vijiji vyote. Tumeona namna ambavyo...

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde unapewa taarifa na Mheshimiwa Getere.

**MHE.BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba CHADEMA katika miaka ijayo itakapokuwa kwenye madaraka tutahakikisha tunafanya utafiti wa kina kuhusu vyanzo mbalimbali vya nishati hatimaye kutunga sera ya kupata nishati hizo. Kwa taarifa kamili ni kwamba mpaka leo CHADEMA haina chanzo cha nishati, kwa hiyo anachosema Silinde ni sawa tu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde, tafadhali.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nimesema kuongoza nchi faida zake ni wananchi kunufaika. Sisi Rais wetu na Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kujitoa muhanga kujenga kinu cha kufua umeme katika maporomoko ya Rufiji. Haya ni maamuzi makubwa ambayo *impact* yake itaonekana wakati Watanzania watakapoanza kunufaika na ndio maana hakuna Mbunge humu ndani anayesimama na kusema umeme huo nisipewe humwoni. Kwa hiyo ni kweli kwamba Serikali imepatia na iendelee kujenga huo umeme ambao utatunufaisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa kwenye vijiji ambavyo vilikuwa vimesahaulika kabisa, tumeona mawaziri wetu wakiwasha umeme mpaka kwenye nyumba za nyasi, nyumba za tembe, kule waliko Watanzania, hili ni jambo jema. Tumeona umeme unawashwa mpaka Loliondo, kwa babu wa kikombe, hili ni jambo jema. Kwa hiyo nataka nimsihi sana Mheshimiwa Waziri aendelee.

Mheshimiwa Spika, nimeachiwa hapa taarifa na jirani yangu na mimi ni mtu muungwana Mheshimiwa Mwamoto amesema nizungumzie habari ya Kata ya Image. Kwa bahati nzuri naomba ku-*declare interest,* Kata ya Image ndiko nilikoolea mimi, Waziri apeleke umeme kwa wakwe zangu pale Image katika Jimbo la Kilolo na wakwe zangu nao kule wafurahie waseme na mzee alitaja ili mtoto wao aendelee kubaki mikono ni mwangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye suala la kuongoza nchi ni suala ambalo hata wenzetu wameonyesha kwamba kuna kipindi unahesabu faida, ukiona faida ni kubwa unachukua huo huo uamuzi. Tumeona CHADEMA ni chama cha kidemokrasia na maendeleo lakini tumeona demokrasia hawaitendi, wana Mwenyekiti ana miaka 20 kwa sababu gani, pengine wanaona kuna faida kubwa kuendelea na huyo Mwenyekiti. Kwa hiyo wakati mwingine huwezi kuona faida ya moja kwa moja mpaka watu

wakuelimishe kwamba hapa sasa unatoka kwenye reli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika,Jambo lingine ambalo naliona hapa naona hapa tunazungumzia madeni ya *TANESCO*. Mheshimiwa Waziri hapa nataka anisikilize kwa makini sana. *TANESCO* imekuwa na madeni makubwa sana...

**SPIKA:** Mbona hakuna anayesimama upande huu huo msumari. *(Kicheko)*

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, *TANESCO* ina madeni makubwa sana na madeni haya yanatokana na *capacity charge* za makampuni, makampuni haya matatu yanaipa mzigo mkubwa sana *TANESCO.* Kuna *IPTL*, kuna *Aggreko*, kuna *Symbion,* haya makapuni kila kampuni moja kwa mwaka linaitia deni *TANESCO* karibu bilioni 635, sasa hii si sawa. Serikali iondoe haya makampuni, iondoe mitambo yao, wanaipa *TANESCO* madeni makubwa sana, wanaagiza mafuta, wanaagiza vitu gani, matokeo yake ni kwamba tunapoteza fedha nyingi na tunaipa *TANESCO* mzigo mkubwa sana wa madeni.

Mheshimiwa Spika, vilevile ukiangalia kwa hesabu tu za shule ya msingi ukiondoa mitambo ya haya makampuni matatu utaokoa karibu trilioni mbili, maana ni trilioni moja na bilioni 930 na kitu, kwa hiyo utakuwa umeokoa karibu trilioni mbili.  Hii itasaidia sana kuboresha uendeshaji wa *TANESCO* na wao watafika mahali watafanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimeona linatupa tabu, umeme ukikatika kutokana na mvua inawachukua muda mrefu *TANESCO* kwenda kushughulikia kwa sababu tuna umeme sehemu nyingi vitendea kazi vichache, magari machache ya *TANESCO,* mafundi wachache sasa wanachukua muda mrefu na kupoteza muda mrefu na kupoteza fedha nyingi, maana hivyo vijiji vina wateja tayari.

Mheshimiwa Spika, nimeona kuna kipindi Ndebo walikosa umeme, Mvumi *Mission* walikosa umeme inachukua mpaka wiki moja na nusu sasa hii si sawa, tuwarahisishie, aidha kwenye maeneo ambayo wanaona udongo wake haustamili sana wakati wa mvua wapitishe umeme chini au wanaweza kutumia umeme wa nguzo za zege, ukitumia umeme wa nguzo za zege ukazipitisha umeme juu maana yake eneo hilo hata kama mvua ikinyesha zege lile linazidi kujiimarisha.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Tano, haya maamuzi wanayoyafanya ni maamuzi ya utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu. Hatuwezi kurudi nyuma kwa sababu tuliwaahidi Watanzania na wenzetu hawa ambao wanatupinga nao ni maamuzi ya chama chao, lakini hakuna mmoja hapa anayesema hataki umeme, sisi tuendelee kuwahudumia na wao kwenye majimbo yao tuwahudumie. Tunapopitisha hii bajeti tunapitisha pamoja na kusaidia majimbo ya Upinzani wa nchi hii kwa sababu kule kuna Watanzania, tunawahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tuwahudumie wananchi wote kwa sababu mwakani nataka nikuhakikishieni kutakuwa na mabadiliko makubwa sana kupitia hii Wizara ya Nishati, Watanzania wamewashiwa umeme mpaka vijijini kitu ambacho kilikuwa ni ndoto, mwakani wanakwenda kuitunza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuipigia kura ambazo hazijawahi kupigwa kwenye Bunge hili, ambazo hazijawahi kupigwa kwenye nchi hii kwa sababu kazi iliyofanyika. Umeme uzuri wake ni kitu kinachoonekana kwa macho, kwa hiyo kila wanapokwenda akina Mheshimiwa Subira tunawaona na wananchi wanavyowapokea tunawaona, hawawezi kuwashangilia vile halafu kesho wakatunyima kura, haiwezekani! Kwa hiyo wanatufanyia kazi njema sana, wanatupa hoja za kwenda kuyasemea hata majimbo yao kwa sababu wanawasikia wanavyokataa bajeti wanawasikia, wanavyokataa umeme wanawasikia, lakini sisi wana CCM kwa sababu tumebeba dhima ya kuongoza Taifa hili tunapeleka umeme nchi nzima bila kujali Mbunge wa Jimbo hilo kasema nini humu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana kazi ya kusambaza umeme iongezeke nguvu, vinginevyo kama Waziri atatuhakikishia kwamba anayo awamu nyingine ya nne, lakini kama ni awamu zile zile tatu maana yake hii ndio *finally.* Sasa kwenye *finally* kusiwe tena na kulegalega maana wametuambia kuna *REA* awamu ya kwanza, awamu ya pili na ya tatu, hatuna *REA* awamu ya nne. Kwa hiyo *speed* yao lazima iwe kubwa kuhakikisha kuwa mambo yanafanyika na yanafanikiwa ili kutupa hoja za kwenda kuwaambia wananchi umeme upo au haupo, wanasema upo, piga kura kwa Magufuli, shughuli imekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema gharama za kuendesha nchi ni kubwa, umeme wa maji utatuletea punguzo kubwa sana la gharama na hivyo kuifanya nchi yetu iweze kusonga mbele. Kwa hiyo naomba sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama hapa vijiji vyangu avikumbuke; nimeomba umeme Kijiji cha Huzi, Kijiji cha Manda, Kijiji cha Ciifukulo, Kijiji cha Muheme, Kijiji cha Mpwayungu umalizike pale na Mvumi Mission tuhakikishe maeneo yote Chihembe yanapata umeme na kule nilikozaliwa mimi ili wananchi wenzangu waweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, leo tumeona saluni zinafunguliwa vijijini, tumeona watu wanachomelea madirisha vijijini, tunaona vijana wanajiajiri kwa kupitia sekta hii ya umeme. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuhakikishie kumalizika kwa *REA III* itakuwa ni lini ili vijiji vyote viweze kupata umeme na mambo yaweze kwenda.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Lusinde.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Wizara hii ya Nishati ambayo ni Wizara muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa. Sasa nitashauri mambo kadhaa katika Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, soko huria kwenye usambazaji wa umeme; kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi kuhusu usambazaji wa umeme ukiwa wa kusuasua, hivyo nashauri Serikali kukubali suala la soko huria ili kuleta ushindani na kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, umeme wa upepo; Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza nguvu ya kipesa na kutoa kipaumbele kuwasaidia watumiaji wengi ambao wana hali ya chini ili waweze kutumia umeme ambao utakuwa wa bei nafuu na utawanufaisha wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Umeme Vijijini; kumekuwa na malalamiko makubwa juu ya mgao wa umeme unavyotekelezwa kwa kuwa kuna kuruka baadhi ya vijiji aidha kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Ni vyema suala hili likafuatiliwa kwa ukaribu na umakini mkubwa sana ili kuondoa malalamiko yanayowakabili wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* wapewe ushindani; *TANESCO* wamekosa ufanisi kiutendaji kwa sasa wanafanya kazi kwa mazoea, ni vyema kuwe na makampuni ili kuleta matokeo chanya na kuleta ufanisi kwa utekelezaji wa ugawaji umeme na nidhamu kwa matumizi ya pesa.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme jazilizi; kumekuwa na ubaguzi mkubwa na watu wengine kujiona wanyonge pale wanapoona wananchi wengine wanapata umeme huku wengine wakikosa wakati wako eneo moja. Pia maeneo ya taasisi yepewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi walipwe kwa wakati; kumekuwa na changamoto kubwa katika utendaji pale ambapo inatokea mkandarasi hajapewa malipo yake inapelekea kazi na miradi mbalimbali kusimama na kupelekea wananchi kuinuka kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, bei halisi ya kuunganisha umeme; kumekuwa na mkanganyiko wa bei halisi ya umeme kwa wananchi wanapokuwa wanatakiwa kuunganishiwa pale

ambapo *REA* inaishia bei zao zimekuwa tofauti kwa wananchi. Nashauri Serikali kufuatilia jambo hili na kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyobakia katika Mkoa wa Rukwa; tunaomba kujua ni lini maeneo hayo yatapata umeme kwani maeneo hayo yaliyobaki yakipata umeme yatasaidia kupunguza vifo vya akinamama na mtoto pia itawasaidia watu kiuchumi katika viwanda na biashara ndogondogo.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii hasa katika suala la miradi ya umeme vijijini *REA III* hasa kwa Mkoa wa Iringa. Hadi sasa jumla ya wateja 3,541tu kati ya wateja 13,556 ndio wameshaunganishiwa umeme katika vijiji 67 kati ya vijiji 179. Hii spidi ni ndogo na vijiji vingi havijapata umeme huu hasa Jimbo la Kalenga, Kata ya Luhota, Vijiji vya Tagamenda, Wangama, Kitayawa na Kata ya Mgama na Mseke kuna baadhi ya vijiji havina umeme.

Mheshimiwa Spika, nashauri hata vijiji vilivyowekewa umeme ni nyumba chache sana zenye umeme na hata maeneo ya shule, zahanati nazo bado hazijapata umeme. Hivyo Serikali iweze kuweka umeme katika Jimbo na Kata zake zote pamoja na vijiji vilivyopo katika jimbo hilo. Niliuliza swali la msingi na majibu yalikuwa kwamba hii *REA III* itamaliza matatizo katika jimbo hilo na mkoa kwa ujumla, naomba bajeti hii iziangatie hilo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, umeme unaleta maendeleo kwa wananchi na kuongeza uzalishaji katika viwanda na itapelekea kuinua uchumi wa nchi yetu. Naiomba Serikali kupeleka umeme wa *REA* katika Jimbo la Mufindi Kusini. Vijiji vingi ambavyo havijapata umeme kabisa katika Jimbo la Mufindi Kusini ni kama ifuatavyo:-

(1) Kata ya Idunda, Vijiji vya Idumulavanu, Ikangamwani na Mkangwe;

(2) Kata ya Itandula, Vijiji vya Ihawaga, Nyigo, Ipilimo na Ikiliminzowo;

(3) Kata ya Mtambula, Vijiji vya Ipilimo, Iyegela, Nyakipambo, Mtambula na Mzumbiji;

(4) Kata ya Kasanga, Vijiji vya Ihomasa, Kilolo na Udumka;

(5) Kata ya Kiyowela, Vijiji vya Magunguli, Kiyowela na Isaula;

(6) Kata ya Idete, Vijiji vya Itika, Holo na Idete:

(7) Kata ya Maduma, Vijiji vya Wangamaganga, Maduma na Ihanganatwa;

(8) Kata ya Nyololo, Vijiji vya Njonjo, Lwingulo na Nyololo Shuleni;

(9) Kata ya Mninga, Vijiji vya Mkalala, Ikwega, Itulituli na Kitilu;

(10) Kata ya Luhunga, kijiji cha Ihefu;

(11) Kata ya Malangali, Vijiji vya Isimikinyi, Kingege na Itengule;

(12) Kata ya Ihowanza, Vijiji vya Idope, Ipilimo, Igenge na Kiponda.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupeleka umeme katika kata na vijiji vyote ambavyo nimevitaja, pia kuna vitongoji zaidi ya 30 havijapata umeme, zahanati, vituo vya afya, shule za msingi na shule za sekondari bado hazijapata umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Spika, kata na vijiji hivyo *survey* tayari na baadhi ya kata na vijiji ambavyo nimevitaja nguzo tayari bado waya na sehemu nyingi nguzo na waya tayari bado

kuwasha. Naiomba sana Serikali kukamilisha mradi huu wa umeme wa *REA* ili wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kufanya shughuli zao na kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu na Watendaji. Pongezi kwa kuzalisha umeme na kuwa na ziada ya *MW* 300 na hivyo kutokuwepo mgao wa umeme. Rufiji *Hydro Power MW* 2,115. Kuongezeka kwa kasi ya kuwaeleza umeme vjijini na kufikia vijiji 7,127 kati ya vijiji 12,268 na kufikia Juni 2020 vitafikia 10,268. Pongezi kwa uamuzi wa kutoza 27,000 kuunganisha umeme vijijini japo lina changamoto na linakwamisha wananchi hasa inapotakiwa kununua nguzo, maelekezo shilingi 27,000 ndani ya mita 30.

Mheshimiwa Spika, *REA III,* mzunguko wa kwanza, lengo vijiji 10,278 *by June* 2020, mzunguko wa pili lengo vijiji 1,990 kuanza Julai 2020.

Mheshimiwa Spika, Wanging'ombe vijiji 54 hivi sasa havina umeme kabisa, mzunguko wa kwanza vijiji na vitongoji 48, vijiji 38 na vitongoji 10 pogram *todate* vijiji vinne na vitongoji vitano. Mkataba unaisha Disemba, 2019. Swali, atakamilisha vijiji 39 ndani ya miezi sita? Mkataba umeonesha anasambaza *line* kubwa kilomita 95 wakati uhalisia kufikia vijiji 48 ni kilomita 150 mpaka leo *addendum* ya *scope* na muda haijasainiwa.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi Mufindi *power JV Hegy Engineering,* utendaji wa kazi hauridhishi kabisa, bado maeneo ya vijiji 27 vilivyo kwenye mkataba aidha hajapeleka nguzo kubwa au hajatandaza *wire* au hajaanza hata kupeleka nguzo ndogo. Mkandarasi huyu hata hivyo vijiji vinne na vitongoji vitano inachukua zaidi ya miezi mitatu kuwasha umeme toka wateja wailipe *TANESCO* kwa madai kuwa mita zilifungwa bila kusajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Meneja wa *TANESCO* Wilaya hana gari la kufuatilia utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kuunganisha umeme kwa wananchi 27,000 iwe ni ndani ya mradi au vinginevyo. Maelekezo ni kwamba, Sh.27,000 ni ndani ya mita 30; nguzo moja Sh.391,000, nguzo mbili Sh.450,000, halafu nguzo inakuwa mali ya *TANESCO* utakuta watakaofuata wanalipa Sh.27,000 tu. *TANESCO* wapewe bajeti ya kuweka nguzo.

Mheshimiwa Spika, hivi vijiji vimepewa *scope* ya wastani wa kilomita mbili, kwa hiyo eneo kubwa la kijiji na vitongoji havijapewa umeme. Sasa maeneo haya yaliyosalia pamoja na vijiji ambavyo havijafikiwa vimewekwa kwenye awamu ipi? Kwani kwenye hotuba *page* 61 Waziri ameongelea kuhusu idadi ya vijiji ambavyo havitafikiwa ifikapo Juni 2020, hajasema chochote kuhusu vijiji vilivyopewa *scope* kidogo, *page* 65 haielezei *scope* jazilizi na hakuna bajeti.

Mheshimiwa Spika, uendelevu wa mradi huu kabambe wa *REA;* mwaka jana nilishauri sambamba na kuwekeza fedha nyingi kwenye ujenzi wa mradi Serikali iwekeze fedha ya kutosha za matengenezo ili kuiwezesha *TANESCO* kuhimili mahitaji ya matengenezo, sijaona mpango huo kwenye bajeti hii. Mfano 90% *Road Fund* ni matengenezo; 7% *Road Fund* ni mwendeleo ujenzi mpya; 2% *Road Fund* ni utawala. Wilaya ya Wanging'ombe *REA II* transfoma 30. *REA III* transfoma tisa zimeungua wako gizani. *Seven transformers are replaced but two not yet for more than six months.*

Mheshimiwa Spika, mikataba; yapo majukumu *(obligations)* za mwajiri *client* na yapo majukumu *(obligations)* za mkandarasi. Mkandarasi lazima alipwe kwa wakati *(30 days)* baada ya kuidhinisha hati ya madai. Mkandarasi asipofikisha lengo la utekelezaji zipo hatua za kuchukua. Kila mwezi kuna *Progress Site Meeting,* hizi lazima zisimamiwe vizuri na *Consultant* na *client*. Tusisubiri mwisho wa muda ndio tuchukue hatua au zinaanza kuzuka hoja eti mkandarasi hana uwezo, swali alipataje kazi? Tathmini ya uwezo kikazi na kifedha ilifanyike *(due diligence)?*

Mheshimiwa Spika, orodha ya vijiji vilivyomo *REA III round I* navyo ni Ihanja, Lusisi, Mungate, Itambo, Udonja, Ujange, Kasagala, Lugoda, Ikwega, Matowo, Itowo, Ilulu, Gonelamefuta, Masage, Mapogoro, Ukomola, Saja, Igomba, Isimike, Mtewele, Ujindile, Uhambule, Msimbazi, Igelango, Mng'elenge, Ufwala, Katenge, Mbembe, Itandula, Mpululu, Igelehedza, Igula, Mayale, Ing'enyango, Ivigo, Luduga sekondari.

Mheshimiwa Spika, vijiji visivyokuwepo kwenye REA III *round* 1. Idunda, Masaulwa, Ikwavila, Uhenga, Mbembe, Ikulimambo, Idenyimembe, Igenge, Idindilimunyo, Iyayi, Igando, Hanjawanu, Mpanga, Malangali, Wangamiko, Litundu.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika Jimbo la Tunduru Kusini kuna vijiji vitano tu kati ya vijiji 65, hivyo naomba vijiji vya nyongeza nilivyoomba viingizwe kwenye *REA* III, awamu ya kwanza, Vijiji hivyo ni Semeni, Mtina**,** Angalia, Nasya, Tuwemacho, Chemchem, Ligoma, Mkoteni, Namasakata, Luwingu, Nalasi, Chilundundu, Lipepo, Mchoteka na kadhalika ili kupunguza idadi kubwa ya vijiji visivyokuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo naomba Serikali inapopanga vijiji waangalie sana Halmashauri zenye majimbo zaidi ya moja kuchukua vijiji kila upande wa jimbo ili kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme unawekwa kwenye vijiji vingi ni vizuri *TANESCO* wakafikiria ofisi ndogo katika tarafa ili kutoa huduma kwa haraka kwa wateja wake.

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya *REA* kuna changamoto ya mafundi wanaoweka nyaya *(wiring)* kwenye nyumba za wananchi kuwa na gharama za juu kuliko uhalisia wa kazi, ni vizuri *TANESCO* wangetoa mwongozo kwa

wakandarasi na mafundi wanaofanya *wiring* katika majumba ya wananchi juu ya bei na gharama za kufanya *wiring*.

Mheshimiwa Spika, viongozi/*management* ya *TPDC* wateuliwe viongozi wa kudumu badala ya kuwa na makaimu kila siku ambapo wanakosa ujasiri wa kutoa maamuzi kwa kuhofia vyeo vyao kuyeyuka na kwa kuwa mpango kazi uliopo unaonyesha matumaini ya Shirika/*TPDC* kukua ni vyema basi *management* ya kudumu ikawekwa badala ya kuweka makaimu katika kila idara ya *TPDC*.

Mheshimiwa Spika, gharama ya bomba la gesi ichukuliwe na Serikali badala ya kuwatwisha mizigo *TPDC* ili kupunguza bei ya gesi kama inavyolalamikiwa na wawekezaji wengi. Hii itasaidia kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutumia gesi katika kuendesha viwanda vyao na kwa matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Spika, *TPDC* iharakishe usambazaji wa gesi majumbani ili kuongeza kiwango cha gesi kinachotumika na kuongeza pato la *TPDC* na Serikali kwa ujumla.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika suala la Ziwa Rukwa, kulikuwa na fununu ya upatikanaji wa gesi ya *helium* katika Ziwa Rukwa, je, hali ya utafiti mpaka sasa Serikali inasemaje. Je, kuwepo kwa gesi hiyo katika Ziwa Rukwa hakuna athari za kiafya kwa wananchi na watumiaji wa ziwa hilo. Serikali ina mpango gani wa kuweza kuvuna gesi hiyo na kuitumia?

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, nachangia kwa maandishi Wizara ya Nishati kama ifuatavyo na naomba Waziri anipe majibu stahiki:-

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme wa *REA* Mtwara Mjini, hotuba ya Waziri imesema ataweka utaratibu vijijini kote bei ya *REA* iwe 27,000/=, lakini Mtwara Mjini hii *program* ilikuwepo lakini ikaondolewa. Sababu za msingi hakuna, naomba Waziri atupe majibu kwa nini bei hii imeondolewa Vijiji vya Mtwara Mjini ambavyo wamebatiza jina la mitaa.

Mheshimiwa Spika, mkuza wa gesi Mtwara-Lindi; ilisemwa mote mlimopita bomba la gesi mngepelekewa umeme kwa gharama ya *REA* yaani 27,000/=tu, lakini Mtwara Mjini kata takribani nane bomba hili la gesi limepita. Cha ajabu wananchi wa kata hizi watozwa laki tatu mpaka tano kwa ajili ya kuunganisha umeme wakati sera inasema shilingi 27,000 tu kwenye huu mkuza wa gesi. Waziri kwa nini anatukandamiza Wanamtwara Mjini?

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa umeme vijijini/ mitaa ya pembezoni mwa Mtwara Mjini; kila siku Waziri nikimuuliza anasema maeneo ya pembezoni mwa Mji wa Mtwara yatapelekewa umeme kwa mfumo wa ujazilizo. Mpaka leo Waziri amepeleka sehemu moja tu ya Mbawala Chini kwenda kulambisha kidogo tu. Maeneo ninayoyalalamikia kila siku ni: Mbae-Mkangala; Lwelu-Dimbuzi na Mkangala - Mkunjanguo mpaka Mwenge na Mtawanya- Namayanga.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya ya pembezoni ya Mji wa Mtwara yanaitwa mitaa lakini Wizara haitaki kupeleka umeme kabisa. Waziri atuambie kwa nini anatunyanyasa wana Mtwara Mjini kwa kukataa bila sababu kupeleka umeme mitaa hii wakati umeme wote kusini unatoka Mtwara Mjini? Maeneo haya kila moja haizidi kilomita tatu kutoka vyanzo vya umeme lakini Serikali haitaki kupeleka mtandao wakati gharama ni nafuu sana.

Mheshimiwa Spika, gesi majumbani Mtwara Mjini; imepelekwa majumbani Masaki, Dar es Salaam kwa miaka miwili sasa lakini pale inapotoka hii gesi Wanamtwara tupo tayari kununua hii gesi lakini Serikali haitaki kutuletea. Anachofanya Waziri ni danganya toto tu na kuahidi kuwa mradi wa Mtwara utaanza, lakini hata mimi Mbunge wa Jimbo sina taarifa hata moja juu ya utaratibu wa hiyo gesi majumbani. Nimemuuliza Mheshimiwa Waziri anasema utaratibu bado lakini Masaki anakoishi yeye kapeleka gesi anatumia gesi kupikia, pale Mtwara inapotoka gesi anasema mchakato unaendelea. Hali hii ni uonevu mkubwa na

ukandamizaji wa Wanamtwara ambao tumekuwa tunalalamikia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 90 wa hotuba ya Waziri amesema mchakato wa kupeleka gesi Uganda unakamilika. Haiingii akilini hata kidogo gesi iende nje kutumiwa majumbani wakati pale inapotoka Mtwara ni nyumba 300 tu wakati kila nyumba Mtwara inahitaji hii gesi nafuu ya Serikali. Haikubaliki.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza viongozi kwa kazi nzuri wanazofanya. Mheshimiwa Waziri Dkt. Medrad Kalemani na Naibu Waziri Mheshimiwa Mgalu, hongereni sana. Mchango wangu utajikita katika maeneo matatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji vilivyo kwenye *line* kubwa Mtwara-Nanyamba Newala, vijiji takribani nane vipo chini ya *line* hii. Nimpongeze Waziri kwa maagizo yake ambayo aliyatoa hivi karibuni akiwa Mtwara kuwa vijiji hivyo vipewe umeme. Nashauri *TANESCO* Mtwara wawezeshwe ili waweze kutekeleza maelekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Majengo; kituo hiki kipo Kata ya Njengwa na hakuna umeme. Namshukuru Waziri kwa kuelekeza *TANESCO* Mtwara kuwa waanze mpango wa kuleta umeme katika kituo hiki. Nashauri msisitizo utolewe ili kiweze kupata umeme ili kiweze kutoa huduma zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kusambaza gesi majumbani; mradi huu ni muhimu na naomba fedha zitengwe za kutosha ili idadi ya nyumba/kaya zitakazopewa gesi ziongezeke katka Miji ya Mtwara, Lindi na Dar es Salaam. Pia na maeneo mengine na wilaya zake na si Makao Makuu ya Mikoa tu.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa umeme katika baadhi ya Mitaa-Nanyamba Mjini; naomba Mitaa ya Madina, Namkuku na Kilimanjaro iliyopo Nanyamba Mjini iwekewe umeme.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Hongera nyingi kwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wataalam wa Wizara. Mambo ya msingi:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Wizara ifanye *fast track* ya miradi ya kuunga Mkoa wa Kigoma kwenye gridi ya Taifa:-

(a) Tabora-Kigoma na Nyakanazi-Kigoma. Miradi hii ni muhimu sana, vinginevyo Mkoa wa Kigoma utabaki nyuma kama ilivyo sasa, lazima tuonyeshe tofauti.

(b) Mradi wa Malagarasi *Hydro Power MW* 45.4; mradi huu ni muhimu sana kwa nchi na Mkoa wa Kigoma, kupata *MW* 45.4 ku-*feed* kwenye *grid* ni kitu kizuri na muhimu sana. Ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba wapeni kipaumbele mradi huu, tumeusubiri sana. Hoja ya upungufu wa fedha haina nguvu ya kimkakati, ikibidi tukope fedha tujenge mradi huu, ni muhimu sana.

(c) Malipo ya fidia; Malagarasi na Kidahwe itakapojengwa *sub-station* ya *grid*. Walipeni fedha hizi haraka ili kazi ianze kwa jinsi ratiba ya utekelezaji ilivyopangwa. Miradi hii kwa Kigoma si tu ni muhimu, hii ndiyo roho ya mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, pili, *REA III* Kigoma, Kasulu, Buhigwe, Uvinza na Mradi huu ulizinduliwa kule Rusesa, Kasulu *DC* mwaka jana 2018. *Speed* ya mradi huu ni ndogo sana, mkandarasi aongeze nguvu. Tangu uzinduzi ule, maeneo mengi hata vifaa havijapelekwa yaani nguzo, nyaya na kadhalika. Tafadhali kasi iongezeke.

Mheshimiwa Spika, tatu, mradi wa ujazilizaji wa maeneo *(densification round two)*. Halmashauri ya Mji wa Kasulu-*TC*, kata nyingi zaidi ya tisa zilipata umeme wa *REA II,* tatizo/shida ni kwamba, maeneo karibu yote umeme umefika sehemu moja tu. Mfano umeme umefika sokoni, umeme umefika Ofisi ya Mtendaji na kadhalika. Umeme haujafika kwenye mitaa, vitongoji walipo wananchi wetu wengi. Nishauri *strongly*, Mkoa wa Kigoma sasa uingizwe kwenye huu

mradi wa ujazilizi hasa katika Mji wetu wa Kasulu. Ikiwa ni heshima kwa Serikali mikoa iliyopata shida ya kuanza *REA III* basi ipate nafuu ya kupata mradi huu.

Mheshimiwa Spika, Kijiji/Kata ya Mrufiti, kata hii ilisahaulika wakati wa *survey*, nilimshauri *Regional Manager TANESCO* Kigoma akiingize kijiji hiki ambacho pia ni kata ili iende sambamba na maeneo ambayo yamefanyiwa *survey* ya Kigondo, Muhunga, Ruhita, Ngumbigwa na sasa Mrufiti. Hii ni muhimu sana ili wananchi hawa wasionekane wametengwa kwa sasa. Maeneo yote ya jirani yamefanyiwa *survey* hiyo, hii ya kusema Mrufiti isubiri *phase two* ya *survey* iondoke. Wananchi hawa wanataka umeme leo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kuwawezesha Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kujituma na kujitoa kwa maslahi ya maendeleo ya kuwasambazia umeme wananchi hadi vijijini na vitongoji vyote nchini hadi sasa wana asilimia ya kuridhisha na matumaini ya kutimiza azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ya ahadi ifikapo mwaka 2025 umeme uwafikie wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Meneja wetu wa *TANESCO,* Ndugu Chambua kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na changamoto zilizopo ndani ya Mkoa wa Rukwa.

(1) Wakandarasi hawajapatiwa nyongeza ya vifaa vya kupeleka umeme kwenye Taasisi za Serikali (zahanati, vituo vya afya, shule za msingi na sekondari zetu).

(2) Nguzo zilizosambazwa zisiwe picha kwa wananchi, ni vyema zikakamilishiwa zoezi na umeme kupatikana

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli na jitihada za Waziri na Naibu Waziri kwa moyo wa dhati wa kuitumikia

Wizara hii, bado Mkoa wa Rukwa tunahitaji umeme kwani kazi iliyofanyika bado vijijini Mwambao wa Ziwa Tanganyika, Ziwa Rukwa bonde zima, mpakani mwa Zambia na Congo DRC hali ni ngumu bado. Tunaomba umeme vijijini zaidi, tunashukuru hiyo jitihada ya kupatiwa umeme wa gridi ya Taifa kuingia Sumbawanga ni tija ya pekee kwetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba jitihada iongezeke kwa kusambaza umeme Mkoa wa Rukwa na kutuwezesha kwa kuongeza nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Merdad Kalemani, Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Subira Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutumikia Watanzania kwa kuhakikisha kaya zote nchini zinapata umeme. Mungu awabariki sana. Pia nawapongeza Watendaji wote wa Wizara kuanzia Katibu Mkuu, Dkt. Khamis Mwinyimvua, Wakurugenzi na Mameneja wote wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, sekta ya umeme au nishati ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda nchini. Ukuaji wa sekta ya viwanda unategemea sana uwepo wa nishati ya umeme wa kutosha na wa bei nafuu. Nchi kama Marekani, China, Japan na South Korea zimepiga hatua katika maendeleo ya viwanda ni kutokana na uwepo wa vyanzo vingi vya umeme.

Mheshimiwa Spika, kasi ya usambazaji wa umeme kwa baadhi ya maeneo ni nzuri lakini kuna maeneo kasi ya usambazaji ni ndogo sana. Mfano, katika Jimbo la Lupembe *speed* ya Mkandarasi wa *REA* ni ndogo sana. Tuna vijiji 22 havina umeme lakini tangu mwaka jana 2018, Mkandarasi ameanza kusambaza umeme katika vijiji viwili tu na kila kijiji amesambaza kwenye mtaa mmoja tu katika Vijiji vya Ihang'ana na Iyembele. Pia amepeleka nguzo katika Kijiji cha Ninga tangu mwezi Januari lakini mpaka sasa kazi haijaanza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Lupembe kuna wakulima wengi wa mazao ya chai, matunda, miti ya mbao, mahindi na parachichi. Mazao haya yanahitaji viwanda vya kuongeza thamani lakini tatizo limekuwa umeme. Mfano, wakulima wamenunua kiwanda cha sembe katika Kijiji cha Ninga tangu 2016, lakini hakijaanza kufanya kazi kutokana na kukosekana kwa umeme. Pia wakulima wa nanasi wa Kijiji cha Madeke wana kiwanda cha kuchakata nanasi, lakini kiwanda hakifanyi kazi kutokana na kukosekana kwa umeme. Hivyo ni muhimu kuangalia uwezo wa hawa Wakandarasi kwani wanakwamisha juhudi zote za Waziri na Naibu Waziri za kuwaletea maendeleo wakulima kupitia huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kwenye maeneo ya viwanda umeme unapokuwa umekatika kutokana na kuungua kwa *transformer.* Wawekezaji wamekuwa wakiambiwa wanunue *transformer* wenyewe na wajiunganishie, hii imekuwa ikiwaathiri wakulima. Mfano, Jimboni kwangu Lupembe tuna viwanda viwili vya chai na kutokana na eneo la Lupembe kuwa na mvua nyingi zinazoambatana na radi hupatwa na tatizo la kuungua kwa *transformer* na kiwanda kutoendelea kufanya kazi mpaka *transformer* ipatikane, wakati mwingine huchukua wiki mbili mpaka tatu.

Mheshimiwa Spika, hii imekuwa ikiathiri wakulima wa chai na kupoteza uchumi wa wakulima hawa, hivyo nashauri Wizara kwenye maeneo ya viwanda tuwe na *transformer* za ziada au za akiba ili pindi kunapotokea kuungua kwa *transformer* kufanyike *replacement* mapema ili kuokoa uchumi wa wakulima hawa. *TANESCO* wapeleke *transformer* na wafunge kuliko kuwaachia wawekezaji wajitafutie *transformer* zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Wizara kwa kutoa *offer* ya punguzo la bei ya kuunganishiwa umeme kwa bei ya shilingi 27,000 kwa *REA* na *TANESCO,* hili litaharakisha usambazaji wa umeme vijijini. Nashauri Mheshimiwa Waziri awaagize Mameneja wote wa *TANESCO* kwa kutoa waraka

maalum na Wabunge wapate nakala yake. Hii ni kutokana na kwamba bado wananchi kwa baadhi ya maeneo wanakataliwa kulipia, wanaambiwa kulipia mpaka kuwepo na nguzo ya kuingizia umeme kwenye nyumba yake kumbe wangelipia hizi fedha zingesaidia kununua waya, nguzo na vifaa vingine, lakini pia wananchi wengi wakipata umeme wananchi watalipia bili za umeme na shirika litaongeza makusanyo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma; mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda nchini. Mradi wa Mchuchuma ukianza utatusaidia kupata umeme wa bei nafuu na wa kutosha, lakini kupitia mradi huu tutapunguza makatizo ya umeme yanayotokea wakati wa kiangazi au mvua inapopungua na shughuli za uzalishaji zitaendelea vizuri kwa kuwa kutakuwa na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, *scope* ya miradi ya umeme kwa baadhi ya maeneo ni ndogo sana. Wakandarasi wamekuwa wakieleza kwamba usambazaji wa umeme unategemea *scope* waliyopewa. Kuna vijiji ni vikubwa sana mfano, katika Jimbo la Lupembe, *scope* ikiwa ni kilometa mbili maana yake itatosha kitongoji kimoja tu na hivyo eneo au kitongoji kilichokosa umeme kuanza kulalamika kwa kutopata umeme hivyo ni muhimu kuangalia na aina ya kijiji chenyewe ili angalau kuwapa umeme wananchi wote waliopo kwenye kijiji hicho. Hii itasaidia kuondoa lawama na manung'uniko kwa sisi viongozi wa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, narudia kuwapongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa kujituma kwao katika kuhakikisha kila kaya inapata umeme. Wanafanya kazi kwa kujituma kama vile ni kazi zao binafsi, kwa kweli wamekuwa mfano mzuri wa kuigwa na Wizara nyingine. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Wizara hasa Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote kwa juhudi kubwa wanazofanya kuhakikisha kuwa nchi yetu inapata umeme wa *REA* na wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, la pili; namshukuru Mheshimiwa Waziri yeye binafsi kwa jitihada ya kupeleka umeme katika chanzo cha maji-Makuyuni. Wananchi wa Monduli wanamshukuru sana na wanamwombea kwa Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru pia kwamba katika mpango wa *REA III, phase III* Julai mwaka huu Monduli katika vijiji takribani 28 tumewekwa katika mpango, lakini kwa bahati mbaya vijiji viwili muhimu vimeachwa. Ombi letu, vijiji hivyo viongezwe yaani Kijiji cha Lashaine, Kata ya Lashaine na Kijiji cha Migombani, Kata ya Majengo. Hata hivyo, katika REA Awamu iliyopita *line* kubwa imepita katika vijiji, lakini wananchi katika vitongoji vingi hawajaunganishwa, nini mkakati wa kusaidia wananchi hao kupata umeme?

Mheshimiwa Spika, ushauri wa jumla; Serikali iwajengee uwezo *TANESCO* ikiwemo rasilimali watu ili waweze kutekeleza miradi ya *REA* badala ya kuwatumia Wakandarasi ambao wamekuwa wanachelewesha kazi. Hii itapunguza gharama na miradi itaisha kwa wakati.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali nawapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara ya Nishati kwa hotuba nzuri na kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa Mradi wa *Stiegler's* kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini kwetu, huu ni mradi wa ukombozi. Tunahitaji umeme mwingi sana wa *megawatts* 2,100 za *Stiegler's* zitatupaisha katika huduma za maji, afya, elimu, viwanda, reli *(SGR)* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa miradi ya *REA* ahadi zitekelezwe. Kijiji cha Kondo, Kata ya Zinga kilikuwa katika orodha ya *REA III*, lakini mpaka mwisho wa mradi (Juni, 2016)

mradi haukutekelezwa na katika *REA IIIA* Kondo haimo, lakini Mheshimiwa Waziri aliahidi miradi ambayo haikutekelezwa katika *REA II* itapewa kipaumbele katika *REA III*. Naomba Mheshimiwa Waziri aelekeze Mradi wa Kijiji cha Kondo utekelezwe haraka wananchi hao wamesubiri muda mrefu sana, tangu 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa ufanisi wa miradi ya *REA* nashauri *REA* izingatie mapendekezo ya Wabunge yaliyowasilishwa kwa utaratibu uliowekwa yaani kupitia *TANESCO* (W) na *TANESCO* (M). Katika Jimbo la Bagamoyo, vitongoji saba (Kata ya Denda) vyenye umeme viliorodheshwa katika *REA IIIA* wala havikupendekezwa na Mbunge wala *TANESCO* (W) wala *TANESCO* (M). Wataalam wa *REA* wazingatie mawasiliano ya Wabunge ikiwezekana mapendekezo ya Wabunge ndiyo yafanyiwe kazi ilimradi yamepitia utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, pongezi; hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wataalam wote, Wakuu wa Taasisi hususan *REA* na Watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kutekeleza malengo kama yalivyoanishwa katika Ibara ya 43(c), 43(f) na 43(g) kwa mfano, Ilani ya CCM imetekelezwa na inaendelea kutekelezwa kwa kiwango kikubwa. Hongera kwa Wizara, Serikali kwa upana wake chini ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, hongera sana kwa CCM. Tukiendelea hivi na pengine kuongeza kidogo kasi na ufanisi, sekta ya nishati inakwenda kupaisha nchi.

Mheshimiwa Spika, hali ya usambazaji umeme chini ya *REA;* Jimbo la Tunduru Kaskazini; Mheshimiwa Waziri kwanza nashukuru kwa kazi kubwa iliyofanyika Tunduru Kaskazini, hata hivyo nimeambatisha hapa orodha ya vijiji ambavyo bado vinahitaji kuwekewa msukumo ili navyo vinufaike na maelekezo ya Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa umeme Tunduru; Mheshimiwa Waziri kwa miaka mingi tangu tupate uhuru hali ya upatikanaji umeme Tunduru ilikuwa duni sana. Tunashukuru kwa kutuunganisha katika gridi ya Taifa kupitia Mahumbika-Lindi-Mtwara *circuit*. Pamoja na mafanikio haya tunaomba umeme wa gridi ya Taifa kutokea *Route* ya Makambako. Songea-Namtumbo usiishie Namtumbo bali uendelezwe hadi kufikia Tunduru ili upatikanaji wa umeme Tunduru uwe wa kutosha na kuaminika zaidi.

Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni orodha ya vijiji visivyokuwa na umeme Tunduru-Kaskazini katika Hamashauri ya Wilaya ya Tunduru.

| **Na.** | **KATA** | **VIJIJI** | **VITONGOJI VIKUBWA** |
|---|---|---|---|
| 1. | Jakika | Kindamba<br>Jaribuni | |
| 2. | Kidodoma | Legezamwendo<br>Machemba | Maji ya Swela |
| 3. | Ligunga | Twendembele | Mbarikiwa |
| 4. | Nakapanya | Tulieni | Mchololo |
| 5. | Namiungo | Nammanga<br>Nangolombe<br>Mnenje<br>Pachanne | Mtandika |
| 6. | Majimaji | | Mgeta<br>Songambele |
| 7. | Namwinyu | | Changarwawe B |
| 8. | Sisi kwa Sisi | Lelolelo<br>Sevuyanke<br>Nakatete | |
| 9. | Masonya | Nambarapi<br>Mkalekawana | |
| 10. | ML. Magharibi | Mkonda<br>Malombe | Msinjili |
| 11. | Ngapa | Ngapa<br>Mnazimmoja<br>Chawisi | Ngapa Mtoni<br>Jiungeni |
| 12. | Muhuwesi | | Temeke<br>Mwangaza |
| 13. | Mindu | Liwangula | |
| 14. | Namakambale | | Rwanda |
| 15. | Matemanga | Fundimbanga | |
| 16. | Mchangani | Mchangani<br>Ngalinje<br>Kidugalo | |
| 17. | Nandembo | Tumaini<br>Amka<br>Nangungulu | |
| 18. | Kalulu | Rahaleo<br>Mbungulaji | |
| | **Jumla** | **30 (27)** | **14** |

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Kata tano za Tinginya, Nakayaya, Mlingoto Mashariki, Nanjoka na Majengo vina umeme na kimoja kilichobaki kwa Kata ya Nampungu kiko kwenye mpango wa *phase III, round I.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitongoji vilivyoorodheshwa ni vikubwa na vinajitegemea na vina shughuli nyingi na watu wengi.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Nangungulu na Amka viko jirani na Nandembo lakini vinajitegemea, pia Kijiji cha Mchangani ni kikubwa sana na kina eneo muhimu lisilokuwa na umeme.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Nishati, Katibu Mkuu na Wakuu wa Idara zote kwa kazi kubwa wanazofanya za kusambaza umeme nchini, Urambo ikiwemo, tunashukuru sana. Naomba jitihada za kujenga kituo cha kupoza umeme Urambo ziendelee, nawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Spika, naomba maeneo yafuatayo yapate umeme. Orodha ya awali imeletwa Wizarani. Kata Kapilula eneo la Ulasa B, Kata ya Urambo, eneo la Ubalani, Mabatini, Boma *Village*, Kata ya Kiyungi eneo la Tulieni na Kata ya Imalamakoye eneo la Imalamakoye D. Taasisi-Magereza Urambo - *pump* ya maji, Shule ya *St. Lucia* - Kata ya Ukondamoyo na Shule ya Magole - Kata ya Vumilia. Tunaomba umeme wa *REA* ufike vijiji vyote vilivyobaki.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuchelewa kukamilika miradi ya umeme jua katika Visiwa vya Ukerewe; mradi wa usambazaji umeme kwenye visiwa mbalimbali vya Ukerewe unaendelea kwa kusuasua sana. Mfano, Kisiwa cha Ukara (JUMEME), mradi umesimama kwa muda mrefu kwa sababu mbalimbali hali inayokatisha tamaa wananchi waliokuwa wanasubiri kwa hamu. Ushauri wangu, Wizara itie msukumo ili miradi hii ikamilike kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, bei ya umeme unaozalishwa na JUMEME kuwa na bei kubwa mno; bei ya umeme unaozalishwa na JUMEME ni kubwa sana kiasi ambacho kinakatisha tamaa wananchi kuutumia umeme huo. Mfano, *unit* moja katika Kisiwa cha Ukara (Eneo la Bwisya) ambapo tayari wameanza kutumia huduma hiyo ni Sh.3,000. Bei hii ni kubwa sana kiasi ambacho wananchi wanashindwa kumudu na kusitisha huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili tayari limeongelewa na kuachiwa *EWURA* kutoa maelekezo, basi naomba Wizara iweze kufuatilia kwa karibu na kuisukuma *EWURA* iweze kutoa maelekezo ili wananchi wanaotumia umeme huu wafarijike na kuongeza watumiaji jambo litakalotia moyo wawekezaji hawa vilevile.

Mheshimiwa Spika, kukatikakatika kwa umeme kwenye eneo la Ukerewe; kumekuwa na tatizo la kukatikakatika kwa umeme kwenye Visiwa vya Ukerewe. Maelezo yanayotolewa ni kuanguka kwa nguzo kila mvua ikinyesha, hali hii inaathiri sana uchumi wa visiwa vya Ukerewe. Ushauri wangu, itafutwe suluhu ya kudumu ya tatizo hili ili tatizo hili la kukatika mara kwa mara kwa umeme liishe na kuwaondolea hasara wananchi wa Ukerewe wanaoshughulika na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kusuasua kwa Mradi wa *REA.* Pamoja na jitihada kubwa za Wizara, bado vijiji vingi na vitongoji havijaweza kupata umeme na hata maeneo yaliyofikiwa na umeme, wigo wa watu wanaopewa umeme huo umekuwa mdogo sana na hivyo tija kutoonekana. Mfano, katika kijiji chenye kaya zaidi ya 300 unapopeleka umeme kwenye kaya 10 tu ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia mradi wa ujazilizi uende kwa haraka hasa Wilayani Ukerewe ili kuondoa tatizo la nishati ya umeme kwenye maeneo yaliyorukwa.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwanza kuunga mkono hoja iliyopo mezani. Pili,

kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara kwa kazi na jitihada ambazo wamefanya hususani katika kuwapelekea Watanzania umeme.

Mheshimiwa Spika, binafsi nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitomshukuru Waziri na Naibu wake kwa ziara zao walizofanya Jimboni kwangu, hakika zimezaa matunda.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, naomba sasa nijielekeze juu ya vijiji vyangu ambavyo havijapata umeme. Kilindi ina vijiji 102 na vitongoji 615, lakini ni vijiji 50 ambavyo mpaka sasa vitakuwa au vinatarajia kuwa na umeme, vijiji 52 havina umeme kabisa. Niombe sana tena vijiji 52 vilivyobaki vipatiwe umeme na naamini kabisa vijiji hivi navyo vitapata katika awamu ya tatu ya *REA III.*

Mheshimiwa Spika, kwa hali ya jiografia ya wilaya yangu ilivyo ina changamoto nyingi sana, hii ni pamoja na kukatika kwa umeme mara kwa mara na hii inasababishwa na idadi ya watumiaji imeongezeka na chanzo pekee cha umeme ni kutoka Mkata, Wilaya ya Handeni. Kwa kiasi kikubwa umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara ni kuwa kero kubwa kwa watumiaji, lakini pia hii imekuwa sehemu ya Ofisi ya *TANESCO* Kilindi kuendesha ofisi kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, natambua jitihada za Wizara za kufanya *interconnection network* ya kutoka Mbigili, Wilaya ya Kiteto hadi Kufungu kilomita 55; mradi huu ni muhimu sana kwani utakuwa ni suluhu ya kupata umeme wa uhakika. Pia ningeomba kama tungepata *network interconnection* kutoka Kikunde hadi Kukivu kilomita 41 ambayo itasaidia Vijiji vya Ludeva, Mafalila, Tunguli, Mtoro na Kitingi vitafaidika na umeme.

Mheshimiwa Spika, vijiji tajwa hapo juu vipo mbali na Makao Makuu ya Wilaya, mfano Kijiji cha Kikunde, Kata ya Kikunde umeme umetokea Wilaya ya Mvomero, Morogoro. Niiombe sana Serikali iitazame Kilindi kwa Kijiji cha Tatu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, natoa mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *REA* awamu ya III ilipanga kupeleka umeme Wilaya ya Nkasi vijiji 51. Wilaya yenye Majimbo mawili ya uchaguzi lakini Jimbo langu lilipata vijiji 12 tu; pamoja na maombi ya nyongeza nimekuwa napewa maneno ya faraja bila utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Spika, Mawaziri na wataalam lazima wajue sikujileta hapa, nililetwa na wananchi lazima wagawe *resources* za nchi kwa usawa. Mara zote nikionesha maombi ya kunisaidia napewa maneno ya kufariji tu, hakuna hata kijiji kimoja kilichoongezwa katika vijiji 15 nilivyoomba vya nyongeza. Naomba Waheshimiwa Mawaziri wangu nawapenda sana na nimeisemea hapa Bungeni Wizara nikiwa Mjumbe wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa wanipe Vijiji vya Katani, Malongwe, Wampembe, Izinga, Ng'undwe, Sintali, Nkana, Mkomanchindo, King'ombe, Mlambo, Kilambo, Mpasa, Tundu, Lolesha, Kala, Mwinza, Lyapinda, Lupata, Msamba, Kisambara, Ninde na Nakasanga ili kuleta usawa.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutoa mwongozo rasmi kuwezesha *TANESCO* kuendeleza pale *REA III* inapoishia kabla ya kukabidhi mradi. Niwapongeze kwa kazi na hasa kwa kuanza kutuelewa watu wa Mafinga kwamba kutokana na uwepo wa viwanda vya mazao ya misitu, uhitaji wa umeme ni mkubwa, hivyo tunahitaji transfoma zenye *capacity* kubwa. Tayari tumepokea transoma mbili kati ya tano ambazo Mheshimiwa Waziri alituahidi wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais, hata hivyo, kuna jambo ambalo nashauri litolewe mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sisi Mafinga baada ya wananchi kuona umeme unakuja, walijiandaa kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kununua mashine kubwa za

kuchana mbao, hata hivyo kutokana na *scope* kuwa ndogo, *REA III* haijawafikia wananchi wa aina hiyo ambao wapo tayari kujigharamia kwa kujiwekea nguzo kutoka pale ambapo *scope* ya *REA III* awamu ya kwanza imeisha. Hata hivyo, kwa kuwa utaratibu wa kiukandarasi na mikataba, *TANESCO* hawawezi kuendeleza pale mkandarasi alipoishia kwa kuwa mradi bado haujakabidhiwa rasmi kwa *TANESCO* na hasa ukizingatia kuwa kuna miezi kumi na miwili ya matazamanio.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, naomba Wizara itoe mwongozo rasmi wa kuruhusu hasa maeneo mahususi ambayo wananchi wapo tayari kujigharamia kwa nguzo kama ilivyo katika baadhi ya maeneo ya Mafinga. Naamini kwamba nimeeleweka, maana kuna maelezo lakini hayajanyooka kwa maana kwamba kanuni na taratibu zinataka *TANESCO* aendelee baada ya kukabidhiwa mradi na ndiyo maana nashauri kuwa patolewe mwongozo rasmi kuhusu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Mafinga kuwa na wilaya ya ki-*TANESCO;* suala hili nimelileta mara kadhaa, hata hivyo sijui kama naeleweka. Mufindi ni wilaya ambayo ina viwanda vingi vya chai, karatasi na viwanda vya mazao ya misitu. Hata makusanyo (*revenue)* inayokusanya ni makubwa kushinda hata baadhi ya mikoa. Hivyo, hili ni eneo ambalo lina *potential* kubwa sana. Hata hivyo, shughuli za viwandani zinapoteza wastani wa 30% ya muda wa kufanya kazi kutokana na ama kukatika umeme au hitilafu hasa nyakati za mvua. Kwa kuwa tunategemea *connection* iliyopo Mgololo, ikitokea *fault* yoyote, umeme unakatwa ili kurekebisha hizo *faults.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi letu, tuwe na *TANESCO* Mafinga (kama ilivyo Dar ambapo kuna wilaya za *TANESCO* nje ya wilaya za kiutawala mfano Tabata, Mikocheni na kadhalika). Tunaomba hivi kutokana na hali halisi ya uhitaji na pia kusogeza huduma karibu kwa wateja, lakini pia kwa kuwa eneo hili lina *potential* kubwa maana yake ni kuwa tutaongeza *revenue* ya *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, pia hii itawezesha *TANESCO* Mafinga kuhudumia viwanda vya mazao ya misitu na wakazi wa maeneo jirani wakati *TANESCO* Mufindi itahudumia viwanda vya chai na wakazi wa Mufindi. Mimi siyo mtaalam lakini naamini nimeeleweka, na rejea zangu za maandishi kwa barua zipo katika ofisi za *TANESCO* na *REA.*

Mheshimiwa Spika, *densification* hasa Kitelewasi, Shule ya Sekondari Mnyigumba na kadhalika. baadhi ya vijiji kama vile Kitelewasi ambapo kuna Shule ya Sekondari Mnyigumba walipata umeme *REA II* ambapo *scope* haikufika maeneo yote ikiwemo Shule ya Sekondari Mnyigumba ambapo tulihitajika kulipia milioni 78. Suala hili nimeshalifikisha kwa maandishi na barua Wizarani na *REA,* hivyo naomba *densification* iweze kujumuisha maeneo ya Kitelewasi na Kijiji cha Kikombo.

Mheshimiwa Spika, vijiji mbadala na upatikanaji wa *materials* kwa ajili ya *TANESCO;* kuna maeneo ambayo tumewasilisha *REA* kupitia *TANESCO* kwa ajili ya *reviewed scope* ambapo kuna eneo Ifingo, Kinyanambo Sekondari, *Banda Beach,* Lumwago na Isalavanu *Primary School*. Pia kuna maeneo ambako *line* kubwa ilipaswa kujengwa na mkandarasi lakini tayari maeneo hayo yalishajengwa *line* kubwa na hivyo tunaomba gharama zilizokuwa zijenge *line* kubwa, basi mkandarasi aelekezwe kupeleka umeme maeneo ya nyongeza ya Lumwago, Zanzibar na *Banda Beach.* Haya yote hasa kuhusu vijiji mbadala yapo tayari *REA.*

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa *materials;* kama nilivyosema awali, yapo maeneo *TANESCO* wanaendelea kwa mfano Mwongozo, Ifungo na Makamadoresi ambako kuna shule ya watoto wadogo inayoendeshwa na Masista. Tunaomba *TANESCO* wapelekewe *materials* kwa wakati.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi

wanayoifanya kwenye Wizara hii, wao pamoja na watumishi wote kwenye Wizara hii kwa juhudi kubwa wanazofanya za kuwaletea maendeleo katika Sekta hii ya Nishati hasa ya umeme. Wananchi wanaona juhudi yao katika kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa *LNG* Lindi; naiomba na kuishauri Serikali kuharakisha mazungumzo juu ya utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa nchi yetu. Hata hivyo, katika kuharakisha huko hakuondoi umakini wa kuzingatia maslahi mapana kwa Taifa letu na rasilimali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, *REA* awamu ya tatu kwa Mkoa wa Lindi haijafanya vizuri kwani hadi leo vijiji vingi vya Mkoa wa Lindi havijafanikiwa. Mfano Wilaya ya Liwale yenye vijiji 76, katika awamu ya tatu kulikuwa na vijiji 14, ni vijiji vitatu tu hadi leo vimewashwa umeme.

Sasa awamu ya tatu, mzunguko wa pili imeanza kutekelezwa kwenye baadhi ya mikoa, Liwale bado tuko awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza ambayo hakuna chochote kinachofanyika, japo *REA* awamu ya pili nayo haikufanya vizuri kwani hadi leo zipo taasisi hazijapata umeme kama vile shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kumbadilisha mkandarasi wa Mkoa wa Lindi ambaye ameshindwa kwenda na mkataba. Serikali kushindwa kumbadilisha mkandarasi huyu ni kukiri madai ya mkandarasi huyu kuwa Serikali haitoi fedha, ndiyo maana anashindwa kufanya kazi. Je, ni kweli kuwa Serikali haina fedha za kumlipa mkandarasi huyu?

Mheshimiwa Spika, sambamba na mradi wa *LNG* – Lindi, naomba kuishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Elimu kukiwezesha Chuo cha *VETA* Lindi kuanzisha masomo yanayohusiana na masuala ya gesi ili kuwawezesha wakazi au vijana wa Mikoa ya Lindi na Mtwara kushiriki vyema kwenye tasnia hii ya gesi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, naiomba Serikali kutoa kipaumbele kwa vijana wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, pale inapotokea nafasi kuwawezesha Watanzania kushiriki katika tasnia ya gesi, yaani kimasomo ndani na nje ya nchi ili Wanalindi waweze kuona manufaa ya moja kwa moja kutokana na kugunduliwa kwa gesi katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa matumizi ya gesi majumbani ni muhimu sana kwani utasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira. Pia wananchi wataona moja kwa moja manufaa ya kuwepo kwa gesi hiyo. Mradi wa matumizi ya gesi majumbani kwa Mkoa wa Lindi bado kabisa haujaanza. Kwa hiyo nashauri kufikiria kuanza kwa mradi huu kwa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, ninaposema Mkoa wa Lindi naiomba Serikali itambue kuwa Liwale ni miongoni mwa Wilaya za Mkoa wa Lindi hivyo miradi hii inaporatibiwa wakumbuke na Liwale, hata wakandarasi nao wafahamishwe kuwa Liwale nayo iko Lindi. Mfano Kampuni za *Shell* na *Equinor* zimeanza kutoa huduma *(incentives)* kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini Wilaya ya Liwale hawana habari nayo, kana kwamba Liwale haiko Lindi.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuishauri Serikali kuendelea kuwekeza kupitia Kampuni ya *TPDC* kwani sasa kampuni hii haijawezeshwa vya kutosha kuweza kukidhi majukumu yake. Miradi mingi ya kampuni hii imeshindwa kufanya vizuri kutokana na ukosefu wa fedha. *TPDC* ni lazima ipewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Liwale nayo iko Mkoa wa Lindi, nayasema haya kwa kuwa Mawaziri wengi huishia Wilaya za Kilwa, Nachingwea, Ruangwa na Lindi na kusema kuwa wamemaliza ziara ya Mkoa wa Lindi. Jambo hili limewafanya hata wakandarasi kuacha kutekeleza miradi mbalimbali kwani wanajua kuwa haitakaguliwa na Waheshimiwa Mawaziri, hakuna Waziri anayekuja Liwale kukagua miradi ya maendeleo ikiwemo *REA.* Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati aje Liwale aone haya ninayoyasema. Kati

ya vijiji 76, vijiji vyenye umeme havifiki hata 15, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naiomba Wizara wawaruhusu wawekezaji wa umeme jua, Kampuni ya *Power Conner,* waweze kutuletea umeme sisi tulio pembezoni tusioweza kufikiwa na umeme wa *REA.*

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati. Awali ya yote nitambue changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hii ya Nishati japo Serikali kupitia Waziri na Naibu Waziri watazipunguza kama siyo kuzimaliza kabisa. Vivyo hivyo naamini *document* niliyompatia Waziri wa Nishati juzi tarehe 27 Mei, 2019 inayohusu tatizo la umeme Mtaa wa Shanko, Kata ya Vwawa itapatiwa ufumbuzi kwa kuwa eneo hili la Shanko limekuwa kama Kisiwa maana limezungukwa na umeme lakini lenyewe halina umeme.

Mheshimiwa Spika, eneo hili upande mmoja kuna kilomita mbili tu toka sehemu ya umeme na upande mwingine kilomita nne, hivyo Serikali ione namna ya kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, mwisho japo siyo kwa umuhimu, naomba Serikali iwakumbuke wananchi wa Kata za Mara na Magamba Jimbo la Mbozi, kata hizi hazina umeme kabisa kijiji hata kimoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa wanayofanya hasa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini *(REA)*. Hata hivyo kasi ya utekelezaji wa mradi huu hasa kwenye Wilaya ya Karagwe na Jimbo la Korogwe Vijijini sio ya kuridhisha. Kwenye mradi huu kwenye Awamu III mzunguko wa kwanza Korogwe ilipangiwa vijiji 16 mpaka sasa umeme umewashwa kwenye vijiji saba tu.

Mheshimiwa Spika, tulileta maombi ya kupelekewa umeme kwenye vijiji 67 katika Mradi wa *REA,* awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza. Ni vyema Wizara ituambie baada ya bajeti hii tutapata umeme kwenye vijiji hivyo vyote au hapana?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na shida ya kuunganisha umeme kwa wakati, viko Vijiji vya Kulasi, Kibaoni na Mswaha Majengo vimesimikwa nguzo tangu mwaka 2018 mwezi Oktoba, lakini mpaka sasa umeme haujafika katika vijijji hivyo. Mkandarasi anasema tatizo ni tofauti ya *transformer* kati ya *size* inayotamkwa kwenye mkataba ambayo ni 33 *kv* na *size* ya *line* iliyopo ambayo ni 11 *kv*. Tofauti hii haijafanyiwa kazi muda mrefu na kusababisha malalamiko.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara Korogwe tarehe 19 Mei, 2019 alitoa maelekezo kuwa Kijiji cha Mahenge kipelekewe umeme. Umeme huo unatoka Kijiji cha Kerenge Kibaoni, Jimbo la Korogwe Vijijini lakini kuna vitongoji viwili vya Antakae na Mianzini vinapitiwa na umeme huo ukienda Mahenge. Naomba sana vijiji hivi visirukwe.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kupongeza Wizara na hasa utendaji uliotukuka wa Waziri na Naibu wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa dhati kabisa ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme kule Rufiji. Ni wazi kuwa umeme wa maji utashusha gharama za umeme hivyo wananchi wengi kumudu gharama, lakini pia uwekezaji utakuwa rahisi kumudu ushindani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ilipata umeme kwa mara ya kwanza mwaka 2013 kwa mpango maalum wa Serikali. Vijiji vilivyopatiwa kipindi hicho ni 23 kati ya 93 kwa bahati mbaya sana *REA* awamu ya kwanza nay a pili Nanyumbu ilikosa. *REA* awamu ya tatu Nanyumbu ilipatiwa Vijiji 13 tu. Niliomba nyongeza ya vijiji 17 ili kufanya vijiji 30, ombi ambalo Waziri alikubali kwenye mkutano wa hadhara katika uzinduzi wa *REA* awamu ya tatu pale Michiga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunatarajia kufikia asilimia 84 ya vijiji vitakavyopata umeme ifikapo 2020, naomba kufanyika upendeleo wa maeneo yaliyobaki nyuma kama Wilaya ya Nanyumbu. Vijiji vilivyopo kati ya Mangaka na Lumesule ambapo *HT* imepita na vijiji hivyo kukosa umeme, vipewe kipaumbele katika utekelezaji wa *REA III*.

Mheshimiwa Spika, Mjini Mangaka, Makao Makuu ya Wilaya ya Nanyumbu maeneo mengi hayana umeme, hasa Mtaa wa Mchangani, nashauri eneo hili lifanyiwe kazi haraka. Mji wa Mangaka unapata maji toka kwenye bwawa la Kijiji cha Mara ambapo maji yanasukumwa kwa kutumia jenereta ambapo linaharibika mara kwa mara pia gharama za uendeshaji huwa juu.

Mheshimiwa Spika, naomba umeme uende katika eneo hili. Endapo tutapeleka umeme eneo hili tutakuwa tumevipatia vijiji vya njiani umeme ambavyo ni Matimbeni *KCU* na Sengenya *KCU*.

Mheshimiwa Spika, kasi ya mkandarasi anayefanya kazi Mkoani Mtwara ni ndogo, hadi sasa ni kijiji kimoja tu ndio kimewashwa na vijiji vingine ni hatua ya kusimika nguzo.

Mheshimiwa Spika, nashauri katika kutengeneza mpango wa kupeleka umeme eneo fulani REA izingatie ushauri wa wataalam wa eneo husika, kwani nimeona makosa ambayo kama aliyepanga angekuwa ni mwenyeji baadhi yake yasingetokea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu kuelekea Serikali ya viwanda nchini, hivyo, kupitia hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeishauri Serikali kwa sababu Wizara hii imeelemewa na inahitaji uzalishaji mkubwa na usambazaji wa kutosha kwa walipakodi, hivyo iko haja sekta ya uzalishaji na usambazaji vikajitegemea ili ifanye kazi kwa ufanisi na wananchi na wananchi wafikiwe na umeme kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, uunganishaji wa huduma za umeme; bado kuna tatizo gharama ziko juu, usumbufu kwa wananchi ambao tayari wameshaunganishwa na waliokamilisha mchakato lakini bado hawapati umeme, mijini na vijijini bado kuna tatizo. Tanzania ni nchi ya 83, kati ya 190 duniani kushindwa kuunganisha umeme kwa viwango, hivyo naishauri Serikali, iongeze juhudi katika kuwekeza kwenye ujenzi wa mabwawa na umeme wa upepo ili kupunguza pia gharama za umeme.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha gharama za umeme na Mataifa mengine Marekani 0.12, Ethiopia senti 2.4, Afrika Kusini 7.4, Misri 4.6, China na Korea senti 8.0 na Tanzania inalipa zaidi ya senti 10.7 dola kwa *unit.* Hiki ni kiasi kikubwa tofauti na nchi nyingine na hii inapelekea gharama za uzalishaji kuwa juu, *production costs* na hivyo kupelekea bidhaa kuwa juu nadhani Serikali ya Viwanda haitafikia malengo kama haitaweza kupunguza gharama hii.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli Rais kwa jinsi anavyoiongoza nchi yetu. Hata hivyo, Watanzania wanakiri kuwa Mheshimiwa Rais amechelewa kupokea uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Medard Matogolo Kalemani Waziri wa Nishati, Naibu Waziri na waandamizi wake kwa jinsi wanavyotumikia nafasi zao. Aidha, tunawaombea utume mwema katika kutimiza majukumu yao kwa Taifa la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimesikitika kukosa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara hii. Hoja yangu ni kutaka Mheshimiwa Waziri wakati wa kutupa hitimisho lake atuambie ni lini mradi wa *REA III* utafikisha umeme katika Makao Makuu ya Kata za Gunyoda, Muray, Silaloda, Gunyoda kwa kuwa mradi wa *REA* awamu ya kwanza ulifika Mbulu 2007 mpaka leo kuna vijiji 38 na kata tano ambazo bado *line* kubwa

haijafika ukiacha vijiji vingi ambavyo umeme umepita bila kufika kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Spika, naomba uchunguzi wa kina ufanyike katika mradi wa umeme wa *REA 1 – II – III* kuhusu idadi ya nguzo zilizopelekwa kwani wananchi wanalalamika kuwa ni nguzo nyingi zinazoletwa katika halmashauri ya mji wakati huo mradi hauendi wala kusambaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Kalemani alitoa ahadi ya kupeleka umeme katika Kata ya Muray toka mwaka 2016 akiwa Naibu Waziri mpaka leo umeme haujafika. Hivyo tunaelekea uchaguzi, kauli ya Mheshimiwa Waziri ni kauli ya Mheshimiwa Rais, hivyo basi, naomba kauli ya Serikali vinginevyo nitashika shilingi ni lini umeme wa *line* kubwa utafika kwenye Kata za Muray, Gunyoda, Silaloda na Soheda kupitia Mradi wa *REA III* katika Jimbo la Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Spika, la pili, Serikali ina mkakati gani wa kusambaza chombo cha Umeme Tayari (UMETA) ili kupunguza gharama kubwa ya nguzo, waya na kazi zingine katika maeneo ya vijijini kwani mahitaji ya umeme katika kaya za vijijini ni taa, kuchaji simu hivyo chombo hiki ni muhimu sana

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maeneo mengi ya *REA* awamu ya I – II – III yamerukwa katika Jimbo la Mbulu Mjini na kwa kuwa kuna shule nyingi za msingi, sekondari, Makanisa yaliyoachwa toka 2008. Nashauri ziara za viongozi wetu hususan Mawaziri inapotokea basi wawasiliane na Waheshimiwa Wabunge badala ya *TANESCO* kupanga ratiba ya ziara hizo ili Mbunge naye atoe ushauri wake kumsaidia Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Medard Kalemani alikuja kuzindua Mradi wa Umeme wa *REA* Jimbo la Mbulu Mjini katika Kata ya Ayomohe 2018 mwezi Mei lakini mpaka

leo hakuna majengo yaliyosambaziwa hali hii imewapa mshangao wananchi wa Kata ya Ayamohe, naomba Waziri afanye tena ziara mapema mwaka huu ili kuleta msukumo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nachukua nafasi hii kuwaombea watumishi wetu wa *TANESCO* Mkoa na Wilaya ya Mbulu waliotangulia mbele za haki Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake usio na mwisho. Aidha, naomba Wizara iwateue watendaji wa nafasi hizo ili kuimarisha utendaji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Napenda pia kuwapongeza uongozi wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya wakisaidiana na watendaji wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliniahidi huduma ya umeme katika vijiji vyangu 50 vilivyobakia na ambavyo kampuni ya *SPENCON* ilishindwa kazi waliyopewa. Naomba kujua upelekaji wa umeme wa *REA* umefika wapi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Mamlaka ya *TPDC* bado inakabiliwa na changamoto za madeni na ukusanyaji usioridhisha na wadaiwa. Kwa taarifa ambazo zinaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania hasara ya shilingi bilioni sitini na nne na milioni mia tano arobaini na tatu (64,543,000,000) limepata.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo shirika haliwezi kujiendesha kibiashara. Nimwombe Mheshimiwa Waziri ni wakati wa kuwa na mpango mkakati wa kuhakikisha wanalisaidia shirika hili madeni yote yanalipwa ili liweze kujiendesha kibiashara kwa manufaa ya Taifa.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekit, naomba kuchangia katika hoja hii kama ifuatavyo; kwanza naomba kuwashukuru kwa jitihada ya kuhakikisha umeme unaenea vijiji vyote vya Tanzania, hususan katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji vya Matola, Mamanyolo, Kitulile, Luponde, Lugenge na vijiji vya Wilaya ya Ludewa Makete na Wanging'ombe bado havina umeme. Naomba Waziri atusaidie kuhakikisha vijiji vyote vvya Mkoa wa Njombe vinafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, pia hapa Dodoma kuna maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme kama vile Kata ya Mtumba Mtaa wa Vikonje A karibu na majengo ya VIGUTA wananchi wanaomba umeme.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Gesi Asilia. Wananchi wengi wameshapata uelewa wa kutumia nishati ya gesi. Lakini tatizo ni kwamba gesi ni gharama. Naiomba sana Serikali ishushe bai ya gesi ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Medard Kalemani, Naibu wake, Mheshimiwa Subira Mgallu pamoja na watendaji wote wa Wizara. Mungu awatie nguvu kwa kazi yao hii ngumu, tuonaona wanavyochapa kazi. Maoni yangu ni kwamba katika Wilaya yangu ya Bukoba Vijijini bado kuna kata nyingi ambazo umeme haujafika, ni nyumba chache zimepata umeme, *REA I, II* ilikuwa unarukaruka nyumba nyingi, nikiwa na maana vitongoji na vijiji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu tusaidiane ili walau wapate nao mgao huo. Kuna wenye viduka vyao wanahitaji vitu vingine kuweka katika friji lakini wanashindwa, wanatumia jenereta. Mafundi

wa magari kuchomelea vyuma umeme ni shida wasaidie wananchi ili kazi zao ziende vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine, katika vijiji hivyo kuna vitongoji ambako kuna zahanati; katika zahanati hizo kuna dawa zinazopaswa kuhifadhiwa katika friji; umeme hawana na hivyo dawa zinaharibika. Niwaombe hilo liangaliwe kwa jicho la huruma, siwezi kutaja ni vijiji vingapi, ni vingi havina umeme.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu najua ninyi ni wasikivu san sana. Maoni yangu msiyatupe katika *dustbin* tufikirie tupatiwe walau sehemu kubwa, wanufaike na umeme.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawatia moyo Mungu awabariki sana, lakini tukumbuke sana Bukoba Vijijini umeme ni shida. Ahsante.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho zuri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kutimiza ndoto ya Hayati Mwalimu Nyerere ya kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa kuzalisha umeme na Rufiji *Hydro Power,* maarufu *Stiegler's Gorge.* Ushauri wangu, miundombinu wezeshi kuelekea eneo la mradi husuan barabara ya kutoka Kibiti kwenda Mloka iwekwe lami kurahisisha usafiri kati ya meneo hayo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa *REA* katika Wilaya ya Mafia unaendelea vizuri na tunaishukuru sana Wizara na Serikali. Hata hivyo mradi wa kupeleka umeme wa jua *(solar)* katika visiwa vidogo vya Jibondo, Chole Jauni na Bwejuu ulikuwa uanze tangu Mwezi Septemba, 2018 lakini mpaka sasa hakuna dalili ya kuanza kwa mradi huo. Nichukue fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri atuharakishie kuanza mradi huo na wananchi tulishaahidi na wamekuwa wakiulizia sana.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mafia inapata umeme unaoalishwa kwa kutumia mafuta ya *diesel* na ni miongoni mwa wilaya chache ambazo bado hazijafungamanishwa na *grid* ya taifa. Natambua juhudi za Serikali katika kutuletea nishati mbadala kama umeme wa jua na umeme wa upepo. Ningependa kuishauri Serikali, kutokana kukua kwa shughuli za uzalishaji wa viwanda mahitaji ya umeme katika Kisiwa cha Mafia yanakaribia kufika *megawatt* 5. Namna bora kwa sasa ni kutuletea umeme kutoka nje ya Kisiwa cha Mafia kupitia uzamishaji wa nyaya chini ya bahari *(sub-marine cables)* katika umeme unazalishwa kwa vyanzo vya gesi kutoka Somanga Fungu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ujazilizi *(Densification)* kwa Vijiji vya Wilaya ya Mafia. Nilete ombi rasmi kwa Vijiji vya Bweni, Kanga, Jimbo, Banja, Juju, Kiwenje, Balemi, Kifinge, Kunjwi, Kibada, Gonge, Ndagoni, Marimbani, Kiegeani, Chemchem, Mlongo, Mibulani na Dongo. Vijiji hivi vimepitiwa tu na mradi wa *REA* katika awamu hii.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mafia imebahatika kuwa na kisiwa cha gesi eneo la Ndagoni kilichochimbwa na kampuni ya *(M and P).* Kwa bahati mbaya kwa awamu ya kwanza walikosa gesi baada ya kuwekeza fedha nyingi ilipokuja sheria mpya ya gesi *(M and P)* wanalazimika sasa kuomba upya leseni ya uchimbaji. Ushauri wangu kwa Serikali ni kuangalia namna ya kuleta *amendments* ya sheria kutoa mwanya kwa makampuni kama haya kuendelea na kazi za uchimbaji wa gesi katika Kisiwa cha Mafia.

Mheshimiwa Spika, *(M and P)* wamelazimika kutumia zaidi ya dola milioni moja kufukia kisima kule. La mwisho ni bei ya gesi asilia kwa viwanda kama Coca-Cola, Goodwill, Dangote n.k. ni kubwa, ipunguzwe.

Mheshimiwa Spika, nasukuru naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani

na Mheshimiwa Naibu Waziri Subira Mgalu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha wananchi wanapata umeme.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo mawili. Kwanza maeneo ambayo hayana umeme. Katika Jimbo la Mufindi Kaskazini Kata ya Mpangatazara yenye Vijiji vya Mpangatazara na Kimbwe hakuna umeme kabisa. Pia katika Kata ya Ikwila hakuna umeme Kijiji cha Ikwila, Ilangamoto, Ugunza Kata ya Igombavanu, Vijiji vya Uhembila na Matikitu Kata ya Sadani Vijiji vya Ufosi na Mbugi, Kata ya Kobanga Kijiji cha Kipanga Kata ya Mdabulo Kijiji cha Ilasa, Kata ya Mapanda kijiji cha Chozo, Uhafiwa Ihimbo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kuhusu mahusiano yetu ya wananchi wa Tarafa ya Kibengu na *TANESCO.* Mara ya mwisho mimi pamoja na Mheshimiwa Diwani wa Mapanda pamoja na Wenyeviti wa Vijiji wa Kata ya Mapanda pamoja na *TANESCO* tulifanya kikao kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani na *TANESCO* waliahidi kuboresha miundombinu kwenye Barabara ya Uhemi, Uhafiwa mpaka Ihimbo; na barua waliniandikia mimi Mbunge kama mwakilishi wa wananchi. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa tunaenda mwaka wa pili hata kilometa moja hawajatengeneza.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Mheshimiwa Waziri aingilie kati. Juzi nilikutana na *DG* wa *TANESCO* naye aliahidi kama mwanzo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni gharama kubwa ya kuingiza umeme wa bwawa la Mwenga lililopo Wilaya ya Mufindi. Gharama zimekuwa kubwa sana kuliko zilizoelekezwa na Serikali, pia wana tabia ya kuwatishia watu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri aje katika jimbo langu kama alivyoahidi ili aone hali halisi na matatizo wanayoyapata wananchi kutokana na ukiritimba na wawekezaji wa Mwenga *Hydroelectric power.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuwapongeza Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Wizara hii ya Nishati katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Naishauri Serikali kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, pia naishauri Serikali ianze kutumia nguzo za zege katika usambazaji wa umeme mijini na vijijini maana ni madhubuti na pia tutaepuka na uharibifu wa mazingira kwa kukata miti hovyo kwa ajili ya kupata nguzo za miti.

Mheshimiwa Spika, tatu naishauri Serikali ipunguze gharama ya uunganishaji wa umeme hususan maeneo ya mijini maana ni ghali sana. Ikipunguzwa wananachi watakuwa na uwezo wa kugharamia na kupata umeme maeneo mengi ya nchi yetu. Kuna vijiji vimepitiwa na nguzo za umeme jirani kabisa lakini hadi sasa vijiji hivyo havina umeme. Serikali ione sasa haja ya kuvipatia vijiji hivyo umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nne bei ya umeme hususan mijini kwa matumizi ya majumbani kwa *unit* ni ghali mno. Naishauri serikali hii ya wanyonge angalau ipunguze bei ya umeme kwa *unit* maana ni kubwa sana. Pia naishauri Serikali kuhusu *PINOT Project* ya usambazaji gesi majumbani kwa bei nafuu, iliyofanywa maeneo ya Mikocheni Jijini Dar es Salaam. Huduma hii isambazwe katika maeneo mengi ili iweze kuwafikia wananchi wenye kipato cha chini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ianzishe kozi katika vyuo vyetu vikuu hapa nchini kwetu vya kudahili wanafunzi kusomea masuala ya gesi ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha kutoka hapa hapa nchini. Pia gharama za kusoma kozi ya gesi nje ya nchi, kwa mfano Uturuki, China na kadhalika ni gharama kubwa sana. Hivyo kozi hii ikianzishwa katika vyuo vyetu wanafunzi watapata fursa ya kusoma kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iajiri watendaji wa watumishi wa kutosha katika Wizara wengi wamekaririshwa na hawawezi kutoa maamuzi katika maumbo mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawaombea afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake ili waweze kutekeleza majukumu yao ya kuwatumikia Watanzania katika kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo nchini mwetu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nilizungumza juu ya hoja hii, lakini muda wa dakika tano ni mdogo sana. Hivyo nina jambo la pili ambalo ni kuhusu ubora wa mafuta ya petroli na dizeli hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la 10, Bunge lilichukua hatua ya pekee ya kuzuia wenye vituo vya mafuta kuchakachua mafuta ya petroli na dizeli kwa kuichanganya *petrol + kerosene* na *diesel + Kerosene.* Lengo la wafanyabiashara ni kupata faida kubwa sana. Hivyo, Bunge likapandisha bei ya *kerosene* iwe karibu sawa na *diesel* au *petrol.*

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa miaka mitano sasa tatizo la kuchakachua mafuta ya *petrol* na *diesel* limerudi upya. Takriban vituo vyote vya mafuta leo katika Miji ya Mwanga, Moshi, Arusha, Dodoma, Dar-es-Salaam, Morogoro, Singida, wanauza mafuta yaliyochakachuliwa. Yaelekea kuwa, wafanyabiashara wanaoleta mafuta ya taa kwa bei rahisi kutoka nje (bila kodi) na kuyasambaza nchi nzima. Nchi yetu inapata hasara kubwa sana kwa kutumia mafuta ya kuchakachua, yanaharibu magari, *pump,* mitambo na viwanda.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanatokea na *EWURA* wapo. *EWURA* walishindwa kazi ndiyo maana Bunge likachukua hatua. Sasa mafuta yanachakachuliwa sana, huu ni wakati wajue kuwa si heshima kuendesha ufisadi. Waziri wawajibishe *MD* na *Management* yote ya *EWURA,* weka watu walio tayari kufanya kazi na Dkt. John Pombe Magufuli.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kubwa kwako Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa *REA* na *TANESCO.* Umeme utekelezaji unaendelea, lakini nguzo hakuna na waya. Nimeenda juzi nyumbani mafundi wanakaa wanangoja vifaa. Hata hivyo, nashukuru kwa kuongeza *scope,* asanteni, ila hiyo ndiyo inayoshusha *performance* ya utekelezaji wa Ilani.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* haina hasara kamili kutokana na kulazimika kama shirika la nchi kupeleka umeme hata maeneo yasiyolipa kwa sasa kama kichocheo cha uchumi na si tu kibiashara. Serikali inatimiza jukumu hilo kupitia Shirika lake la *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, hongereni kwa *Stiglers* na pia, kuwapa gesi Dangote. Viwanda oyee!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, umeme ni nishati muhimu sana na bila umeme wa uhakika tusitarajie Tanzania ya Viwanda wala maendeleo ya kasi. Kwa bahati nzuri sana Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi sana ikiwemo upepo, makaa ya mawe, gesi asilia na maji. Tunatambua kuwa umeme wa maji ndio ulio na bei rahisi zaidi, ila angalizo la chanzo cha maji ni mabadiliko ya tabianchi.

Inashangaza sana kuona tumeshadadia mradi wa *Stiegler's Gorge* bila kuchambua kwa kina uwezo wake *(sustainability).* Ni lazima tujiulize maswali yafuatayo; je, baada ya miaka mitano na kwa kuzingatia mabadiliko ya tabianchi tutakuwa na maji toshelezi? Hasa ikizingatiwa mvua ndicho chanzo kikuu? Swali la pili, je, athari za kimazingira zimezingatiwaje, hasa kuzingatia ukatwaji mkubwa wa miti?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbai zilizofikiwa kwa mradi huu na kwa kuwa kufanya kosa si kosa bali kurudia kosa, naomba kwa heshima kabisa Serikali ibadili msimamo wake na kuacha kabisa mradi huu ambao athari zake ni kubwa kuliko faida.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu nimehoji sababu ya wateja wa umeme kulipia nguzo wakati nguzo hizo zinakuwa mali ya *TANESCO?* Kwa nini wakati tuna simu za *Tanzania Postal & Telecommunications* hatukulipia nguzo? Sasa ni sababu zipi zinafanya aliyewahi na kununua nguzo 10 wale wateja wapya watakaotumia nguzo zangu wasinilipe fidia? Wao watalipa *service charges* tu?

Mheshimiwa Spika, umeme wa *REA* ni muhimu sana hivyo, tunaomba *REA III* iongezwe kasi ili vijiji navyo viweze kuendelea na kupunguza kasi ya vijana kuhamia mijini.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, napendekeza Wizara ione umuhimu wa kuleta Sheria ya Mafuta Namba 21 ya Mwaka 2015 Bungeni ili Bunge liweze kufanya marekebisho ya sheria hii. Ni rai yangu Serikali iweze kurejesha mamlaka ya Waziri katika kutoa leseni za vitalu, lakini pia, vibali vya uchimbaji wa *gas & oil.* Ni ushauri wangu Serikali iweze kuondoa sharti la sheria la asilimia 3 kwenye Mfuko wa Rasilimali ya Gesi na Mafuta ili kuruhusu matumizi ya Mfuko wa Rasilimali ya Gesi na Mafuta kwenye miradi ya maendeleo. Mathalani shughuli za usambazaji wa gesi majumbani.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha kuona umuhimu wa kutoa fedha yote kama ilivyoombwa na Taasisi ya *TPDC* juu ya uanzishwaji wa Kituo cha *CNG (ie, Compressed Natural Gas)* Mlalakuwa, Ubungo. Taasisi hiyo kupitia Wizara ya Nishati imeomba kiasi cha takribani TShs. bilioni 16; hapa ninapochangia mabasi ya *UDART,* yaani mabasi ya mwendokasi 300 yatakayoingia Tanzania Mwaka wa Fedha 2019/2020 yote yatatumia *CNG.* Mbali na hapo, tayari *TPDC* imeshapokea maombi ya wateja wakubwa wanne, wawili Kigamboni, wawili Kibaha, Pwani. Ninaona tuna sababu ya msingi ya kuhakikisha *PST* kupitia Wizara ya Fedha inatoa fedha zote kama ilivyoombwa na Taasisi ya *TPDC.*

Mheshimiwa Spika, pia ninashauri Serikali i-*support* pendekezo pamoja na kiasi cha fedha kilichoombwa na

Wizara katika ukarabati wa *Tank Number 8* la kuhifadhi *oil & gas,* yaani *Strategic Oil & Gas Reserve Tanks,* kwani kwa kufanya hivi Wizara itaondokana na adha ya ukodishaji wa maghala ya kuhifadhi mafuta na gesi. Tanzania leo hii ina *reserve* ya gesi kiasi cha futi za ujazo trilioni 57.54, lakini pia, Tanzania ina lita za petroli milioni 125.22, dizeli lita milioni 94.78 pamoja na mafuta ya taa na ya ndege lita milioni 18.34. Hivyo ninaona umuhimu mkubwa wa Wizara ya Fedha kuona umuhimu wa kutoa fedha zote za ujenzi na ukarabati wa *Tank Number Eight* kama ilivyoombwa na *TPDC.*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe nchi ya Japan ambayo haina gesi ardhini ina *reserve* kubwa ya *gas & oil,* na hata Trinidad; zote hizi zina *reserve* kubwa ya gesi kwa sababu walikubali kwanza kuwekeza kwenye miundombinu ya kuhifadhi *oil & gas.*

Mheshimiwa Spika, na mwisho, *NAT Oil* ambayo ni Taasisi ya Serikali kwenye biashara ya gesi na mafuta; ninashauri kwa moyo dhati Sheria ya Petroli iletwe Bungeni, ili *TPDC* iweze kushindana na kampuni za kigeni, kwa mfano *Trafigura Oil & Gas Company from Singapore*, Kampuni ya Addax, kampuni ya Uswizi iliyowekeza kwenye tasnia ya gesi na mafuta ambayo pia ndiyo kampuni ya *Oyrx. Vilevile* hata Kampuni ya *TOTSA from France* yenye umiliki wa *Total* pamoja na Sahara *from* Nigeria.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Asante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kwenye sekta hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na usalama. Tumeshuhudia shughuli nyingi za maendeleo zikikwama kwa ajili ya ukosefu wa nishati. Akina mama wajawazito wanapoteza maisha pale wanapojifungulia kwenye zahanati/vituo vya afya ambavyo havina umeme na wanatumia *torch* kuzalishiwa. Kwenye hospitali kubwa ambazo hazina *generator* ikiwa mgonjwa anafanyiwa *operation* na umeme ukakatika basi kuna vifo vya mama na watoto hutokea ikiwa ni pamoja na wagonjwa wengine wenye kufanyiwa *operation.*

Mheshimiwa Spika, umeme unasaidia uchumi wa nchi yetu kwani wananchi wetu wataweza kujishughulisha na uchakataji wa mazao ghafi, viwanda mbalimbali vikubwa na vidogo vitaanzishwa, wafanyabiashara wa chini, kati na juu wote watafaidika. Lakini muhimu kuliko yote ni usalama kwa raia, maana mwanga, hasa vijijini utasaidia sana kupunguza uhalifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huu naomba Waziri na Naibu Waziri ambao wamekuwa mara kadhaa wakizunguka kufuatilia utekelezaji wa miradi, hasa ule wa *REA,* lakini maeneo mengi ya Mji wa Tarime hayana umeme. Mji wa Tarime una kata nane, lakini umeme ni chini ya asilimia 40. Umeme upo Kata ya Bomani kwa asilimia zaidi ya 90, Kata ya Nyamisangura ina umeme kwa asilimia 50 tu, Kata ya Nyandoto ni kwa asilimia 20, Kata ya Kenyamanyori ni chini ya asilimia 20. Maeneo ya Kogete, Tagotha, Mubali**,** Kenyamanyori *Cnetre,* Lobasa, Kebaga *Mining,* Makao, Nyamitende, havina umeme. Kata ya Katare nayo ina umeme chini ya asilimia 30, maeneo ya Nkongore yenye zahanati, shule ya msingi na sekondari havina umeme. Kata ya Nkende nayo haina umeme kwa zaidi ya asilimia 70 za wakazi wake, maeneo ya Magena yenye Kituo cha Afya na shule ya msingi, Katare, Itebe, Nyamihito, Nyamitende, Kata ya Nyandoto, maeneo ya Kewoje, Nyagisesa wanapojenga Mji Mpya na nyumba za Askari Polisi na Kanda Maalum Tarime/Rorya.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Mji wa Tarime ndio Makao Makuu ya Wilaya ya Tarime, ni mji wa kimkakati maana upo mpakani. Wenzetu upande wa Kenya umeme unawaka vyema na kutoa mandhari nzuri wakati wa usiku ilhali upande wa Tanzania Mji wa Tarime ni giza totoro. Ni vyema Serikali ikatoa kipaumbele kwenye miji kama Tarime iliyokaa kimkakati. Nitaomba *commitment* ya Serikali maana *REA* inapita kwenye baadhi ya maeneo tu kwenye kijiji na kata na si wakazi wote. Hii inaleta mtafaruku mkubwa na wananchi wanahisi kubaguliwa. Ni rai yangu Serikali kuhakikisha Mji wa Tarime kata zote nane za Nkende, Nyandoto, Katare, Turwa, maeneo ya Buguti, Nyamisangura,

Bomani, Kenyamanyori na Sabasaba wapatiwe *either* umeme wa *REA,* hasa kata za pembezoni, *densification,* na umeme wa *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, lakini ya umuhimu naomba kuwasilisha, lakini bila kusahau mradi wa Kinyerezi ambao kwa kweli Serikali ikiwekeza vyema itasaidia sana kupunguza kero ya umeme. Ila nishauri Serikali kupeleka wataalam nje ili waweze kuwa na ujuzi kwenye uendeshaji wa mradi wa Kinyerezi, na pia utengenezaji wa mitambo inapoharibika au kui-*service* kuliko sasa kuipeleka mitambo Marekani kwa ajili ya *service.*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana na kwa wanavyojitoa katika kuwatumikia Watanzania na kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata umeme vijijini kwa maendeleo yao; lakini pia kwa kutekelea Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, mkandarasi wetu Wilaya ya Nyang'hwale kasi yake sio nzuri sana ya kusambaza umeme. Sababu anazozitoa anadai kwamba yeye amekwamishwa na upungufu wa nyaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ili kuhakikisha usambazaji huu wa umeme kwa Wilaya ya Nyang'hwale tutatulieni tatizo hilo la nyaya kwa wakandarasi wako. Ukizingatia tunaenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mtaa na Uchaguzi Mkuu 2020.

Mheshimiwa Spika, pale Makao Makuu ya Wilaya ya Nyang'hwale, yaani Khalumwa tayari umeme upo ila baadhi ya maeneo mengi ya Mji wa Khalumwa hayana umeme na sababu kuu ni upungufu wa nguzo na nyaya. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tutatulie mapungufu hayo, wananchi wako tayari kufunga umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Umeme wa *REA*. Tumeshuhudia Mawaziri wakizindua umeme kwenye nyumba za tembe, nyumba za nyasi, nyumba ambazo kwa upepo kidogo tu zitaanguka. Hivi kuna haja gani kuweka umeme ambao siku nyumba zikianguka mnaweza kusababisha madhara? Tumeshuhudia mijini tu shoti ya umeme nyumba zinaungua na kuteketea. Kwanini Wizara isingeshirikiana na *TASAF* kwanza zikaboreshwa nyumba za Watanzania (kaya) maskini kabla ya umeme?

Mheshimiwa Spika, umeme *REA Phase ll.* Katika Manispaa ya Morogoro Kata ya Mindu inapitiwa na umeme wa *grid* ya taifa lakini wananchi wake hawana umeme katika baadhi ya maeneo. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Morogoro na wananchi walitoa malalamiko hayo; kwanini mpaka sasa wananchi hawapati umeme?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu *Stieglers George Project.* Watanzania wanapaswa kuona mkataba huo. Tafiti zilizofanywa na *World Energy Resource* zinaonesha kuwa *project* hiyo itatumia fedha nyingi zaidi ya kiwango kinachotarajiwa. Ni vyema Watanzania tukawekwa wazi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kidunda Morogoro uliokuwa na mpango wa uzalisha umeme *MW 20,* ulikuwa na mkakati wa kuendeleza kilimo, kutoa maji kwa wakazi wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga na kadhalika. Kuna haja gani Serikali kuanzisha *project* hazi-*take off* mna-*jump* kwenye *new project?* Kidunda bado tupo *Stiegler's*, gesi bado tumekimbilia *Stieglers?*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mradi wa umeme Kinyerezi, Dar es Salaam- Arusha kupitia Kibaha-Chalinze, wakazi wa Kata ya Kinyerezi kwenye mitaa ya Kiboga na Kifuru walifanyiwa tathmini kwa ajili ya kupisha mradi wa njia ya umeme tangu mwezi Septemba, 2016, lakini mpaka sasa mwaka wa tatu wamesimamisha shughuli za maendeleo na Serikali hawaelezi chochote. Katika majumuisho yake Mheshimiwa Wizara ieleze ni lini hasa wananchi hao watalipwa fidia?

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ieleze katika Kata za Jimbo la Kibamba za Kwambe, Mbezi, Msigani, Goba, Saranga na Kibamba yapo maeneo mpaka sasa umeme haujafika. Ni lini *TANESCO* itahakikisha maeneo yote yanafikishiwa umeme? Katika kata hizo kuna kawaida pia ya umeme kukatikakatika na kupungua nguvu *(low voltage).* Serikali katika swali langu Bungeni iliahidi ufumbuzi lakini mpaka sasa tatizo hilo limeendelea.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada nyingi anazofanya Waziri Kalemani katika kuhakikisha kwamba Tanzania yote inawaka umeme ifikapo 2021 bado jitihada hizi zinakwamishwa na baadhi ya watendaji na wakandarasi. Mawaziri wa Wizara hii wameongea mara nyingi kuwa umeme ukifika kwenye kijiji chochote utafika kila taasisi, kitongoji, lakini kinachofanyika Tanzania hii ni tofauti na kauli za Mawaziri. Katika Wilaya ya Karatu Vijiji vya Huduma, Khusumay, Kauam, Rhotia, Losetete umeme haujaenda kwenye vitongoji bali umeishia kwenye *centers* za vijiji wananchi wanalalamika sana kwani imeme haujafika kwenye vitongoji.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limesababishwa wa timu za *survey* ambazo hazikuwasilishwa viongozi wa wananchi. Timu hii maeneo mengine walikwenda hata siku za jumapili na walifanya wenyewe bila kushirikisha viongozi wa wananchi. Niishauri Serikali itoe maelekezo ya kutosha ili *survey* inapofanyika viongozi wa wananchi washirikishwe ili maeneo yote yafanikiwe.

Mheshimiwa Spika, leo ni mwezi wa tano mwishoni na bado katika Wilaya ya Karatu, Vijiji vya Bugeu, Ayalaliyo, Endanyawe, Kambifairu, Umbang Laja, Quvus. Lositete, Endalals, Bawakta, Mangola Juu pamoja vitongoji vyake bado umeme haujafika. Wananchi wameshajiandaa katika maeneo hayo na wanasubiri wakandarasi. Niombe Waziri uwaelekeze wakandarasi ili wakamilishe kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Waziri, Dkt. Kalemani kwa kutoa *transformer* tisa ili kuunga visima tisa vya

maji kwenye umeme. Kwa niaba ya wananchi wanaotumia visima hivyo nimshukuru sana Waziri. Hata hivyo, nimuombe Waziri afuatilie *transformer* moja ambayo haijafungwa katika kisima cha Endamavamek, kijiji hiki kiliombewa *transformers* mbili lakini imefungwa moja tu.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Nishati. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuwasilisha hotuba hii kwa umakini mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Bomba la Mafuta Kutoka Uganda – Tanga. Napenda kuipongeza Serikali na Wizara kwa kufuatilia kwa karibu sana juhudi za kufanikisha mradi huu wa bomba la mafuta kutoka Uganda – Tanga, Tanzania. Tuna bahati kubwa kupata fursa hii ya kipekee. Pamoja na vigezo kadhaa vilivyotumika kutupatia mradi huu lakini kigezo cha amani na usalama katika nchi yetu pia kinapaswa kuzingatiwa na Watanzania. Hivyo ni wajibu wetu Watanzania sote kupitia Serikali na Wizara kuilinda amani hii na kuthamini fursa hii tuliyopewa na jirani zetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu; katika jambo hili kwa Serikali ni kuendelea kuwashirikisha wananchi wote wa maeneo husika kwa kuwaelimisha faida na hasara zake. Wananchi wa maeneo hayo watakapopata elimu watajiweka katika nafasi ya kujiona kuwa bomba hili ni lao na watachukua hatua za kulilinda na kulienzi.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati kwa njia ya maandishi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Kalemani, Waziri wa Nishati pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi nzuri wanayofanya ya

kusimamia shughuli nzima ya usambazaji wa umeme katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umakini wa Wizara katika usambazaji wa umeme bado kumekuwa na changamoto ya wakandarasi wa kutekeleza miradi ambapo huchukua muda mrefu tofauti na mikataba inavyotaka. Nazidi kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa kusimamia umeme wa *REA.* Ombi langu ni kwamba wazidi kusisitiza vituo vya afya na shule yote ili kuweza kurahisisha huduma husika.

Mheshimiwa Spika, kabla sijahitimisha mchango wangu, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, aliwahi kuahidi umeme wa uhakika Kata ya Kibakwe, Wilaya ya Magu na bado wananchi tunakumbuka ahadi hiyo na tuna matumaini makubwa juu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani na Naibu Waziri Mheshimiwa Mgalu, wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu mradi wa *REA.* Liko tatizo eneo langu la Tabora Kaskazini. Mkandarasi hafanyi vizuri, kasi yake ni ndogo sana. Niliomba kipaumbele eneo la vijiji anavyotoka Mbunge ambako kuna vijii barabarani; Vijiji vya Kasenga, Majengo, Kanyenye, Ikongolo, Nzubuka na Izugawima. Vijiji hivi vyote viko barabarani na ndiko Mbunge anakotoka.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri rafiki yangu, ndugu yangu niletee umeme katika vijiji hivyo ni muhimu sana. Kuna shule za msingi tano na shule za secondari mbili na zahanati pekee katika kata hiyo ya Ikongolo. Nakushukuru sana sana Mheshimiwa Waziri tafadhali sana; vijiji vya Kasenga, Majengo, Ikongolo, Kanyenye na Nzubuka

ni muhimu sana. nakuomba Mheshimiwa Waziri Kalemani. Natanguliza shukrani.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Baada ya kuunga mkono hoja hii muhimu ya Wizara ya Nishati, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuitoa Tanzania gizani na kutupatia nishati ya kuendeshea viwanda.

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuishukuru Serikali kupitia Waziri kwa kututengea fedha kutoka fungu la *TANESCO* kwa ajili ya kupeleka umeme Makao Makuu ya Tarafa ya Ketumbeine yenye vijiji 20 ambavyo tangu mradi wa *REA* kuanzishwa nchini hadi leo hawajafaidika bado kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya ufanisi na uendelevu wa mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge,* naomba kushauri Serikali iwekeze kwa makini katika zoezi la kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya kupeleka maji kwenye Bwawa la *Stiegler's Gorge* yahifadhiwe na kutunzwa kwa gharama yoyote.

Mheshimiwa Spika, pili, katika usanifu unaoendelea na ujenzi wa *Stiegler's Gorge Dam,* ni vizuri Serikali izingatie na kujipambanua namna ya kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi. Serikali iwekeze katika kuwatafutia wananchi wanaotegemea maji ya vyanzo vinavyopeleka maji hadi Bwawa la *Stiegler's Gorge* vyanzo vya mbadala ili maji yote yaelekezwe katika mradi huu wa kuzalisha umeme kwa ajili ya utoshelevu na uendelevu wake majira yote ya mwaka hata katika majira ya ukame.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake ayajibu maswali mawili yafuatavyo; moja, ni lini vijiji 30 vya Wilaya ya Longido ambavyo bado havijafikiwa na umeme wa *REA;* watapata nishati hii? Ni vijiji vingapi vimeingizwa katika bajeti ya mwaka huu wa 2019/2020?

Mheshimiwa Spika, kuna vijiji ambavyo vimeshafikiwa na umeme lakini makazi yameongezeka na kuna vitongoji vingi havijapelekewa umeme bado. Mwaka huu wa fedha 2019/2020 Serikali imetenga fedha za kufanya ujazilizi katika vijiji vya Wilaya yangu ya Longido. Kati ya maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa mradi wa ujazilishi ni pamoja na vijiji vya Mundarara kwenye machimbo ya madini ya Ruby, Mairowa (Kata ya Engarenaibor), Namanga, Longido, Olmolog, Elerai, Kamwanga na vijiji vyote 20 vya Tarafa ya Ketumbeine ambavyo bado havijafikiwa na umeme wa *REA.*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nashukuru na natamka tena kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Ningependa kupata majibu ya Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya usambazaji umeme ndani ya Jimbo la Mlimba, pia ulipwaji wa fidia kwa wananchi kama nitakavyoainisha hapo chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa *low cost* ambao ulitekelezwa Jimbo la Mlimba tangu Kata ya Mchombe hadi Idete. Mradi huo pamoja na viongozi kadhaa kutembelea na kuzisikia na kuziona changamoto na kuahidi kuzitatua tangu mwaka 2017/2018; zilizosababishwa na mkandarasi; za kupitisha nguzo kwa rushwa na kukwepesha mradi eneo la makazi na kupitisha porini. Eng. Msofe tulipoongozana naye aliwasikia wananchi Kata zote za Idete, Namwawala, Mbingu, Igima na Mchombe.

Mheshimiwa Spika, Pia Waziri Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Mbunge alifanya ziara na kusikia kilio hicho na kuahidi wananchi na kumuagiza meneja ahakikishe anapeleka umeme kwenye mradi huo na Wizara itapeleka vifaa vya mradi huo ili wananchi wapatiwe umeme. Lakini hadi leo hakuna mabadiliko yoyote kwenye mradi huo na kufanya maagizo yote na ahadi ni hewa. Je, ni lini sasa Wizara itatatua matatizo kwenye mradi huo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufikishaji wa umeme kwenye maeneo ya huduma za umma kama shule, zahanati na masoko. Niliuliza swali Bungeni na kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri kuhusu mradi unaoendelea sasa, ambapo unapita jirani na Sekondari Kata ya Kamwene lakini mkandarasi hana bajeti ya kupitisha umeme na Waziri aliagiza umeme upelekwe huko na Sekondari ya Matundu Hill, Idete; lakini hadi leo hakuna utekekelezaji. Je, ni lini agizo hili la Waziri litatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia kwa wananchi wa Kata ya Utengule, Jimbo la Mlimba ambao walikubali kupisha mradi wa umeme mkubwa kutoka Kihansi kwenda Wilaya ya Malinyi. Wananchi wa Kijiji cha Mpanga walifanyiwa tathmini tangu mwaka 2014; pamoja na ahadi nyingi lakini hadi leo hwajalipwa.

Mheshimiwa Spika, nimeambatisha *document* za ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini kituo cha kupoza umeme kitajengwa Ifakara ili wananchi wa Kata ya Mofu ndani ya Jimbo la Mlimba watapelekewa umeme kama Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani ulivyoahidi? Kwamba Kata hiyo hiyo watapelekewa umeme baada ya kituo hicho kujengwa?

Mheshimiwa Spika, nasisitiza, kwamba Mheshimiwa Waziri awe na ufutiliaji wa karibu wa wakandarasi kwani miradi mingi inafanywa chini ya kiwango. Kwa mfano, mradi wa Mchombe - Idete, mradi wa Kihansi – Malinyi na kadhalika. Pia naomba kituo cha Mlimba kiongezewe gari la kazi kulingana na miundombinu yetu ambayo ni mibovu, hivyo meneja na mafundi hushindwa kufikia maeneo.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Wizara hii ikiongozwa na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi zote zilizo katika Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, Juhudi ziendelee za kutafuta vyanzo vingine tofauti vya kuzalisha umeme ambavyo viko hapa nchini. Vyanzo hivyo ni kama vile jotoardhi, umeme wa upepo, jua, maporomoka ya maji *(hydropower)* yaliyopo maeneo mbalimbali, urania na vinginevyo. Vyanzo hivi vitasaidia nchi yetu kuwa na uhakika wa umeme na wa kutosha vikisaidiana na miradi mikubwa inayoendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Umeme wa Rufiji ndio mkombozi na chachu ya maendeleo hapa nchini. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa uamuzi wa busara na wa kimapinduzi ambao utakumbukwa na vizazi vijavyo. Mradi huu utapunguza gharama za uzalishaji viwandani pamoja na kupunguza bei ya umeme kwa wananchi wetu maskini.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watendaji wetu wa kizalendo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya ya kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele wakiitikia wito wa kazi wa Jemedari wetu Mkuu, Kamanda wa maendeleo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Tanzania; Mwenyezi Mungu awabariki Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Jiji la Dodoma, kuna maeneo ya pembezoni hakuna umeme. Ninaiomba Serikali kupitia *REA* iwapatie umeme wananchi wa maeneo ya Kata ya Mbalawala, Kijiji cha Lugala, Kitongoji cha Matangizi na maeneo jirani ili wananchi wale wanufaike na umeme kwani wanapata taabu kwenda Nala kusaga nafaka zao na mahitaji mengine yanayotokana na huduma ya umeme. Hali hii ni shida kwao.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, kazi yenu ni njema sana, chapeni kazi na *TANESCO & REA* iendelee vyema, kazi zake zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ili niweze kuchangia kwa maandishi. Kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mradi wa Umeme; Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu *(REA III).* Natoa pongezi kwa jitihada ya Serikali ya malengo ya June 2020 kufikia Vijiji 10,278 na kufikia June 2021 Vijiji vyote vitakuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi Mkoa wa Morogoro katika Wilaya saba za Morogoro Vijijini, Mvomero, Gairo, Kilombero, Ulanga na Malinyi havijafikiwa na umeme, umeme umefika kwenye *centers* tu, nazo ni nyumba chache. Naomba umeme Awamu hii ya Tatu vijiji hivi kwenye Wilaya hizi vipatiwe umeme (Mpaka June 2020).

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Kujazilizia Umeme. Kuna Vitongoji vilivyorukwa kama Kimamba D Wilaya ya Kilosa, Vitongoji vya Mtego wa Simba, ikiwemo Chekeleni (karibu na Mikese Fulwe) ambavyo vimerukwa na umeme. Natanguliza shukrani kwa Naibu Waziri kwa sababu ulifika na kuwapatia umeme wananchi wa Kimamba A.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba umeme kwa vitongoji vilivyorukwa vya Kimamba A. Mheshimiwa Naibu Waziri alifika Mtego wa Simba (Morogoro Vijijini), nashukuru umeme wamepata, ila ziliwekwa *transformer* mbili sasa kwenye Kitongoji cha Zahanati ambapo kuna *transformer* ya pili na nguzo tayari zipo; ni muda mrefu sasa karibu mwaka mzima umepita.

Mheshimiwa Spika, tunaomba umeme kwa hivyo vitongoji vilivyorukwa (kwenye mradi wa kujazilizia).

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi pia kwa kupeleka gesi asilia majumbani, gesi itakuwa bei ya chini. Mheshimiwa Waziri kuna Mkakati gani wa kufikisha gesi hii kwenye Miji ya

Kibaha (Mkoa wa Pwani) na Mji wa Morogoro (Mkoa wa Morogoro)?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Mradi wa Umeme Mto Rufiji. Natoa pongezi kwa Serikali kwa mradi huu, Serikali tusonge mbele kwani tunahitaji umeme mwingi kwa mambo mbalimbali. Jambo lingine muhimu, miundombinu (barabara) za kufikia mradi zitengenezwe kwa wakati. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayoendelea, Jimbo la Mbeya Vijijini ambalo kwa kiasi kikubwa vijiji vyake vinalizunguka Jiji la Mbeya bado kuna kata tatu na Vijiji hakuna umeme.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iharakishe kuwa inapeleka umeme kwenye Vijiji vya Kata ya Maendeleo, Itawa na Kata ya Shizuri, ikiwa na vijiji vingine 42 ambavyo bado havijafikiwa na umeme. Kutokana na uchumi mzuri wa maeneo hayo kutakuwa na manufaa mapana kwa taifa letu na hata kuongeza kipato kwa Shirika la *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na faida za umeme unaotokana na jotoardhi, napendekeza pia Serikali iweke msukumo mkubwa wa upatikanaji wa umeme wa chanzo hiki cha jotoardhi ambao unategemea kuongeza *MW* 200.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Najiunga na Waheshimiwa Wabunge wote waliompongeza sana, Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Dkt. Medard Kalemani, Mbunge Chato na watendaji wote wa Wizara yake kwa usikivu, ushirikiano, weledi, ufanisi anaoutumia kutekeleza

majukumu yake kwa bidii sana. Kwa kweli tunamwombea heri na afya njema katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ileje katika Mkoa wa Songwe imekua mfaidika mkubwa wa REA awamu zote. Ileje ni Wilaya ambayo imekuwa nyuma kwenye eneo la miundombinu ya aina zote, kwa hiyo kupata umeme kutasaidia sana katika kuchochea maendeleo kiuchumi katika Wilaya hii.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya I na II aliacha vijiji vingi bila kuwekewa miundombinu ya umeme, ni mahali ambako laini kubwa imepita lakini watu hawajaunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, kati ya vijiji 71 vipo vijiji 24 ambavyo bado havina umeme. Ninaviorodhesha hapa kwa hatua za Mheshimiwa Waziri na watendaji wake.

Mheshimiwa Spika,

| Na. | Kata | Na. ya Vijiji | Kijiji |
|---|---|---|---|
| 1. | Bubigu | 1 | Mabula |
| 2. | Chitete | 2 | Chitete |
| 3. | Mbebe | 3 | Shinji |
| 4. | Ibaba | 4 | Shuba |
| 5. | Hale | 5 | Hega & Iwala |
| 6. | Humba | 7 | Yenzebwe na Nkanka |
| 7. | Ndola | 8 | Ibezya |
| 8. | Malangali | 9 | Chembe & Bulanga |
| 9. | Kalembo | 11&12 | Mbagala & Ibandi |
| 10. | Ikinga | 13 & 14 | Ibeta & Bwipa (shida kubwa) |
| 11. | Ngulilo | 15, 16 & 17 | Ngulilo, Shiringa & Ndapwa |
| 12. | Ngulugulu | 18, 19 & 20 | Chikumbulu, Kisyesye & Bujura |
| 13. | Lubanda | 21 | Mbembati |
| 14. | Luswisi | 22 & 23 | Makoga & Chibila |

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana Waziri atusaidie kwa hili.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia kwa maandishi Hotuba ya Wizara ya Nishati. Nianze kwa

kuipongeza Wizara na hasa Waziri Kalemani na Naibu wake kwa namna ambayo wamekuwa wasikivu na wachukuaji wa hatua wa haraka katika suala zima la kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi walikuwa nje ya *REA Phase II;* sasa Mheshimiwa Waziri na timu yako nikuombe *REA Phase III* isitupite tena. Watu wetu wamekuwa wavumilivu na kusubiri ahadi ya utekelezaji wa *REA III* ambavyo nina imani Vijiji kama, Kitumtu, Minyushe, Igelansoni, Mtunduru, Mwami, Kintandaa, Masweya, Germany, Msosa, Ishombwe, Iyumbu, Magunguruka, Kipunda, Mlandala na Vijiji vyote.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikimsumbua sana Mheshimiwa Waziri kuhusu *REA II*, baada ya mkandarasi kushindwa kumaliza vijiji vya *REA II;* ambapo aliondolewa na kupewa mkandarasi mpya ambapo makubaliano yalikuwa nikumnunulia vifaa lakini mpaka leo *REA* wameshindwa kununua vifaa na kumkwamisha mkandarasi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba sana katika suala la *Tipper* Serikali ianzishe *one stop center* ya kuhifadhi mafuta badala ya utaratibu wa sasa wa kila muagizaji kupakua mafuta kutoka nchini na kuyapeleka kwenye matanki yao. Hili linapelekea kuwepo kwa wizi mkubwa ambao Serikali haiwezi ku-*control* kiwango cha mafuta yanayopakuliwa kutoka kwenye meli kwenda kwenye matanki ya kuhifadhi.

Mheshimiwa Spika, faida ya mafuta yote kuhifadhiwa *Tipper* ni kwanza tutaweza ku-*control* na kuwa na uhakika wa kiwango cha mafuta yanayoingia nchini na kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa jitihada kubwa

wanazofanya pamoja na kwamba bado kuna baadhi ya changamoto zinazotakiwa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya vijiji katika Mkoa wa Tanga bado havijafikiwa na mradi wa *REA.* Pamoja na kwamba jitihada za Wizara tunaziona lakini tunaomba kasi zaidi ili vijiji vilivyobaki vipate umeme.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Bomba la Gesi la Hoima ulenge zaidi kuwanufaisha wananchi wazawa wa maeneo husika kwa kuwapa elimu ya kutosha juu ya *opportunities* zilizopo na ni jinsi gani wanaweza kuzifikia. Pia, ikibidi wasaidiwe mitaji au mikopo maana kwa kufanya hivi wananchi hawa ndio watakuwa walinzi wa kwanza wa miundombinu ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niiombe Wizara itoe elimu ya kutosha juu ya matumizi ya gesi asilia majumbani na viwandani na kuongeza kasi ili ienee kwa watu wengi zaidi, maana manufaa yake ni mengi na ni makubwa kwa ustawi wa nchi yetu kiuchumi na hata katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niiombe Wizara iangalie maeneo ambayo miradi hii inatekelezwa; kwa mfano Kinyerezi. Jamii inayozunguka miradi hii ipate faida na kufikiriwa kwa mfumo wa *give back to the society.* Unakuta miundombinu; mfano ni eneo lililopo mradi wa Kinyerezi, barabara ya kuendea katika mradi huu ni mbovu sana na magari yenye mizigo mizito yanaenda katika mradi yakichangia, hivyo kuwapa hali ngumu sana wananchi wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nipende kupongeza juhudi kubwa za Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri na ari mliyonayo katika kuhakikisha nchi yetu inaondokana na giza.

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali ilipe fidia kwa wananchi ambao wanapitiwa na miradi ya umeme ili wawe marafiki wa miradi hiyo na waweze kuilinda.

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la fidia kwa wanachi wa Mkoa wa Pwani, Kibaha eneo la Kiluvya, Mpiji, Mikongeni na Chalinze. Niombe Serikali ikutane na wanachi hawa kuwapa moyo na kuwaeleza kinachoendelea. Tathmini imefanyika miaka mingi ikifuatiwa na katazo la kutoendelea na shughuli yoyote katika eneo hilo. Hii imewapa umaskini wananchi hao kwani nyumba zao zimechakaa na kuanguka lakini hawana uwezo wa kujenga kwa hili katazo.

Mheshimiwa Spika, ninajua mpango wa usambazaji na uuzaji wa umeme ni wa *TANESCO,* naona si vyema kulitwisha hili shirika shughuli zote.

Mheshimiwa Spika, nishauri kupunguza urasimu wa kulipa waathirika wa hitilafu za umeme. Kumekuwa na shida pale iwapo hitilafu inatokea, ulipaji wake umekuwa wa shida.

Mheshimiwa Spika, nishauri Serikali juu ya utaratibu wa kuunga umeme kutoka kwenye nguzo ambayo mtu amenunua bila yule anayeungiwa kurudisha angalau nusu hasara kwa aliyeweka nguzo. Mfano mtu amelipia nguzo tano na kuungiwa umeme, kazi ambayo ingefanywa na *TANESCO* au mteja huyo ambaye wanaenda kumuungia wanaenda kuchukua kwenye nguzo za mteja ambaye alinunua bila hata ridhaa yake, hii siyo nzuri sana.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani, imetutendea makuu. Miradi ya *REA III* na Makambako – Songea 220kv *grid* imetutoa matongotongo sisi Wana-Namtumbo. Katika mwaka huu wa fedha wa 2018/2019 Namtumbo imenufaika kwa baadhi ya vijiji vyake kuwashiwa umeme. Nikuombe Mheshimiwa Waziri tufikishie shukrani zetu

sisi Wana-Namtumbo kwa Kiongozi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizowezesha mtukune sisi Wana-Namtumbo katika sekta hii ndogo ya umeme. Hakika tumepata kiongozi anayetujali hata sisi wakazi wa Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Waziri atatekeleza kauli yake aliyoitoa Namtumbo tarehe 05/04/ 2019 mbele ya Mheshimiwa Rais kuwa vijiji vyote na vitongoji vyote vya Wilaya ya Namtumbo vitafikishiwa umeme. Katika kulitekeleza hili, nikuombe uwakumbushe *REA* kusaini *addendum* inayompa ridhaa na nguvu mkandarasi wa *REA III* wa Namtumbo kusambaza umeme kwenye vijiji vyote vilivyobaki, hususan vijiji vya Kata za Limamu, Ligera, Lisimonji, Lusewa, Msisima na Magazini. Maeneo hayo ndiyo yanayotarajiwa kuunda Wilaya ya Sasawala ambapo Lusewa ndiyo makao makuu. Lusewa kwa sasa ni mamlaka ya mji mdogo na hivyo ni muhimu sana kutufikishia umeme wa uhakika kutokana na uchumi wa eneo hilo. Hongera sana wewe, Naibu wako na watendaji wote wanaokusaidia.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati kwa maandishi. Napenda kuwapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha wanazima vibatali nchi nzima na kuwasha umeme maeneo yote ya vijijini na mijini.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Kibiti tunashukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hadi leo vipo vijiji ambavyo havina umeme ambavyo nguzo na waya tayari kwa muda mrefu lakini cha kushangaza hadi leo umeme bado haujawaka kutokana na tatizo la *transfomer*. Vijiji hivyo ni Nyamatanga, Kikale na Ruaruke; naomba vijiji hivyo viangaliwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibiti lina jumla ya Kata 16, vijiji 58 vitongoji 42 vipo katika visiwa vya Bahari ya Hindi kama Mfisini, Kivimbuni, Salale, Msala, Mbwera na maeneo mengine ambayo hadi leo havina umeme kabisa. Naomba Serikali yangu sikivu ituangalie kwa jicho la kipekee katika visiwa vyetu vya Kibiti.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hivyo, Wilaya ya Kibiti ina Mji Mdogo Kibiti ambapo ina jumla ya vitongoji 39 ambavyo baadhi ya vitongoji havina umeme kabisa; kama vile Makina, Zimwini, Nyambangala, Mroso, Bumba, Ugezi, Kikota, Penda Miwaga, Penda na Kimbuga.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na *team* yote ya Wizara kwa utekelezaji wa majukumu yao pamoja na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Pongezi pia kwa *TANESCO* kwa uendelezaji mzuri wa taasisi kufikia matokeo chanya hadi 2019 kutoa gawio kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro kama hatua za dharura hazitachukuliwa dhidi ya mkandarasi wa *REA III, M/S State Grid* mradi huu hautokamilika kutokana na uwezo hafifu wa mkandarasi huyo Mkoani Morogoro katika *REA III.*

Mheshimiwa Spika, mkandarasi huyu *State Grid* alishindwa kumaliza mradi wa *REA II* katika Mkoa wa Lindi (2012 - 2016). Hata hivyo la ajabu bado mkandarasi huyu anaendelea kupewa kazi tena katika Mkoa huohuo wa Lindi na Morogoro, licha ya mapungufu makubwa katika utendaji kazi katika miradi ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi ameonesha waziwazi kushindwa kazi kwa sababu zifuatazo; uwezo finyu kiufundi, fedha, vifaa vya kufabyia kazi na usafiri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali aidha itengue mkataba au wamlazimishe mkandarasi aweke wakandarasi

wadogo *(sub- contracting)* au wasaidiane na timu ya ufundi *TANESCO* Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuzalisha umeme wa *Stiegler's Gorge Power Project* katika kutengeneza masuala ya mazingira/huduma kwa jamii imeelekeza zaidi katika upande wa *Lower Rufiji* kwa kuweka miradi kama ya mabwawa, skimu za umwagiliaji n.k. Mradi huu umesahau/ umeacha kabisa upande wa *Upper Rufiji* ambapo ndiko kunakozalisha maji kwa kuendesha mradi wote mfano Mto Kilombero na bonde lake linazalisha adilimia 65 ya maji yote ya mradi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni muhimu wangepima upya mradi na kuona namna gani wanaweka miradi ya kijamii na mazingira katika maeneo ya *Upper Rufiji* (Wilaya ya Malinyi, Ulanga, Kilombero) kutekeleza miradi ya skimu za umwagiliaji n.k ili kuwezesha kulinda mazingira wezeshi kuweka uendelevu wa Mto Kilombero.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme wa *REA III* Jimbo la Mikumi.  Ninatambua kuwa mkandarasi wa *REA III* katika Jimbo la Mikumi ni *State Grid* lakini bado kazi ya kuleta umeme kwenye Jimbo la Mikumi inasuasua sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kijiji cha Udung'u kilichopo katika Kata ya Vidunda ambacho kipo kwenye mpango huu; na awamu hii mkandarasi ameshindwa hata kwenda kufanya *survey* na hakuna shughuli yoyote iliyofanyiwa kazi. Tunaomba kujua, ni lini wananchi hawa watapelekewa huduma hii muhimu?

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Vidunda bado hakijafanikiwa kwa namna yoyote ile, hata nguzo bado hazijapelekwa; wananchi wanataka kujua tatizo ni nini? Maana walinisikia nikiuliza swali Bungeni na walimsikia Naibu

Waziri Mheshimiwa Subira Mgalu akiwahakikishia kuwa nguzo zipo.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Ulaya. Mheshimiwa Waziri amekuwa akituahidi mara kwa mara kwamba Kata hii ya Ulaya itafikiwa, na alifanya ziara kwenye kata hii na akatembelea na Kituo muhimu cha Afya cha Ulaya ambacho hakina umeme na kinahudumia Tarafa nzima ya Ulaya yenye Kata za Ulaya, Mhenda na Zombo. Hata hivyo mpaka leo hii hakuna shughuli yoyote inayohusu umeme inayoendelea katika Kata hii muhimu ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kata ya Tindiga. Kwenye Kata ya Tindiga hakuna shughuli yoyote inayohusu umeme inayoendelea ingawa nayo ipo kwenye mpango wa *REA III,* kwenye awamu hii; Kata ya Tindiga ina Vijiji vya Tindiga A, Tindiga B, Malui, Kalukwambe na Malangali. Tunaomba kujua, ni lini kata hii na vijiji vyake vitapatiwa umeme?

Mheshimiwa Spika, Kata ya Zombo. Nguzo zimeanza kushushwa katika Kata ya Zombo lakini zoezi hili bado linasuasua na Serikali ilituambia itaunganisha umeme huu kutoka Kata ya Masanze kwenye Kijiji cha Changarawe. Kata ya Zombo ina vijiji vitano, ambavyo ni; Zombo Lumbo, Kigunga, Nyameni, Nyali na Madudumizi. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea umeme kwenye vijiji hivi?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kata ya Mhenda. Kata ya Mhenda ipo katikati ya Kata ya Mikumi maeneo ya Ihombwe na Kata ya Ulaya. Sasa tunaomba sana Serikali itusaidie kutuletea umeme kwenye Kata hii muhimu ya Mhenda yenye vijiji vya Mhenda, Ilakala, Nyaranda na Maili 60. Tunaomba sana Serikali itusaidie tupate umeme kwa wakati kama walivyotuahidi.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Chonwe. Kijiji hiki kipo katika Kata ya Vidunda na kipo kwenye mpango huu wa *REA III* awamu ya kwanza, lakini mpaka leo hakuna jitihada zozote zilizooneshwa na Serikali na mkandarasi hajawahi hata kufika.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mikumi. Ikumbukwe kuwa Mikumi ni Jimbo la Kitaliii na kwenye Kata ya Mikumi kumekuwa na uwekezaji mkubwa sana wa hoteli za kitalii na *camp sites.* Pamoja na hayo, kwenye Kata ya Mikumi, katika hali ya kustaajabisha na kusikitisha maeneo ambayo yana uwekezaji wa hoteli za kitalii hayana umeme. Maeneo haya ni; Kikwalaza na maeneo ya Tambukareli ambako kuna Mji Mpya wa Kiserikali wa Mikumi. Kwenye maeneo ya Kikwalaza wenye hoteli wanalalamika sana kwamba wanapata gharama kubwa sana za kuendesha hoteli zao kwa kukosa umeme, kiasi kwamba inawalazimu kutumia majenereta makubwa sana, kitu ambacho kinawagharimu sana kwenye uendeshaji wa hoteli zao.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Tambukareli kuna maeneo ambayo leo watu wa *TANESCO* – Mikumi wamekuwa kimya na wamesababisha wananchi kushikwa na butwaa. Sasa wananchi wanataka kujua; Serikali ilipojibu swali langu Bungeni waliahidi kwamba kwa kuwa kuna shughuli za kitalii na zinaongeza Pato la Taifa letu basi wangetoa kipaumbele kwenye Kata hii ya Mikumi na maeneo yake haya ya Kikwalaza na Tambukareli. Je, ni lini tutapatiwa umeme kwenye maeneo sambamba na maeneo ya Barabara Kuu ya Tanzania kwenda Zambia, hasa maeneo ya Msimba na Ng'apa?

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Umeme Jazilizi *(Densifications).* Maeneo ya Ruaha Mbuyuni, Malolo A, Malolo B. Mgogozi na Chabi yaliyoko kwenye Kata ya Malolo yamepitiwa na nguzo za umeme uliopo karibu. Nilishawahi kuuliza swali na Mheshimiwa Waziri alinijibu kuwa kuna pesa zimepatikana kutoka kwa wahisani na kwamba maeneo haya pamoja na maeneo ya *PWD,* Dodoma, Kipekenya, Dodoma Isanga, Munisagala na Chabima yaliyopo kwenye Kata ya Masanze na maeneo ya Gezaulole, Mbamba, Kiduhi vilivyopo kwenye Kata ya Kilangali; je, ni lini wataunganishwa na umeme?

Mheshimiwa Spika, Kata ya Uling'ombe. Hii ni kata ambayo ni muhimu sana kwa kilimo na madini na inapakana

na Jimbo la Kibakwe ambalo lina umeme. Tunaiomba sana Serikali itupatie umeme kwenye Kata hii muhimu yenye vijiji vya Uleling'ombe, Mlunga, Ibanda na Lugawilo ili nishati hii ikatumike kukuza uchumi wa wananchi wa maeneo haya kwa kuchakata mazao na shughuli za madini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe pongezi za dhati kwa Wizara ya Nishati, nikianza na Mheshimiwa Waziri Kalemani, Naibu Waziri Subira Mgalu pamoja na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu. Kazi kubwa imefanyika katika awamu hii ya tano chini ya Serikali makini inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli ya kuhakikisha vijiji, vitongoji na kaya zote zinapata umeme ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa mradi wa REA III tayari umepeleka umeme katika maeneo yote ya liyopitiwa na msongo wa umeme wa Kilovoti 400 yenye urefu wa kilomita 670. Kero ilikuwa kubwa, hata hivyo ni imani yangu kwa sasa wananchi hawa watajenga imani kubwa kwa Serikali yao makini. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa ya kuzima vibatari vyote katika kaya zote ifikapo 2025, bado kuna vijiji vingi sana havijapatiwa umeme katika Mkoa wa Manyara. Niiombe Wizara kupitia kwa Mheshimiwa Waziri kuuangalia mkoa huu kwa jicho la huruma kwani mpaka sasa vijiji vilivypata umeme ni vichache kuliko ambavyo bado havijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, changamoto hiyo ya mkoa wetu hasa vijiji vyake ni kwamba kutokuwekeza umeme kunaziathiri zaidi taasisi mbalimbali za kijamii kama vile shule za sekondari, zahanati pamoja na vituo vya afya. Jambo hili linalorudisha nyuma maendeleo ya wananchi wetu na hata wengine kutopata huduma stahiki hasa ya kitabibu.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sana naomba nigusie suala la deni kubwa la *TANESCO.* Deni hili limekuwa kubwa sana kwa kuwa linachagizwa na gharama ya upelekaji wa miundombinu ya gesi kutoka Mtwara. *TANESCO* ndiyo

wanaoligharimia bomba hilo la gesi, jambo ambalo linafanya gesi hiyo kuwa ghali na umeme kuuzwa kwa bei kubwa sana. Umeme wa *TANESCO* utauzwa kwa bei nafuu pale tu ambapo Serikali itaipunguzia *TANESCO* gharama ya miundombinu ya gesi bomba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Tunaendelea sasa upande wa Serikali, wachangiaji bado ninao wengi, lakini sasa kwa muda uliopo haitawezekana kila mmoja kupata nafasi, tuwiane radhi kwenye Wizara nyingine nikiona majina haya yaliyobaki tutahakikisha mnapata *priority.* Dakika tano tano Waheshimiwa kwa sababu ya hali halisi ya muda. Tunaanza na Naibu Waziri wa Fedha, dakika tano, atafuata Naibu Waziri Mazingira, dakika tano.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri kaka yangu Dkt. Mendrad Kalemani na dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi kubwa wanayoifanya, hakika Taifa linaona na wananchi wetu wanaona na naamini wako kwenye mikono salama sana kwa hiyo waendelee kuchapa kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa maneno mafupi sana. La kwanza ni kuhusu mradi wetu wa Rufiji *Hydro Power Project*. Nimesema wiki iliyopita wakati nachangia hapa nikasema Serikali yetu imejiandaa vizuri hatuna wasiwasi na malipo yoyote kuhusu Mradi huu wa Rufiji *Hydro Power Project* na ndio maana tumeshalipa shilingi bilioni 723, sio kwamba tumefanya makosa, hapana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa inafahamu kabisa kwamba bajeti uliyotupitishia hapa na Bunge lako Tukufu ilikuwa ni shilingi bilioni 700 kamili lakini mpaka sasa tumelipa bilioni 723.598 ni kwa sababu ya umuhimu wa mradi huu na Waheshimiwa Wabunge wamehoji kwamba zimetoka wapi pesa nyingine, hizi bilioni 23.

Mheshimiwa Spika, naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba mamlaka ya kufanya uhamisho wa Mafungu kutoka Fungu moja kwenda Fungu lingine ni mamlaka ya Waziri wa Fedha na Mipango. Kunapokuwa na jukumu muhimu, jukumu la msingi ambalo halitakiwi kusubiri mamlaka hiyo Bunge lako Tukufu kupitia Sheria ya Bajeti na kanuni zake alipewa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anafanya uhamisho wa fedha kutoka Fungu moja kwenda Fungu lingine. Hii bilioni 23.598 Mheshimiwa Waziri amehamisha kutoka Fungu 21 - Hazina kwenda Fungu 58 ili mradi huu uweze kutekelezwa na Taifa letu liweze kupata faida iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, asubuhi wakati najibu swali hapa niliona kulikuwa na mshangao na mshangao wenyewe ni kwamba kodi haichangii kwenye bei ya bidhaa yoyote inayozalishwa. Kwa Tanzania kwa sasa hivi gharama kubwa kwenye viwanda vyetu ni umeme, umeme wetu ni wa bei ya juu na ndio maana Mheshimiwa Rais wetu alipobeba Ilani ya Chama cha Mapinduzi aliahidi ndani ya miaka mitano, bei ya umeme itashuka na haiwezi kushuka, hakuna miujiza ya kushuka kama hatutotekeleza Rufiji *Hydro Power Project,* naye Mheshimiwa Rais kwa sababu aliahidi ni mtekelezaji na sasa tunatekeleza. Naomba nimwambie Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu tuko tayari Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza mradi huu bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulisemea ni kuhusu deni la *TPDC* na Waheshimiwa Wabunge wamesema kwamba Serikali imeiachia *TPDC* kulipa deni hili. Uhakika wa suala hili na ukweli wake ni kwamba deni hili kwa sasa linalipwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi siyo *TPDC,* ni Serikali kuu ndio inayolipa deni hili na deni lenyewe ni deni la mkopo kwa ajili ya kujenga Bomba la gesi na kuna deni kwa ajili ya mkopo wa Mnazibay. Madeni haya yalichukuliwa kutoka katika Benki ya *Exim Bank* China na yote haya tumeanza kuyalipa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, cha msingi tu tunachotakiwa kufahamu, mkopo huu ulikopwa na Serikali kupitia *TPDC* kwa makubaliano kwamba miradi hii itakapotekelezwa *TPDC*

itairejeshea Serikali fedha hizi. Hii kwa sababu ni mradi wa maendeleo ambao lazima ulete faida ndani ya Taifa letu, ndio maana Serikali ikasema kwa sababu miradi hii haijaanza kuzalisha vizuri Serikali inalipa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kutupatia takwimu, wale mliokuwa mnaulizauliza mmesikia sasa zilizolipwa ni bilioni 723.598. Tunaendelea na Naibu Waziri Mazingira.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wetu wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa vizuri juu ya mradi wetu wa kufua umeme wa Rufiji. Ni kweli kabisa kwamba mradi huu una umuhimu mkubwa sana katika uchumi wetu, lakini hatua tuliyofikia ni *point of no return.*

Mheshimiwa Spika, hofu ambayo imejengwa ni juu ya vyanzo vya maji, na mimi niseme tu nimefanya ziara katika Mikoa sita ambayo inapatikana mito mikuu mitatu inayolisha Bonde la Mto Rufiji. Mto Luwengu ambao unachangia zaidi ya asilimia 19, Mto Ruaha Mkuu unachangia asilimia 15.5 na Mto Kilombero ambao unachangia asilimia 65.5. Vyanzo vya maji vya mito yote hii mitatu viko salama. Ningeomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba maeneo yote ambayo mito hii imeanzia vyanzo viko salama. Kazi tuliyonayo sasa ni ku-*maintain* vile vyanzo vya maji, lakini maji yanakopita mpaka kwenda kwenye Bonde

la Mto Rufiji ndiko kazi tunayoifanya kuanzia sasa. Kwa hiyo nimefika mpaka *Stiegler's Gorge* kwenyewe kwa kweli maji yapo ya kutosha na mradi huu utakuwa ni mradi wa mfano na utakuwa ni mradi endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira Serikali imeweka utaratibu mzuri sana. Vile viumbe hai tunavi-*reserve;* tukishamaliza mchakato mzima wa lile bwawa maana yake viumbe hai vile vinarudishwa na shughuli inaendelea kama ilivyo. Vilevile bado pale kutakuwa na faidi nyingi, wameeleza Waheshimiwa Wabunge vizuri; utalii, kilimo na vitu vingine vyote.

Mheshimiwa Spika, pia imezungumzwa tutavunja mkataba wa *World Heritage,* kitu ambacho siyo kweli. Mkataba huu wa *World Heritage* umekuja baada ya *program* hii kuanza, sasa *program* hii ikishaanza *Selou* kuwa *World Heritage* maana yake ule mkataba unakubaliana na program iliyokuwepo. Kwa hiyo nisingependa jambo hili lizungumzwe kwa kupotosha Bunge hili; kwamba tayari mkataba huu umekuja wakati program yetu ya *Stiegler's Gorge* ilishakuwepo *before. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaandaa *master plan* kwa ajili ya ku-*maintain* vile vyanzo vya maji kama Wizara ya Mazingira na sisi tayari tumefungua ama tumeshaweka Ofisi ya Baraza la *NEMC* pale pale. Yuko mratibu ambaye atakuwa anashughulika na mazingira, pale pale kwenye eneo la *Stiegler's Gorge*. Kwa hiyo nilitaka niwaondoe hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili la mradi huu .....

**TAARIFA**

**SPIKA:** Kwa nusu dakika, Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, *yeah,* nilitaka nimwambie rafiki yangu nimpe taarifa kwamba *Selous* kuwa ni *World Heritage* si leo, hata Bunge lililopita Serikali ilipotaka kuchimba *Uranium* ilituma baadhi ya wajumbe kwenda Urusi kuomba *UNESCO* itoe kibali tuchimbe *Uranium*.

Sasa ukisema Selous hiyo *World Heritage* imeanza leo, nilikuwa nakupa taarifa kwamba tulianza muda mrefu, huu mradi wetu umeikuta Selous tuko *World Heritage* tayari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri malizia dakika moja.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nimsaidie kaka yangu Mheshimiwa Msingwa, nimefika Iringa bahati mbaya hukuwepo lakini ningeweza kukupa elimu zaidi, mradi umeanza tangu Nyerere kaka, si Bunge lililopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee, nilitaka nimsaidie kwenye hili. Unapokuwa na umeme wa kutosha sisi watu ambao tuna-*deal* na eneo hili la mazingira ni msaada mkubwa sana, huwezi kuzungumzia asilimia tatu ya Selous. Watu wanapopata umeme leo wamesema Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaacha kutumia kuni, mkaa na vitu vingine vyote, watu wata-*transform* kutoka kwenye matumizi haya wanaanza kutumia umeme. Nilitaka niwaondoe hofu mradi huu tunauhitaji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru sana watu wanaongelea sana Selous. Nilifanya kazi Selous enzi hizo naijua vizuri ndani nje. *Attorney General,* Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika tano.

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa muda na mimi niweze kuchangia hitimisho la hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Mheshimia Spika, katika mchango wangu nitajielekeza moja kwa moja kwa hoja aliyoitoa Mheshimiwa Hawa Ghasia katika mchango wake ambapo alizungumza kwamba katika mazingira ya sasa hivi inaonekana kama hakuna leseni mpya ambazo Mheshimiwa Waziri amezitoa katika sekta hii ya gesi. Pengine sababu mojawapo ya

kutokuwa na leseni mpya zinatolewa ni kwa sababu hii mikataba iliyopo ya utafutaji na uchimbaji wa gesi iko kwa *AG;* na akaniomba kama ninaweza kwa sababu nipo, nizungumzie suala hili ili kuweza kumuepusha Mheshimiwa Waziri na kuondolewa shilingi yake; nami napenda nilizungumzie hili kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, kama unafahamu uliunda Kamati ya kuangalia sekta ndogo ya gesi pamoja na uvuvi. Kamati ile ilikuja na taarifa yake na ilikuja pia na mapendekezo yaliyokuwa katika taarifa ile. Mojawapo ya mapendekezo kama mnavyofahamu vizuri kabisa ilikuwa kwamba iko haja ya kurejea hii mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa gesi *(production sharing agreements),* na kazi hiyo ikapewa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo ni kweli kabisa kwamba mikataba hiyo anaishughulikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichukue nafasi hii kueleza tu tumefika wapi katika zoezi hilo. Tulianza kazi na zoezi la kuipitia hiyo mikataba yote, tuliunda timu ilipata wataalam kutoka Wizara mbalimbali na sekta mbalimbali za Serikali; na tukaanza hiyo kazi. Ilitulazimu tuanze kwanza kwa kuwajengea uwazo hii timu ili iweze kufahamu ni kitu gani inakifanyia *review.* Hilo zoezi lilikamilika, baada ya zoezi hilo lilifuata sasa zoezi la kuipitia mikataba yenyewe; na timu hii imekaa kwa karibu kipindi cha miezi miwili na imefanya kazi ya kupitia ile mikata yote kumi na moja ambayo inahusika na utafiti na uchimbaji wa gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya zoezi hilo tuligundua kwamba kuna kitu ambacho ni muhimu sana kukiangalia, kwa kiingereza wanaita *economic and financial modeling.* Kwa sababu hapo ndipo siri nzima ilipolala, kama mnapoteza au kama mnafaidika au kama mnapata iko kwenye *economic and financial modeling.* Kwa hiyo tukaweka tena awamu nyingine ili timu hii ikae na ikafanya kazi hiyo kwa kipindi cha takriban mwezi mmoja. Ninavyozungumza timu hiyo imemaliza hiyo kazi ya kuangalia *economic* and *financial modeling. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, walichokifanya katika zoezi hili ilikuwa ni kuangalia *financial* na *economic modeling* gani ilitumika katika hizi *PSAs.*

Kwa hiyo, baada ya hiyo kazi wakagundua kwamba ni lazima turudi tena tuangalie sisi kama nchi tunapendekeza *economic* na *financial modeling* ipi. Sasa katika hilo zoezi la tatu ambalo nimelitaja, timu hii inakutana tena kuanzia tarehe 6 Juni, na itamaliza kazi yake tarehe 25 Juni.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwa ufupi kwa sababu mambo mengi bado yapo kwenye taarifa hii, zoezi hili limetufanya tuelewe matatizo mengi yaliyo kwenye mikataba hii na mapungufu ambayo tunahitaji tuyafanyie kazi. Pia, kikubwa kabisa tutakachokipata kwenye zoezi hili litatufahamisha yaani lita-*inform* tunapoanza majadiliano ya *LNG,* kwa sababu hii mikataba mingi ilisukwa kwa namna ambayo baadae ingekuja ku-*influence* chochote ambacho tungekubaliana kwenye *LNG.*

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu niliyokuwa napenda kushirikisha na kwa ujumla ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri nikupe dakika kumi na tano, karibu sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili kwa mara ya pili ili niweze kuchangia hoja ya Wizara yetu ya Nishati na nianze kusema naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ya pekee kwa miongozo yake na kwa kuendelea kuniamini kuhudumu katika sekta hii ya Nishati. Namshukuru pia Makama wa Rais Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mheshimiwa

*Chief Whip* wetu kwa maelekezo mbalimbali anayoyatoa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nikushuruku wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge pamoja na Kamati yetu ya Nishati na Madini kwa miongozo mbalimbali mnayotoa katika sekta yetu ya nishati. Kipekee nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa namna ambavyo anaongoza Wizara yetu na kazi nzuri anayoifanya nchi nzima kwa weledi, uaminifu na kipaji ambacho alicho nacho na nimtakie kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niishukuru familia yangu, mume wangu Juma Mtemvu, wazazi wangu, watoto wangu na familia yote Vilevile nikishukuru chama changu Chama Cha Mapinduzi pamoja na Wajumbe wa UWT, Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Pwani pamoja na viongozi wetu wa Serikali katika mkoa huu na wanachama kwa namna ambavyo wananipa ushirikiano katika majukumu yangu ya Unaibu Waziri lakini pia ya Kibunge ndani ya Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Wabunge wa Bunge hili kwa namna ambavyo wamechangia hoja yetu na mashirikiano wanayotupa siku zote, kwa ushauri wao na maelekezo ya mara kwa mara; kwa kweli wameitendea haki hoja yetu. Takribani Wabunge 100 wamechangia, 50 wamechangia kwa maandishi na wengine 50 wamechangia kwa kuzungumza.

Mheshimiwa Spika, umenipa dakika 15 lakini nataka niseme yote yaliyojadiliwa ndani ya Bunge lako tukufu tumeyapokea, na kwa kuwa majibu yatakuwa ya kimaandishi kwa kila mmoja hoja yake aliyochangia itoshe tu nichangie kwa ujumla wake na kama nilivyotanguliza kusema kwamba nimewashukuru sana. Mjadala wetu huu leo ulijielekeza kwenye suala zima la masuala ya Nishati na hususan asilimia 80 ya waliochangia walijielekeza kwenye mradi wa *REA.* Mradi wa *REA* awamu ya tatu ambao

umelenga kufikisha vijiji vyote umeme takribani 12,268 ifikapo 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, tumesikia changamoto, tumesikia mlivyotuelekeza, tumesikia namna gani Watanzania wanahitaji nishati hii ifike vijijini. Tumepokea pongenzi; lakini siku zote nasema anayekupongeza anahitaji zaidi. Pongezi mlizozitoa leo mnahitaji tufanye kazi zaidi tuyafikie maeneo mbalimbali, tufikie vijiji vyote 12,068 ili kuweza kuleta tija na tuwaunganishie vijiji vyote. Ila nataka niseme moja, kwamba mradi huu kwa kweli wa *REA* awamu ya tatu pamoja na hoja kwamba umechelewa. Tumeshawa-*categorize* wakandarasi, tunatambua wakandarasi ambao wanafanya vizuri na tunatambua wakandarasi ambao bado kasi yao haijawa nzuri. Naomba niliarifu Bunge lako Tukufu, kwamba tunavyopima mradi huu wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na miradi mingine inayoendelea tupime baada ya kuwafungulia *letter of credit,* ambayo ilikuwa mwezi wa sita mwaka jana 2018.

Mheshimiwa Spika, kwa miezi 24 wa mradi huu, matarijio yetu mradi huu utakamilika Juni, 2020. Kwa kuwa ndani ya Bunge hili na asilimia kubwa ya maswali ninayoyajibu pamoja na Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani yanahusu masuala ya nishati vijijini. Tumeweza kuwahamasisha na kuwasimamia wakandarasi, na hii tunawaahidi wakamilishe mradi ifikapo Desemba, 2019 ili miezi sita inayosalia iwe miezi ya kuunganisha wateja na ya kurekebisha mapungufu mbalimbali. Kwa hiyo niwatoe hofu Wabunge wote waliochangia hoja hii, kwamba pamoja na Watendaji wetu ambao wanafanya kazi vizuri wakiongozwa na Dkt. Khamis Mwinyimvua na Wenyeviti wetu wote wa Bodi zetu hizi. Kwa kweli jambo hili litawezekana na tuahidi tu kwamba itawezekana.

Mheshimiwa Spika, la pili, tumesikiliza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Hotuba hii ilionesha kwamba hakuna jambo lolote ambalo limefanyika; tangu Serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani hakuna mradi wowote uliokamilika. Pamoja na kuchangia kwangu, nitaomba

mwongozo wako ni nini kifanyike inapotokea hotuba yenye nia ya kupotosha na kulipotosha Bunge lako. Kwanini nasema hivyo, tumesema kwenye taarifa yetu tangu Serikali ya awamu ya tano imeingia madarakani kwanza kiwango cha uzalishaji wa umeme kimeongezeka. Sasa hivi tuna *Mega Watt* takribani 1,604 kutoka Mega *Watt 1,200* za mwaka 2015. Vilevile tumesema mradi wa *Kinyerezi II Extension* ulioanza awamu hii ambao umezalisha *Mega Watt* zaidi ya 244 umekamilika. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, mradi wa Makambako - Songea wa *KV 220* umezinduliwa, umekamilika. Kana kwamba haitoshi mradi wa kusafirisha umeme wa Iringa – Shinyanga *KV 400* umezinduliwa umekamilika. Pamoja na miradi mbalimbali ambayo tumeisema na tumesema, kwamba sasa tunakuwa na *Megawatt 300* za ziada tofauti na upungufu wa *Mega Watt 100* mwaka 2015. Kwa hiyo ni wazi kabisa Serikali ya Awamu ya Tano imetenda katika kipindi hiki kifupi cha miaka hii mitatu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa pia utolee mwongozo wako ni suala zima la Taarifa ya Kambi ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuonesha kwamba Serikali inaikwamisha sekta ya nishati na tathmini na namna ambavyo amekuwa amefanya *analysis,* inashangaza. Nimshauri Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Waziri Kivuli pengine wakati anaandaa taarifa yake ahusishe na watu wa fani nyingine. Kwa sababu utaona namna ambavyo amekuwa anafanya *analysis* hususan ya fedha zilizopelekwa kwenye Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* amelipotosha Bunge lako Tukufu. Utaona katika *analysis* yake aliyoifanya kwa mfano ya mwaka 2015/2016 ameishia Desemba, 2015. Wote tunafahamu mwaka wa fedha wa Serikali unaishia tarehe 30 Juni, hii inafahamika. Unapofanya tathmini ya kuonesha Desemba 2015 unakuwa na hoja binafsi na si hoja ya kulipa uelewa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nataka niitaarifu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa mwaka 2015/2016 Wakala wa Nishati Vijijini ilipokea bilioni mia mbili tisini na tano

na arobaini ikiwa ni asilimia 81 ya fedha zilizotengwa. 2016/2017 ilipokea bilioni arobaini mia tano tisini na tano ikiwa ni asilimia 75 iliyotengwa. 2017/2018 ilipokea bilioni mia tatu sabini na nne ponti tano ikiwa ni asilimia 80. Mwaka tunaouzungumza 2018/2019 mpaka sasa na hata taarifa ya Kamati yenyewe ambayo Naibu Waziri Kivuli ni Mjumbe wa Kamati hiyo mpaka sasa *REA* imepokea asilimia 81. Kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haiiwezeshi *REA,* isingewezekana kwa kipindi kifupi cha miezi 36 vijiji takribani 5,019 kupelekewa umeme. Kwa hiyo ni wazi kabisa Bunge lako limepotoshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kana kwamba haitishi, Bunge lako pia limepotoshwa kwenye taarifa ya hasara za Shirika la *TANESCO*. Tumepokea changamoto zote zilizoelewa, lakini hasara za Shirika la *TANESCO* zimekuwa zikipungua. 2015/2016 zilikuwa bilioni 949, 2016/2017 zimekuwa bilioni 265, 2017/2018 *TANESCO* ilipata hasara ya bilioni 112. Kuliaminisha Bunge lako, na kwa kuwa taarifa hii inaingia kwenye *hansard,* kwamba hasara za *TANESCO* zikiwa zimeongezeka hususan awamu ya tano, tutaomba mwongozo wako vinginevyo taarifa ambazo za upotoshaji ziondolewe kwenye *hansard* ya Bunge ili kupata taarifa sahihi. Niko tayari ku-*submit audited report* za *TANESCO* kuthibitisha hoja yangu ninayojenga sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hasara hizo lakini *TANESCO* imekuwa ikiwekeza kwenye fedha zake za ndani, kwenye miradi ya uzalishaji na miradi ya *distribution.* Mwaka 2015/2016 *TANESCO* iliwekeza bilioni 205, mwaka 2016/2017 *TANESCO* iliwekeza bilioni 220, mwaka 2017/2018 *TANESCO* imewekeza bilioni 233. Tunaona miradi yote hiyo, ujenzi wa *sub-stations line* ya Mtwara, kituo cha Maumbika ni fedha za ndani ya TANESCO. Ujenzi wa *Sub-station* maeneo mbalimbali, uunganishaji wa *grid* ya taifa kwenye maeneo mbalimbali ni fedha za *TANESCO.*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa suala zima la *LNG.* Ni kweli, natambua *concern* za Wabunge kwamba mazungumzo yamechelewa, lakini nataka nilitaarifu Bunge

lako Tukufu mazungumzo haya yalikwama baada ya wabia wa mradi huu kutofautiana. Isingewezekana Serikali ikaendelea na mazungumzo ilhali wabia hawa wametofautiana. Hata hivyo pale kila mbia alipotaka tuzungumze pamoja na Serikali ikatoa baraka zake mazungumzo haya yameanza kwa kasi na yanataraji kukamilika Septemba, 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie dakika chache kueleza uzoefu wa mazungumzo. Mfano Canada ilipojenga *LNG* yao, mazungumzo yalichukua miaka saba (7), Papua New Guinea ilipojenga *LNG* yao mazungumzo yalichukua miaka minne (4). Sambamba na hilo hata Msumbiji hapa walichukua mazungumzo mwaka mmoja na nusu lakini pamoja na kwamba mazungumzo haya hayakuingiliana kwenye masuala ya mkataba mkataba. Timu yetu hii tumeshaipeleka nje nchi za Indonesia, tumeipeleka Msumbiji, Papua Guinea, Trinidadi *and* Tobago na Qatar kwa ajili ya kuona namna gani nchi hizi zilifanikiwa wakati wa haya mazungumzo ya *LNG.* Kama ambavyo Wabunge wa Mkoa wa Lindi wamesema kwa kuwa mazungumzo yameshaanza na kwamba wawekezaji wanaendelea vizuri ni imani yangu mradi huu mkubwa ambao utatumia takribani trilioni 69, utatekelezeka.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumzia mradi wa Rufiji *Hydropower,* na kwa kuwa natoka Mkoa wa Pwani ni mdau wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imetolewa takwimu hapa, bei ya umeme unaozalishwa na maji ni shilingi 36, bei ya gharama ya umeme unaozalishwa na gesi ni shilingi 147. Mheshimiwa Silinde alitolea mfano kwamba mradi wa *Kinyerezi One Extension,* bilioni 60 iliyotajwa kwenye kitabu ni fedha za kumalizia. Mradi huu umegharimu Dola za Kimarekani milioni 188 ambapo ni kama bilioni 454. Kutaka kutuaminisha bilioni 60 inaweza kuzalisha *Megawatt 150* ni kulipotosha Bunge lako. Hata taarifa yetu ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma, ukurasa wa 34 ilieleza kinaga ubaga kiasi cha fedha iliyotumika. Kwa hiyo Waheshimiwa

Wabunge pamoja na michango yenu mizuri ninaomba michango hiyo ijielekeze kwenye takwimu zinazotolewa, isiwe na nia ya kupotesha, tunajenga nyumba moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli tunategemea kufika uchumi wa kati 2025, tunahitaji umeme mwingi zaidi. Mmetaja miradi mbalimbali lakini gesi hiyo katika taarifa yetu hatujaiacha, uko mradi mpya wa kuzalisha *Megawatt 300* katika Mkoa wa Mtwara kwa kutumia gesi. Uko mradi pia *Kinyerezi IV* na *VI* ambayo inaandaliwa, inaonesha kwamba gesi hatujaiacha na bado tunaimba huo wimbo kwa sababu gesi inatarajiwa kutumika kwenye viwanda, gesi inatarajiwa kutumika kwenye viwanda vya mbolea, gesi inatarajiwa kutumika kwenye kuendesha magari. Kwa hiyo kusema kwamba sasa hivi wimbo hatuimbi, tunaimba wimbo wa umeme wa bei nafuu kwa ajili ya viwanda na kwa ajili ya kushusha bei ya watumiaji wa umeme wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi binafsi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ujasiri wake. Ndani ya Wizara ya Nishata hatutarudi nyumba, tunatambua umeme ukiwa mwingi tumeshaanza kujenga miundombinu ya kusafirisha, ya kuuziana na nchi za jirani. Leo tunajenga Singida – Namanga kwa ajili ya ku-*connect* nchi ya Kenya, tuna mpango wa kujenga Masaka Mwanza kwa ajili ya kuunganisha na nchi ya Uganda. Zipo nchi zinahitaji umeme mwingi; umeme ni biashara. Mradi huu ukishakamilika una uwezo wa kuzalisha trilioni 9 kwa mwaka kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali. Kwa hiyo nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge pamoja na maneno yote hatutarudi nyuma, mwendo mdundo katika mradi huu wa *Rufiji Hydropower. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi wakazi wa Mkoa wa Pwani hususan Kibiti na Rufiji tunatambua mradi huu, bwawa hili litatusaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunatambua fursa za ajira lakini tunatambua vijiji 37 vitakavyounganishiwa umeme katika maeneo ya Morogoro na maeneo ya Mkoa wa Pwani. Si hivyo tu, tunatambua kwamba nia ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ya kutaka bei ya

umeme ipungue kutoka senti 11 *USD* ya sasa na kadri itakavyowezekana. Haya yote yatawezekana baada ya *energy mix* ya kutosha hususan ya kuongeza umeme wa maji. Tunatambua, na tumepokea maoni ya kutumia nishati ya jadidifu na ndiyo maana tumetangaza *tender* kuwaalika wawekezaji binafsi *Megawatt 950* kwenye upepo, kwenye maji na kwenye makaa ya mawe; na kana kwamba haitoshi, joto ardhi pia.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru wote ambao mmechangia hoja yetu na tutaendelea kufanya kazi. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunakushukuru sana, tunajua muda hautoshi lakini umejitahidi kuutumia ipasavyo. Mwana mahesabu huyu, kwa hiyo ukikorofisha mahesabu anakasirika kabisa; na mimi ninamuelewa maana Spika wenu pia ni scientist, kwa hesabu yuko vizuri. *(Makofi)*

Sasa ndugu zangu ndiyo maana wakati ule tulipoanza tukawa tunajaribu kuingilia kati mapema na kuanza kuainisha baadhi ya maeneo ambayo yana matatizo na mkalalamikia wenyewe mngependa hotuba zetu zibaki *intact* kadri inavyowezekana. Sasa limekuja tatizo jipya hili la unaweka takwimu zisizokuwa sahihi halafu una-*argue* kwa takwimu potofu halafu zinatumwa kwenye mitandao na kila mahali dunia nzima; Watanzania na watu wengine wanasoma; hili ni jambo ambalo si sahihi, si zuri hata kidogo. Kwa sasa bado hatuna hakika lakini hayo ndiyo maneno ya Serikali, tungependa *at same point* jioni ya leo Msemaji wa Upinzani aseme kidogo kuhusu hizi takwimu. Hata kama Mheshimiwa Mnyika hayupo lakini Kambi ipo maana hii ni taarifa ya Kambi. Katika maeneo ambayo yametajwa hapo tupate maelezo kama ni kufuta basi mfute na kadhalika, lakini itumike kama ni funzo huko mbele. Unapotumia takwimu jitahidi sana kuwa mkweli kwa sababu takwimu hazidanganyi, hazidanganyi, bora ukipiga blaa blaa. Kwa hiyo tunawapa nafasi mpaka

jioni hiyo *at some points* tutapenda kufahamu haya mambo yanakujaje hapa, kama mko sahihi basi mtasimamia *your ground,* kama hamko sasa basi ni vema. Katika maeneo hayo yako kama matatu, manne hivi. *(Makofi)*

Baadhi ya matangazo niliambiwa Waheshimiwa bado mambo yenu hayajakaa vizuri upande wa stahili zenu. Malipo yote yalishafanyika, kuna utaratibu tu, kautaratibu ni karefu kidogo kule *BoT.* Tunaamini *by* kesho saa hizi kila mtu atakuwa yuko vizuri; kwa hiyo nilitaka kuwataarifu, kwamba *by* kesho saa hizi kila mtu atakuwa yuko vizuri. Kwa maana ya Bunge kila kitu kimeshamalizika, yaani liko nje ya Bunge kwa maana ya *BoT* na mabenki ambayo yanatuhusu. Nimefanya mawasiliano nikiwa hapa na majibu ni hayo kwamba watajitahidi sana *by* kesho saa hizi kila kitu kitakuwa vizuri, hakuna mtu atakuwa anadai chochote. *(Makofi)*

Kuhusu ile safari ya Misri, kama nilivyosema bado tunaendelea kuifanyia kazi, lakini mlichukulie *serious* Waheshimiwa Wabunge. Nalirudia mara kwa mara ili li-*sink* kwamba safari hii kule kutakuwa na Burundi, Uganda nafikiri na Kenya; Kenya na Tanzania tupo. Takriban Wabunge wote wa Burundi watakuwa kule, Wabunge karibu wote wa Uganda watakuwa kule, Wabunge wa Kenya watakuwa kule na wananchi wao. Sasa itakuwa ni kitu cha ajabu kwamba Wabunge wa Tanzania hatupo, itakuwa haipendezi hata kidogo. Ndiyo maana nalipigia debe. Mahesabu kamili yatakuja hapo baadae tunaendelea kuwasiliana na Serikali lakini kwa vyovyote vile haizidi dola 1,500. Hiyo 1,500 itahusisha kwa yule ambaye atakaa siku 11 mfululizo, siku 11 mfululizo, usafiri wa anga kwenda na kurudi, chakula, malazi; na siku ya zile mechi tatu za Tanzania za mwanzo kuanzia na ile Tanzania na Senegal usafiri wa kwenda uwanjani na kutoka uwanjani kurudi katika hoteli waliyofikia, lakini pia kataangaliwa kautalii ka aina fulani katika nchi ile ya Misri.

Ni *opportunity* ya aina yake haijawahi kutokea, ningependa kuwashawishi sana tuweze kufika huko. Kwa hiyo tuendelee kujiandaa kila mtu kwa wakati wake kwa sababu gharama ni zetu na mimi pia najaribu kuangalia uwezekano

kama tutapata mahali chochote kile, tutatangaziana ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapunguza hizi gharama tutafanya hivyo kama tutapata. *(Makofi)*

Basi, baada ya maneno hayo nisitishe shughuli za Bunge hadi Saa Kumi Kamili jioni ya leo, ahsante sana.

*(Saa 7:00 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10:00 jioni)*

*(Saa 10.00 Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Nishati

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wakati wa kumwita Mheshimiwa mtoa hoja ambaye ni Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani. Mheshimiwa Waziri, karibu sana na una si zaidi ya saa moja. Mheshimiwa Waziri, karibu sana.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia katika sekta yangu ya nishati na nikushukuru sana kwa kunipa hii fursa nikiwa msemaji wa karibu na mwisho.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia ningependa nitoe shukrani kwanza kabisa kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo thabiti katika kutekeleza shughuli za Wizara yetu, hakika tunamwombea kila la heri katika usimamizi wa shughuli zake za kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan anavyotuelekeza kusimamia miradi hii

na sughuli mbalimbali za Wizara yetu na niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake thabiti, sisi kama Mawaziri kutusimamia kutekeleza majukumu ya Serikali. Niendelee kumshukuru sana Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kusimamia vyema Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Serikali ya mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia nikushukuru wewe mwenyewe kwa miongozo mahiri sana katika shughuli za Bunge. Nadhani kila mtu ni shahidi, hongera sana Mheshimiwa Spika. Namshukuru sana Mhshimiwa Tulia Ackson, Naibu Spika. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote katika michango yetu tuliyopata, ushauri na maoni mbalimbali. Nikiri kwamba yote tutakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Subira Mgallu jinsi anavyonisaidia katika shughuli mbalimbali katika Wizara lakini katika kufuatilia mambo ya utekelezaji wa Wizara yetu. Niendelee kuwashukuru sana watendaji wa Wizara yetu na taasisi zake pamoja na bodi zake zikiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara yetu Dkt. Mwinyimvua.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chato napenda popote walipo niwashukuru sana kwanza kwa kunifikisha hapa, lakini pia kwa kuniombea kutekeleza majukumu ya Serikali huku na shughuli ya jimbo naendelea nayo. Hongereni sana wananchi wa Chato, tuko pamoja na ninyi, tembeeni kifua mbele.

Mheshimiwa Spika, niipongeze na kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu Violeth Kalemani ambaye ananiwezesha, kuniandaa vyema kusimama mbele ya Bunge lakini hata katika utekelezaji wa majukumu ya Kiserikali, mama Vaileth na watoto wako, watoto wangu pia, hongereni sana na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba sasa nirudi kwenye michango ya

Waheshimiwa Wabunge. Kwanza tumekiri kupokea mawazo na ushauri juu ya hoja mbalimbali za maandishi takriban 58 na michango mingine ya kuzungumza 52, kwa hiyo tuna jumla ya michango 110, lakini tunatambua bado michango mingine itaendelea kuja na sisi tunasema m bele ya Bunge lako Tukufu tuko tayari kuipokea na kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, naomba nijielekeze kwa jumla jumla haitakuwa rahisi kujibu hoja moja baada ya nyingine. Nitaanza na kuchangia katika mradi muhimu wa kipaumbele katika Taifa letu wa kuzalisha umeme kutokana na maporomoko ya Mto Rufiji, *megawatt 2,115.*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hoja hii imejadiliwa sana na bila shaka hakuna Mtanzania hadi sasa asiyejua umuhimu wa mradi huu. Kilichobaki Waheshimiwa Wabunge na Watanzania hebu tuunge mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wetu, tuutekeleze mradi huu, tufike tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili nina mambo matatu makubwa, la kwanza ni la ufahamu tu, hivi mradi huu unachukua eneo gani linalosemwa kwamba likiharibika ustawi wa jamii utakosekana? Hifadhi ya Selous ina ukubwa wa kilometa za mraba 50,000, eneo linalochukuliwa na mradi kwa ujumla wake kwa maana ya miundombinu yote ni kilometa za mradi 914.2 sawa na asilimia 1.8 ya eneo lote, hilo ni jambo la kwanza, ni muhimu sana Watanzania tukaelewa. La pili, katika hilo, tuta litakapojengwa eneo lile ni eneo dogo zaidi ukilinganisha na eneo lote la Selous ambalo ni kilometa za mraba 0.025 sawa na asilimia 0.025, eneo dogo sana.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kuelezea sana katika hilo. La pili, mradi huu utakapokamilika utatupatia *megawatts* 2,115, uwezo wetu wa sasa wa umeme tulionao tuna jumla ya *megawatts* 1601.92 haufikii hata umeme tutakaopata kutokana na mradi huu. Kwa hiyo hapa naeleza manufaa ya haraka ya mradi huu.

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la uharibifu wa mazingira limetajwa sana. Ni suala la kujiuliza wala halihitaji elimu ya juu sana. Leo hii tunapoongea wananchi wa Dar es Salaam wanatumia mkaa kwa mwezi magunia 5 00,000 ambapo kila gunia lina kilo 100, hapo ni Dar es Salaam peke yake. Wananchi wa miji mingine matumizi yao katika masuala ya nyumbani ni asilimia 68 lakini wananchi wa vijijini matumizi yao ya mkaa ni asilimia 27, lakini matumizi ya kuni ni asilimia 73, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ukijumlisha mkaa unaotumika Dar es Salaam na maeneo mengine, ukajumlisha mkaa unaotumika vijijini na maeneo mengine pamoja na kuni zinazotumika vijijini pamoja na mengine ni sawa na tani moja ya futi za ujazo ya mkaa pamoja na kuni zinazotumika ambayo inaweza ikavunwa katika eneo la hekta za ukubwa wa futi za ujazo 10 mpaka 12. Maana yake ukataji wa mkaa na kuni ni mkubwa zaidi tukiachia kutekeleza mradi huu kwa sababu Watanzania wengi wataendelea kutumia kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hapa hoja ya bure ni hii, hivi tukiacha kutekeleza mradi huu, tukaendelea kukata kuni na mkaa kwa hali hii hivi nani anaharibu mazingira. Tukiutekeleza mradi huu utatuwezesha kusambaza umeme mpaka vijijini. Kusambaza umeme mpaka kwenye miji, kusambazia umeme Jiji la Dar es Salaam linalotumia mkaa mwingi na hivyo kuokoa uharibifu wa mazingira. Kwa hiyo *summary* yangu katika hilo suala la mazingira, kuutekeleza mradi huu ni kutunza mazingira zaidi kuliko kuacha kuutekeleza mradi huu. Hii ni hoja ya msingi sana, ya bure kabisa na niwaombe Watanzania watusikilize, watufuate, tuutekeleze mradi huu. Tuepuke kuharibu mazingira yetu. Hiyo ni hoja ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, gharama za mradi; ili uzalishe *megawatt* moja ya mradi huu, upate *unit* moja ya umeme utatumia shilingi 36 tu basi. Kwenye vyanzo vingine hali ikoje? Kwenye gesi nianzie hapo na haina maana kwamna naiponda gesi, nitaizungumza vizuri na yenyewe,

kwenye gesi tunatumia shilingi 147 kwa *unit,* moja kwenye *solar* tunatumia shilingi 103 kwa *unit* moja, kwenye upepo tunatumia shilingi 103.2 kwa *unit* moja, kwenye makaa ya mawe shilingi 118 kwa *unit* moja. Ukienda kwenye *nuclear* ambayo bado ni 65 ambayo ndiyo inafuatia kwa wepesi pamoja na jotoardhi. Sasa tujiulize tunataka umeme wa ghali au mwepesi, tunataka tuzalishe umeme wa gharama nafuu ili Watanzania wa Maneromango kule waununue wa bei ya chini, hilo ndilo lengo la Serikali. Kwa hiyo gharama ya utengenezaji na uzalishaji wa mradi huu bado ni mwepesi ukilinganisha na miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, umeme mchanganyiko; Waheshimiwa Wabunge na Watanzania naomba niseme kutekelezwa kwa Mradi wa Rufiji hakumaanishi hata kidogo (kamwe) kutotekeleza kutumia gesi, kutotumia *solar* na miradi mingine. Tunakwenda na umeme mchanganyiko, Waingereza wanasema *energy mix* na ndiyo maana leo umeme mkubwa tunaotumia hapa nchini kwa sasa ni umeme wa gesi asilia ambao katika jumla ya *megawatts* 1601.92 t unatumia gesi yenye umeme wa sasa *megawatts* 884 sawa na asilimia takriban 60 ya umeme tunaozalisha. Maana yake bado tuna kipaumbele cha kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali ya gesi. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, matumizi ya gesi sio kuzalisha umeme tu, yako matumizi zaidi ya mara tano ya matumizi ya kuzalisha hiyo. Mpango wetu, tumegawanya mpango wa matumizi sahihi na endelevu ya rasilimali ya gesi kwa miaka 30 ijayo ambayo iko *subject to review* na yenyewe. Kwa sasa tumetenga takriban 8.8 kuzalisha umeme peke yake, lakini bado kwenye gesi hiyo hiyo tuna futi za ujazo 4.3 kwa ajili ya viwanda vitakavyokuja. Tunataka tujenge viwanda vya mbolea na *petrochemicals* na ni gesi hii hii tutaitumia. Hayo ni matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, pia tunataka tuwasambazie Watanzania gesi hii ili itumike kwenye viwanda vidogo vidogo na viwanda vingine ambapo napo tumetenga takriban futi

za ujazo 3.65 ili ziweze kujenga viwanda. Vile vile tunategemea Watanzania baadaye wasiendelee kukata kuni na kutumia mkaa itumike gesi hii kwa matumizi ya nyumbani ambako nako tumetenga futi za ujazi 1.2 kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na katika magari.

Mheshimiwa Spika, leo nimeleta gari linalotumia gesi. Kama ingewezekana kukanyaga ukumbini, ningependa sana likanyage mkaliona lakini kwa Waheshimiwa ya Wabunge na kwa ruhusa yako mara baada ya Bunge hili liko pale nje, Wabunge mnaruhusiwa kutazama muangalie miundombinu kwenye gari inavyotumia gesi. Lipo gari tumelileta kama mfano muone yanavyotumia gesi ambapo kwa sasa tuna magari zaidi ya 200 yanayotumia gesi kutoka magari 80 mwaka juzi, napo tunasonga mbele. Najaribu kuonesha matumizi ya rasilimali ya gesi ambayo wengi wanadhani inasahaulika, hata kidogo! Tunakwenda kuitumia kwa usahihi na usawa ule ule.

Mheshimiwa Spika, matumizi mengine katika gesi naendelea kupambanua kidogo kwa ruhusa yako. Gesi hii tunataka tuwe na viwanda vya vyuma, tutakuwa na ujenzi mwingi sana kwenye ujenzi vya uchumi wa viwanda ambavyo tumetenga futi za ujazo trilioni 1.1 kwa ajili ya viwanda *special* vya vyuma na bado sasa tunataka kujenga *LNG. LNG* Waheshimiwa Wabunge itatumia gesi kwenye mpango wetu, kila mwaka tumetenga gesi tani milioni 10 kila mwezi kwa ajili ya *LNG* tunayotaka kuijenga na *LNG* itahitaji gesi nyingi sana. Maana yake Waheshimiwa Wabunge, matumizi ya gesi bado yako pale pale hayajasahaulika kwenye umeme na kwenye masuala mengine.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye umeme, bomba la Madimba, bomba hili linaendelea kutumia gesi hii. Limesemwa kwamba uwezo wa bomba ni mkubwa kuliko mahitaji kwa sasa lakini suala jepesi la kujiuliza hata unapotaka kujenga kiwanja cha ndege, hivi unaogopa kujenga kiwanja kikubwa kwa sababu una ndege moja? Ni afadhali ujenge kiwanja kikubwa utakaponunua ndege 100 zitatua pale. Nataka nilieleze Bunge lako Tukufu, bomba hili

kwa sasa hivi na nimshukuru Mheshimiwa *CAG* wakati anakagua mwaka jana alisema matumizi yake ni asilimia sita ya gesi lakini mpaka sasa nataka niwaambie Waheshimiwa kupitia Bunge lako Tukufu mpaka sasa hivi matumizi ya gesi wala sio asilimia sita, imeshavuka! Imeshafika asilimia 16 na bado tunakwenda na hapa tumefungua tu mradi wa Kinyerezi namba II mwaka jana wenye *megawatts* 248.

Mheshimiwa Spika, tutaongeza *megawatts* 185 mwezi Agosti mwaka huu tutakapokamilisha Kinyerezi Na.I *extension.* Tutaongeza gesi nyingine kwenye kutumia, kwa sasa hivi gesi tunayotumia kwa siku ni milioni 120 milioni futi za ujazo kwa siku. Kwa hiyo gesi inaendelea kuingia kwenye kuzalisha umeme. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba pamoja na kutumia Mradi huu wa Mto Rufiji, bado matumizi ya umeme mchanganyiko ikiwemo gesi tunaendelea kuitumia.

Mheshimiwa Spika, tuna miradi mitatu mikubwa ya kuzalisha gesi katika umeme ikiwemo Kinyerezi I, Kinyerezi III yenye jumla ya *megawatts* 600 lakini tutaanza kwa awamu na *megawatts* 300 kwa *phase one* na *phase two.* Tuna Mradi wa Mtwara ambao tunaanza kuutekeleza mwakani nao wa *megawatts* 300 wa gesi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na ndugu Watanzania, matumizi ya gesi bado yapo pale pale. Nilikuwa najaribu kuwaondoa wasiwasi Watanzania kwamba kutumia maji katika kuzalisha umeme kwamba tunasahau matumizi ya gesi, la hasha hata kidogo, Mheshimiwa Rais yuko makini, Watanzania tuko makini, Waziri anayeongea yuko makini na Wabunge wako makini, tunaomba mtuamini. Hiyo ni hoja ya kwanza ambayo ningependa nichangie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, umeme wa upepo. Imeelezwa hapa kwamba katika Mabunge yaliyopita tulieleza nia yetu ya kuzalisha umeme wa upepo kwa haraka haraka, lakini nataka niwaeleze wachangiaji, nimeeleza gharama za kuzalisha umeme kwa upepo, *solar* na kadhalika lakini katika miradi ambayo tulitaka tuitekeleze ukiwemo

Mradi wa Singida na Same kupitia *Geo Wind* na *Wind East Africa* wazalishaji hawa walitaka tununue umeme kutoka kwao kwa senti za Marekani 13 kwa *unit,* jambo ambalo tungefanya hivyo tungeingiza mzigo mkubwa sana kwa Watanzania kupitia *TANESCO* kwa kununua umeme huo.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa niaba ya Watanzania ni afadhali tuchelewe lakini tuhakikishe safari yetu tutafika salama kuliko kuwahi ukaenda kuishia korongoni. Tungetekeleza miradi hiyo tulikuwa tunakwenda kuwaangamiza Watanzania. Tulichofanya kwanza ni kuanza kupitia upya hizo bei za Watanzania kutakiwa *TANESCO* kununua, *EWURA* wamekamilisha, tunakwenda sasa kuzalisha umeme huo kwa bei pungufu ili kusudi *TANESCO* wakiununua Watanzania wanunuaji wasibebeshwe mzigo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapitio hayo ndiyo maana imetuchukua muda, kwa sasa hivi tutakwenda kama mzalishaji yuko tayari ndiyo maana tumetangaza Novemba mwaka uliopita kwamba kama kuna mzalishaji binafsi na tunawataka sana wazalishaji binafsi tunachotaka ni umakini wa masharti aje badala ya kuendelea na kujadiliana, majadiliano yasiyoisha muda wake. Tumeweka viwango kwamba mzalishaji wa umeme wa upepo kama yuko tayari kutuuzia *unit* moja kwa senti saba za Marekani na kushuka chini, huyo aje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makaa ya mawe, kama yuko tayari kutuuzia kwa dola senti sita huyo aje. Kwa *solar* kama anataka kutuuzia kwa dola senti tano huyo aje ili *TANESCO* wakiununua umeme huo atakuuzia wewe mlaji kwa bei ya chini. Tungenunua kwa bei ya senti 13 kama baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanashabikia tukimbilie tulikuwa tunakwenda kuishia korongoni. Kwa niaba ya Watanzania, kama Waziri niliyepewa dhamana, tutakuwa makini katika hili ili kutowabebesha mzigo Watanzania ambao ni wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Spika, nimelieleza vya kutosha kwa nini hatukukimbia kuutekeleza, lakini tunakwenda kuutekeleza

lakini tunakwenda kutekeleza kwa utekelezaji makini kwani Serikali iko makini, tutaifanya hivyo kwa niaba ya manufaa ya Tanzania. Hapo nimejibu suala la upepo kwa nini hatukutaka kufanya hivyo kwa sababu kuna watu walitaka tutoe maelezo.

Mheshimiwa Spika, hasara kwa *TANESCO,* hivi hasara ni kitu gani? Kwanza *TANESCO* imepata mizigo mikubwa sana huko nyuma. Kama ni hasara ziko sababu zilizochangia hasara kwa *TANESCO.* Sababu ya kwanza kubwa tulikuwa na miradi mikubwa ya kukodi mitambo, mitambo ya kukodi ya kuzalisha umeme wa mafuta mazito na ninyi wengi tunaifahamu Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Mabunge yaliyopita na Serikali zilizopita kwa kupiga kelele ili Serikali iachane na ununuzi wa mafuta mazito kuzalisha umeme ikiwemo mtambo wa *IPTL, Aggreko, Symbion* na mitambo mingine, kwa nini nasema hivyo? Tulikuwa tunalipa *capacity charges* kila mwaka, zaidi ya shilingi bilioni 635 kwa kampuni moja kuilipa kwenye mtambo mmoja. Hili lilikuwa ni zigo kwa *TANESCO*, hilo tumeachana nalo tangu mwaka juzi, kwa hiyo, hasara zinakwenda zinapungua.

Mheshimiwa Spika, la pili, viko vituo vingi, ukienda Madaba tulikuwa tunatumia mafuta, Ludewa mafuta, Songea mafuta, Mbinga mafuta, Kigoma mafuta, Loliondo mafuta, Mwanza Nyakato mafuta; na mafuta hayo, natoa mfano, Ludewa tu ulikuwa unaweza kununua mafuta ya shilingi bilioni 703, lakini ukiuza umeme unachovuna ni bilioni 331, hiyo ni hasara.

Mheshimiwa Spika, tulichofanya ni kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme mkubwa, ili nchi nzima tuiunganishe kwenye gridi ya taifa tuachana na hiyo mitambo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, mwezi juzi alizindua mradi mkubwa sana wa Makambako-Songea, ambao umetuokolea takribani shilingi

bilioni 9.8 tulizokuwa tunanunua mafuta kwa ajili ya kuzalisha umemem na kuwasambazia Watanzania. Hizi zilikuwa ni hasara kwa *TANESCO* ndugu zangu, sasa tumeachana nazo. kwa hiyo zilikuwepo na mkakati ndiyo hiyo ninayoisema *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ndugu zangu, *TANESCO* ilikuwa inaleta nguzo kutoka *South Africa,* ilikuwa inanunua luku za mita kutoka China, *turansformar* kutoka India, nyaya kutoka nje. Mwaka jana tumepambana na hili, tumesema lazima tujenge viwanda vya ndani, na njia pekee kwa vile vifaa vinavyopatikana nchini ni kusitisha uingizwaji wa vifaa hivi na kuliokolea gharama shirika letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge mliounga mkono jambo hili, wapo lililowaumiza, nafahamu, lakini tunasonga mbele kwa kuokoa gharama na hasara kwa shirika letu. Maana yake nini, tulikuwa tunaweza kununua nguzo moja mpaka kwa shilingi laki nne kwa fedha ya Tanzania. Nguzo kuitoa South Africa na inawezakana hiyo hiyo inazunguka inarudi, bado unatakiwa ui-*clear* bandarini. Suala siyo gharama tu, hata muda. Sasa hivi unaweza ukakimbia hapa Mafinga ukanunua nguzo moja kwa shilingi 80, ni kiasi gani shirika linaokoa gharama hiyo? Hizo zote zilikuwa ni hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *summary* yake, mpaka mwaka juzi shirika lilikuwa na hasara ya shilingi bilioni 349, mwaka jana zimepungua, zimekuwabilioni 122, mwaka huu zinakwisha na kupata faida ya bilioni tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge nataka kusema, nini faida ya sitisho hilo? Kwanza tumeokoa jumla ya shilingi bilioni 162.34 ambazo tumenunua vifaa hivyo, lakini pili tumetengeneza ajira kwa watanzania zaidi ya 3520 kwa ajili ya viwanda hivyo. Kwa hiyo, tulikuwa tuna viwanda vitatu vya nguzo, sasa hivi tuna viwanda tisa, tulikuwa tuna kiwanda kimoja tu cha *transformer*, tuna viwanda takribani vitano. Tulikuwa tuna kiwanda kimoja cha waya, tuna viwanda sita, tulikuwa hatuna kiwanda hata kimoja cha luku,

sasa hivi tuna viwanda vitatu vya luku, ndugu Watanzania naomba tuelewe hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji yetu ya ndani ya vifaa vyote kwa ujumla wake ni nusu ya uwezo wa viwanda vya ndani kwa sasa vilivyojengwa ndani ya miezi saba hadi sasa, hayo ni mafanikio makubwa, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Suala la Madeni ya *TANESCO*. Mwezi januari mwaka 2018, ni kweli *TANESCO* ilikuwa na madeni takribani bilioni 990, lakini sasa hivi inavyolipa yamepungua sana, na inaedelea kuyapunguza, na mkakati wa kumaliza madeni yote kwa shirika hili ni ifikapo mwaka 2026, madeni yote *TANSECO* itakuwa imeyamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, madeni yake yanapungua limefikia bilioni 957, lakini tumemuomba mhakiki wa Serikali ayahakiki madeni haya. Yako madeni mengine yanabishaniwa na yako madeni mengine wala si halali; ni matumaini yetu yatapungua sana. Katika madeni hayo *TPDC* kimsingi, ambaye ndiye anayeuza gesi kwa kiasi kikubwa kwa *TANESCO* ndiye aliyekuwa na madeni makubwa, 480, lakini sasa yameshuka mpaka 340. Kwa sababu sasa hivi *TANESCO* ina uwezo wa kulipa, badala ya kulipa bilioni saba kwa wiki sasa hivi ina uwezo wa kulipa bilioni tisa kwa wiki, katika madeni ya *TPDC*.

Nalielezea Shirika la *TANESCO*kwa ujumla wake jinsi ambavyo sasa hivi limejipambanua. Silitetei kama shirika la umma lakini kwa kwa sababu sasa hivi lina uwezo wa kuwahudumia Watanzania. Zipo changamoto, lakini lina uwezo wa kuwahudumia Watanzania, na tunakokwenda lita-*improve* zaidi. kwa hiyo nimeona niseme hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa kuhusiana na madeni, kwa vile *TANESCO* ina uwezo wa kulipa madeni na kwa vile sasa hivi *TANESCO* haipati ruzuku kutoka Serikalini, tumemwomba Mheshimiwa Rais na ametuelekeza, shirika hili ni kubwa halina haja ya kuombaomba, shida ilikuwa ni usimamizi na sisi tunalisimamia. Kwa hiyo tangu mwaka juzi

shirika hili halipati ruzuku kutoka Serikalini, linajiendesha lenyewe. Zaidi ya hapo linapata faida ya ongezeko ya asilimia 1.5 mwaka juzi na mwaka jana ni 7.6. Kama nilivyosema, ni matumaini yetu, kuanzia mwaka huu na miaka inayokuja, shirika la TANESCO litaanza kutoa gawio Serikalini. Hayo ni mafanikio, nilitaka kueleza kwamba pamoja na madeni hayo, lakini jitihada za kuyalipa ni kubwa na ni matumaini yetu yatakwisha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme moja katika suala la umeme vijijini. Ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri; mwaka 2008 tulikuwana vijiji 506 vilivyokuwana umeme, 506, mwaka 2015 tulikuwa na vijiji 2018 vilivyokuwa na umeme. Leo hii tunapoongea umeme vijijini tumeunganisha vijiji 7127, tunapoongea hapa. Mradi unapotekelezwa tunajua kunakuwa na changamoto nyingi sana. Mradi huu utakwisha mwezi juni mwakani, ni matumaini yetu utakapokamilika mwezi juni mwakani, utafikisha vijiji 10,128 vyenye umeme, sawa na asilimia 84 na tutabakiza vijiji 1990 katika ya vijiji 12,268. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Watanzania, sisi kwa sasa ndiyo vinara, ndio tunaoongoza kwa nchi ya Afrika Mashariki kutandaza umeme vijijini kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wakenya pamoja na kuwa na umeme wa MW 2,003, lakini wana asilimia chini ya 43 kupeleka umeme vijijini. Waganda, mpaka wametuomba tupeleke vijiji sita vya mfano nchini kwao ili nao waone umeme vijijini, na tumewapelekea vijiji vya mpakani, vikiwemo Nangoma pamoja na Umurushenya, tutaendelea kuwapelekea. Huu ni mfano kwa nchi yetu inavyopiga hatua.

Mheshimiwa Spika, lakini zipo changamoto katika suala hili; moja ya changamoto katika maeneo haya kwanza ni uelewa, kwamba hauwezi ukawa wa pamoja kwa wakati mfupi. Kazi yetu ni kuendelea kuwaelewesha wananchi na washirika wengine ili kusudi tuutekeleze mradi huu kama ilivyodhamiliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, mnatupa ushirikiano mkubwa sana katika kupeleka umeme vijijini, nawapongeza sana sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi napenda niseme shukrani mlizotupa katika kupiga hatua kwenye umeme vijijini naomba ziwarudie Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tutaendelea kutoa ushirikiano ili tupeleke umeme katika vijiji vyote. Lipo jambo lilizungumzwa hapa, kwamba viko vijiji 55 kwamba vilikuwa hewa. Nataka niseme, kwenye miradi hii mikubwa changamoto zipo; lakini kubwa, hata Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, unaweza ukakuta kijiji kina vitongozi saba, lakini kati ya vitongoji saba ni kitongoji kimoja ndicho kimepelekewa umeme. Swali la kujiuliza, vitongoji vingine tuviache kwa sababu tulishapeleka kitongoji kimoja cha kijiji kile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini unapopelekea umeme, hukiiti kitongoji, unaita kwa jina la kijiji. Kwa hiyo mnakuta majina mengine yamerudiwa hata zaidi ya 100, lakini tunapokwenda kule la kwanza ni kufanya *survey* ili kuona ni sehemu gani ya kijiji kilichopelekewa umeme, hakina, ndipo eneo hilo lipelekewe umeme. Nimeona nitoe ufafanuzi katika jambo hilo na kama kuna mahala ambapo kuna kuwa na *oversight* lazima tufanye *replacement* na tunafanya hivyo kwa kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nichukue nafasi hii kusema kwamba utekelezaji wa miradi hii tutaendelea kufanya usanifu ili kuwa na usahihi wa kutosha. Hata hivyo, tuko tayari kupokea mawazo na ushauri wa Wheshimiwa Wabunge ili tuweze kufanya marekebisho ya kuimarisha kazi hii.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, ningependa sana niseme, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania; ni kweli tunapopeleka umeme vijijini maeneo

ya taasisi yanasahaulika sana, na ni changamoto si tu kwa shirika na kwa mkandarasi hata wasimamizi wa taasisi hizo. Nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge watusaidie kupitia wenyeviti wa halamshauri na wakurugenzi, maeneo yote ya taasisi ambayo yako kwenye vijiji vyenye umeme, niombe sana yalipiwe ili taasisi zote za umeme ziendelee kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, iko changamoto ya Waheshimiwa Wakurugenzi, Wenyeviti wa Halmashauri kuilalamikia Serikali, kwamba Kituo changu cha Afya hakina umeme, Zahanati haina umeme, shule haina umeme, lakini sababu haijalipiwa. Niwaombe sasa tutumie nafasi hii tulalamike tukiwa tumeshafanya malipo. Nami nitumie nafasi hii kuelekeza Shirika la Umeme *TANESCO* pamoja na wakandarasi popote watakapoona taasisi ya umma, iwe kilomita 100, iwe kilomita tano, ipelekeeni umeme, ili mradi pamelipiwa. Waheshimiwa Wabunge nimeeleza kwa msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, nitoe maelekezo kwa wakandarasi, Shirika la Umeme *TANESCO* na wadauwengine wanaosambaza umeme, kwa niaba ya Serikali, popote pale, taasisi ya umme itakapokuwa, kutoka kwenye kijiji chenye umeme au eneo lenye umeme, iwe kilomita 100, iwe kilomita 20, iwe kilomita mbili, pelekeni umeme kwenye taasisi hiyo ili mradi imelipiwa gharama zake, nadhani limekaa sawa, elfu ishirini na saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali ya awamu ya tano, na mimi nilisema niliposimama kwenye Bunge lako Tukufu, awamu iliyopita mwaka uliopita, nilieleza kwamba tutapeleka umeme mpaka kwenye nyumba za matembe. Watu walikuwa wanadhani tunatania, mpaka kwenye nyumba za makuti, walikuwa wanadhani tunatania, tuko *serious*na jambo hili. Nyumba yoyoye ya mtanzania, mtanzania anamuishi, ndimo humo humo tutampelekea umeme, humo humo tutampelekea umeme. Atakapohama nasi tutapeleka umeme atakakoelekea,tunajali maisha ya watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elfu 27 lengo lake ni kuhakikisha Watanzania wote wanapata umeme. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa maelekezo mazuri, kwa kujali Watanzania wa maisha ya kawaida. Tumefanya maamuzi, kupitia Bodi ya Shirika letu la *TANESCO*, kwamba umeme unaopelekwa vijijini, uwe wa *REA*, uwe unaopelekwa na *TANESCO*, ili mradi unapelekwa vijijini, kuanzia Mei mosi mwaka huu kuunganishwa umeme ni elfu 27 tu, basi. Iwe *TANESCO*, iwe *REA*, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, tukatoe elimu hii na mimi nimesimama hapa kupitia Bunge lako Tukufu, Watanzania wote wanisikie, wandarasi wote wanisikie, TANESCO wanisikie, Wabunge mnisikie, na mimi najisikia hivyo, gharama ni elfu ishirini na saba *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala *secular* lilishatoka na Waheshimiwa Wabunge mtapewa.

**SPIKA:** Hebu liweke vizuri, Mheshimiwa Waziri, hapo kwenye 27 hebu irudia tenaili Wabunge waondoke nayo vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kwa ruhusa yako. Kuanzia tarehe moja, Mei mwaka huu kupitia Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO),* bodi imepitisha na *secular* ilishatoka na imeshaanza kufanya kazi, gharama ya kuunganisha umeme katika maeneo yote ya vijijini; iwe unapelekwa na *REA*, iwe unapelekwa na *TANESCO*, au yeyote aliyepewa kazi na Serikali, gharama ni elfu ishirini na saba tu basi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima ya Bunge lako, nitoe maelekezo kwa mameneja wote wa kanda, mikoa, wilaya, wa *TANESCO* na Makao Makuu, walisimamie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Niendelee, Kukatika kwa Umeme. Katika maeneo ambayo pia tumeimarisha sana ni pamoja na eneo hili. Pamoja na kukatika kwa umeme katika baadhi ya maeneo, Serikali inachukua hatua za maksudi sana kuhakikisha kwamba jambo hili halijitokezi sana. Katika

maeneo ya Dar es Salaam, nitoe taarifa kwa wananchi wa Dar es Salaam na Watanzania, shida inayotokea sasa hivi tulipata *break-down* ya *engine* moja, lakini Serikalikupitia kwa Mheshimiwa Rais wetu, tumeleta mashine ya MW 240 ambayo inafungwa sasa hivi kwa Dar es Salaam, ambayo ni matumaini yetu, ndani ya mwezi mmoja itakamilika. Kwa hiyo, maeneo yote ya Dar es Salaam na watanzani kwa sababu inajengwa kwenye gridi ya taifa, umeme utakuwa ni wa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania waendelee kuvumilia, kwa sababu ziko changamoto nyingi, lakini matumaini yetu umeme utakwenda kuimarika na kukatika itapungua sana.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu *LNG*. Mradi wa *LNG* umeelezwa sana, na mimi ningependa kurudia. Dhamira ya kutekeleza mradi huu iko palepale. Mradi wa*LNG* utatekelezwa, nimetaja gesi tuliyotenga na hatua tuliyofikia sasa hivi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Nape na Wabunge wengine wa Lindi, tuliokuwa nao hivi juzi katika semina tuliyoifanya. Tumekutana na wadau, tumekutana na wawekezaji pamoja na Serikali, tumekubaliana, majadiliano yataongeza *speed*. Ni matumaini yetu watamaliza mapema, ikiwezekana mwakani, ili utekelezaji uanze kufanyika na ujenzi utaanza miaka mitano ijayo na huu mradi utachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumetenga mpaka fedha kwa ajili ya kufidia wananchi ambao wataathirika na mradi huu. Hii ni kuonyesha *commitment* ya Serikali kwa lengo la kuutekeleza mradi huu. Niseme tu kwamba ndugu zangu wananchi wa Lindi na Watanzania wote mradi hu ni mkubwa, tumeupa kipaumbele na utatekelezwa bila kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala kurudiwa mikataba hapa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameeleza. Iko mikataba ya rasilimali ya gesi, nikopongeze Mheshimiwa Spika, mwaka jana uliunda Tume Maalumu, kwa

ajili ya kufuatilia na kukagua umuhimu, dosari na changamoto za mikataba hiyo. Nitoe shukurani sana kwako na kamati iliyofanya kazi hiyo; lakini nirudie kusema, Serikali inachukua hatua madhubuti sana.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ameshanza zoezi hili, ni matumaini yetu litakamilika. Lakini lengo letu kubwa, maama liko jambo limezungumzwa, la kutotoa leseni; lengo letu kubwa, ipo hatari ya kutoa leseni kwenye masharti ambayo ni hasi kwa Watanzania. Tunataka tujiridhishe, kuondoa wasiwasi, kwamba masharti yatakayoingiwa yatakuwa ni sahihi na bora kwa Watanzania baada ya mikataba hii kupitiwa vizuri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, chukua muda kwa umakini, fanya kazi kwa umakini, toa kitu cha makini, tufanye kazi ambayo itakuwa na tija kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Usambazaji wa Gesi Majumbani. Tumeeleza katika taarifa yetu. Bila shaka katika eneo hili, kati ya maeneo ambayo watanzania watakumbuka sana utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ni pamoja na kutekeleza miradi ya kusambaza gesi majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisirudie hasara ya mkaa pamoja na mambo mengine yanavyofanyika, lakini ni kubebesha mzigo kwa Watanzania. Watanzania wengi kwa sasa hivi, wengine unaweza kukuta wanakula mlo mmoja kwa sababu ya kuogopa gharama ya matumizi ya kupikia. Mradi huu utaokoa gharama kwa kiasi kikubwa. Mradi huu tumeanza kuutekeleza maeneo ya Dar es Salaam, tumeshaunga wateja zaidi ya 200 na yako maeneo mengi kwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na mikondo minne, mkondo wa kwanza wa kupeleka gesi ni ule unaotoka Ubungo, kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam- Mlalakua mpaka Tegeta; mkondo wa pili unakwenda mpaka Mikocheni, mkondo wa tatu unakwenda mpaka Keko na mkondo wa nne unakwenda mpaka maeneo ya Chanika. Kwa hiyo ni matumaini yetu baada ya kusambaza vizuri gesi

hii Watanzania, hasa wananchi wa Dar es Salaam watatumia gesi hii kupunguza ukakasi wa maisha.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili muhimu, tulichoanza kufanya, gesi kwa sasa hivi, ambayo tumeanza kuisambaza, ina punguzo la asilimia 40 ya gharama ya matumizi ya kawaida ya sasa hivi ya gesi asilia. Kwa sababu mitungi inayokuja kwa sasa wananchi wanalipa zaidi ya shilingi 50 na 57,000, lakini kwa matumizi ya gesi hii wanayounganishiwa, gharama yake itakuwa ni chini kwa asilimia 40 ya bei na gharama hiyo ya mitungi ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vilevile wananchi wanatumia mkaa, nimetaja hasa mkaa wa kilo 100, utakuwa na punguzo si chini ya asilimia 35 mpaka 45. Kwa hiyo, utawapunguzia ugumu na ukakasi wa masiha wananchi kwa ajili ya kutumia rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, Umeme wa *Grid* Kigoma na Katavi. Yako maeneo tunakubali, kwamba Serikali bado inayafanyia kazi. Tumeanza kutekeleza, tuna miradi miwili, mradi wa kwanza ni wa kupeleka umeme mkubwa wa kV 400, kutoka Iringa kupita Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga. Utekelezaji wa mradi huu umeshaanza, umbali wa kilometa 624. Pia tuna eneo la kutoka Sumbawanga - Mpanda - Kigoma hadi Nyakanazi. Utekelezaji wa eneo hili sehemu yake bado na tunaendelea na majadiliano kupata wawekezaji ili tuanze kuutekeleza. Tumeona tuanze kupeleka umeme mwingine kutoka Nyakanazi kupita Kigoma hadi Geita, utekelezaji wake umeanza.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kunusuru Kigoma kwa sasa kwa haraka, ni huu mradi wa kuusafirisha umeme wa kV 132 kuutoa Tabora kupitia Urambo kwenda Nguruka hadi Kidahwe, umbali wa kilometa 391, utekelezaji umeanza na matumaini yetu kwamba tunaweza kukamilisha ifikapo juni mwakani. Kwa hiyo, wananchi wa Kigoma, katika eneo hili wawe na matumaini kwamba nao wataacha kutumia mafuta mazito na kuwapunguzia gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Katavi, tutachukua umeme kutoka Tabora vilevile utapita Ipole kwenda Inyonga mpaka Nsimbo umbali wa kilometa 383. Utekelezaji unaenda sambamba na Mradi wa Kigoma. Miradi yote miwili itagharibu takribani dola za Marekani milioni 92.8. Utekelezaji wa miradi hii ni muhimu sana kuutaja ili pembe zote nne za nchi yetu ziweze kupata umeme wa gridi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Rukwa ni kweli yako maeneo ambayo hayana gridi kwa sasa tunachukua gridi kutoka Zambia takribani megawati nane lakini yako maeneo tutatoa umeme kutoka maeneo ya Kigoma kupeleka Katavi hadi Rukwa wakati tunakamilisha Mradi mkubwa wa Sumbawanga hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge pamoja na kueleza maeneo hayo, lakini ningependa pia nizungumzie huu Mradi wa Bomba la Mafuta. Hivi sasa tumeanza kutekeleza Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda, tunafahamu kwamba imechukua hatua kufikia hadi sasa, lakini napenda kutoa taarifa tu katika Bunge lako Tukufu kwamba, mradi huu tunaendelea vizuri. Hivi sasa tuko katika hatua za mwisho kabisa za kumaliza majadiliano na majadiliano yakikamilika hatua inayofuata ni kuanza ujenzi. Nimpongeze sana Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi wiki iliyopita ameshafanya semina kwa ajili ya tathmini ya wananchi watakaopisha miradi wakati wa ujenzi.

Mheshimiwa Spika, wakati tunafanya majadiliano hatua za awali za ujenzi zimeshaanza, kwa sasa tunachofanya ni kufanya maandalizi ya kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa bomba, maandalizi ya kulipa fidia na kwa ajili ya kujenga vituo 16 vitakavyopitiwa na mradi huu. Hatua hii ni kubwa, ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huu na ningependa nitoe taarifa kwamba utekelezaji wa mradi huu bado uko pale pale na tumepanga utakamilika ifikapo mwaka 2023, kwa sababu kwa sasa umechelewa kidogo, lakini muda wa kuutekeleza ni uleule, miezi 36.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza hapa, nilizungumza suala la *IFAD* watekeleze wataalam wetu, Huyo *IFAD* alikuwa ni Mkandarasi ambaye ni *Consultant* ambaye alikuwa anasimamia miradi ya ujenzi wa *backbone*, ilikuwa kuna hoja kwamba amefanyiwa malipo ya ziada ya milioni 97. Napenda kulieza Bunge Tukufu jambo hilo kwanza lishakuwa *close* na Mheshimiwa *CAG* na wala siyo jambo la kujadili kwa sababu alishalipa kulingana na makato ambayo yalifanywa kulingana na mkataba wake. Kwa hiyo jambo hili napenda tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anataka kujua usahihi wa jambo hili kuwa usahihi wenyewe uko katika hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumza kwa sasa ambalo ni vema sana niwaambie Watanzania ni makusanyo na mapato ya shirika letu. Si kwamba narudia naeleza eneo dogo na sehemu niliyokwishaeleza kwa sasa Shirika la Umeme *(TANESCO)* wako wananchi na baadhi ya watu wanasema ligawanywe, ningependa kuchukua nafasi hii kuwaeleza Watanzania kwamba jamani umeme ni usalama, umeme ni biashara, umeme ni uchumi, sipingani na wanaosema shirika ligawanywe, lakini ningependa sana tuwe makini katika kuchukua hatua za kulimega shirika hili kabla hatujafanya hivyo. Kwa nini nasema hivyo? Ukisema uzalishaji ufanywe na mtu binafsi na amiliki mitambo ya kuzalisha maana yake atakuwa na mamlaka ya kusema leo nazima umeme nakarabati nchi nzima, matokeo yake nchi mnaweza mkaingia gizani, hilo ni jambo mahususi Watanzania tulielewe tunaweza tukaligawa lakini lazima tuwe makini katika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika usambazaji, ni matumaini yangu kama tutaipatia shirika na bahati mbaya ikiwa ni shirika binafsi lisambaze umeme mpaka vijijini ni mashirika machache na wengi wameshajaribu na kushindwa, yatakayoweza kufanya hivyo, matokeo yake watapenda kupata faida kubwa na Watanzania wengi uwezo wao ni mdogo jambo la msingi hapa kitakachokuwa Watanzania

watashindwa kumudu na hivyo azma ya Serikali ya kupeleka umeme nchi nzima itashindikana. Ningependa kutoa wito Watanzania tutoe maoni namna bora ya kulifanya shirika letu liimarike zaidi badala ya kuligawa vipande vipande. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru ulipokuwa unazungumza umeme mchanganyiko, mtu akasema kuna umeme *solar* muhimu sana kuweko kwenye gridi ya Taifa, ulimjibu mpaka nikasema kumbe Mheshimiwa Spika ni mwanasayansi. Unaweza ukatumia ukaweka umeme wa upepo kwenye gridi ya Taifa megawati 1,000, umeme wa upepo megawati 1,000, lakini umeme wa *solar* unategemea jua.

Kwa hiyo siku jua limeshuka utakosa megawati 1,000, siku jua limeshuka na inategemea na mpango mkakati, hili jambo lazima lielezwe kwa sayansi sana, namwona sana Mheshimiwa Heche anataka kuamka lakini ajiandae na ufafanuzi wa kisayansi.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa katika gridi ya Taifa *standard* katika kataifa yote umeme wa *renewable* kwenye *absorption* ya umeme haitakiwi azidi asilimia 15, kwa sababu ya kuogopa *risk*. Kwa hiyo kama tuna megawati 1,600 tunatakiwa tuingize umeme wa *renewable* walau asilimia tano mpaka 15 ikizidi hapo unaiweka nchi katika hatari ya kukosa umeme itakapotokea dharura hiyo. Napenda niseme na kupongeza kwa *argument* hiyo, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, umeme wa upepo kulingana na stadi tulizonazo *speed* maana *potential* tuliyonayo kwenye umeme wa upepo ni *speed* ya upepo, *speed* ya upepo tuliyonayo kwa sasa hivi ni *speed* ya kuanzia *4.5 meter per second* mpaka *meter 9.0 per second*. Kwa hiyo ikipungua *speed* maana yake unakosa umeme wa upepo vilevile, haya ni masuala ya kisayansi sana, lakini napenda niyaseme kwa maana ya uelewa Waheshimiwa Wabunge. Kubwa unapokuwa na umeme mchanganyiko na hasa unapokuwa na umeme mwingi wa maji gharama yako itakwenda kupungua. Wenzetu wa Misri ambao wana

umeme zaidi ya megawati 4,000 wa maji ndiyo maana bei yao iko chini ya dola 4.6 dola za Marekani, sisi yetu iko juu kwa sababu tumetumia pia gharama kubwa kwenye ku-*compute* gharama za umeme na kwa sababu hatujazalisha umeme mwingi wa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napenda kutumia nafasi hii kurudia tu kusema kutumia umeme wa maji, kutumia umeme wa gesi, kutumia umeme wa makaa ya mawe ni muhimu sana, lakini yako mambo mawili ya kuzingatia kwanza gharama ya kuijenga mtambo huo na ya pili gharama ya kuwauzia wateja walaji wa mwisho utakapokamilika mradi huo. Ndiyo maana tunasema mara baada ya miradi hii kukamilika na masuala mengine yanayoendelea, ni matumaini yetu kwa Serikali yetu makini inakwenda kutazama upya bei kwa gharama za umeme ili kuwapunguzia mzigo Watanzania ambao tunatumia kodi yao kuzalisha umeme huu kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliyotaka kueleza ya msingi nimeyaeleza, sasa ningependa nitumie nafasi hii kwa niaba yako na Waheshimiwa Wabunge nishukuru kwa michango yao, kuna mengi ya kusema mengine tutaendelea kuyaeleza na kwa sababu hiyo mengine tutayaeleza kwa maandishi tutaleta ufafanuzi kwenye Bunge lako tukufu na mengi tumeomba yaiingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa maelezo ya uchambuzi wa hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge walizozitoa katika michango yao. Tunakushukuru sana kama mtoa hoja wa hoja hii ya Serikali, Katibu sasa.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kif. 1001 - *Administration & Human Resources Management*................Sh. 3,034,746,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jitu Vrajlal.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba ufafanuzi katika jambo moja ambalo mpaka sasa hivi bado sijapata kuielewa vizuri, Sera yetu ya Nishati ni kuwa na uzalishaji wa nishati na matumizi ya nishati jumuishi yaani *energy mix* iwe ya uhakika na vyanzo vyote viweze kutumika. Pia huko nyuma tayari tulishawekeza kwa sehemu kubwa kwa gharama kubwa katika bomba la gesi kuleta gesi na kwa sasa hivi kwa takwimu ambazo tumepata inatumika kwa asilimia sita au saba tu, je, kwa nini badala ya kuwekeza kwenye gharama kubwa kwenye uzalishaji wa nishati kwa njia nyingine kwa nini tusingetumia gharama hizo kuongeza uzalishaji wa gesi na matumizi ya bomba hilo la gesi ili baadaye sasa ndiyo tuje tuwekeze huko kwa sababu tayari tulishawekeza kwa sehemu kubwa katika bomba hilo la gesi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona angalau tungefikisha asilimia 90 au asilimia ikiwezeka asilimia 100 ili matumizi yake yaweze kupatikana na iwe ni nishati kwa ajili ya kuzalisha umeme, nishati kwa ajili ya viwandani, pia nishati kwa ajili ya majumbani huko kama ni Dar es Salaam na baadaye isogee kwenda Mikoani.Kwa nini Serikali isifikirie jambo hilo? Naomba kupata ufafanuzi wa jambo hilo ili na mimi nipate uwelewa vizuri. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi wa suala hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt, Kalemani tafadhali.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge Jitu kabla sijasahau aniachie shilingi tukafanye kazi lakini kubwa nimeeleza kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba hili ningependa sana kusahihisha habari za upotoshwaji unaosemwa, labda imenukuliwa vibaya katika maeneo mengi. Sasa hivi tunachukua asilimia 15 na wala siyo sita hilo la kwanza, imepita sita la kwanza, lakini la pili bomba hili kwenye matumizi ya rasilimali ya gesi nchini tumepanga matumizi ya miaka 30 ijayo ya awali na mpango ni kutumia bomba hili kwa zaidi ya miaka 100 ijayo Watanzania wataendelea kuwepo, mahitaji ya gesi yataendelea kuwepo, kwenye kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumejenga bomba hili lenye nchi 32 upana wake la Songosongo lina nchi 16 lilikuwa dogo. Lengo lake ni nini ili mahitaji yakiwa makubwa mbeleni basi iweze ku-*pump* gesi nyingi zaidi tuzalishe umeme mwingi zaidi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sasa hivi tunasema ni asilimia 15, lakini mwaka 2045 bomba hili litafikia asilimia 352. Kwa hiyo hata hivyo bado ni dogo itabidi tujenge hata bomba lingine huko mbeleni kwa mahitaji ya miaka mingi ijayo. Kwa hiyo bado hili siyo *white elephant* ni jambo muhimu sana katika hili. Tunaposema umeme mchanganyiko, tunasema kwamba tunatumia hii gesi kuzalisha umeme wakati huo bado na miradi mingine ya kuzalisha umeme inaendelea. Nimwombe Mheshimiwa Jitu aelewe nimeeleza vizuri hapo, nilikuwa nataka nifafanue tu wa bomba na mahitaji ya miaka 30 ijayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Richard.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Sina haja ya kushika mshahara wa Waziri, lakini nitahitaji maelezo ya kina. Katika uchangiaji wa

Waheshimiwa Wabunge mbalimbali hapa ndani waliweza kuzungumzia suala la matumizi mabaya ya fedha za upande wa umeme vijiji - *REA* ambao umefanywa na kampuni ya IFAD takribani dola za Kimarekani 44,725. Tunaelewa kabisa katika sera ya matumizi bora ya fedha pamoja na udhibiti, tunahitaji kudhibiti matumizi ya fedha za umma, ningeomba nipate ufafanuzi au kauli ya Serikali nini kilichojiri juu ya tuhuma hizi za dola 44,000 katika Mfuko wa *REA*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati ufafanuzi, kuhusu jambo hilo.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbogo kuuliza swali hili. Ni kweli kwanza niseme kuna kampuni ilikuwa inaitwa IFAD ilikuwa inasimamia miradi ya kujenga Mradi wa *backbone* kutoka Iringa, Dodoma, Singida hadi Shinyanga, huyu ni *Consultant* ambaye kimsingi alilipwa shilingi milioni 99.2 ambayo sawasawa na dola 44,200 na kadhalika, lakini baadaye ikaonekana kwenye malipo alilipwa kimakosa. Kwa hiyo akaanza kukatwa na akakatwa zote zikaisha na bahati nzuri wakati *CAG* anakagua kwenye taarifa yake ya terehe 15 nadhani Desemba alishalifunga jambo hili. Kwa hiyo nitoe taarifa tu kwamba lilishafungwa na wala si jambo tena, kwa hiyo lishakuwa *cleared.* Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda nipate ufafanuzi kwenye suala la mazingitra hasa tunapozungumzia Mto Ruaha ambao ni mto mkuu na Mto Ruaha sasa kutokana na uharibifu wa mazingira umekuwa ukipeleka maji kidogo sana katika Bonde la Mto Rufiji kwa maana ya Mto Rufuji, Ruaha inapeleka asilimia 15.5 tu. Hata hivyo, ukiangalia mito mingine ambayo imetunzwa vizuri na mazingira yake yamewekwa vizuri, uoto wa asili uko vizuri kama Mto Lwegu ambao unatokea kule Namtumbo unaingiza maji kwa asilimia 19. Pia ukiangalia Mto Kilombero nao unaingiza maji katika Mto Rufiji kwa asilimia 65.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nipate ufafanuzi wa Serikali, ina mpango gani wa kuweka mazingira wezeshi ambayo yatarudisha hali ya uoto wa asili katika mto Ruaha ambao umeharibiwa sana kutokana na mifugo, kilimo na shughuli za kibinadamu zinazoendelea pembezoni mwa mto huo? Kama sitapata maelezo mazuri, basi nakusudia kuondoa shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ufafanuzi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mazingira tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru. Kwanza nimwombe dada yangu Mheshimiwa Jacqueline hana sababu ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ni kweli shughuli za kibinadamu zimefika mahali zinazidi uwezo wa mto kwa sababu ya kilimo ambacho si rafiki, lakini kwa asilimia kubwa watu wale wanachimba mitaro ambayo haina uwezo mitaro inayotumia maji mengi sana na maji yanasambaa. Sasa Ofisi yetu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira tumeshaweka utaratibu kwamba tutakapopata fedha za *climate change* tutaelekeza nguvu kule kuhakikisha kwamba tunawaelimisha wakulima na kuhakikisha eneo lile lote tunalisimamia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, umeridhika?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo ya Serikali juu ya suala la mazingira mimi niombe tu kwamba Serikali ijikite kikamilifu katika Mto huu wa Ruaha kuhakikisha kwamba wanasimamia na wananchi wapate elimu ya kutosha kama anavyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira ili mwisho wa siku mto huu na wenyewe uweze kurudisha uoto wake na uweze kuweka maji mengi ambayo yatakuwa ni mchango mkubwa katika Mto Rufiji ambao tunautegemea katika Mradi wa *Stiegler's. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi sina haja ya kuondoa shilingi ya Mheshimiwa Waziri

isipokuwa napenda tu waimarishe maeneo hayo ili mwisho wasiku tuendeee kupata huduma ya umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline. Kuna ushauri mkubwa hapa Mheshimiwa Naibu Waziri Mazingira ni kwa Mto Kilombero, lile eneo kubwa ambalo ni Ramsar *site, wetland* ya Mto Kilombero limelika kwa sehemu kubwa, tusipookoa Mto Kilombero tutapata tabu.

Kwa hiyo, tujitahidi sana na hawa watani zangu Wasukuma walioingia kule, Mheshimiwa Kalemani asiwaonee huruma, *something as be done* kule kwenye eneo chepechepe, sijui wanaita eneo oevu la Mto Kilombero. Lile li-*vono* linakunywa maji mengi sana ambayo ndiyo linaachia kidogokidogo yanaishia Mto Rufiji.

Sasa kwa wakati huu kuna watu wanahamia huko, wanaharibu kwelikweli na kwa sababu haikuwa ni *Game Reserve*, wala haikuwa ni *National Park*, wala *any protected area* yenye *status* kubwa, basi ni vuzuri hilo eneo tuliloliokoa tulipandishe *status* ili *preservation* yake au *conservation* yake iwe na uhakika zaidi maana limeshapungua *almost half.* Hivyo, tulipandishe hadhi hilo, tuwe na uhakika nalo, tulifanye liwe *secured* na hilo lingine tuangalie namna ya matumizi yake.

Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline. Mheshimiwa Ester Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda nipate maelezo ya Mheshimiwa Waziri, hasa nikiangalia unendeshaji wa mfuko wa rasilimali ya gesi na mafuta. *TPDC* ni *Parastatal organization* ambayo kwa sasa haipati ruzuku yoyote kutoka Serikalini; lakini *TPDC* ina jukumu kubwa la kulipa mkopo wa *Exim.* Amesimama pale Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akasema kwamba Serikali inalipa, lakini ukweli na uhalisia uliopo, baada ya Serikali kulipa hesabu zinakuwa *reflected*

*TPDC;* kwahiyo ni dhahiri bado *TPDC* ana mzigo huo hakuna namna anaweza kukwepa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TPDC* ana miradi mingi; ana mradi wa *CNG* ambao utagharimu takribani bilioni 16 kwa Mwaka wa Fedha ujao lakini katika huu *CNG* tayari *UDART* ameagiza magari 300 yatakayotumia hiyo *CNG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapoangalia mfuko huu wa rasilimali ya gesi na mafuta tulitarajia pia utumike kwenye masuala ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo hivi ninavyoongea *TPDC* imshawekeza, ina fungu lake, ina takribani bilioni 102 lakini hakuna namna yoyote ambayo *TPDC* imewahi kufaidika na ruzuku kutoka kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Sheria ya *Oil and Gas Revenue Management Act* 2015, Ibara ya 17(1)(c)(i) (aa) inasema wazi pale kwamba fedha zilizopo kwenye mfuko zinaweza kuhamishiwa na kwenda kwenye *consolidated fund* ili kwenda kutumika; kwa maana ya asilimia 60, kwenye masuala ya uwekezaji na asilimia 40 kwenye masuala ya ku-*train HR.* Pamoja na sheria kutoa mwanya huu wa kuweza kusaidia baadhi ya *projects* za maendeleo kwa *TPDC* lakini mpaka sasa hakuna namna yoyote *TPDC* inavyoweza kutumia mfuko huu katika kufanya miradi yake mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri katika hili, na nisipopata majibu ya kuridhisha niko tayari kushika mshahara wake ili tuweze kupata majibu ambayo yatatupelekea kupata nyumba 1,000. Umetuambia utatupatia nyumba 1000 zitakazotumia gesi. Kwahiyo ninaomba majibu yatakayojitosheleza katika hili. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Hebu irudie tena, hoja yako halisi sasa ni nini hapo?

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie; kwenye ule mfuko tunaambiwa kwamba lazima mfukoufikie asilimia tatu ya

*GDP,* kitu ambacho hakiwezekani. Ili *TPDC* iweze ku-*qualify* kutumia ile *fund* ni lazima ifikishe asilimia tatu ya *GDP* kitu ambacho hakiwezekani lakini...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana umeeleweka Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri "haiwezekani" ufafanuzi ni nini?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimia Mmasi katika swali lake la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mwaka 2015 tulifanya mabadiliko makubwa sana ya kisheria katika taasisi hii. moja ya mambo muhimu sana yaliyofanyika kwenye sheria ile kwanza ni kuliondolea Shirika la *TPDC* kufanya shughuli kama Shirika la Serikali bila kufanya biashara, kwahiyo likapewa majukumu ya kufanyakazi kibiashara. Maana yake ni nini? Kwamba rasilimali hii ya gesi, na Waheshimiwa Wabunge mlishiriki sana katika hili, imilikiwe na Watanzania wote, ni rasilimali ya Watanzania wote. Kwahiyo ikakubalika na ikawa kisheria, kwamba kuanzishwe mfuko chini ya Sheria ya fedha. Sheria ilitamka ili rasilimali ile pamoja na mambo mengine itumike sana kuendeleza uwekezaji kwenye gesi na mafuta, ndilo lengo lake kubwa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili; *TPDC* sasa hivi inafanya kazi kibisahara, ndiyo mana na yenyewe imeanza sasa kutengeneza makampuni yake tanzu ili ijiendeshe kibiashara. Kwahiyo ni matumaini yetu hili la *GDP* asilimia tatu kwasababu ndiyo imeanza siyo muda mrefu ni matumaini yetu *TPDC* itafikia kiwango hicho na itakuwa na sifa ya kupewa hizo pesa. Ni kweli kati ya fedha hizo kama nilivyosema ni asilimia 60 watapewa kulingana na kuendeleza sekta ya gesi. Ni matumaini yetu kwamba lengo la mfuko huu ni zuri, cha msingi tutalisimamia vizuri kama Serikali ili *TPDC* wanapokuwa wanahitaji kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kimitaji iweze kupata kutokana na hili fungu. Kwahiyo ni matumaini yetu, na tumejipanga vizuri an Wizara ya Fedha na Taasisi nyingine ili *TPDC* itakapokuwa inahitaji uwekezaji kupitia fungu hili iweze kusaidiwa. Kwahiyo msimamo wa *TPDC*

kutumia vyanzo vile na mapato yale uko pale pale isipokuwa iliwekwa kwenye dhamana ya Serikali ya Mfuko Mkuu badala ya kuwa na sekta moha kusimamia rasilimali hiyo kubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester umeridhika?

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakusudia kutoa hoja kwasababu majibu ya Mheshimiwa Waziri bado sijayaona yanajibu hitaji hili. Kwahiyo ninaomba kutoa hoja, Wabunge wote waniunge kwasababu tunahitaji Shirika hili liwe na tija kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ili liweze kufanyakazi kibisahara lakini pia liweze ku-*record* faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja katika hili.

**MWENYEKITI:** Lakini hoja hiyo iwe inajadili nini sasa?

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachojadili hapa tunataka tuone Wizara inachukua juhudi mahsusi katika kuona kwamba hili hitaji la Kisheria la asilimia tatu linaondoka, au la lipunguzwe kwenda kwenye asilimia moja kwasababu asilimia tatu ya *GDP* ni *unrealistic, it's is very unrealistic* kwahiyo *concern* yangu kubwa ni kwamba ninatoa hoja Wabunge wajadili na waniunge hoja yangu mkono ili Waziri aridhie kwamba hii asilimia tatu ipungue angalau iende kwenye asilimia moja.

**MWENYEKITI:** Mimi nilifikiri hoja yako ingekuwa ya maana zaidi kama ingekuwa basi itoke iwe sifuri maana yake kama ni tatu au moja maana yake ni *subjective.* Bahati mbaya hukuungwa mkono pia, kwehiyo tunaendelea. Upande huu sina jina hata moja, upande wa CUF hakuna, CHADEMA hakuna. Mheshimiwa Jesca Kishoa. *(Kicheko)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashika shilingi kwenye suala zima ambalo nahitaji maelezo kutoka Serikalini kuhusiana na

bomba la gesi ambalo linagharimu takribani Dola za Kimarekani milioni 1.2 kutoka *Exim Bank*-China. Mkopo huu una utata mkubwa sana na inavyosemekana, kwa taarifa zilizopo ni kwamba gharama halisi za bomba la gesi na gharama ambazo tunalipa kufidia deni lile...

**MWENYEKITI:** Maelezo yako yana tofauti sana na ya Mheshimiwa Jitu Soni?

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes,* nikimaliza utaelewa vizuri.

Gharama halisi ya bomba la gesi na gharama tunazolipa haviendani. Kuna taarifa kwamba tunalipa zaidi (ziada) ya Dola za Kimarekani milioni 400. Kwasababu hiyo nilikuwa naitaka Serikali ikubali kuunda Tume ya kufanya uchunguzi kwenda kuchunguza gharama halisi ya bomba la gesi na mkopo tuliokopa kutoka China.

**MWENYEKITI:** Sidhani kama umeeleweka, hebu rudia tena kidogo. Yaani Serikali iunde Tume ili kuchunguza hilo kuna haja hiyo kweli? Hebu rudia tena.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya uchunguzi iundwe ya Bunge na lengo kubwa...

**MWENYEKITI:** Nilifikiri umesema Serikali iunde Tume ndiyo maana nikawa napata tabu.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** ...na lengo kubwa ni kutaka kuangalia gharama halisi ya bomba la gesi na wathaminishe na mkopo tuliokopa kutoka *Exim Bank,* bila hivyo nitatoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa hoja yako atakuwa anaulizwa nani sasa hapa? Maana sijui kama Waziri ni *authority* ya kusema Bunge liunde kitu fulani au lisiunde, sina uhakika, au, Waheshimiwa Wabunge hili letu wote. Ni kama pendekezo lako kwa Bunge si ndiyo? Haya ufafanuzi Mheshimiwa Waziri

kuna haja ya kuunda Tume kama hiyo? Yaani kuna haja ya Bunge kuunda chombo cha namna hiyo? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mimi kwanza sijamuelewa vizuri lakini sioni sababu, lakini kwanini? Labda kama ana uhakika kuna gharama fulani ambayo iko nje ya pazia ambayo hatuijui aiseme yeye maana gharama ya uwekezaji ya mradi huu inajulikana ni bilioni 1.225 Dola za Marekani, sasa kama anasema ichunguzwe gharama basi labda ana gharama nyuma ya pazia aseme yeye kama kuna gharama nyingine lakini *otherwise* hatuoni sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Linarudi kwako Jesca. *Issue* hapa Waheshimiwa Wabunge anayo-*raise* labda kama hatujamwelewa, inaelekea ana wasiwasi na gharama iliyotumika kulijenga hilo boimba enzi hizo mana yake limeshakamilika *on one side* na mkopo uliochukuliwa kwa ajili ya gharama hiyo wakati huo kitu kama hicho*, please* tumerudi kwako.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nirudie kwa ufupi kidogo; kuna utata kwenye gharama halisi zilizotumika kujenga bomba la gesi na gharama ambazo tumekuwa tunalipia ujenzi wa bomba hilo kama mkopo. Sasa nilichokuwa nataka ni kwamba iundwe tume ya kuchunguza gharama halisi za ujenzi wa bomba la gesi ni kiasi gani? kwasababu inavyoonekana bomba la gesi thamani yake na mkopo tunaolipa haviendani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi nimekuona umesimama na Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa nia ya Mheshimiwa Mbunge, lakini tunatawaliwa na Kanuni ya 101, na Kanuni ya 101 tukishafika hapo ni Kanuni ambayo inaelekeza mjadala katika Kamati

ya matumizi na katika Kamati ya matumizi tuseme masharti ya majadiliano katika Kamati ya matumizi yameelezwa na yanatakiwa kulenga katika masuala yale ya jumla ya Kisera. Sasa jambo mahususi la namna hii ukiangalia kwenye nyongeza ya Kanuni zetu, ziko Kamati ambazo zinashughulikia masuala ya kiuchunguzi ikiwemo Kamati ya PAC.

Kwa hiyo mimi hoja hii inapoletwa sana sana ni hoja inayokuja kwenye Kiti cha Spika kwasababu wewe ndiwe mwenye mamlaka ya kuagiza Kamati zote zilizoundwa ndani ya Bunge kushughulikia jambo lolote ambalo unaona ni jambo mahususi. Lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 101 ya shughuli za Kamati sasa tulizonazo sasa hivi Kamati ya Bunge zima masuala ya Kisera hoja hii itatupa shida sana ya kuijadili na kuifanyia uamuzi kwa mujibu wa Kanuni hiyo ya 101.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Jesca kwa vile hoja yako ni ya kulitaka Bunge liunde tume nakushauri turudi tu kwenye Kanuni ziko taratibu za kuleta hoja mahususi kwa ajili ya kulitaka Bunge linde tume kwa jambo lolote mahususi. Kwahiyo rudi kwenye zile taratibu zetu zile, zipitie halafu ujenge hoja kwa wakati mwingine uilete tutaipima kwa wakati huo. Hatuundi tume katika utaratibu huo ambao umekuja nao kwa sasa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka halafu Mheshimiwa Heche ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi nahitaji ufafanuzi kwasababu sera ya taifa hasa katika Wizara hii ya Nishati ni kupeleka umeme kwa wananchi wetu wote ifikapo 2021; na suala hili limepewa hii mamlaka ya *REA* (umeme vijijini); lakini mpaka leo hii kwa mujibu wa takwimu ambazo hata Mheshimiwa Waziri alitusomea hapa kwamba Vijiji vingi badi havijafikiwa na umeme na muda ambao ulikuwa umeelekezwa Kisera tumeshakwenda zaidi ya nusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nahitaji kupata ufafanuzi, kwamba ni kwa namna gani tunaweza tukalifikia hili lengo la kupeleka vijijini iwapo kwa *speed* hii ya kusuasua ambayo, *speed* yenyewe kwanza inaonekana kabisa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wana-*speed* kubwa zaidi kuliko ya wakandarasi. Sasa nataka nipate ufafanuzi nione kwa namna gani tunaweza kuifikia sera hii. Nisipopata majibu ya uhakika nakusudia kutoa shilingi ili Wabunge wenzangu tuweze kulijadili suala hili muhimu sana kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka kwa kweli ni ukweli usiopingika Waziri na Naibu mna-*speed* nzuri, kubwa lakini wakandarasi, kama alivyosema Mheshimiwa Kuchauka mkitoka nyuma Wakandarasi wenu wako likizo. Mheshimiwa Naibu Waziri ufafanuzi tafadhali, wakandarasi wataendaje na *speed* yenu ninyi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya lkuchangia hapa. Mheshimiwa Kuchauka ameelezea namna ambavyo tunaweza tukafikia lengo letu la kuunganisha vijiji 12,268 ifikapo 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumeeleza katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na pia tulipokuwa tunachangia hoja, kwa sasa ni ukweli kwamba wakandarasi zaidi ya loti 29 wameanza kazi katika maeneo mbalimbali. Hata hivyo ukiangalia muda ambao tunalinganisha leo vijiji, tunapozungumza mwezi wa tano tuna vijiji takribani 7,127 lakini kazi zinaendelea na matarajio ya Wizara kwa kuwa kwa sasa hivi vifaa vingi vinavyotumia kwenye miradi hii vinapatikana na viwanda vya ndani vina uwezo, tunatarajia Mwezi Juni, 2020 tutakuwa na vijiji takribani 10,128. Kwahiyo vijiji vitakavyosalia kama 1900 hivi vitafanyiwakazi, na tuna uhakika 2020/2021 vijiji vyote vitafikiwa na umeme, kazi itakayobaki ni kuendelea kusambaza kwenye maeneo ya Vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo kwa kuwa amesema, ni kweli kuna baadhi ya Wakandarasi hawafanyi vizuri na tumewaanisha akiwemo Mkandarasi wa Mkoa wa Lindi; tumeshawapa maelekezo na tumeunda timu maalum za kuongeza usimamamizi. Kwahiyo, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri niwathibitishie Wabunge wote kwa kweli kwa namna ya mikakati ambayo tumeweka ndani ya Wizara, ndani ya *REA* na ndani ya *TANESCO* ya kuimarisha usimamizi mradi huu utakamilika na lengo litafikiwa.

Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka umeridhika?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaendani na uhalisia kwasababu ukizungumza na Wakandarasi na haya majibu yanatotolewa ni tofauti sana; na sasa hivi tuko kwenye *REA* Awamu tatu, sehemu ya pili na mjue kwamba muda wenyewe nao umebaki mchache. Mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge naomba kutoa hoja mnisaidie kuunga mkono ili tuweze kujadili sual hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Tutapata baadhi tu maana naona Bunge zima limesimama, tuanze na Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kuchauka. Ni kweli kabisa kasi ya usambazaji umeme vijijini haipendezi kabisa, na mimi kwangu Waziri amefika, Naibu Waziri amefika lakini bado wakandarasi wale ambao wamewaweka; kwenye maeneo yetu wakandarasi

watatu; ambao wametengeneza *joint venture* wanashindwa kupelaka umeme katika vijiji viwili ambavyo viko ndani ya umbali ambao hauzidi hata kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo tungependa kabisa Serikali iweke msisitizo, hili jambo liko kwenye Ilani ya Chama na imeeleza wazi kabisa kwamba mwisho wa usambazaji umeme vijijini ni Mwaka 2020/2021. Sasa tungependa kuona msukumo wa dhati kabisa wa kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapatiwa umeme katika maeneo yetu. Ninavyozungumza mimi hapa bado kata nne hazijapatiwa umeme kabisa katika Jimbo la Mlalo. Kwahiyo naunga mkono kabisa hoja ya Mheshimiwa Kuchauka, tunaomba kasi iongezwe katika usambazaji wa umeme vijijini.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na hoja ya ndugu Kuchauka. Hapa Lazima kuna kitu ambacho hatukijui, *speed* ya *REA III* ni ndogo kupita kiasi, Mheshimiwa Waziri amekuja Kigoma mara tatu, ametoa maagizo mazito na sisi tukafurahi, lakini *as we speak, nothing is happening*. Nadhani kuna tatizo mahali kwa nini *speed* ya *REA III* imekuwa ndogo sana kupita kiasi. Wakandarasi wapo lakini hawafanyi kazi lazima kuna kitu ambacho pengine Serikali watueleze ambacho kiko *behind the scene*, lakini hata hivyo nadhani haijitoshelezi kumnyang'anya pesa yake...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri umesikia Tanga wanavyosema, umesikia Kigoma, hebu twende Kagera Mheshimiwa Lwakatare mambo mazuri huko Kagera.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni magumu. Naungana na hoja ya Mheshimiwa Kuchauka kwa misingi ya kwamba liko tatizo la msingi na huenda haliko wazi sana kutufanya sisi kama Bunge kufahamu nini kinachoendelea na ndio maana wakati mwingine tukataka ili kukata mzizi wa fitina hao wakandarasi wakaonana na Kamati ya Bunge kwa niaba ya Bunge tujue

kulikoni. Maana yake ukienda kwa wakandarasi wanasema tatizo ni Serikali, Serikali inasema tatizo ni wakandarasi, kuna fumbo la imani. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Twende Kilimanjaro kule Rombo, nyie mlipata umeme tangu zamani hamhitaji. *(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sipendi tumlaumu sana Mheshimiwa Waziri Kalemani pamoja na Naibu wake na sipendi nimlaumu kwa sababu jana tulizungumza hapa kuhusu fedha ambazo zimekuwa *ring-fenced* kutumika kinyume na mpango ambao Bunge limeelekeza. Sasa hii shida kila ambaye anaifuatilia wakandarasi hawana fedha, sasa kuna wakandarasi ambao wanafanya kazi hovyo, hao Serikali iwadhibiti lakini Serikali yenyewe pia ijiangalie kwa nini zile fedha za *REA* tulizo *ring-fence* zinatumika kwa matumizi mengine. Sasa hili sio suala la Mheshimiwa Waziri Kalemani ni suala la Serikali nzima. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hongoli, kule Njombe.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kuchauka. Mfano kwangu kuna vijiji 22 havina umeme na mkandarasi alishaanza kazi tangu mwaka jana, lakini mpaka leo hii ni vijiji viwili tu vimepelekewa umeme navyo ni kitongoji kimoja kimoja. Kwa hiyo ni shida ni kwamba Wizara wanafanya kazi vizuri sana lakini wakandarasi sijui kuna shida gani na maagizo wamekuwa wakipewa lakini hawatekelezi. Sasa naomba tujaribu kuangalia kuna shida gani kama wanavyosema wenzangu kwenye hao wakandarasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Basi nafikiri tumeshaona *sample* ya nchi nzima, Mheshimiwa Kuchauka rudisha shilingi bwana sijui Liwale ni vijiji vingapi mpaka sasa hivi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante...

**MWENYEKITI:** Hapana, ngoja Mheshimiwa Waziri kwanza aseme kidogo nilisahau.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *concern* ya Mheshimiwa Kuchauka ni *concern* ya kila Mbunge na ni *concern* ya kila Mtanzania. Kila Mtanzania na Waheshimiwa Wabunge anataka umeme leo leo na wala sio kesho, hiyo ni shauku ya kwanza kwa kila Mtanzania. La pili, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tunapeleka umeme kwenye nchi nzima, vijiji vyote lakini kimoja baada ya kingine, nataka kwanza nipongeze Serikali na Bunge hili kwa kutenga hizi fedha, nimetoa takwimu pale kwamba sisi ni wangapi Afrika kupeleka umeme vijijini. Inawezekana tunajilinganisha kidogo, lakini kuna hoja ya msingi hapa kuna ukweli baadhi ya wakandarasi hawafanyi kazi vizuri, lakini kuna ukweli baadhi ya wakandarasi walianza kazi wamechelewa kwa sababu za msingi hasa Kigoma na Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mwananchi wa Katavi na mwananchi wa Kigoma hawezi kutarajia kuunganishiwa umeme leo kwa sababu mkandarasi ana miezi miwili tu ameanza kazi. Kwa hiyo, hiyo ni hoja ya msingi hapa Waheshimiwa Wabunge niahidi na Mheshimiwa Naibu Waziri wangu sisi ni wapole sana, lakini katika suala la *REA* ni wakali kweli kweli, tutaendelea kuzidisha ukali katika hili. Nashukuru na tunalipokea Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, yako maeneo wakandarasi wameshavuka asilimia 80 na nitoe taarifa kupitia Bunge lako Tukufu, wakandarasi tumewapa muda wa miezi 24 ya kutekeleza kazi, swali sasa hivi wana miezi mingapi, sasa hivi ana miezi tisa waliotangulia kati ya miezi 24. Kwa hiyo bado tuna miezi 15 wengi wetu na wachache wana miezi 20, hivyo wananchi wavute subira vijiji vyote vitapelekewa umeme. Mpango huu uko pale pale kimoja baada ya kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya pili muhimu sana, hapa ninapoongea tunazo wilaya na halmashauri 15 nchini ambazo vijiji vyake vyote tumeshavipelekea umeme, kazi

iliyobaki ni vitongoji tu ila na halmashauri hizo ni pamoja na Mafia, ni pamoja na Rufiji nimebakiza Ngarambe, lakini nimebakiza maeneo machache sana...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Kuchauka umesikia maneno ya Mheshimiwa Waziri tafadhali.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote walioniunga mkono na waliochangia. Kwa kweli hili tatizo ni kubwa sana, kama nilivyotangulia kusema kwamba *speed* ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kama ndio ingekuwa sambamba na *speed* za wakandarasi, hali hii isingekuwa hivi ilivyo sasa hivi. Kwa mfano mzuri tu mimi kwenye halmashauri yangu nina Kata 20 nina Kata nne tu ambazo zina umeme *full*, kata sita zina umeme kijiji kimoja kimoja, kata nyingine zote zilizobaki zote hazina umeme kabisa, kwa hiyo kwa kuzingatia *speed* ya Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri nawarudishia shilingi ila kwa maombi maalum kwamba mwongeze *speed* ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka ufafanuzi ni kwa nini miradi mingine mingi kwa mfano Ruhuji, Rumakali yenye megawati 220, Ziwa Ngozi kule *geothermal* zaidi ya megawati 5,000, Mtwara megawati 3,00, imekuwa *abandon* na nguvu nyingi kwa sababu ukiangalia *geothermal* kwa watu ambao tuko *serious* huwezi kupeleka pale bilioni 36 peke yake na ule ndio umeme wa uhakika kuliko maji ambao tunasifu hapa wakati maji hatuna uhakika nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunachukua zaidi ya trilioni nane tunakwenda kuwekeza kwenye mradi mmoja na hatusemi ukweli hapa kwamba hilo bwawa litachukua miaka mingapi kufikia *optimum production* ya megawati hizo 2,115. Kwa mfano Akasombo Dam ilichukua miaka 12 kufikia *optimum production*, Aswan High Dam ilichukua miaka nane,

sasa hawatuambii hapa tutaanza na megawati ngapi, watu wanaimbishwa humu kana kwamba kesho bwawa likikamilika megawati 2,100 zimekamilika. Sasa nataka ufafanuzi Mheshimiwa Waziri kwa nini wana-*abandon* hii miradi na kuchukua pesa hizi za Watanzania zote kuziwekeza kwenye mradi mmoja na hawasemi tutachukua miaka mingapi kufikia *optimum production*.

**MWENYEKITI:** *Issue* yako ni *geothermal* si ndio.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *energy mix,* sera yetu tunazungumza kuhusu *energy mix*, tumezungumza hapa maji, mengine Rumakalli na Ruhuji ni maji, tumezungumza gesi, nimezungumza *geothermal,* lakini kwa nini Serikali ichukue pesa zote inaingiza kwenye mradi mmoja na kupunguza kasi kubwa sana ya miradi kingine ambayo tunajua muda wa ku...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tumeshakuelewa

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Na bahati nzuri ulisema hutakamata shilingi kwa hiyo...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Nimesema nakamata shilingi kama ufafanuzi haujanitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri tuendelee. Ahsante lilishakupita bwana. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ningependa nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na hoja za Mheshimiwa Heche. Kwanza nipende kufanya masahihisho kidogo huu mradi haugharimu trilioni 8.8 ni trilioni 6.5, sio trilioni 8.0, hayo ni masahihisho ya kwanza. La pili hatuja-*abandon* Rumakali wala Ruhuji, tumeeleza kwenye mpango wetu humu na muda wa utekelezaji na hii Rumakali na Ruhuji tunaanza kuitekeleza

kuanzia mwaka ujao. Pesa tumetenga na pesa za kuanzia zimo kwenye taarifa yetu, lakini tunakwenda na miradi pia ya Jotoardhi, tuna mpango wa kuanza nitoe taarifa tu kukamilisha kupata megawati 100 za jotoardhi sio kazi ya mchezo, unahitaji uwekeze sana kwenye *drilling,* tunaanza na megawati 30, Wakenya wameanza miaka mingi lakini bado wana megawati 200 za jotoardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwanza hatuja-*abandon* tunakwenda sambamba na miradi yote na nimeitaja na tunaanza kuitekeleza na mingine iko kwenye utekelezaji. Ni matumaini yetu utekelezaji wa miradi hii kipaumbele tulichokitoa sisi tunaamini kiko sawa, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuunga mkono tutekeleze miradi yote hii kwa sababu hatuja-*abandon* hata mmoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri...

**MWENYEKITI:** Hakuna *abandonment.*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano amezungumza Jiothemo tangu mwaka 1984 hata Sheria ya *Geothermal* haijaletwa Bungeni kutungwa, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri anajua hili na anajua ninachokizungumza. Leo Wakenya wanatumia megawati 800 ya *geothermal* anayozungumza na ni rafiki yangu anajua ninachokisema ni kweli kwa ajili ya nchi hii, 60% ya umeme na umeme wa *geothermal* ukishapatikana ndio moja kwa moja tutatumia milele.

Sasa naomba nitoe hoja Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono tujadili kwa nini Serikali inapeleka pesa kwenye mradi mmoja na ku-*abandon* miradi mingi ambayo tulikuwa nayo kwa ajili ya *energy mix* ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Jamani wengine mbona mmekaa chini, haiwezekani bwana wawe hawana hoja. Nitajieni Katibu. Mko wengi kweli, sasa nawapa dakika mbili mbili tu, tuanze na Mheshimiwa Bobali, atafuata Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Heche kwa sababu moja ya kuwa na *energy mix* na fedha ambazo zinapelekwa kwenye mradi wa *Stiegler's Gorge* si vibaya, lakini pia kungekuwa na uwekezaji kwenye miradi mingine kama vile gesi ambayo tayari tulishawekeza fedha nyingi na miradi ya *geothermal* na maji na ni Sera ya Taifa kwamba kuwa na mpango wa *energy mix* kulingana na upatikanaji katika maeneo, lakini pia hizi *source* za *energy* ni muhimu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi naunga mkono.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. TEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 73 ameeleza kwamba ametenga shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuchoronga visima vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunarudi kwa alichokisema Mheshimiwa Heche, tunachokihitaji hatuwezi ku-*relay* kwenye *source* moja ya umeme, tumeona katika historia ya nchi hii umeme wa maji umetuangusha, ni lazima tuwaze *alternative source of energy.* Kuna mtu amesimama hapa ameongelea upepo, hivi upepo si upo *automatic* na utaendelea kuwepo kwa nini hatuwekezi huko, jotoardhi tu sio eneo moja tu wale wenyewe wataalam wa jotoardhi wanakwambia maeneo mengi, Kagera, wapi kuna viashiria vya uwepo wa jotoardhi, ina maana ni vitu viko tayari ni kazi za *annex* na kupata umeme baada ya kuhangaika na miradi mingine mikubwa hatujui hata kama tutaweza kuiweka kwenye.... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Saleh.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Leo hapa Mheshimiwa Simbachawene asubuhi alizungumza habari ya *energy mix* na ndio kinachosemwa kwamba tuwekeze katika *energy mix,* hali tunayokwenda nayo hivi sasa, tunaweza tukakwama tukawa hatuna pa kwenda, kuna *option* za *solar*, kuna *option* nyingine, leo Mheshimiwa Waziri taarifa pengine Waheshimiwa Wabunge walikuwa hawajui, anakuja kutuambia Bungeni kuwa matumizi ya gesi yamefikia aslimia 16, mimi ndio kwanza nimejua leo. Wakati tungekuwa tunajua kwamba hii gesi inatumika kiasi hicho au ingekwenda zaidi kiasi hicho tungeona inaji-*mix* na kuwepo, kwa mfano kwa nini Taasisi za Serikali hazitumii gesi, kuna nyingi tu tungeweza kwenda. Kwa hivyo alichosema Mheshimiwa Heche ni kwamba tusiwekeze mayai yetu yote katika mkoba mmoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameelezea vizuri sana na nimeelewa kwamba hiyo ni *economical issue* kwamba tumeenda na *priority,* lakini pia tusingeweza kuchukua vyanzo vyote tukaviwekea hela kwa sababu tungezima shughuli zingine zote za maendeleo. Si hilo tu tumeangalia kigezo kimoja kwamba sio tu hii tunayowekeza ambayo Mheshimiwa Waziri amesema, tunaendelea pia na *extension* ambayo hata Waheshimiwa Wabunge wamekuja kuliongelea.

Mhshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, wenzetu wanawaza kama vile hiki ndio kizazi cha mwisho yaani kama vile ndio tunaishi kizazi cha mwisho, kuna vizazi vingine vitafuata...*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kama vile hii ndio bajeti ya mwisho.

**MHE. MWIGULU L. NCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo, kuna vizazi vingine vinakuja na hii sio bajeti ya mwisho, tutamaliza hiki, tutaenda *source* zingine , lakini pia vizazi vingine vitakuta *source* zingine vije viendeleze, si kwamba gesi walikuwa hawaijui, si kwamba upepo walikuwa hawaujui,

hauondoki ni *resource* zetu za Tanzania na bajeti inaporuhusu tutakuja kuendelea kufafanua vinavyoendelea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika dakika mbili na Mheshimiwa Maige jiandae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Serikali haijajibu kabisa hoja ya Mheshimiwa Heche kwamba tunaanza kupata umeme wa *Stiegler's* lini na kwa kiasi gani na bwawa litafikia *optimum production* lini, sasa kwa sababu Serikali...

**MWENYEKITI:** *Issue* yake ni *energy mix*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali haijajibu u- *justify* kwamba tusiwe na *energy mix* , basi naomba kwa Mamlaka yako kwa sababu Serikali imeshindwa kufuata policy hiyo ya *energy mix* kuwekeza kwenye upepo, jua na jotoardhi, hela ambazo tumewekeza kwenye hiyo miradi mingine ni ndogo sana ukilinganisha na *Stiegler's* kwa sababu Serikali haijafanya hayo kwa mamlaka yako yako tutumie hii Sheria yetu ya *Natural Wealth and Sovereignty (Permanent Resource) Act,* Kifungu cha 12 tuletewe huo mkataba wa *Stiegler's* hapa Bungeni ili tuufumue na hatimaye tufanye uamuzi wa kulinda *energy mix,* pesa tuelekeze kwenye vyanzo vingine vilivyosambaa kwenye maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maige tafadhali dakika mbili.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono mawazo ya Mheshimiwa Heche, anaongelea kitu kimoja, vilevile anaongelea mambo ya *geothermal* ambao pia sidhani kama anaelewa vizuri, nayo pia ni maji kutoka chini, nataka tuunge mkono Serikali, Serikali katika kipaumbele chake imeweka miradi mingi ambayo inashughulikia sio mradi mmoja, lakini kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Serukamba wa mwisho.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Serikali na nadhani kwa sababu wenzangu hatujasoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri. Ukisoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri *page* ya 33 wanasema gesi asilia Kinyerezi megawati 240, *extension* megawati 185, kuna Mtwara megawati 300, zote hizi kuna upepo megawati 200 na megawati 600 makaa ya mawe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utararibu)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Tunaongelea *energy mix* maana yake ni kwamba tutumie vyanzo vyote, hapa tofauti yetu ya wenzetu hawaelewi kwamba huu mradi mmoja wa maji una megawati 2,000 kwa hiyo lazima pesa zake ziwe nyingi, huku kwingine tunaongelea megawati 300, megawati 600, hapa ni suala la namba tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Inaelekea hapa Bungeni, hesabu ni tatizo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema hata huo Mradi wa *Geothermal* Serikali inaweka fedha kidogo hizo fedha ndio zinaanza. Kwa kweli suala la *geothermal* nenda Kenya, suala la uchunguzi linatumia muda mrefu sana lazima uwe na fedha nyingi sana, lakini pia ili ufanikiwe huwezi kusema naacha nafanya uchunguzi niache ambako kuna umeme tayari kwa maana ya gesi, haya makaa ya mawe na maji. Kwa hiyo, nadhani kwa maana ya *energy mix,* Serikali inafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Heche naomba amwachie shilingi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Waziri sasa, Naibu Waziri ili tumrudishie Mheshimiwa Heche.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nataka kuongezea kwa upande wa Serikali kwamba hii *energy mix* pia inategemea gharama za uwekezaji, kwa mfano kwenye chanzo cha *geothermal* unatumia Sh.10,029 kwa megawati moja na maporomoko ya maji unatumia Sh.6,063 kwa megawati moja kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema vizuri Mheshimiwa Serukamba, tunachotazama hapa nadhani ndani ya Bunge pia kuna Wachumi, tunaangalia *economies of scale,* kutumia *input* kwa ajili ya kuzalisha *output* zaidi, miradi mingine inayotajwa ni midogo midogo, sisi tulitaka tufikie lengo la megawati 10,000 ifikapo 2025. Kwa hiyo huwezi ukasema hii *energy mix* ukaacha kutumia chanzo kikubwa hiki cha Rufiji *Hydro Power* kwa megawati 2,115 ukasema kwamba *energy mix* yako ukaipeleka kwenye upepo, maji na kadhalika. Hata hivyo, nataka kusema Serikali inatambua umuhimu wa vyanzo vingine na ndio maana hotuba yetu imejielekeza kwenye vyanzo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nimwombe Mheshimiwa Heche, mjumbe wetu wa Kamati aturudishie shilingi ili tuendelee kufanya kazi na kwa kuwa, yeye ni Mjumbe wa Kamati tutaenda kwenye Kamati watatushauri tutaendelea kujielekeza kwenye miradi mingine. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Heche mrudishie shilingi bwana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wakati mwingine huwa nasikitika sana. *Group* la *elite* linatumia nafasi waliyopata kupotosha nchi, kupotosha watu bila sababu ya msingi kwa sababu, ngoja niseme kidogo; Mtera leo tunavyozungumza *production* pale ni *below 40 percent.* Umeme wa maji *siltation* ikianza tayari bwawa

linaanza kushindwa ku-*produce* umeme kwa kiwango kile kilichotakiwa. Sasa sijui kwa nini tunapotosha watu hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana Waziri kwa makusudi hajasema tunapoanza, bwawa litakapokamilika tunaanza na megawati ngapi na tutafikia lini megawati 2,115. Wanafanya makusudi kwa sababu wengine humu wanaamini siku bwawa likianza tu megawati 2,115 zinaanza siku hiyo.

**MWENYEKITI:** Haikuwa hoja yako, tungejadili hiyo...

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja ngoja!

**MWNEYEKITI:...** hoja yako ilikuwa *energy mix. (Kicheko)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najibu hoja za watu hapa. *Geothermo* mathalani tumeanza na Wakenya tangu mwaka 1964, anajua rafiki yangu Mheshimiwa Serukamba, wao kufikia mwaka 75 wameshatunga sheria leo wana *megawatt* 800. Sisi hata sharia, nimesema hapa na Waziri hajajibu kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri tusitumie Bunge hili kupotosha watu. Hoja yetu ni kwamba ukichukua hii miradi yote Rumakali, Ruhuji, ukachukua *geothermo* ukichanganya upepo Singida; na nikukumbushe tu ulituteuwa kwenda Marekani sisi na *initiative* ya *Power Africa* tulikuwepo; *the whole world* ina-*shift* kwenda kwenye *renewables. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gujarat juzi India umeme gigawati 5, *megawatt* 5,000 kwa trilioni nane tu za Kitanzania, wa *solar.* Mimi ninachozungumza ninakijua vizuri sana. Kwa hiyo mimi nafikiri twende kwenye kura wale wanaosema tuchukue hela zote...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, wewe Mjumbe wa Kamati bwana, hizi hoja si uzipeleke kwenye Kamati, kuliko kamati hii ya kwangu mimi?

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema tuamue kwa kura, najua watashinda. Wale wanaosema hela zote ziende huko na wale tunaosema pesa hizi zingegawanywa kwenye vyanzo mbalimbali zituletee umeme... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** ...tupige kura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nitawaji wanaoafikiana na Mheshimiwa Heche.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja yako imeshindwa Mheshimiwa Heche. Sasa kwa sababu ya muda, wakati wa mjadala ple lilijitokeza jambo ambalo ni vizuri kama Kamati ya Bunge tungejaribu kulisikiliza pia. Mheshimiwa Naibu Waziri alisimama kwa jambo maalum, wakati huo Mheshimiwa John Mnyika hakuwepo, lakini sasa yupo.

Mheshimiwa Mnyika unadaiwa kulidanganya Bunge, sasa hukuwepo, ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri afafanue kidogo baada ya hapo basi wewe na kambi yako mtufafanulie maana ni *serious allegation.* Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali na kanuni ututajie.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 64, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(a), ambayo inahusiana na kutoa Taarifa za Uwongo Bungeni, lakini pia nitatumia Kanuni ya 63(1)(a) mpaka (5) kuthibitisha kwamba, baadhi ya taarifa zilizotolewa kwenye Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni zilikuwa

na nia ya kupotosha; na ninaomba nithibitishe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Kambvi Rasmi ya Upinzani Bungeni ukurasa wa nne, ikiwa mapitio ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati, katika ukurasa huo wa nne kumekuwa na taarifa imetolewa kwamba, kati ya shilingi bilioni moja na milioni 692 zilizoidhinishwa na Bunge mpaka Disemba, 2018 zilitolewa bilioni 275 na kwamba, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inashindwa, kutoa fedha ya maendeleo, utoaji hauridhishi kutokana na sera zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alikuwa na nia ya kulipotosha Bunge kwa sababu ametumia takwimu za Disemba ilhali anajua fika kwamba, kwa sasahivi tupo Mei. Taarifa yake hii ilivyoingia kwenye *Hansard* itakuwa na nia ya kulipotosha Bunge wakati mpaka sasahivi zimeshapokelewa kiasi cha asilimia 87 ya pesa zilizotengwa katika bajeti ya mwaka 2018/2019, na ushahidi ni taarifa yetu ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri na ushahidi mwingine ambao ninawasilisha Mezani kwako ni Hotuba ya Kamati yetu ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili pia, katika Taarifa ya Kamati ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ukurasa wa tano alieleza hasara za Shirika la *TANESCO.* Ninaomba nimnukuu; kwamba hasara zimekuwa zikiongezeka mfululizo kuanzia mwaka 2015/2016 mpaka 2017/2018 ambapo hasara zilifikia kiasi cha bilioni 346.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo taarifa hapa ya *TANESCO* ambayo imekuwa *audited* ikionesha hasara zilivyokuwa zinapungua. Kwa mwaka 2015/2016 *TANESCO* ilipata hasara ya bilioni 349.55, kwa mwaka 2016/2017 *TANESCO* ilipata hasara bilioni 265.297, kwa mwaka 2017/2018 *TANESCO* imepata hasara ya bilioni 112.56. Naomba niwasilishe Mezani Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ni kwamba, ni upotoshaji katika ukurasa

wa 6 kwamba, kuonesha tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani hasara kwa Shirika la *TANESCO* zimekuwa zikiongezeka ilhali kiuhalisia zimekuwa zikipungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukurasa wa 25 wa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alikuwa, namnukuu, kwamba ni ukweli kuwa *REA* kuonesha kwamba, Serikali haiiwezeshi *REA* na kwamba, pesa zake ambazo zimekuwa *ring fenced* zilikuwa hazitolewi kama ilivyokusudiwa na katika *comparison* aliyofanya Mheshimiwa Mnyika inaonesha kabisa alikuwa na nia hasi kwa sababu alikuwa anatumia vipindi ambavyo tofauti na Mwaka wa Fedha wa Serikali ambao unajulikana ni kuanzia tarehe moja Mwezi wa Saba wa mwaka husika mpaka tarehe 30 Mwezi wa Sita wa mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo ninayo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2015/2016 ambayo inaonesha kiasi gani kilichopokelewa na Wakala wa Nishati Vijijini. Ninayo Taarifa ya mwaka 2016/2017, kiasi ambacho kimepokelewa na Wakala wa Nishati Vijijini na ninayo Taarifa iliyoishia Juni, 2018 kiasi ambacho kimepokelewa na Wakala wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niwasilishe katika Meza yako; na kwa mwaka tu niusome wa 2017/2018 kiasi cha asilimia 80 ya fedha zilizotengwa zimepokelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Mnyika naomba nimkumbushe kiwango kinachotengwa kwenye mapato ya Wakala wa Nishati Vijijini kinategemea makusanyo ya tozo ya mafuta, namna mafuta yanavyoingia ndani ya nchi. Kwamba inategemea ukikusanya sehemu utawasilisha hiyohiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho katika kitabu chake ameainisha na kulipotosha Bunge, kwamba pesa za *REA* zinakwenda *TANESCO* kufanya miradi ya nishati vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tunao ushahidi kwamba pesa zote zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya nishati vijijini *REA* inawapa wakandarasi na *TANESCO* haijapata kufanya kazi za *REA.* Kwa hiyo hii maeneo haya manne ni tuhuma nzito ambazo zilikuwa na nia ya kulipotosha Bunge lako Tukufu, lakini hii inasoma kwenye *Hansard,* naomba utumie Kiti chako kuondoa haya maeneo haya, asante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mnyika hoja nzito hizi, kwamba ulikuwa na nia hasi katika maeneo hayo maane kwenye hotuba yako. Nakupa muda, muda wetu ni mdogo lakini jitahidi basi kuutumia vizuri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umempa muda wa kutosha sana Mheshimiwa Naibu Waziri naomba na mimi unipe muda wa kutosha tu wa kujibu hizo hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba hakuna taarifa yoyote iliyotolea kwa nia hasi, taarifa zote zimetolewa kwa nia njema na kwa maslahi ya umma na ni taarifa za ukweli. Zinaweza zikawa zinatofautiana vipindi, lakini ni taarifa za ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya madeni ya *TANESCO* na hali mbaya ya shirika la umeme la *TANESCO* katika Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayokwenda mpaka Machi, 2018 imeeleza kwa miaka kadhaa *TANESCO* imekuwa na mwenendo usioridhisha wa kupata hasara mfululizo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, hasara iliyopatikana ilikuwa shilingi bilioni 346.4, na kwa hesabu za miezi 18 hadi Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2015 hasara ilikuwa shilingi bilioni 124.46. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali mbaya na isiyoridhisha ya maji ya kuzalisha umeme kwa nguvu za umeme na ongezeko la gharama za uzalishaji. Pia hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2016 madai yameongezeka kwa asilimia 23 hadi shilingi bilioni 958 kutoka shilingi bilioni 738 zilizoripotiwa awali. *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** ... tumsikilize kwa sababu ni *figures.* Kwa sababu ni *figures* tumsikilize vizuri zaidi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii inaendelea kwa hiyo ...

*(Hapa, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, na taarifa hii inaendelea, hii ni *Report* ya *CAG* ya Machi, 2018 na tumeinukuu kwenye taarifa yetu. Kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri aseme hii *Report* ya *CAG* ni ya uwongo? Kwa hiyo, aseme hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile ninayo taarifa hapa. Taarifa ya Utendaji wa Shrika kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma, taarifa ambayo iliwasilishwa mbele ya kamati miezi kadhaa baada ya Taarifa ya *CAG.* Hii ni taarifa ya mwezi Oktoba, mwaka 2018 ambayo nayo inaeleza kuhusiana na namna ambavyo bado kuna madeni *TANESCO,* bado kuna madai *TANESCO,* n.k., na inaambatanishwa kwenye hii taarifa mwenendo wa mapato na matumizi ya *TANESCO* na kunawekwa *Financial Statement* hapa kwa makadirio inayoonesha kiwango ambacho tumekinukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali haikubaliani na hii taarifa, kama ambavyo iliwasilishwa mbele ya Kamati, ilikuwa ni wajibu wa Serikali kuja kutoa hapa taarifa Bungeni ambayo yenyewe inaiona ni ya kweli. Sisi kwa sababu tume-*relay* kwenye Taarifa ya Serikali hatuwezi kuitwa waongo kwa kunukuu Taarifa za Serikali yenyewe na Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya kwamba, tulisema mwezi Disemba, pesa zilizopelekwa ni shilingi bilioni 275. Waziri hajakataa kwamba mwezi Disemba tulisema taarifa ambayo ni ya uwongo, alichokisema Waziri ni kutoa *update report* ya mwezi Juni. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri

atuambie, mpaka mwezi Disemba tulipotoa taarifa yetu kiwango cha pesa kilichokuwa kimepelekwa je, kinazidi kile tulichokisema? Ili tuitwe waongo athibitishe kwamba, ile taarifa yetu ya mwezi Disemba ni ya uwongo, sio atoe taarifa ya mwezi Juni. Maana sisi tumesema taarifa ya Disemba ambayo Serikali iliitoa mbele ya kamati na bahati mbaya ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Alichokuwa anauliza kwa nini uchague Disemba wakati ...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:...** subiri, mbona mnakurupuka? Tulieni kidogo, kazi yangu ni kuweka mambo sawa. Taarifa ulikuwa unasoma jana, lakini unachukua takwimu za Disemba, 2018, ndio ilikuwa hoja hapa.

*(Hapa, baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

**MWENYEKITI:** Tumpe nafasi ajibu.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Serikali kutoa taarifa, Serikali imeondoa utaratibu wa zamani wa kutoa taarifa kila robo mwaka tungeipata robo mwaka, imeweka utaratibu wa kutoa taarifa nusu mwaka na ndio taarifa ya Disemba.

Kwa hiyo kama taarifa imetoka Disemba taarifa nyingine inakuja mwezi Juni na hizi ni taarifa za ndani ya kamati na ndani ya Serikali yenyewe; sasa ukinukuu taarifa hizo unaitwaje muongo? Unaitwaje muongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa ijibu hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante muda, inatosha, inatosha. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Inatosha Mheshimiwa John. Utapata nafasi tena ngoja... *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sababu yaliyosemwa ni mengi...

**MWENYEKITI:** ...ngoja kidogo aliyekuwa anaongea naye, tulia kidogo...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tulia kidogo, naomba utulie kidogo, umeshayapitia karibu yote, ameshayapitia karibu yote, kuna bado ambalo halijawa sawa?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kwamba, kwa sababu yeye amesema *impromptu* hapo na ameainisha maeneo mengi, nimejibu machache, nipewe nafasi sasa na mimi kupitia *Hansard* haya niliyosema, ili kuleta vielelezo vingine vya ziada hoja kwa hoja, kipengele kwa kipengele, ziada ya hivi ambavyo tayari nimeshaviweka hapa mezani. Zaidi ya hivi nilivyoviweka mezani tulete vielelezo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nikwambie hizi taarifa tunazozitumia sisi, pamoja na kuwa Mheshimiwa Spika uliniondoa kwenye Kamati ya Nishati na Madini toka wakati

mbalimbali ni Waziri Kivuli, tunafanya kazi kama timu, tunazipata kutoka ndani ya Serikali yenyewe, ndani ya kamati na vyanzo mbalimbali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali, upotishaji unaendelea au umekwisha?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza upotoshwaji haujakwisha...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** ...aah, ndio, naomba nisikilizwe.

**MWENYEKITI:** Hapana, naomba tusikilizane. Mjadala huu una afya tu, wala msiwe na wasiwasi, tusikilizane.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja aliyoisema kwamba, ametumia takwimu za Disemba mimi sikusema kwamba, nilisema ametumia nia hasi ya kuonesha, ndio...

*(Hapa, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**...ndio, katika hoja hiyo kwamba, na yeye maelezo yake kwenye kitabu hiki Serikali haiiwezeshi *REA* na ndiyo maana...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Tulia! Tulia! Tulia! Tulieni!.

Naomba tusifanye fujo tumpe nafasi, kama nilivyokuwa namlinda Mheshimiwa Mnyika kwamba, msipige (Makofi) tumsikie. *No,* tusikilizane, endelea Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimemsikiliza Mheshimiwa Mnyika, bado ninasimama kwenye hoja zangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilisema ametumia takwimu za kupotosha Bunge, nilisema kuhusu masuala ya hasara na sikusema madeni ya *TANESCO* na kuhusu hasara Taarifa yake ilionesha tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani hasara ya *TANESCO* imekuwa ikiongezeka na ndipo mimi nilipotumia takwimu, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali nikisoma takwimu za hasara ambazo nimesema 2016 Juni, hasara ilikuwa bilioni 349…

**MWENYEKITI:** Hilo Mheshimiwa Mnyika amekamatwa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eeh, hii hapa.

**MWENYEKITI:** Eeh, hii hapa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Eeh.

**MWENYEKITI:** Enhee. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba lithibitike, lakini la pili hili alilosema kwamba, ametumia vipindi tofauti.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Naomba tutulie.

**MHE. MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Tutulie, tutulie, tutulie, ili Mheshimiwa Mnyika atakapokuwa anajibu ajue anajibu nini, sasa mkipiga kelele itakuwa ngumu kujua, ndiyo Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo linaanza ukurasa wa 22 wa hotuba yao, namna ambavyo amefanya *analysis* ya pesa zinazoenda *REA* akamalizia kwa kusema Serikali ya Awamu ya Tano haiiwezeshi *REA;* na ndipo nilipokuja kusema hata anaposema wanafanya kwa mashirikiano mmoja wa Naibu Waziri Kivuli ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati. Kama kweli kulikuwa na mashirikiano Kamati ya Nishati na Madini imetoa Taarifa yake na mtiririko wa fedha zilizokwenda *REA* kama ambavyo imekusudiwa kwa kipindi cha mpaka Mei, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni wazi takwimu hizi zikiachwa, taarifa hii ikiachwa ya kuonesha Serikali ya Awamu ya Tano haiiwezeshi *REA* si kweli kwa sababu, nyakati zote imetoa pesa zaidi ya asilimia 80 kwa hiyo, ni upotoshwaji. Naendelea kusimama na hoja zangu na niko tayari kuja kuthibitisha kwa vigezo na kwa vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaposema kwamba sheria ilibadilishwa kuleta taarifa; umetupangia ratiba ya vikao vya kamati; mpaka kamati ya kushughulikia masuala ya bajeti tunakwenda na utekelezaji wa mwaka wa fedha husika mpaka mwezi huo, kisha ndipo tunajadili bajeti. Ingekuwa kama Serikali kama alivyosema taarifa ni mara mbili kwa mwaka kungekuwa hakuna haja ya vikao vya kamati kuelekea kipindi cha Bunge, na kwamba itatoa taarifa za *current* taarifa kwa hiyo, naendelea kusimama taarifa imepotoshwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana, tutalitolea uamuzi hili jambo tutakaporudi pale kwenye Bunge zima.

Kif. 1001 – *Administration & Human Resources Management*..................Sh. 3,034,746,000
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*...........Sh. 899,560,000
Kif.1003 – *Policy and Planning Unit*...............Sh. 1,321,544,000

Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 428,444,000
Kif. 1005 – *Legal Service Unit*...............................Sh. 591,546,000
Kif. 1006 – *Government Communication Unit*..............................................Sh. 502,069,000
Kif. 1007 – *Procurement Management Unit*......Sh. 455,916,000
Kif. 1008 – *Environment Management Unit*........Sh. 364,240,000
Kif. 1009 – *Management Information System Unit*........................................Sh. 577,098,000
Kif. 2001 – *Minerals*.................................................................Sh. 0
Kif. 2002 – *Madini Institute*.....................................................Sh. 0
Kif. 2004 – *Tanzania Diamond Sorting Agency (TANSORT)*...........................................Sh. 0
Kif. 2005 – *Eastern Zone*..........................................Sh. 0
Kif. 2006 – *Western Zone*.......................................................Sh. 0
Kif. 2007 – *Lake Zone*................................................Sh. 0
Kif. 2008 – *Northern Zone*.........................................Sh. 0
Kif. 2009 – *Southern Zone*.........................................Sh. 0
Kif. 2010 – *Central Zone*..........................................................Sh. 0
Kif. 2011 – *Central Zone*............................................Sh. 0
Kif. 2012 – *Southern Western Zone*............................Sh. 0
Kif. 2013 – *Lake Victoria Eastern Zone*.........................Sh. 0
Kif. 2014 – *Lake Nyasa Zone*..........................................Sh. 0
Kif. 3001 – *Electricity and Renewable*.............Sh. 2,105,051,000
Kif. 3002 – *Petrolium and Gas*.......................Sh. 16,059,95,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## KITABU CHA NNE

## MATUMIZI YA MAENDELEO

### Fungu 58 – Wizara ya Nishati

Kif. 1001 – *Administration and Human Resources Management*..............Sh. 2,400,000,000
Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*................Sh. 1,850,000,000
Kif. 2001 – *Minerals*..................................................Sh. 0

Kif. 3001 – *Electricity and Renewable Energy*......................................Sh. 2,073,125,658,000
Kif. 3002 – *Petroleum and Gas*....................Sh. 39,078,342,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge Linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Mheshimiwa Waziri taarifa, tafadhali.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kanuni ya 104(3)(a) na (b) kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Sasa kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwamba sasa niwahoji kuhusu kukubali kwenu kupitisha Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/2020 – Wizara ya Nishati yaliidhinishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yote ya wataalam kupitia mashirika yote kwa kazi kubwa sana ambayo mmekuwa mkiifanya na tunawapa moyo sana. Pongezi hizi kwa kweli zimetolewa na karibu na kila Mbunge kutoka pande zote mbili za Bunge hili. Wamefurahia sana na kupongeza sana spidi yenu ya kazi, Naibu na Waziri mwenyewe mnapiga kazi kwelikweli. Kwa kweli msisitizo ulikuwa hasa kwenye umeme vijijini wale wakandarasi hebu wavute soksi sasa waende na spidi yenu, inaonekana spidi yenu hawawezi kui-*match,* hakuna mwenye mashaka kuhusu utendaji kazi wenu lakini sasa wale jamaa kidogo wavute soksi. *(Makofi)*

Tunajua kabisa katika eneo la nishati tumetoka kwenye kipindi ambacho miaka ya nyuma huko lilikuwa ni eneo lenye mgogoro mkubwa sana na tunajua sababu zake. Tulikuwa na madeni ya ajabu ajabu mmeeleza wenyewe mara *Aggreko,* huku sijui nani huku *IPTL, SONGAS* huku nani sijui, yaani tabu tupu, *Symbion* na kadhalika lakini taratibu tumeanza kuelekea mahali ambapo sasa tunaanza kuona mwanga kwa mbali. *(Makofi)*

Uwepo wa *Stiegler's Gorge* utapunguza sana uwezekano wa majenereta haya, kwa hiyo vita yake si ndogo katika kujenga *Stiegler's Gorge* sababu wanajua hawa *possibility* ya hizi mashine zao za dizeli chafu hizi itakuwa tumeondokana na huo upuuzi. Kwa hiyo, unapotaka kujikomboa lazima utapata *forces* zinazokupinga, kwa hiyo tuendelee jamani, tutatue tatizo la kukatikatika kwa umeme na tunaisubiri kwa hamu sana *densification project* itasaidia sana kusahisha maeneo ambayo yalipata umeme lakini bado yana matatizo. *TANESCO* pia kama ulivyosema leo, uunganishaji umeme uwe wa 27,000 nchi nzima, tunakupongeza mno na habari hii tutaipeleka nchi nzima. *(Makofi)*

Tunaomba tu *TANESCO* nao wakae mkao wa kusambaza umeme yaani kwa spidi ile ambayo unaielezea kama wangefanya *study* ya haraka *TANESCO* na kuona wateja ambao hako mbali sana wale wa nguzo moja, nguzo mbili na nguzo tatu nchi nzima wata-*hook millions of* kaya zikaingia katika kuwa wanalipa bili za mwezi, tunaweza ku-*double* hata ku-*triple* mapato ya *TANESCO* katika muda mfupi sana; nguzo mbili, nguzo tatu. Siku hizi Watanzania wanajenga nyumba nzuri sana, nyumba unazikuta zipo vijijini lakini hazina umeme, kisa kijiji hicho kilishapitiwa na ile *line* moja iliyopita tu kwenda kijiji kingine. *(Makofi)*

Sasa wakifanya hilo zoezi *TANESCO* wakawapata hawa wateja na wako wengi, hawa wananchi hawajawahi kutembelewa na Afisa yeyote wa *TANESCO* kwamba bwana wewe nguzo iko pale, ile habari ya nguzo mbili, nguzo tatu kama walivyokuwa wanaeleza Wabunge kwamba analazimika mmoja ndiyo anunue halafu wenzake wote ndiyo waunganishiwe; tukiliangalia hili vizuri, kwa *spirit* ile ile uliyonayo Waziri na Naibu wako wakiichukua hii tutafanikiwa, kwa sababu mteja akishaunganishiwa, huyo ni mteja wa *TANESCO,* labda mpaka hiyo nyumba ije ivunjike. Kwa hiyo, tukiwapata wengi maana yake na fedha zitakuwa nyingi na uwezo wa shirika utaongezeka na kadhalika. *Stiegler's* itakapokuja na huo umeme mkubwa ikute basi huku nako tumeshawapata wateja wengi sana katika kuwaunganisha. *(Makofi)*

*Otherwise* tunawapongeza sana wote kwa spidi kubwa na kwa kweli msione hivi, watu wanajua kwamba kura za mwakani 2020 nyingi sana kwa CCM zitakuwa ni kura zinazotokana na umeme wa *REA* yaani Mheshimiwa Rais mwakani enh, labda waende ambako hakuna umeme ndiyo utapata kura, wapi sasa?

Kwa hiyo, tunawaongeza mnafanya kazi takatifu sana na inayotuweka mahali pazuri sana na ni ukombozi kwa watu wetu ukiacha habari ya siasa na kura, ni ukombozi mkubwa sana kuwapelekea watu nishati ya umeme. Ni jambo kubwa sana la maendeleo, hatukuamini na hatukutarajia kwamba

katika muda huu mfupi kiasi hiki tunaweza katika eneo la nishati ya umeme tukawa tumefika mbali kiasi hiki, hongereni sana. *(Makofi)*

Sasa lile jambo letu sijui hata niliamuliaje?

**WABUNGE FULANI:** Liache tu.

**SPIKA:** Niliache tu?

**WABUNGE FULANI:** Ndio.

**SPIKA:** Kilichodhihirika hapa ni kwamba kwa kweli Mheshimiwa Mnyika amechapia, amepiga na uongo ndani yake. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni kwamba jamani tunajifunza, hizi hotuba tujaribu kuwa *realistic* kadiri inavyowezekana, yaani umakini wa kuandika hizi hotuba za Bunge uzidi kuongezeka kwa sababu zinasomwa na watu hata nje ya chumba hiki, tunazipiga kwenye mitandao hata waliopo nje *diaspora* na wengine wanasoma.

Waheshimiwa Wabunge, takwimu ni kitu muhimu sana, kwa hiyo ni vizuri kwenda na takwimu sahihi ila unaweza uka-*argue* wewe mwenyewe unavyotaka kipinzani, kikuunga mkono, lakini takwimu ibakie kuwa ni takwimu inayotusaidia wote ili hata anayesoma a-*make his/her own opinion* kutegemeana na takwimu ile, lakini akishapata *wrong statistics* inamfanya afanye *wrong conclusions*.

Kwa hiyo, ni kuwakumbusha wenzetu wote tunaoandika hotuba mbalimbali; Kamati, Kambi ya Upinzani na kadhalika. Kesho tunaendelea na Wizara nadhani ya Mheshimiwa Lukuvi kesho kushokutwa?

**WABUNGE FULANI:** Kesho Mambo ya Nje.

**SPIKA:** Sawa, kesho Mambo ya Nje na kesho kutwa na kadhalika, kama kuna takwimu ni vizuri takwimu zile zikakaa vizuri za ukweli ila una-*argue* vipi sasa hiyo *it's up to you.*

Mwisho, naomba niwakumbushe tena Waheshimiwa Wabunge kwamba tukitoka hapa, tunakaribishwa kuhudhuria futari ambayo imeandaliwa kwa ajili ya Wabunge wote. Nikisema hivyo na watumishi wa Bunge pia mnaalikwa wote; watumishi wa Bunge ni sehemu yetu. Kwa hiyo, wote mnaalikwa kushiriki katika futari hiyo ambayo itakuwa mara tu baada ya kuahirisha shughuli hizi za Bunge katika Hoteli ya Morena. Ukifika pale Morena ni kule kwa nyuma kwenye *swimming pool* siyo ndani pale kwenye hoteli, kwa hiyo ukifika unapitiliza kwa upande wa *swimming pool.* Nimeambiwa Bodi nzima ya *CRDB* imekuja kwa ajili yetu na wamejipanga kwa kweli kutoa futari ambayo itafunika kabisa.

Kwa hiyo, nawaomba asikose hata mmoja wetu, tuweze kushirikiana wote kwa pamoja na wenzetu hawa ambao ni wadau wetu na sisi ni wadau wao katika futari hii muhimu na kipekee mliofunga jamani msipitilize, tupite pale kidogo tu, baraka kidogo.

Basi baada ya maelezo haya, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.10 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*